

**MTINDO WA UWASILISHI WA DHAMIRA ZA UKIMWI KATIKA KAZI  
ZA FASIHI: KIELELEZO CHA TANZU TEULE ZA FASIHI ANDISHI**

**NA  
CHARLES KITUNI WASIKE**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA KITIVO CHA SANAA NA  
SAYANSI, IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA  
ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA  
UZAMIFU KATIKA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA MOI**

**2020**

**IKIRARI****IKIRARI YA MTAHINIWA**

Hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine. Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kutoleshwa bila kibali cha mwandishi na / au Chuo Kikuu cha Moi.

---

**Charles Kituni Wasike**  
SASS/DPHIL/ KIS/04/O9

---

Tarehe

**IKIRARI YA WASIMAMIZI**

Tasnifu hii imewasilishwa ili kutahiniwa kwa idhini na ridhaa yetu kama washauri na wasimamizi wa mzamifu walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Moi.

---

**Dkt. Mosol Kandagor**  
Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,  
Chuo Kikuu cha Moi.

---

Tarehe

---

**Dkt. Samuel M. Obuchi**  
Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,  
Chuo Kikuu cha Moi.

---

Tarehe

**TABARUKU**

Natabaruku kazi hii kwa Mwenyezi Mungu aliyenipa uhai, chanzo cha nguvu na bidii, neema, maarifa na motisha ya kuikamilisha.

## SHUKURANI

Mchakato wa kufanya utafiti na kuandika tasnifu katika kiwango hiki si kibarua rahisi. Ningependa kuchukua fursa hii kuwashukuru wote waliohusika na kuchangia kwa njia moja ama nyingine ufanisi wa kazi yangu. Shukrani zangu za mwanzo na za dhati namtunukia Mwenyezi Mungu kwa kunijalia siha njema kwa kipindi chote nilipokuwa naishughulikia kazi hii. Bila neema na kibali chake, singeweza kufikia hatua ambayo nimeifikia sasa.

Shukrani zangu kuu zawaendea wasimamizi wangu, Dkt. Mosol Kandagor na Dkt. Samuel M. Obuchi wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Moi. Nawapa hongera kwa kunielekeza, kunishauri na kunihimiza niendeleo wakati ambapo nilikuwa naelekea kukata tamaa. Uvumilivu wenu na hekima ya kunishauri, vilinipa msukumo wa kuendelea kupiga hatua hata ingawa mwanzoni ilionekana kama mlima mrefu. Nawashukuru sana kwa msaada wa vitabu, tasnifu, makala na kazi nyinginezo zilizochangia pakubwa ufanisi wa utafiti huu. Ningependa pia kuwashukuru wahadhiri wengine katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi ambao walinipa maoni yaliyochangia kuiboresha kazi hii.

Nashukuru pia wakitubi na wafanyikazi wengine katika maktaba ya Vyuho Vikuu mbalimbali walioniwezesha kuiendeleza na kuikamilisha kazi hii. Maktaba hayo ni pamoja na: Chuo Kikuu cha Kibabii, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia, Chuo Kikuu cha Moi, Chuo Kikuu cha Kenyatta, na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sitasahau kuwashukuru wasomi na wanafunzi wenzangu katika darasa la uzamifu; Dkt. Misiko Wasike na Dkt. Harriet Ibala ambao walinihimiza nijikaze kuikamilisha

kazi hii. Walinifaa kwa ushauri na makala kuhusiana na kazi yangu ya utafiti. Siwezi kuwasahau Dkt. Simiyu Wanjala na Dkt. Edwin Masinde wa Chuo Kikuu cha Kenyatta ambao walisoma kazi yangu na kuitolea uhakiki wa kina. Maoni yao yaliniwezesha kuipiga msasa na kuiboresha kazi hii.

Sina budi kuwashukuru wazazi wangu wapendwa, marehemu mzee James Nandasaba na mama Mary Nabwonya walionichochea, wakanitia moyo na kuniruzuku wakati nilipokuwa shuleni. Aidha, siwezi kuisahau familia yangu ya karibu. Natoa shukrani zangu za dhati kwa mke wangu mpendwa Jane Nesuwu Kituni kwa uvumilivu na kujitolea kwake kunisaidia wakati wa masomo yangu. Ufanisi wangu wa kukamilisha tasnifu hii haungepatikana bila msaada wake wa hali na mali. Ningependa pia kudhihirisha shukrani zangu za dhati kwa watoto wangu wapendwa; Kelvin Khaemba, Keith Wasike, Favor Simiyu na Bildad Kituni Wakhungu. Shukrani zangu spesheli zamwendea kitindamimba wangu Bildad Kituni ambaye alinifaa sana kwa kazi ya kupiga chapa kazi hii wakati alipokuwa likizoni.

Mwisho nashukuru Chuo Kikuu cha Moi na Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika kwa kunipa fursa ya kusomea shahada ya Uzamifu. Mwisho kabisa ningependa kuwashukuru wale wote ambao kwa njia moja ama nyingine sijawataja lakini walichangia katika kukamilika kwa kazi hii ya utafiti. Kwenu nyote mliohusika, nasema MUNGU AONAYE KWA SIRI AWABARIKI.

## IKISIRI

Janga la UKIMWI limekuwa katika jamii zetu kwa zaidi ya miaka thelathini na kwa kipindi hicho zaidi ya watu milioni 34 wameambukizwa ugonjwa huo ulimwenguni. Isitoshe, kulingana na UNAIDS (2012) watu zaidi ya milioni 18 wameaga dunia. Mwanzoni, ugonjwa wa UKIMWI ulisababisha maafa mengi sana na kutokana na sababu hiyo ukawa ugonjwa ulioogopwa sana katika maisha ya mwanadamu. Utafiti huu ulihakiki mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika kazi teule za fasihi andishi. Suala kuu la utafiti huu lilikuwa kwamba tafiti nyingi zilizofanywa hazijazamia mtindo kama kipengele kinachojisimamia na tena maarufu katika kufafanua dhamira. Madhumuni maalum ya utafiti huu yalikuwa: Kuchanganua namna mitindo tofauti ya uwasilishi imetumika kuibua suala la UKIMWI katika kazi teule za fasihi andishi, kubainisha dhamira mbalimbali zinazowasilishwa kwenye kazi teule za fasihi andishi kuhusu UKIMWI, kufafanua dhima ya mtindo katika uwasilishaji wa dhamira na kutathmini mchango wa kazi teule za fasihi andishi katika kukabiliana na janga la UKIMWI. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na ulizingatia muundo wa uchunguzi kifani. Nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo iliyoanzishwa na kutumiwa na Buffon (1930) iliongoza utafiti huu. Nadharia hii hutumiwa kurejelea mkabala wa uchanganuzi wa matini za kifasihi kwa kuchunguza mtindo kwa njia ya kisayansi. Nadharia hii inaweka msisitizo wake katika nafasi ya ujumi katika kazi za usanii. Lugha ya fasihi iliangukiwa kuwa ilitumia ujumi katika kueneza fikra au ujumbe. Ujumi huu ulidhihirishwa katika matumizi ya lugha kisanaa kwa lengo la kuumba wazo na kulisambaza kwa hadhira kwa namna ivutiayo kupitia upeo wa matumizi ya lugha ya kawaida. Kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia hii, mtafiti alihakiki kazi za tanzu tatu za fasihi andishi: riwaya, tamthilia na hadithi fupi zilizoteuliwa kimakusudi ili kupata data faafu iliyotosheleza mahitaji ya utafiti. Mchakato wa uteuzi wa sampuli kimakusudi ulizingatiwa katika uteuzi wa kazi kumi za kisanii zilizounda sampuli kwenye utafiti huu. Uteuzi wa sampuli iliyotumiwa katika utafiti huu ulishirikisha riwaya zifuatazo: *Sitaki iwe Siri* na Matundura (2008), *Ua la Faraja* na Mkufya (2005), *Pendo Katika Shari* na Momanyi (2008) na *Kala Tufaha* na Omar (2007). Tamthilia zilizoteuliwa ni: *Giza* na Jilala (2004), *Kilio Chetu* na Medical Aid Foundation (1995) na *Orodha* ya Steve Reynolds (2006). Hadithi fupi zilizotumika ni: *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* na Iribemwangi (2007), *Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine* ya King'ei na Kobia (2007) na *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine* ya Walibora na Mohamed (2007). Katika utafiti huu, niliteua vifungu vya data nikiongozwa na malengo ya utafiti. Data iliyokusanywa ilirekodiwa na kuchanganuliwa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya Nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Kuhusu lengo la kwanza, utafiti huu umegundua kwamba waandishi wengi walitumia tashbihi, kuchanganya ndimi, methali, taswira na misemo kuwasilisha masuala kuhusiana na UKIMWI. Mintarafu ya lengo la pili, utafiti ulibaini kuwa licha ya tofauti za mitindo na tanzu, wasanii wanafanana katika dhamira wanazowasilisha kuhusu suala la UKIMWI. Kuhusu lengo la tatu, utafiti ulibaini dhima ya mtindo na kutambua namna ambavyo fasihi inaweza kutumika kukabiliana na janga la UKIMWI. Utafiti huu umegundua kwamba mtindo unaotumika kwenye fasihi una athari kubwa ujumbe unavyopokelewa. Mtindo ni kipengele muhimu katika kazi yoyote ya kisanii kwani huifanya ieleweke na wasomaji. Utafiti huu unahitimisha kwamba ujumbe unaofanana kuhusu UKIMWI unaweza kuwasilishwa na waandishi tofauti kwa njia na mitindo tofauti. Utafiti huu unapendekeza kwamba licha ya sayansi, fasihi inaweza kutumika kama mbinu mbadala ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Utafiti huu aidha unapendekeza kwamba watafiti wa baadaye wanaweza kuchunguza suala la UKIMWI katika tanzu zingine kama ushairi na maandishi mengine kwa kuongozwa na nadharia tofauti.

## ABSTRACT

The HIV scourge has been in our society for more than three decades and during that period more than 34 million people have been affected by the disease in the world. In addition, according to UNAIDS (2012) more than 18 million people have died. Initially, the HIV&AIDS disease caused a lot of destruction and consequently, it became the most feared disease in the history of mankind. This study analyses figures of speech and style in selected Kiswahili Literature texts on HIV&AIDS. The statement of the problem is that many studies that have been done on style haven't examined it as an independent and important variable that can be used to analyse themes on broader perspectives. The study was guided by the following specific objectives: to analyse figures of speech and style that are used to expose issues of HIV&AIDS in selected Kiswahili works, to assess how figures of speech and style have been used to present objectives regarding HIV/AIDS in selected Kiswahili works and to analyse the role of style and the contribution of selected Kiswahili texts in the fight against HIV/AIDS. This study was carried out in the library and adopted the case study design. The theory of Stylistics that was pioneered and used by Buffon (1930) guided this study. This theory refers to the method of analysis of literary texts in a scientific way. It puts emphasis on the role of aesthetics of language in literary works. Language and literature employed aesthetics to present ideas in works of art. Aesthetics was presented in the use of language creatively for the purpose of moulding an idea and presenting it to the audience in an impressive way. Guided by the tenets of this theory, the researcher analysed selected works of Kiswahili literature from three genres: novels, plays and short stories that were selected purposefully to arrive at suitable data that would satisfy the requirements of the study. Purposeful sampling procedure was used to select ten literary works that formed the sample size of this study. The selected novels include: *Sitaki Iwe Siri* by Matundura (2008), *Ua la Faraja* by Mkufya (2005), *Pendo Katika Shari* by Momanyi (2008) and *Kala Tufaha* by Omar (2007). Selected plays were: *Giza* by Jilala (2004), *Kilio Chetu* by Medical Aid Foundation (1995) and *Orodha* by Steve Reynolds (2006). Selected short stories were: *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* by Iribemwangi (2007), *Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine* by King'ei and Kobia (2007) and *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine* by Walibora and Mohamed (2007). In this study, I picked specific data text fragments that were clearly aligned to the objectives of the study. Data that was collected was recorded and analysed as guided by specific objectives, together with the tenets of the stylistic theory. Results were presented in a descriptive form. On objective one, the study established that many authors mostly used similes, code mixing, riddles, imagery and sayings to present HIV/AIDS related matters. In light of objective two, the study established that despite the differences in the genres and style, different artists have similar underlying concerns that are presented regarding HIV/AIDS. In respect to objective three, the study established different ways in which Kiswahili literature can be used to fight HIV/AIDS. The study has found out the style that is used in literature has a great effect on determining how the message will be received. Style is a critical component in any literary work for it enables it to be well understood by readers. This study concludes that similar messages of HIV/AIDS can be presented by authors in different ways and styles. This study recommends that other than science, literature can be used as an alternative way in the fight against HIV/AIDS. The study also recommends that future researchers could investigate HIV/AIDS as a societal concern in other genres like poetry and other texts by using other theories.

## YALIYOMO

IKIRARI .....	ii
TABARUKU .....	iii
SHUKURANI.....	iv
IKISIRI .....	vi
ABSTRACT.....	vii
YALIYOMO.....	viii
ORODHA YA JEDWALI .....	xii
FASILI YA ISTILAHU .....	xiii
MAELEZO YA AKRONIMU NA VIFUPISHO .....	xiv
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
<b>MISINGI YA UTAFITI .....</b>	<b>1</b>
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Usuli wa Suala La Utafiti.....	1
1.1.1 Fasihi kwenye vita dhidi ya UKIMWI.....	1
1.1.2 Vipengele vya mtindo katika uwasilishaji wa ujumbe.....	3
1.1.3 Mawasiliano kuhusu UKIMWI na kazi za kisanii zilizoteuliwa.....	5
1.2 Suala la Utafiti .....	9
1.3 Malengo ya Utafiti .....	10
1.4 Nadharia Tete za Utafiti.....	10
1.5 Umuhimu wa Utafiti .....	11
1.6 Sababu za Kuchagua Mada.....	12
1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	13
1.8 Hitimisho.....	15
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>16</b>
<b>MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA.....</b>	<b>16</b>
2.0 Utangulizi.....	16
2.1 Mtindo Katika Kazi za Fasihi .....	16
2.2 Matumizi ya Lugha .....	18
2.3 Tamathali za Usemi .....	19
2.3.1 Tashibihi.....	22
2.3.2 Tashihisi .....	23
2.3.3 Takriri.....	23
2.3.4 Sitiari .....	24



2.4 Dhamira katika Kazi za Fasihi .....	25
2.5 Msingi wa Kinadharia.....	37
2.6 Hitimisho.....	42
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>43</b>
<b>MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>43</b>
3.0 Utangulizi.....	43
3.1 Mbinu za Utafiti.....	43
3.2 Muundo wa Utafiti.....	43
3.3 Eneo la Utafiti .....	45
3.4 Uteuzi wa Sampuli.....	46
3.5 Ukusanyaji wa Data .....	46
3.6 Uchambuzi wa Data.....	47
3.7 Uwasilishaji wa Data .....	48
3.8 Masuala ya Etikeli.....	48
3.9 Hitimisho.....	49
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>50</b>
<b>MITINDO YA KUWASILISHA DHAMIRA ZA UKIMWI.....</b>	<b>50</b>
4.0 Utangulizi.....	50
4.1 Matumizi ya Mbinu za Lugha na Tamathali za Usemi.....	50
4.1.1 Mjadala wa mbinu za lugha na tamathali za usemi.....	52
4.1.2 Tashbihi.....	53
4.1.3 Kuchanganya ndimi.....	77
4.1.4 Methali .....	85
4.1.5 Taswira.....	99
4.1.6 Misemo.....	107
4.1.7 Mdokezo.....	126
4.1.8 Sitiari .....	136
4.2 Hitimisho.....	142
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>143</b>
<b>DHAMIRA KATIKA MAANDISHI TEULE KUHUSU UKIMWI.....</b>	<b>143</b>
5.0 Utangulizi.....	143
5.1 Kuporomoka kwa Maadili ya Jamii.....	143
5.2 Unyanyapaa.....	164
5.3 Dhuluma Dhidi ya Wanawake .....	176

5.4 Utamaushi .....	194
5.5 Usiri Kuhusu Ugonjwa wa UKIMWI .....	202
5.6 Athari ya UKIMWI.....	213
5.7 Ukosefu wa Uwajibikaji .....	221
5.8 Hitimisho.....	223
<b>SURA YA SITA.....</b>	<b>225</b>
<b>DHIMA ZA MTINDO NA NAFASI YA FASIHI KATIKA KUKABILIANA NA UKIMWI.....</b>	<b>225</b>
6.0 Utangulizi.....	225
6.1 Dhima za Kimaudhui .....	225
6.1.1 Kumfikirisha msomaji.....	225
6.1.2 Uhamasishaji wa Jamii.....	228
6.1.3 Kufafanua Mawazo .....	231
6.2 Dhima ya Tamathali za Usemi Kifani .....	234
6.2.1 Kupamba lugha .....	235
6.2.2 Uwezo wa msanii kuchagua muundo na mtindo wa kazi yake.....	237
6.3 Mchango wa kazi teule za fasihi katika kukabiliana na UKIMWI.....	238
6.3.1 Kuepokana na uasherati.....	238
6.3.2 Matumizi ya mipira ya kondomu .....	243
6.3.3 Uwazi kuhusu UKIMWI .....	248
6.3.4 Uaminifu katika maisha ya ndoa.....	253
6.3.5 Kupinga taasubi za kiume .....	257
6.3.6 Kupinga unyanyapaa .....	261
6.3.7 Kutoa elimu, mafunzo na kupunguza bei ya dawa za UKIMWI .....	268
6.3.8 Kuzingatia maadili ya jamii .....	272
6.4 Hitimisho.....	274
<b>SURA YA SABA .....</b>	<b>275</b>
<b>MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI.....</b>	<b>275</b>
7.0 Utangulizi.....	275
7.1 Muhtasari wa Utafiti .....	275
7.2 Mahitimisho ya Utafiti.....	276
7.2.1 Matumizi ya mitindo tofauti ya uwasilishi katika kuliibua suala la UKIMWI kwenye kazi teule za fasihi andishi .....	276

7.2.2 Dhamira mbalimbali zinazowasilishwa kwenye kazi teule za fasihi andishi kuhusu UKIMWI.....	278
7.2.3 Dhima ya mtindo na mchango wa fasihi andishi katika kukabiliana na janga la UKIMWI .....	280
7.3 Mchango wa Utafiti .....	281
7.4 Mapendekezo ya Utafiti.....	282
MAREJELEO .....	284
VIAMBATISHO.....	293
Kiambatisho cha 1: <i>Ua la Faraja</i> .....	293
Kiambatisho cha 2: <i>Kala Tufaha</i> .....	298
Kiambatisho cha 3: <i>Pendo Katika Shari</i> .....	301
Kiambatisho cha 4: <i>Sitaki Iwe Siri</i> .....	304
Kiambatisho cha 5: <i>Orodha</i> .....	306
Kiambatisho cha 6: <i>Kilio Chetu</i> .....	308
Kiambatisho cha 7: <i>Giza</i> .....	310
Kiambatanisho cha 8: <i>Likizo Ya Mauti Na Hadithi Nyingine</i> .....	313
Kiambatisho cha 9: <i>Alidhani Kapata Na Hadithi Nyingine</i> .....	315
Kiambatisho cha 10: <i>Kiti Cha Moyoni Na Hadithi Nyingine</i> .....	316

**ORODHA YA JEDWALI**

Jedwali la 4.1: Mdafao wa ujitokezaji wa mbinu za lugha na tamathali za usemi katika riwaya teule.....	52
---	----

## **FASILI YA ISTILAHU**

<b>Lugha ya kitamathali</b>	Ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum iliyokusudiwa na mtunzi.
<b>Masuala Ibuka</b>	Ni maudhui yanayorejelea mambo ambayo yamezuka katika jamii na yanaiathiri moja kwa moja.
<b>Masuala ya Kimaadili</b>	Ni mienendo bora inayozingatiwa katika jamii.
<b>Matini</b>	Kinachoweza kujisimamia katika kueleza dhana fulani.
<b>Mchakato</b>	Ni mfuatano wa hatua katika utekelezaji wa jambo.
<b>Mkakati wa Mawasiliano</b>	Ni mpango unaozingatiwa kupata matokeo kamili kutokana na mchakato wa mawasiliano.
<b>Uchunguzi kifani</b>	Ni utafiti unaompa mtafiti uhuru wa kuteua jambo moja mahususi ambalo atalichunguza kwa kina.
<b>Virusi vya Ukimwi</b>	Viumbe hai ambao kimaumbile hawajafikia ngazi ya seli wanaosababisha ukimwi.
<b>Waliohasirika</b>	Wenye ukimwi au virusi vya ukimwi.

**MAELEZO YA AKRONIMU NA VIFUPISHO**

<b>ARVs</b>	Antiretroviral therapy (Dawa ya kupunguza makali ya UKIMWI).
<b>Dkt</b>	Daktari.
<b>Khj</b>	Mwandishi ameshatajwa awali.
<b>Mhr</b>	Mhariri.
<b>Taz</b>	Tazama.
<b>TUKI</b>	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
<b>Uk</b>	Ukurasa.
<b>UKIMWI</b>	Hii ni hali ya ukosefu wa kinga mwilini inayosababishwa na virusi vya UKIMWI. UKIMWI hudhoofisha mwili ukawa hauwezi kujikinga dhidi ya virusi.
<b>UNAIDS</b>	Joint United Nations Programme on HIV & AIDS.
<b>VVU</b>	Virusi vya UKIMWI.
<b>WHO</b>	World Health Organisation.
<b>WWVU/U</b>	Wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

## **SURA YA KWANZA**

### **MISINGI YA UTAFITI**

#### **1.0 Utangulizi**

Sura hii ina maelezo kuhusu usuli wa utafiti kwa jumla ambapo nafasi ya lugha na fasihi katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI imefafanuliwa. Aidha, sura hii inaweka wazi suala la utafiti, malengo na nadharia tete zilizoongoza utafiti huu. Isitoshe, imeangazia umuhimu wa mada, sababu za kuchagua mada na kuonyesha upeo pamoja na mipaka ya utafiti. Kwa jumla ni sura inayoweka msingi wa utafiti huu.

#### **1.1 Usuli wa Suala La Utafiti**

Utafiti huu ulilenga kuhakiki mtindo wa maandishi ya UKIMWI katika kazi teule za fasihi andishi. Utafiti huu ulihakiki maandishi teule kutoka riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Waandishi tofauti wana upekee wao katika uwasilishaji wa kazi zao na utafiti huu ulifanywa ili kuubaini upekee huo na athari yake kwa dhamira zinazowasilishwa kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Sehemu hii ya usuli imegawika katika vijisehemu vitatu. Katika sehemu ya kwanza, nimeeleza namna fasihi imetumika kwenye vita dhidi ya UKIMWI. Katika sehemu ya pili, nimeangalia namna vipengele vya mtindo vimetumika katika uwasilishaji wa ujumbe na katika sehemu ya tatu nimeonyesha mawasiliano yanayohusu UKIMWI na kazi za kisanii zilizoteuliwa kwenye utafiti huu.

##### **1.1.1 Fasihi kwenye vita dhidi ya UKIMWI**

Tangu kugunduliwa kwa maradhi ya UKIMWI katika miaka ya 1980 nchini Kenya, jamii imeendelea kuhamasishwa kuhusu jinsi ya kukabiliana na maradhi haya. Baadhi ya makundi yaliyojishughulisha ni kama vile mashirika ya kibinafsi, mashirika yasiyo

ya kiserikali, wanahabari, wanamuziki, viongozi wa kisiasa, asasi za kidini na wasomi. Waandishi mbalimbali wameshughulikia mada ya UKIMWI kupitia tanzu mbalimbali. Kwa mfano, Mutembei (2009) ameshughulikia ushairi kama utanzu uliojadili suala la UKIMWI hadharani. Utafiti wetu ni mpana kuliko wa Mutembei (k.h.j) kwa vile unachunguza mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI kwenye tanzu tatu za fasihi andishi ambazo ni riwaya, tamthilia na hadithi fupi.

Annensia (2015) anasema kwamba sanaa ya nyimbo ni miongoni mwa sanaa ambazo wanajamii wa Kinyankole kutoka Uganda wametumia kwa upekee katika kuzungumzia ugonjwa wa UKIMWI. Katika kufanya hivyo, wanajamii hawa hawako peke yao kwani kuna ithibati kwamba wasanii mbalimbali duniani wamelizungumzia suala hili la UKIMWI kwa mapana na marefu.

Mutembei (k.h.j) anaeleza fasihi kama kiashiria katika kupambana na UKIMWI. Anasema kwamba katika fasihi, matumizi ya mbinu za lugha na tamathali za usemi kama vile sitiari, tashbihi, tashhisi na hata kejeli ni kichocheo kikubwa katika kuelezea na kueneza kampeni dhidi ya kuenea kwa UKIMWI. Utafiti wetu umehakiki mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika maandishi teule ya fasihi na kutathmini mchango wa maandishi hayo katika kupambana na ugonjwa wa UKIMWI.

Kazi mbalimbali za fasihi aghalabu hujishughulisha na masuala anuwai yatokeayo katika jamii kiuchumi, kisiasa na kijamii. Wasanii wa kazi hizo huwasilisha ujumbe kwa madhumuni ya kufunza, kuonya na kuielekeza jamii kwenye njia sahihi. Waandishi wengi wa kazi za fasihi wamejishughulisha na dhamira ya ugonjwa wa UKIMWI kwa ajili ya kuielimisha jamii ili iweze kuchukua hatua stahiki za kuepukana na janga hili. Utafiti wetu umehakiki baadhi ya maandishi teule ili kuibua



dhamira mbalimbali na kutathmini mchango wa maandishi hayo ya fasihi andishi katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI.

Dhamira ambayo sasa imejisimika na kuwa na mizizi katika jamii ni ile inayojadili ugonjwa wa UKIMWI. Nyimbo, mashairi, ngonjera na michezo ya kuigiza ilianza kulizungumzia janga hili hasa kutokea mwishoni mwa miaka ya 1980 (Taz. Mutembei 2001 na 2002). Kwa sasa nyimbo mbalimbali kuhusu UKIMWI, dalili zake, madhara yake pamoja na namna ya kuepukana na ugonjwa huo zinaimbwa katika maeneo mengi. Utafiti wetu umehakiki mtindo wa uwasilishi na dhamira mbalimbali zinazoibuliwa kwenye maandishi teule ya fasihi ya Kiswahili ili kubaini upekee wa maandishi na pia kutathmini mchango wa maandishi hayo katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI.

### **1.1.2 Vipengele vya mtindo katika uwasilishaji wa ujumbe**

Lugha ina vipengele kadha wa kadha vya mtindo ambavyo hutumiwa na wasanii wa kazi za sanaa. Matumizi ya vipengele hivyo hutegemea maudhui, wakati na muktadha maalum. Hivyo basi ili kuelewa maana na ujumbe wa matini ni lazima tuchambue lugha kupitia vipengele vyake ambavyo hubeba maana na ujumbe. Mtindo ni sifa ya kipekee aliyonayo msanii; ni upekee wa msanii katika utunzi wa maneno, msamiati, lugha na muundo wa kazi ya Sanaa. Kila mwandishi au msanii ana upekee wake wa mtindo katika ubunaji wa kazi za Sanaa. Hivyo basi tunapochunguza ama kuchambua ujumbe wa kazi za kifasihi hatuwezi kuepuka vipengele vya kimtindo vya kazi hizo. Kama anavyoeleza Leech (1969) kazi ya fasihi haiwezi kueleweka vizuri bila kuwa na maarifa ya lugha ambayo ndiyo njia ya kujieleza. Kwa hivyo, ili kuelewa kazi ya fasihi ni lazima kuchunguza nduni za kiisimu za lugha fulani na jinsi msanii anazitumia kwa kuzihusisha na malighafi ya kiisimu ili kuelewa kile

kinachowasilishwa. Utafiti wetu unachunguza mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI wa kazi za fasihi kwenye tanzu teule za fasihi andishi. Uhakiki huu unalenga kuhakiki vipengele vya kimtindo katika kazi teule za fasihi andishi na nafasi yavyo katika kuendeleza dhamira za UKIMWI.

Kwa vile vipengele vya lugha kimtindo hubeba ujumbe wa kazi fulani za fasihi, utafiti huu basi unaona ipo haja ya kuchunguza vipengele vya kimtindo vilivyotumiwa katika riwaya, tamthilia, na hadithi fupi teule. Lengo hasa ni kutaka kuchunguza namna wasanii wa tanzu hizo za fasihi andishi wanavyofanana, kutofautiana na kuhusiana katika uteuzi wa vipengele vya kimtindo ili kuwasilisha suala la UKIMWI.

Dhana ya mtindo imeshughulikiwa na wahakiki wengi hasa katika karne hii. Hii inatokana na ukweli kwamba mtindo ndiyo njia kuu inayosaidia katika uelewaji wa maudhui na dhamira zinazoshughulikiwa katika matini husika. Madai haya yanashikiliwa na Simpson (2004) anaposema kuwa uchanganuzi wa kina wa mtindo huifanya kazi ya fasihi kueleweka vyema zaidi. Licha ya kushughulikiwa kwa mapana na marefu, kuna tofauti kubwa sana kutegemea mtazamo na nia ya mhakiki. Dhana ya mtindo ina mawanda mapana na hufafanuliwa na wataalamu mbalimbali kwa njia zinazotofautiana. Maana kuhusu dhana ya mtindo hutegemea zaidi uelewa na mtazamo wa mhakiki na vipengele anavyochagua kuvishughulikia. Ngara (1982) anahoji kuwa mtindo huweza kufafanuliwa kwa kutumia wahusika, msuko, maudhui na lugha.

Katika kazi ya fasihi, fani ina vipengele vya kimtindo ambavyo hutumiwa na wasanii kuwasilisha ujumbe wa kazi za Sanaa. Hivyo basi, utafiti huu umejikita katika vipengele viwili vya mtindo ambavyo ni matumizi ya lugha na tamathali za usemi. Baadhi ya mbinu za lugha na tamathali za usemi ambazo zimezingatiwa katika utafiti

huu ni pamoja na: tashbihi, kuchanganya ndimi, misemo, mdokezo, sitiari, methali na jazanda. Matumizi ya lugha na tamathali za usemi ni vipengele muhimu sana katika ujenzi wa kazi za Sanaa. Baadhi ya watafiti kama vile Mutembei (2002), Mosha (2002), Wamitila (2003), Jilala (2008) na Senkoro (2011) wameeleza kuwa maana ya kazi ya fasihi hujikita katika vipengele vya lugha kama vile sitiari, tashbihi, tashhisi, kejeli, methali, misemo na nahau. Vipengele hivi hutumika na wasanii mbalimbali katika kuwasilisha kazi zao kwa hadhira waliyoilenga. Hivyo basi, utafiti huu utachunguza kipengele cha lugha na tamathali za usemi ili kubaini mtindo wa uwasilishi unaotumiwa na wasanii wa riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule katika kuwasilisha suala la UKIMWI.

Mwandishi wa kazi ya fasihi huteua maneno fulani akiwa na lengo fulani na wala hatumii maneno kwa njia ovyo tu. Ufundi huu wa kuteua ndio hudhahirisha upevu wake wa lugha na hujitokeza katika tamathali za usemi anazozitumia. Hii ndiyo sababu Phythian (1970) akinukuliwa na Wambua (2011) anasema:

Mtunzi wa kazi ya fasihi huchagua maneno fulani baada ya mengine na kuyaweka au kuyapanga mengine katika utaratibu maalum ndiposa yaweze kuoana na mengine ili kuleta maana na athari kwa wasomaji (uk.26).

Kwa hivyo, tamathali za usemi zina mchango mkubwa katika kuifanya kazi ya fasihi ivutie, iwe na msisitizo na mnato mkubwa na hivyo kumhusisha msomaji wa kifasihi katika kupata ujumbe uliofumbika kwenye matini ya kifasihi.

### **1.1.3 Mawasiliano kuhusu UKIMWI na kazi za kisanii zilizoteuliwa**

Mawasiliano ni muhimu kwa wanadamu wote kwa sababu yanawezesha kuimarisha maarifa yao kuhusiana na matukio yatokeayo ulimwenguni. Airhinenbuwa na Obegonm (2000) wanadahili kuwa wasomi wanafanya juhudi kubwa kuibuka na mikakati faafu ya mawasiliano ambayo itachangia katika kuimarisha maisha wakiwa

na ufahamu mpana kwamba kuna watu walio na virusi vya UKIMWI (VVU) katika jamii. Kwa maoni yao, mikakati kama hiyo inapaswa kujikita katika nadharia madhubuti ambayo inaweza kutumiwa katika maeneo na makundi tofauti. Utafiti huu unalenga kutalii maandishi teule ya fasihi kuhusu UKIMWI ili kuona mitindo tofauti ya uwasilishi na namna maandishi hayo yamechangia katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI.

UKIMWI husababishwa na virusi vinavyodhoofisha mfumo wa kinga mwilini na hivyo huufanya mwili kuwa dhaifu kiasi cha kuufanya usiweze kudhibiti magonjwa nyemelezi ambayo husababisha vifo. Kulingana na Robert na wengine (2010), njia kuu inayosababisha maenezi ya ugonjwa huu ni kupitia ngono ya watu wa jinsia tofauti, ikifuatiwa na hali ambapo mama huipitisha kwa mtoto wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua au wakati wa kunyonyesha. Katika utafiti huu, maandishi mbalimbali yaliyotumiwa yamewasilisha dhamira ambapo wahusika mbalimbali wameambukiza wengine UKIMWI kupitia kwa ngono isiyo na kinga.

Utafiti kuhusu virusi vya ugonjwa huo umefanikisha watafiti kutengeneza dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI maarufu kama 'ARV' ambazo zinaongeza maisha ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Dawa za kupunguza makali zimesaidia kudumisha afya, kurefusha maisha na kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Katika baadhi ya kazi zilizotumika katika utafiti huu, dawa za kupunguza makali zilikuwa ghali kiasi cha kuwazuia baadhi ya wanajamii kuzipata. Aidha, jamii nyingine hazikuwa na ufahamu wa dawa hizi ambazo zingesaidia katika kurefusha maisha ya muathiriwa wa UKIMWI. Ukosefu wa mawasiliano bora kuhusu ugonjwa wa UKIMWI ulichangia katika maenezi yake katika jamii.

Sorcar (2009) anadahili kwamba kuelimisha watu kuhusu UKIMWI ni jambo lisilo rahisi kwa sababu hali ya virusi vinavyosababisha UKIMWI (VVU) huhusishwa na masuala nyeti kama vile ngono, matumizi ya kondomu, uasherati, ndoa za jinsia moja miongoni mwa mengine. Masuala haya yote yamewekewa mwiko wa kiisimu na kitamaduni katika jamii nyingi ulimwenguni. Kwa maoni yake, Sorcar (k.h.j), mawasiliano kuhusu masuala nyeti hugeuzwa ili yaingiliane na kaida za tamaduni za jamiilugha husika. Tafiti mbalimbali zimeonyesha jinsi wanajamii tofauti wanavyotumia mbinu na njia mbalimbali za kulijadili suala la UKIMWI. Mbinu hizo ni pamoja na matumizi ya mafumbo, tasfida, uchanganyaji msimbo na utohozi, kulingana na (Moto, 2004, Ogechi, 2005 na Kobia, 2008). Utafiti huu umehakiki maandishi teule ya fasihi andishi ili kuona iwapo mbinu zilizotajwa zimetumika katika kupitisha ujumbe kuhusu UKIMWI.

Fasihi ni kati ya njia zinazotumiwa kama jukwaa la kuhamasisha jamii kuhusu masuala yanayowazingira watu. Ni kutokana na kugundua umuhimu wa fasihi katika jamii ambapo Taasisi ya Elimu Nchini Kenya imependekeza kuwa mada kuhusu masuala ibuka yakiwemo UKIMWI yazingatiwe katika fasihi kutoka darasa la kwanza hadi kidato cha nne. Vilevile, ni somo la lazima kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa chuo kikuu. UKIMWI umejitokeza katika tanzu mbalimbali za fasihi kama vile ushairi, riwaya, hadithi fupi na tamthilia. Mathalan kuna hadithi fupi zilizo na visa vya UKIMWI kama vile *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004), *Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine* (2007), *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007) miongoni mwa maandishi mengine. Mutembei (2009) anasema kuwa kuna mashairi mengi ambayo yamechapishwa katika vitabu na magazeti yanayohusu suala la UKIMWI yakiwa na lengo la kuhamasisha jamii na kuionya dhidi ya maradhi hatari ya UKIMWI yasiyo na tiba. Kwa sababu hiyo, mashairi yalionekana kuwa na nafasi

kubwa katika kushughulikia suala la UKIMWI. Sawa na ilivyo kwa ushairi, tanzu zingine za fasihi andishi zina dhima kubwa katika jamii kama vile kukosoa, kuelimisha, kufafanua utamaduni, kuonya, kufichua hali zinazoizingira jamii, kufariji na kuburudisha.

UKIMWI ni miongoni mwa masuala ibuka yanayoathiri jamii ya sasa na umeshughulikiwa sio tu na wataalam, bali pia na wanajamii wenyewe. Watu mbalimbali wameshughulikia UKIMWI kwa njia tofauti. Lugha teule hutumiwa kama chombo cha kuwasilisha ujumbe na kuhamasisha jamii kuhusu UKIMWI. Kwa mfano, Gachara (2005) amechunguza nafasi ya matumizi ya lugha katika kufanikisha kampeni dhidi ya maradhi ya UKIMWI. Utafiti wa Gachara (k.h.j) unatofautiana na wetu kwa vile yeye aliangalia wazungumzaji wa lugha ya Kikuyu jijini Nairobi na Nyeri huku utafiti wetu umechunguza mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika maandishi teule ya fasihi andishi. Naye Kimani (2006) anaeleza kuwa kuna uhusiano wa picha na matini katika mabango na matangazo ya UKIMWI. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa vile wetu unachunguza mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika maandishi teule ya fasihi huku wa Kimani ukiangalia uhusiano wa picha na matini kwenye mabango kuhusu UKIMWI.

Katika utafiti huu, nimechagua kazi za kisanii ambazo zimeandikwa katika ukanda wa Afrika Mashariki na wakazi wa Afrika Mashariki. Maandishi haya ya kisanii yalichapishwa kati ya miaka ya 1993 na 2008. Kabla ya mwaka wa 1993, kulikuwa na maandishi machache sana ya kisanii kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Hali hii huenda ilisababishwa na baadhi ya watu kutouelewa vyema ugonjwa huu huku wengine wakiuogopa sana. Ni katika kipindi hiki ambapo maandishi ya kisanii yalishirikiana na mikakati mingine ya kufanya UKIMWI kueleweka miongoni mwa watu. Aidha

maandishi haya yaliwapa watu changamoto katika jamii kubadili tabia na mienendo yao kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI. Maandishi haya ya kisanii yanawasilishwa kwa mitindo tofauti kudhihirisha nguvu za mawasiliano kinyume cha unyamavu uliohusishwa na ugonjwa wa UKIMWI ulipotokea mwanzoni.

Mintarafu ya hayo, utafiti huu ulifanya uchunguzi wa kina kuhusu mtindo wa uwasilishi uliotumika na waandishi tofauti kuliibua suala la UKIMWI katika maandishi teule ya fasihi andishi. Utafiti huu ulihakiki riwaya, tamthilia, na hadithi fupi teule za Kiswahili zinazozungumzia ugonjwa wa UKIMWI ili kubaini namna mtindo wa uwasilishi umefanikisha dhamira za kuiasa na kuitahadharisha jamii kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Mtafiti hana ufahamu wowote kuhusu utafiti wa kitaaluma uliofanywa kuhusu mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika tanzu tatu za fasihi andishi; riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule na hivyo utafiti huu ulifanywa ili kuliziba pengo hili.

## **1.2 Suala la Utafiti**

Matini yoyote ya kifasihi inahitaji kusomwa na kueleweka ili ipate kuwa na manufaa katika jamii husika. Ingawa hivyo, kueleweka kwa matini hubainika iwapo msomaji ataelewa mtindo uliotumika katika uwasilishaji. Japo huu ndio ukweli wa mambo, tafiti nyingi zilizofanywa hazijazamia mtindo kama kipengele kinachojisimamia na tena maarufu katika kufafanua dhamira. Lugha ya kitamathali imetumika na wasanii mbalimbali kuelezea masuala yanayohusu UKIMWI katika maandishi ya kifasihi. Tunafahamu kwamba kila mwandishi wa kazi ya sanaa ana upekee wake wa kuiwasilisha kazi yake. Lakini je, upekee huu waweza kuwa na athari yoyote katika uwasilishaji wa kazi za fasihi zinazohusu UKIMWI?

Aidha, dhamira mbalimbali zimewasilishwa na wasanii tofauti kuhusu suala la UKIMWI. Je, mtindo wa uwasilishi kupitia riwaya, tamthilia na hadithi fupi una athari yoyote kwa dhamira zinazowasilishwa kuliibua suala la UKIMWI? Ingawa tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu suala la lugha na UKIMWI, hakuna utafiti tunaoufahamu ambao umechunguza suala la mtindo kwa mtazamo mpana wa maandishi teule ya riwaya, tamthilia, na hadithi fupi. Utafiti huu umebaini pengo hili na unaazimia kuliziba.

### **1.3 Malengo ya Utafiti**

Suala kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza mitindo ya uwasilishi iliyotumiwa na wasanii katika kufanikisha dhamira kwenye riwaya, tamthilia, na hadithi fupi teule zinazoshughulikia ugonjwa wa UKIMWI kama mojawapo ya masuala makuu. Katika kutimiza suala hili, utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi yafuatayo:

- i. Kuhakiki mitindo tofauti ya uwasilishi ilivyotumika kuibua suala la UKIMWI katika kazi teule za fasihi andishi.
- ii. Kujadili dhamira mbalimbali zinazowasilishwa kwenye kazi teule za fasihi andishi kuhusu UKIMWI.
- iii. Kufafanua dhima ya mtindo na kutathmini mchango wa kazi teule za fasihi andishi katika kukabiliana na janga la UKIMWI.

### **1.4 Nadharia Tete za Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

- i. Mitindo tofauti ya uwasilishi hutumika kuibua suala la UKIMWI katika kazi teule za fasihi andishi.
- ii. Dhamira mbalimbali kuhusu UKIMWI zinawasilishwa kwenye kazi teule za fasihi andishi.



- iii. Mtindo una dhima huku kazi teule za fasihi andishi zikiwa na mchango katika kukabiliana na janga la UKIMWI.

### **1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Tafiti nyingi za kiakademia katika viwango mbalimbali vya usomi zimefanywa kuhusu hadithi fupi, riwaya na tamthilia za waandishi tofauti. Katika uchunguzi wetu, hatujapata maandishi yoyote kuonyesha utafiti uliofanywa kuhusu namna matumizi ya lugha na tamathali za usemi zimetumika kuibua suala la UKIMWI katika riwaya nne, tamthilia tatu na hadithi fupi tatu teule zinazozungumzia ugonjwa wa UKIMWI.

Kwa sababu hii, utafiti wetu utachangia katika kuelewa maandishi teule ya fasihi andishi yanayozungumzia masuala ya UKIMWI kwa vile tumeweza kubaini mbinu anuwai za kitamathali ambazo waandishi wametumia kuibua dhamira. Umuhimu mwingine ni kuwa kwa vile Kiswahili kinazidi kupewa umuhimu katika taasisi tofauti kote ulimwenguni, kuna haja ya fasihi iliyoandikwa kuhakikiwa kwa kuchunguza kazi zenyewe ili zieleweke kikamilifu katika kiwango cha matumizi ya lugha, tamathali za usemi na dhamira. Aidha, UKIMWI ni suala ibuka na uhakiki wa maandishi yake utalifanya lieleweke zaidi katika jamii hususan kwa wale watakaosoma maandishi husika. Ni muhimu kuhakiki na kutathmini masimulizi yanayohusu UKIMWI jinsi yalivyo katika tanzu za fasihi andishi kwa kuwa kutaongeza ufahamu wa masuala ya UKIMWI na kuwapatia wanajamii nafasi nzuri ya kufikiria na kuyawazia maradhi hayo ambayo yana uwezo wa kuiangamiza jamii.

Aidha kitaaluma, na hususan upande wa fasihi andishi, utafiti huu una mchango mkubwa kwa vile umefafanua vipengele mbalimbali vya matumizi ya lugha na tamathali za usemi. Ufafanuzi wa vipengele hivi unamfaa sana msomaji wa vitabu vya fasihi kuhusu UKIMWI kwa vile utarahisisha uelewa wa dhamira zilizoibuliwa.

Vilevile , utachangia uelewa wa vipengele vya mtindo katika tanzu tofauti za fasihi ya Kiswahili. Kazi hii inaweza kutumika kama marejeleo muhimu kwa wale wanaozidi kufanya utafiti kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Utafiti huu pia ni muhimu sana kwani umeweka wazi maeneo mengine ambayo hayajafanyiwa utafiti na watafiti wengine.

Isitoshe, utafiti huu ni muhimu katika kuongeza idadi ya maandishi ya kitaaluma kuhusu mawasiliano ya UKIMWI. Zaidi ya kuongeza maandishi yanayohusu fasihi na UKIMWI, utafiti huu una uwezo wa kuwachochea wanafasihi au watafiti katika viwango mbalimbali vya kitaaluma kufanya utafiti zaidi katika uwanja huu wa maandishi kuhusu UKIMWI. Kwa jumla, utafiti huu ni muhimu kwa taaluma nzima ya fasihi hasusan kwa utanzu wa fasihi andishi na uhakiki wa maandishi yake.

### **1.6 Sababu za Kuchagua Mada**

Mtafiti alichochewa na sababu kadha wa kadha katika kuchunguza mtindo katika uwasilishaji wa dhamira za UKIMWI kwenye tanzu za fasihi andishi ya Kiswahili. Sababu moja ni kwamba UKIMWI ni suala ibuka ambalo linaathiri jamii zote ulimwenguni na hivyo halipaswi kuachiwa wataalam wa tiba pekee bali lapaswa kushughulikiwa na wataalam wengine wa lugha na fasihi. Wataalam wasio wa tiba ni wasanii ambao wanalishughulikia suala hili kupitia maandishi yao yanayowahamasisha wasomaji kuhusu athari ya ugonjwa wa UKIMWI.

Sababu ya pili ni kwamba tiba ya UKIMWI bado haijapatikana. Hivyo basi uzuiaji wa maambukizi umebakia njia muhimu ya kupunguza makali ya ugonjwa huu. Kwa mintarafu ya hayo, kuna haja ya kuwa na mwingiliano au ukuruba wa kitaaluma kati ya somo la fasihi na taaluma ya utabibu katika kukabiliana na UKIMWI. Fasihi inaweza kuhamasisha wasomaji licha ya kupendekeza njia bora za kushiriki ngono, kuondoa unyanyapaa na kuchangia kuwapa tumaini walioathirika na walioambukizwa.

Vilevile, mtafiti alichagua mada hii kutokana na sababu kwamba masuala ya UKIMWI aghalabu huwasilishwa kwa mitindo mbalimbali katika tanzu tofauti za fasihi. Pana haja ya mitindo hiyo kufafanuliwa ili wasomaji wengi wa kawaida wapate kuelewa kilichowasilishwa katika maandishi husika.

Sababu nyingine ni kuwa kazi ya uhakiki katika jamii ni kuhamasisha na kuibua mitazamo mipya. Wahakiki wanatumia stadi zao za uhakiki kuelewa jamii ya mwandishi, thamani, falsafa na kuwasilisha ujumbe kuhusu UKIMWI kwa hadhira ya mwandishi. Ni jambo la kimsingi basi kuhakiki na kutathmini umbuji kuhusu UKIMWI na jinsi unavyojitokeza katika tanzu za fasihi ya Kiswahili kwa kuwa utaongeza ufahamu wa masuala ya UKIMWI na kuwapatia wanajamii nafasi nzuri ya kutafakari kuhusu maradhi haya yaliyo na uwezo wa kuiangamiza jamii.

Isitoshe, uchaguzi wa mada hii ulitokana na sababu kwamba tanzu mbalimbali za fasihi andishi ya Kiswahili zinapanua uwanja wa usomaji wa walengwa katika utafiti huu. Aidha tanzu za riwaya, tamthilia, hadithi fupi na mashairi zinaendelea kuwa kipengele muhimu cha somo la fasihi katika shule za msingi, upili na vyuo. Tanzu hizi zina sehemu mahsusi na muhimu katika dhima ya fasihi ya kuhamasisha, kukosoa, kutahadharisha, kufundisha, kuelimisha na kufafanua utamaduni wa jamii. Ili kupatia tanzu hizi dhima yake inayostahiki, uhakiki huu umekusudia kuonyesha jinsi masimulizi haya kuhusu UKIMWI yanavyoweza kuwa usemi wenye kusudi la kuionya jamii dhidi ya mienendo inayoweza kuwatia katika janga hili na kuwapa moyo walioathiriwa.

### **1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulijikita katika tanzu tatu za fasihi andishi ambazo ni; riwaya, tamthilia, na hadithi fupi. Kwa vile kuna maandishi kadha wa kadha kuhusu UKIMWI, utafiti huu

haungeyashughulikia yote. Utafiti huu uliibua data yake kutoka riwaya nne, tamthilia tatu na hadithi fupi sita kutoka kwa diwani tatu za hadithi fupi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Riwaya zilizoshughulikiwa ni: Mkufya (2005), *Ua la Faraja*, Matundura, (2008), *Sitaki Iwe Siri*, Momanyi (2008), *Pendo Katika Shari*, na Omar (2007), *Kala Tufaha*. Tamthilia zilizoshughulikiwa ni; Medical Aid Foundation, (2010), *Kilio Chetu*, Jalala (2004), *Giza*, na Reynolds (2006), *Orodha*. Kwenye utanzu wa hadithi fupi, hadithi zilizohakikiwa zilitoka kwa diwani zifuatazo: Kingei na Kobia (2007) (Wahariri), *Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine*, Iribemwangi (2007), (Mhariri) *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, Walibora na Mohamed (2010), *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine*. Aidha, tanzu hizo tatu ni pana sana na hivyo haingewezekana kushughulikia vipengele vyote vya uhakiki kwa kina. Hivyo basi utafiti huu ulijikita katika baadhi ya vipengele vya mtindo ambavyo ni matumizi ya lugha, tamathali za usemi na mbinu za usimulizi zilizotumiwa na waandishi tofauti kuibua suala la UKIMWI. Sababu kuu ya kuteua vipengele nilivyotaja ni kwamba ni vinatekeleza jukumu muhimu sana katika fasihi na lugha na hivyo pana haja ya kuvifafanua vieleweke zaidi ili vitumike kwa usahihi zaidi. Aidha, utafiti huu ulijadili dhamira kutoka kazi zilizoteuliwa na kuonyesha mchango wa kazi husika katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo ndiyo ilitumiwa kuongoza utafiti huu. Data mahsusi kutoka kwa maandishi teule yaliyotumiwa ndiyo iliyotumiwa kuibua matokeo ya utafiti huu. Nina hakika kwamba maandishi yaliyoteuliwa ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi kuhusu UKIMWI, yametupa sampuli wakilishi na hivyo kuwezesha mtafiti kuwa na data ya kutosha ya kutimiza malengo ya utafiti.

## **1.8 Hitimisho**

Sura hii imetoa msingi wa utafiti kwa kuangazia masuala mbalimbali. Miongoni mwa yale ambayo yamezungumziwa katika sehemu hii ni usuli wa suala la utafiti na suala la utafiti. Aidha, sura hii imeorodhesha malengo na nadharia tete zilizoongoza utafiti huu, ikatoa upeo wake na hatimaye kuangazia umuhimu wa utafiti. Sura inayofuata inaangazia mapitio ya maandishi na misingi ya kinadharia ambapo nadharia iliyoongoza utafiti huu imejadiliwa.

## **SURA YA PILI**

### **MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA**

#### **2.0 Utangulizi**

Sura iliyotangulia imeshughulikia usuli wa utafiti, suala la utafiti na malengo ya utafiti. Vilevile, imeorodhesha nadharia tete zilizoongoza utafiti huu, kuweka upeo na kueleza umuhimu wa utafiti huu. Sura hii imeangazia yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti na hatimaye imezungumzia nadharia iliyoongoza utafiti huu.

#### **2.1 Mtindo Katika Kazi za Fasihi**

Wamitila (2008) anaeleza kuwa mtindo ni elementi muhimu sana katika kazi ya kifasihi. Ili kuweza kubainisha sifa za kimtindo za kazi ya fasihi, mchanganuzi wa matini au kazi ya kifasihi anapaswa kuchunguza mambo mengi katika kazi inayohusika. Mambo hayo ni kama vile uteuzi wa msamiati wa mtunzi, miundo na mipangilio ya sentensi, uteuzi wa matumizi ya tamathali za usemi na jazanda, usawiri wa wahusika, motifu na dhamira zinazokaririwa katika kazi za watunzi na hata sifa za uakifishi hasa zinazoelekea kukiuka njia za kawaida za kuakifisha.

Kila mtunzi ana mtindo wake ambao ni tofauti na mtindo wa mtunzi mwingine. Hili hubainika katika uteuzi na utumizi wa vipengele vyote vya kimtindo. Hata watunzi au waandishi waliokulia katika mazingira sawa, lazima watatofautiana katika namna ya kutumia vipengele vya mtindo katika kazi zao.

Uteuzi wa vipengele vya kimtindo hutegemea ubunifu wa kisanii alionao msanii. Hivyo basi, mtindo hujumuisha vipengele vifuatavyo ambavyo vinahusiana sana kwani vinajumuishwa katika vipengele vya lugha:

- i. Uteuzi wa msamiati

- ii. Miundo na mpangilio wa sentensi
- iii. Uteuzi wa tamathali za usemi
- iv. Motifu
- v. Lugha
- vi. Usimulizi

Vipengele hivi vya mtindo vimetumika katika uchambuzi na ubainishaji wa vipengele vya tamathali za usemi katika maandishi teule kuhusu UKIMWI katika kuyaafikia malengo ya utafiti huu. Kutokana na wingi wa vipengele vilivyobainishwa hapo juu, si rahisi kushughulikia vipengele vyote vya mtindo, na hivyo utafiti huu ulijikita katika kuchunguza baadhi ya vipengele vya lugha tu katika mtindo.

Mtindo unaweza kuhusishwa na lugha iliyoandikwa, ingawa lugha ya kifasihi kwa kawaida inahusishwa na matini zozote za kifasihi. Katika uandishi wa fasihi, mtindo hutumiwa kwa maana nyingi. Mtindo unaweza kuwa mazoea ya lugha kama wanavyosema wanamtindo Crystal na Davy (1969). Ingawa hivyo, Ngara (k.h.j) anahoji kuwa mtindo huweza kufafanuliwa kwa kutumia wahusika, msuko, maudhui na lugha. Japo mtafiti anakubali kuwa vipengele vya mtindo ni vingi, utafiti huu utajikita katika tamathali za usemi na matumizi ya lugha.

Mtindo huweza kuhusisha mazoea ya lugha ya mtu binafsi au jamii lugha. Hii ndiyo maana ambayo huwajia watu akilini wanapozungumza kuhusu mtindo wa uandishi wa mtu fulani, mtindo wa kuzungumza na wa kutoa hotuba hadharani. Mtindo ni upekee wa kujieleza katika maandishi au mazungumzo. Ni jinsi waandishi huandika na pia ni njia tofauti za watu wanavyozungumza au kuandika katika miktadha ya kawaida ya kila siku. Kulingana na Miles (1971), mtindo na umbuji ni kama uteuzi wa kisanii wa kibinafsi wa kila mtunzi.

Mtindo unaelezwa kuwa sifa za lugha inayotumiwa. Mjadala umekuwepo kuhusu mtindo, swali likiwa; “Mtindo unarejelea nini au nani?”. Maoni ya Leech na Short (1981) ni kwamba, mtindo unaweza kurejelea yaliyoandikwa na pia yaliyosemwa kuhusu fasihi na aina zote za lugha zinazotumiwa siku baada ya siku. Leech (2007) anaeleza kuwa mtindo kwa tafsiri ya kijumla ni jinsi lugha inavyotumika katika muktadha fulani, inavyotumiwa na mtu kwa madhumuni fulani. Leech anasisitiza kuwa, kwa kawaida mtindo huhusishwa zaidi na matini ya fasihi andishi.

Mtindo wa uwasilishaji wa mawazo ni miongoni mwa mbinu za kimtindo ambazo mwandishi huzitumia kuyaibua mawazo yake katika matini za fasihi. Leech na Short (2002) wanaeleza kwamba mtindo wa uwasilishaji wa mawazo hutuwezesha kuyajua mawazo ya mwandishi na hata yale ya wahusika wake. Msingi huu unatuwezesha kuelewa na kuyaeleza maudhui na dhamira za mtunzi wa kazi husika. Masebo na Nyangwine (2008) wanaeleza kwamba dhamira ni wazo kuu au mawazo mbalimbali yanayojitokeza katika kazi ya fasihi. Kulingana na maoni yao, dhamira hutokana na jamii na zaweza kuwa za kisiasa, kijamii, kiuchumi au hata kitamaduni.

Mwandishi wa kifasihi hutumia mbinu anuwai kuwasilisha ujumbe wake kwa namna ambayo itaufanya uvutie, ueleweke na kisha kukubalika. Hivyo basi mbinu anazoteua mwandishi na kuzitumia katika uwasilishaji wake huathiri pakubwa namna kazi aliyoiandika itakavyopokelewa na kisha kuupitisha ujumbe wake kwa njia aliyoidhamiria.

## **2.2 Matumizi ya Lugha**

Katika fasihi, matumizi ya lugha hurejelea mbinu ambazo msanii anatumia kuwasilisha ujumbe wake. Matumizi haya ya lugha aghalabu huangaliwa kama mtindo wa mtu binafsi au mazoea yake katika uandishi wa fasihi. Kwa mintarafu ya hayo, kila



mwandishi ana uhuru wa kuteua na kuibuka na mbinu zake za kutumiwa kuwasilisha ujumbe wake. Aghalabu, matumizi ya lugha hutawaliwa na msimamo ama mtazamo wa msanii pamoja na lengo ama azma yake. Isitoshe, elimu na mazingira ya mtunzi huchangia pakubwa katika uteuzi wake wa lugha. Wataalamu Syambo na Mazrui (1992) wanaeleza kwamba mwandishi bora ni yule anayeweza kutumia msamiati, tamathali za usemi na miundo mingine ya lugha kumfanya msomaji awe na hisia fulani kwa upande wake. Mbatiah (2001) anaeleza kwamba fasihi ni tungo zinazotumia lugha kuweka pamoja upya tajriba za mwanadamu na kuwasilisha hisia na ujumbe mahsusi. Kulingana na fasiri na mawazo ya hawa wataalamu kuhusu fasihi, ni bayana kwamba lugha ndicho chombo kinachotumika katika kufanikisha mawasiliano. Maelezo yao yalitufaa sana katika utafiti wetu kwa maana tulichunguza mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika maandishi teule ya fasihi andishi.

### **2.3 Tamathali za Usemi**

Tamathali za usemi ni vifananishi au viwakilishi vya dhana moja kwa dhana nyingine tofauti au zinazotofautiana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum iliyokusudiwa na mtunzi. Kwa mujibu wa Wamitila (2003) tamathali za usemi hutumiwa kuelezea fungu la maneno au hata neno, ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine.

Mbatiah (2001) anaeleza kwamba tamathali ni ukiushi wa kimaksudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya semantiki na sintaksia ili kuleta maana mpya au msisitizo. Matumizi ya tamathali za usemi ni muhimu kwa vile huwezesha ujumbe mkali au nyeti kuwasilishwa bila matokeo ya kuhujumu mpokezi wa ujumbe.

Wamitila (2008) ni mmoja wa wataalamu ambao wameshughulikia dhana ya tamathali za usemi. Wamitila anazungumzia tamathali za usemi kama ‘lugha ya kitamathali’. Anasema kuwa dhana ya tamathali inatumiwa kwa upana ili kujumlisha sifa nyingi za kimtindo ambazo hutumiwa katika kazi za kifasihi. Dhana hii hutumika kuelezea aina ya ukiushi wa kimaksudi katika matumizi ya lugha, na ukiushi huu unaweza kuwa wa kimaana au wa kimuundo. Katika ukiukaji huu, neno au kifungu fulani hutumiwa kwa maana ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi.

Lugha ya kitamathali huwa na umuhimu mkubwa katika utunzi wa kazi za kifasihi. Wamitila anabainisha majukumu matatu makuu ya lugha ya kitamathali. Kwanza, ni urembeshaji wa kinachozungumziwa au kurejelewa na lugha hiyo na kukifanya kiwe na mvuto mkubwa wa kisanaa au kiumbuji; pili, ni jukumu la ufafanauji au uelezaji wa kinachohusishwa na tamathali maalum; na tatu, jukumu la uthibitishaji, yaani kukifanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti fulani. Majukumu haya matatu yanaweza kuhusishwa na lengo kuu la kuzua lugha au usemi wenye uwezo wa kushawishi kama anavyosema Wamitila (2008).

Senkoro (2012) anaainisha tamathali za usemi kuwa ni sitiari, tashbihi, metonomia, tashihisi, majazi, taashira na kejeli. Mulokozi na Kahigi (1979) wanaeleza kuwa, tamathali za usemi zinazotumika zaidi katika ushairi ni tashbihi, tashihisi, kejeli, metonomia na sitiari. Kwa mujibu wa Mulokozi na Kahigi (k.h.j) mifano zaidi ya tamathali za usemi ni: misemo, balagha, kwelikinzani, taswira na kinaya.

Kwa mujibu wa Senkoro (1982), tamathali za usemi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu maana, mtindo, maandishi ama hata mazungumzo. Aidha, tamathali za usemi hutumiwa kwa namna ya kupamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu wa lugha.

Mulokozi (1984) naye anafafanua tamathali za usemi kama tungo au kauli fupi za kisanaa zenye kubeba maana au mafunzo ya kijamii. Tamathali huchora picha kwenye akili ya msomaji ili kumwezesha kuelewa ujumbe kwa urahisi. Inabainika kuwa tamathali za usemi, licha ya kuipamba kazi ya fasihi, hufumba ujumbe wa mwandishi. Hii humhitaji msomaji kuufumbua ujumbe wa kazi hiyo kutegemea muktadha wake. Usanii hupatikana katika ukiushi wa kawaida wa lugha iliyozoeleka. Hiki ndicho anachokisisitiza Jakobson akinukuliwa na Njogu na Chimera (1999) anapoeleza kuwa fasihi ni matumizi ya nguvu dhidi ya lugha ya kawaida kimaksudi.

Tamathali za usemi pamoja na uainishaji wake ni dhana iliyoshughulikiwa na wataalam mbalimbali. Wataalam walio maarufu katika uainishaji wake ni pamoja na Holman (1960), Kuhenga (1977), Mbatiah (2001), na Senkoro (2011). Wataalamu hawa wote wanakubaliana kuwa tamathali za usemi ni ukiushi wa kimaksudi wa lugha ya kawaida katika fasihi. Hii ina maana kuwa maandishi wa fasihi huchukua lugha ya kawaida na kuifinyanga upya ili kuzalisha maumbo mapya katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii.

Kazi yoyote ya fasihi huwa na maana ya nje na maana ya ndani. Ili kupata maana ya ndani, msomaji au msikilizaji wa matini ya fasihi anahitajika kuchambua ubunifu wa mwandishi katika ujumi wa kazi husika. Utafiti ulilenga kushughulikia maana hii ya ndani kupitia uchanganuzi wa tamathali za usemi zilizotumika katika kazi teule za fasihi andishi. Ni wajibu wa kila mhakiki wa matini za fasihi kujaribu kuonyesha namna kila neno katika utungo wowote huwa na maana na umuhimu wake hasa kulingana na vile lilivyotumiwa.

Utafiti huu ulichunguza tamathali za usemi ili kuafikiana na lengo la kwanza la kazi hii. Utafiti huu uliongozwa na mhimili wa nne wa Nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo

unaosema kuwa mwandishi hutumia lugha kiufundi na athari za ujumi haziwezi kutenganishwa na matumizi ya kisanaa katika kazi anayoiandika. Mhimili huu uliuongoza utafiti huu katika kutambua na kuzishughulikia tamathali za usemi zinazojitokeza katika kazi teule za fasihi andishi.

Mbinu zote za kitamathali zina mchango mkubwa katika kuifanya kazi ivutie, iwe na msisitizo na mnato mkubwa, kuvutia nadhari ya hadhira na kuziathiri hisia zao. Hivyo basi, tamathali za usemi ni mojawapo ya vigezo vya kupimia ubunifu na umbuji katika kazi fulani. Mbinu hizi zina uamali katika uwasilishaji wa dhamira ya kifasihi. Katika sehemu ifuatayo, tutaelezea tamathali chache zilizotumika katika utafiti huu kulingana na malengo ya utafiti.

### **2.3.1 Tashibih**

Wasanii mbalimbali wametoa vijejezi vyao kuhusu tamathali ya usemi ya tashibih. Msokile (1993) anasema kwamba tashibih ni tamathali ya usemi inayohusisha vitu vitatu; kizungumziwa, kifananishi na kiungo. Kizungumziwa ni kitu halisi ambacho huzungumziwa na kitu kinacholinganishwa kwa fumbo. Kifananishi kipo katika mawazo na huzingatia maana iliyo dhahania. Kiungo ni sifa zipatikanazo katika kitu kinachozungumziwa. Kazi kuu ya kiungo ni kuhusisha vitu vyote viwili katika kuunda maana. Hii ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia waziwazi. Tashibih ni usemi wa kimlinganisho utumiao maneno au viungio kama vile mithili ya, kana kwamba, kama, kama vile, tamthili ya, sawa na, na kadhalika. Kuna mifano kama vile; mweusi kama makaa, mweupe mithili ya theluji na mrefu kama twiga. Mifano hii ni tashibih kwa sababu inalinganisha vitu kwa kutumia viunganishi.

Wamitila (2004) anasema kuwa tashibih ni misemo ya kilinganishi ambayo hukieleza kitu au sifa zake kwa kukilinganisha na kingine ili kuikuza sifa yake. Anazidi kusema

kuwa tashbihi huweza kuangaliwa kitaalam kwa njia mbili kuu. Kwanza, tashbihi huweza kuangaliwa kama usemi wa kilinganishi ambapo vitu viwili hulinganishwa. Pili, tashbihi inaweza kuangaliwa kama usemi wa kilinganishi ambao umefumbata maana fulani. Njia ya pili ndiyo msingi wa kueleza tashbihi kama mojawapo ya tamathali za usemi. Aina hii ya pili ndiyo tutakayoirejelea katika utafiti wetu. Mbali na tashbihi, wasanii aidha hushirikisha matumizi ya tashihisi. Mbinu ya tashihisi ndiyo tumeshughulikia katika sehemu ifuatayo.

### **2.3.2 Tashihisi**

Tashihisi ni usemi ambapo sifa ya uhai huhamishiwa kwenye kitu kisicho na uhai. Aghalabu tashihisi ni tamathali za usemi ambapo vitu visivyo na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo. Wamitila (2003) anaeleza kwamba tashihisi ni tamathali ya usemi ambapo vitu visivyokuwa hai huwasilishwa au husawiriwa kwa namna sawa na binadamu kwa kuweza kufikiri na kuhisi sawa na afanyavyo binadamu. Tashihisi hutumiwa zaidi na wasanii mbalimbali kama vile washairi ambao kwa mfano hawasiti kusema “kimya hakishi kunena, kitakapo kusimamia, fedha huita wazuri wakitika labeka, maji baridi yaliubusu mwili wake mwororo”. Katika mifano hii, kimya kimepewa sifa ya kibinadamu ya kunena na kusimamia, fedha imepewa sifa ya kuita na maji yamepewa sifa ya kubusu. Hivyo maneno kimya, fedha na maji yametumika kama tashihisi kwa kupewa uhai, yaani sifa za vitu vyenye uhai zimehamishiwa kwenye maneno hayo. Pamoja na tashihisi, takriri pia hutumika na wasanii katika kupitisha ujumbe wao kwa wasomaji. Sehemu inayofuata imefafanua mbinu ya takriri.

### **2.3.3 Takriri**

Takriri ni tamathali ya usemi ambayo hurudiarudia sehemu ya neno, neno ama sentensi kwa kusudi la kuonyesha msisitizo katika kile kinachomaanishwa na

mzungumzaji ama mwandishi. Hussein (1970) anaonekana akitumia takriri kwa kiasi kikubwa katika tamthilia ya *Kinjeketile* ili kusesitiza mambo kadhaa. Kwa mfano, “maji, maji, maji” ni takriri iliyolenga kuzungumzia suala la maji kama dawa ya kimuujiza katika kuwakinga watu dhidi ya risasi. Matumizi ya neno hilo kujirudia mara kadhaa humaanisha si maji ya kawaida.

Msokile (1993) anaeleza kuwa takriri ni marudiorudio ya sauti, silabi, neno, sentensi, wazo au ridhimu ili kuleta athari kwa msomaji wa kazi husika. Katika muktadha wa ushairi, takriri hutumiwa kuonyesha hisia nzito za kishairi. Takriri ni sifa muhimu inayopatikana siyo tu katika mitindo ya kazi za kifasihi bali pia katika maisha ya binadamu yenyewe. Uchunguzi katika kamusi yoyote ya lugha unadhihirisha ukweli kwamba sifa ya urudiaji inajitokeza katika sehemu nyingi ingawa majina yanayotumiwa kuelezea yanatofautiana kutegemea ni nini au nani anayehusishwa na urudiaji huo. Licha ya takriri, wasanii aidha huishirikisha mbinu ya sitiari ambayo imeelezwa katika sehemu inayofuata.

#### **2.3.4 Sitiari**

Wataalamu kadha wa kadha wameifafanua mbinu ya sitiari. Kahigi (1994) anafasili sitiari kuwa ni uhamishaji wa maana kutoka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine. Vikoa vya maana vinavyohusika katika uhamishaji huu huwa vinatofautiana angalau kwa sifa moja ya kimsingi, ambayo ni ya kisemantiki. Kinachohamishwa ni tabia, umbo au kazi ya kitu kwa kuihusisha na tabia, umbo au kazi ya kitu kingine kama wasemavyo Lakoff na Johnson (1980) katika kazi ya Kahigi (1994). Ili kuelewa dhana ya sitiari, tutumie mfano huu: Juma ni simba. Katika mfano huu, hatumaanishi kuwa Juma amegeuka kuwa simba yaani mnyama bali sifa za simba zinahamishiwa kwake, yaani, simba ana sifa ya ukali. Ukali unaonasibishwa na simba unahusishwa na

ukali wa Juma. Muundo wa sitiari una vipengele vitatu: kizungumzwa, kifananisho na kiungo kama wanavyosema Lakoff na Johnson (k.h.j) na Kahigi (k.h.j). Kizungumzwa ni kitajwa, ambapo katika mfano wetu, ni Juma. Kifananishi ni kitu kinachohusishwa na kizungumzwa na katika mfano tulioutoa ni simba. Kiungo ni tabia au sifa zinazounganisha kizungumzwa na kifananishi na katika mfano wetu ni ukali. Hivyo basi kwa kuzingatia tamathali za usemi zilizobainishwa na Senkoro (2012), utafiti ulichunguza lugha ya kitamathali ambapo vipengele vyake vimejikita katika uhamishaji wa maana kutoka katika dhana moja kwenda katika dhana nyingine ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira. Mbali na tamathali za usemi, dhana ya dhamira ni ya ukati sana katika utafiti wetu. Dhana hiyo ya dhamira ndiyo imeshughulikiwa katika sehemu inayofuata.

#### **2.4 Dhamira katika Kazi za Fasihi**

Dhana ya dhamira imeshughulikiwa na waandishi tofautitofauti katika juhudi za kuifanya ieleweke. Masebo na Nyangwine (2008) wanaeleza dhamira kama wazo kuu au mawazo mbalimbali yanayojitokeza katika kazi ya fasihi. Wanaeleza kwamba dhamira hutokana na jamii. Kwa maoni yao dhamira huweza kuwa za kisiasa, kitamaduni na kiuchumi. Katika maandishi yoyote, tunaweza kuwa na dhamira kuu na dhamira ndogo. Wamitila (2002) anasema kuwa dhamira hutumiwa kurejelea mada ya kazi fulani, ujumbe au lengo la kazi hiyo. Ingawa hivyo, kuna mielekeo ya kuitumia neno hili kwa maana maalum kurejelea suala fulani linalojitokeza na kukuzwa katika kazi ya kifasihi.

Dhamira ni jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo na jumla ya maana anayoitambua msomaji katika usomaji wake. Tunaweza kuvumbua maana ya kazi fulani kwa kuisoma kazi hiyo kwa kina na makini, huku tukiuelewa na kuung'amua

uhusiano wa visehemu mbalimbali pamoja na jinsi visehemu hivyo vinavyohusiana na kazi nzima na kuvyaza kitu kimoja. Kuna baadhi ya wahakiki ambao wanashikilia kuwa maana ya kazi haipo kwenye kazi bali huvyazwa na wasomaji wenyewe.

Dhamira kwa upande wake haiyahasishi majibu bali huzua maswali. Katika msingi huu, tunaona kuwa baadhi ya shutuma zitolewazo kuwahusu waandishi wa kifasihi kuwa kazi zao hazipendekezi majibu ya masuala ya kijamii zinahusiana zaidi na tasnifu kuliko na dhamira ya kazi. Wamitila (2008) anaeleza kwamba dhamira ni wazo kuu linaloitawala kazi ya kifasihi kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Wazo hili hukuzwa kwa njia zilizo wazi. Mojawapo wa njia hizi ni matumizi ya anwani ya kitabu kinachohusika. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mui Huwa Mwema*, mhusika Kotini ambaye alikuwa mhalifu anaishia kubadilika kuwa mwema.

Dhana ya dhamira huweza kuangaliwa kwa mtazamo wa nadharia za kihakiki. Katika msingi huu, fasili ya dhamira itategemea mkabala wa kihakiki unaohusika. Ingawa Njogu na Chimera (1999) wanatoa fasili tofauti na hii ya dhamira, wanaelekea kukubaliana na mtazamo uliopo hapa kwa kusema kuwa dhamira ni sehemu ya maudhui. Wamitila (2003) anasema kwamba dhamira ni lengo au wazo kuu ambalo mwandishi analikuza tangu mwanzo mwa maandishi mpaka mwisho. Wamitila (2008) anadahili kwamba watunzi katika kazi za fasihi ni watu ambao huyachukua matukio na visa vinavyotokea katika jamii zao na kuviwasilisha kiubunifu katika riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Kubuni hakumaanishi kudanganya, bali ni kuwasilisha dhamira kwa kutumia mbinu za kisanaa na hususan katika fasihi hujulikana kama fani ili kuleta hamu na hamasa kwa msomaji kuvutiwa kuisoma kazi husika na kuzipata barabara dhamira zilizolengwa na mtunzi wa kazi husika. Msimamo wa mtafiti ni kuwa dhamira ni lengo kuu la kazi ya kisani linalowasilishwa



kutoka mwanzo hadi mwisho wa kazi husika. Aidha, maudhui ni ujumbe wa kinachozungumziwa na mtunzi na hutumiwa katika kujenga dhamira ya mtunzi.

Wataalam mbalimbali wamefanya utafiti ambao unahusiana na wetu japo unatofautiana kwa njia moja au nyingine. Licha ya kutofautiana, utafiti huo umechangia katika kuujenga utafiti wetu. Leech na Short (1981) wametalii mawanda ya mtindo na pia wamejadili kuhusu nadharia ya Uhakiki wa Kimitindo. Aidha, wameangazia kuhusu uhusiano wa mtindo na maudhui na kuainisha viwango vya kuchanganua mtindo. Ingawa kazi yao imejikita katika tanzu zote za fasihi, mchango wao umetuongoza katika kuhakiki mtindo wa uwasilishi wa dhamira katika maandishi teule ya fasihi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Utafiti wao umejikita katika tanzu zote za fasihi ilhali wetu umejikita katika maandishi teule ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule. Kazi ya maandishi hawa imejenga kazi yetu japo tumetofautiana kwa upeo na mipaka.

Kitsao (1982) alichunguza maudhui katika tanzu za riwaya, tamthilia, ushairi na takwimu za kimitindo katika maandishi teule ya fasihi. Yeye alichanganua maandishi teule katika tanzu tatu zilizotajwa kwa kuangalia sarufi, msamiati na kwa kiwango fulani semantiki. Vipengele vya kimitindo vilivyomuongoza kufanya uhakiki ni pamoja na:

- 1) Urefu wa sentensi
- 2) Uchangamano wa sentensi
- 3) Virai kwa kila sentensi
- 4) Aina ya usemi
- 5) Maagizo ya mwandishi kwenye maandishi
- 6) Jumla ya maneno kwa kila mstari

- 7) Idadi ya silabi kwa kila neno
- 8) Aina za maneno
- 9) Msamiati uliotumiwa
- 10) Matumizi ya alama za uakifishaji

Kwa misingi ya vipengele vilivyoorodheshwa, Kitsao (k.h.j) alijikita katika sintaksia, mofolojia, fonolojia na semantiki. Utafiti wa Kitsao (k.h.j) ulihakiki tamthilia na riwaya kama wetu lakini ukatofautiana kwa maana yeye alihakiki ushairi tofauti na utafiti wetu uliohakiki riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Ingawa utafiti huu ulitujenga kwa upande wa maudhui lakini unatofautiana na wetu kwa maana wetu ulijikita katika vipengele vya lugha, tamathali za usemi na dhamira za kazi teule za fasihi andishi kuhusu UKIMWI. Utafiti wa Kitsao (k.h.j) haukuzingatia vipengele vya kisanaa kama vile ridhimu, taswira na vingine vya kubuni vya fasihi na hivyo utafiti wetu ulifanywa ili kuziba baadhi ya mapengo hayo.

Indangasi (1988) anazungumzia masuala kadhaa ya elimumitindo ambapo ameeleza historia ya elimumitindo na viwango vya kuchunguza mtindo kama vile fonolojia, sintaksia, msamiati, semantiki na tamathali za usemi. Uchanganuzi huu umetupatia mwelekeo mzuri wa kuchambua kazi yetu kwa vile tumeshughulikia matumizi ya lugha katika kiwango cha tamathali za usemi. Ingawa hivyo utafiti huu ni tofauti na wetu kwa vile yeye amejikita katika baadhi ya vipengele vya historia na isimu vya nadharia ilhali utafiti wetu umeegemea pakubwa katika vipengele vya matumizi ya lugha ambavyo tutachunguza kama tamathali za usemi, uteuzi na mpangilio wa maneno, sajili za lugha na matumizi ya misemo mbalimbali kwenye maandishi teule ya fasihi.

Msokile (1992) amejadili vipengele mbalimbali vya fani na moja kati ya vipengele hivyo ni mtindo. Anaeleza vipengele vya mtindo kuwa uchaguzi wa maneno, matumizi ya taswira na ishara, maelezo na masimulizi miongoni mwa masuala mengine. Uchambuzi wake wa mtindo umekuwa msingi mzuri wa kuchambua vipengele vya tamathali za usemi katika kazi yetu. Utafiti wa Msokile (k.h.j) unatofautiana na wetu kwa vile yeye amejikita katika kufafanua mtindo ilhali utafiti wetu umehakiki mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika maandishi teule ya fasihi andishi.

Baada ya mwaka wa 1993, wasanii mbalimbali wa fasihi kutoka mataifa ya Afrika Mashariki walishughulikia dhamira za UKIMWI katika kazi zao kwa kutumia mashairi, tamthilia, riwaya na hadithi fupi wakiwa na lengo la kuelimisha, kuonya na kuhimiza walio na maradhi ya UKIMWI kuendelea kuishi. Maradhi haya yameziathiri jamii nyingi kwa njia hasi. Kufikia sasa hatujapata ushahidi uliotolewa kwamba tiba ya ugonjwa wa UKIMWI imegunduliwa katika taaluma ya utabibu kote ulimwenguni. Njia kuu ambayo inatumiwa na jamii dhidi ya ugonjwa huu ni kupitia uhamasishaji. Kwa mintarafu ya hayo, utafiti huu umeazimia kwamba fasihi itaipa jamii jukwaa muhimu la kukabiliana na maradhi haya kupitia uhakiki wa maandishi teule ya fasihi andishi.

Mohamed (1995) amefafanua maana ya mtindo na kuangalia dhana mbalimbali za mtindo. Mjadala wake kuhusu mtindo umekuwa wa manufaa kwa vile umechunguza vipengele vya tamathali za usemi ambavyo pia ni vya kimtindo. Ingawa hivyo utafiti wake unatofautiana na wetu kwa vile yeye amejikita katika kuangalia dhana mbalimbali za mtindo ilhali utafiti wetu umehakiki mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika maandishi ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule. Aidha,

maandishi mahsusi ya tanzu za fasihi andishi yametumika katika utafiti wetu ilhali yeye ameangalia dhana ya mtindo kwa ujumla.

Mohochi (1995) amechanganua vipengele vinne vya fani katika hadithi nne za waandishi tofauti. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti wetu kwani inaangazia kipengele cha kintindo cha lugha ambacho sisi pia tumeshughulikia. Ingawa kuna huo uhusiano lakini kazi hizi za utafiti zinatofautiana. Kazi yetu imeshughulikia mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule huku kazi ya Mohochi (k.h.j) ikijihusisha na vipengele vinne vya hadithi fupi. Kazi hizi mbili zinatofautiana pakubwa kwa upande wa upeo.

Gunduza (1998) alichunguza mchango wa kazi za kifasihi katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu athari za UKIMWI kwa kuchunguza mchango wa washairi nchini Zimbabwe. Utafiti wa Gunduza (k.h.j) ulijenga utafiti wetu kwa vile pia ulihamasisha na kuelimisha jamii kuhusu athari za UKIMWI. Ingawa utafiti huu unakaribiana na wetu kwa kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu athari ya UKIMWI, unatofautiana na wetu kwa vile yeye alishughulikia mashairi ilhali utafiti wetu ulihakiki riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule. Aidha utafiti wetu ulihakiki vipengele vya mtindo licha ya kuonyesha mchango wa kazi za fasihi katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI.

Mbatiah (2000) amehakiki diwani ya *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* na amegusia suala la mtindo katika hadithi fupi. Amefafanua dhana ya mtindo kwa kuonyesha kuwa mtindo huhusishwa na maudhui. Mchango wake ni muhimu katika kazi yetu kwa vile umetuwezesha kuieleza dhana ya mtindo kwa kina. Utafiti wa Mbatiah (k.h.j) umejikita katika hadithi fupi tu ilhali kazi yetu imehakiki maandishi ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule. Licha ya mtindo, utafiti wetu umejadili dhamira

mbalimbali za UKIMWI na kuonyesha namna ambavyo fasihi andishi inaweza kutumika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI.

Page (2000) alifanya utafiti kuhusu sitiari za magazetini kuhusu UKIMWI. Alihitimisha kuwa matumizi ya lugha ya sitiari katika magazeti yaliathiri mtazamo wa jamii kuhusu UKIMWI. Aidha, Page (k.h.j) aliona mbinu hii kama kipengele muhimu kilichotumiwa sana katika matini za magazeti ili kuonyesha namna jamii inavyojadili, inavyoelewa na inavyofasili UKIMWI. Utafiti huu uliujenga wetu kwa vile umeshughulikia kipengele cha mtindo. Ingawa hivyo, utafiti wa Page (k.h.j) ni tofauti na wetu kwa vile yeye alizingatia sitiari katika magazeti ilhali utafiti wetu ulihakiki mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule. Utafiti wetu umehakiki vipengele vingi vya mtindo ilhali yeye amejikita tu katika sitiari.

Wales (2001) amefafanua kwa kina dhana ya mtindo na elimumitindo. Aidha, ametoa fafanuzi mwafaka za tamathali anuwai za usemi. Hivyo basi, kazi yake imetufaa katika kurejelea dhana mbalimbali katika utafiti wetu kuhusu tamathali za usemi. Ingawa hivyo, utafiti wa Wales (k.h.j) unatofautiana na wetu kwa vile wetu umeangalia vipengele vingine kama vile dhamira za UKIMWI na namna ambavyo maandishi teule ya fasihi andishi yametumika katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI.

Ongarora (2002) alishughulikia mtindo katika diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Katika kazi hii, amechambua matumizi ya methali, semi, tamathali za usemi, na mbinu nyingine za lugha. Utafiti huu umetufaa kwa vile katika kazi yetu tumehakiki tamathali za usemi katika riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule. Ingawa hivyo, utafiti huu unatofautiana na wetu kwani huu umehakiki diwani moja ya hadithi

fupi ilhali wetu umehakiki riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule kuhusu ugonjwa wa UKIMWI.

Ochoki (2005) alishughulikia tamathali za usemi za sitiari na jazanda katika riwaya mbili za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1990) za Kezilahabi. Ochoki (k.h.j) alitumia Nadharia mbili ambazo ni Umuundoleo na Umwingiliano matini. Manufaa ya kazi yake kwetu ni kwamba inatupatia ufunuo kuhusu uchanganuzi wa matumizi ya mbinu za lugha kwa vile ameshughulikia baadhi ya vipengele vya mbinu za matumizi ya lugha. Kazi hii inatofautiana na yetu kwa vile yeye aliangalia sitiari na jazanda katika riwaya mbili ilhali kazi yetu ilihakiki mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika maandishi teule ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule.

Kobia (2008) alifanya utafiti kuhusu mafumbo na VVU/UKIMWI katika jamii ya Waluhya Magharibi mwa Kenya. Utafiti wa Kobia ulijikita katika kuhakiki mafumbo yanayotumika kuelezea VVU/UKIMWI miongoni mwa wazungumzaji wa Kiluhya wa mkoa wa Magharibi. Utafiti wa Kobia uligundua kwamba mafumbo yanayotumika kuelezea VVU/UKIMWI katika jamii ya Waluhya yaliichukua hali hiyo kama mkasa, ajali, janga na pia kama mnyama hatari anayerarua mwanadamu. Utafiti wa Kobia ulitofautiana na wetu kwa vile ulijikita kwenye mafumbo peke yake ilhali wetu ulishughulikia mbinu mbalimbali za kimtindo zilizotumika na waandishi wa riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule kuwasilisha dhamira za UKIMWI.

Wanyonyi (2009) alihakiki riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ya S.A Mohamed. Katika kazi yake alishughulikia matumizi ya lugha kama vile lugha ya kitamathali, tasfida, ishara na uashiriaji wa masuala ya balagha. Aidha, alihakiki kazi yake kwa mtazamo wa Nadharia ya Saikolojia Changanuzi. Kazi hii ilisaidia kujenga kazi yetu kwa vile imeshughulikia mbinu mbalimbali za kimtindo sawa na yetu. Ingawa hivyo, kazi yetu

inatofautitana na yake kwa sababu inahusu mtindo wa uwasilishi wa UKIMWI ambao watunzi wa riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule kuhusu UKIMWI wametumia kuwasilisha dhamira zao ilhali kazi yake ilihakiki riwaya moja tu ya *Nyuso za Mwanamke*.

Jansen na wenzake (2010) walifanya utafiti kuhusu ufaafu wa mafumbo katika kueleza masuala kuhusu UKIMWI. Utafiti huo ulitathmini ufaafu wa kutumia mafumbo katika matini zilizotumiwa kufundisha wanafunzi kuhusu UKIMWI mjini Cape Town, Afrika Kusini. Mafumbo yalipotumika katika matini za kufundishia kuhusu UKIMWI, uchunguzi huo ulifichua kwamba wanafunzi wengi waliozisoma walielewa kuliko matini ambazo hazikuwa na mafumbo kuhusu UKIMWI. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwa vile wetu ulihusu mbinu anuwai za uwasilishi wa dhamira za UKIMWI ilhali wa Jansen na wenzake (k.h.j) ulishughulikia mafumbo peke yake. Aidha, utafiti wa Jansen na wenzake (k.h.j) ulihusu matini zilizotumika kufundisha wanafunzi kuhusu UKIMWI ilhali wetu ulihusu mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika maandishi teule ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi.

Olali (2010) amehakiki riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) ambapo alichanganua tamathali za usemi na mbinu za lugha. Utafiti wake ulitufaa sana katika utafiti wetu kuhusu mchango wa lugha ya kitamathali katika kukabiliana na UKIMWI. Ingawa utafiti wake unakaribiana na utafiti wetu kwa vile unashughulikia masuala ya tamathali za usemi, lakini kwa upande mwingine unatofautiana kwa kiwango kikubwa. Utafiti wetu umejikita katika kueleza namna mbinu za kitamathali zimetumika kufanikisha dhamira katika riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule zinazozungumzia masuala yanayohusu ugonjwa wa UKIMWI ilhali utafiti wa Olali (k.h.j) ulihakiki tu riwaya moja ya *Babu Alipofufuka*.

Too (2010) alitafitia tamthilia ya *Nguzo Mama* (1982) ya Penina Muhando. Alitumia Nadharia mbili ambazo ni Umuundo na Semiotiki katika kuchanganulia mbinu anuwai za lugha. Mbinu hizi ni pamoja na tamathali za usemi na mbinu nyingine za lugha. Utafiti huu ulitufaa hususan katika vipengele vya lugha. Ingawaje tafiti hizi kwa jumla zinagusia vipengele ambavyo tumevishughulikia katika utafiti wetu, lakini zinatofautiana kwa vile kazi yetu ililenga riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule zinazozungumzia ugonjwa wa UKIMWI huku kazi ya Too (k.h.j) ikijikita katika tamthilia moja tu ya *Nguzo Mama*. Aidha Too (k.h.j) alitumia nadharia mbili ilhali katika utafiti wetu tuliongozwa na nadharia moja.

Lugwiri (2011) amechanganua tamathali za usemi zilizotumika katika *Utenzi wa Tambuka*. Katika utafiti huu, Lugwiri (k.h.j) ametumia Nadharia ya Kimtindo na anabainisha wazi namna vipengele vya tamathali za usemi vilivyobainika katika utenzi husika. Anabainisha kwamba tamathali za usemi ni mihimili mikuu ya maudhui na dhamira. Utafiti huu ulikaribiana na wetu ingawa tofauti ni kwamba wetu ulihakiki lugha ya kitamathali katika riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule kuhusu ugonjwa wa UKIMWI ilhali utafiti wa Lugwiri (k.h.j) ukijikita katika *Utenzi wa Tambuka* tu ambao ni ushairi.

Kinara (2012) ametafiti kuhusu maudhui ya UKIMWI katika riwaya za Kiswahili. Ameonyesha baadhi ya semi zinazotumiwa kuurejelea UKIMWI na kufafanua athari za maradhi ya UKIMWI kwa wahusika. Utafiti huu umejenga utafiti wetu kwa maana umeonyesha namna ambavyo riwaya mbili zilizotumiwa zinavyopendekeza kuhusu jinsi ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Ingawa hivyo utafiti huu unatofautiana na wetu. Kinara (k.h.j) ameongozwa na nadharia mbili na kuhakiki riwaya mbili tofauti na utafiti wetu ambao umeongozwa na nadharia moja na kuhakiki maandishi



kadhaa ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Aidha utafiti wetu umehakiki maandishi kadhaa katika tanzu tatu za fasihi andishi ilhali uhakiki wa Kinara (k.h.j) umejikita tu katika riwaya. Hivyo basi tafiti hizi mbili zimetofautiana pakubwa katika upeo.

Musumba (2012) aliangazia mtindo unavyojitokeza katika riwaya ya *Watu wa Gehama* ambapo alichambua vipengele mahsusi vya kimtindo vinavyodhihirika katika riwaya hii na kutoa maelezo ya jinsi vilivyoathiri muundo wake na vinavyochangia uwasilishaji wa ujumbe. Vipengele hivyo viliupatia utafiti wetu mwanga wa kutosha kuhusiana na suala tunalolichunguza. Matokeo ya utafiti huu yametufaa sana katika kuchambua vipengele vya tamathali za usemi tulivyoshughulikia. Ingawa hivyo, upeo wa kazi ya Musumba (k.h.j) unatofautiana na wa kazi yetu kwa kuwa alichambua riwaya moja ilhali sisi tulichambua maandishi ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule kuhusu ugonjwa wa UKIMWI.

Nyandiba (2013) alichanganua mikakati ya kiisimu ya mawasiliano katika diskosi za VVU/UKIMWI miongoni mwa Abagusii. Utafiti wake ulifafanua kwa kina mikakati mbalimbali ya kiisimu inayotumiwa na washauri katika mawasiliano kuhusu UKIMWI. Aidha, alifafanua mafumbo yanayotumiwa katika kujadili ngono, sehemu za siri, kondomu na dhana za VVU/UKIMWI. Utafiti wa Nyandiba (k.h.j) ulijenga utafiti wetu kwa vile pia ulitafiti kuhusu mawasiliano kuhusiana na UKIMWI. Ingawa hivyo, utafiti wa Nyandiba (k.h.j) unatofautiana na wetu ambao ulihakiki mitindo iliyotumiwa na waandishi tofauti kuwasilisha suala la UKIMWI. Utafiti wa Nyandiba (k.h.j) ulichunguza lugha iliyotumiwa na washauri wa UKIMWI ilhali utafiti wetu ulihakiki mitindo iliyotumiwa na waandishi tofauti wa fasihi andishi katika kuwasilisha dhamira za UKIMWI katika maandishi teule.

Karanja (2014) ni mtafiti aliyeshughulika na namna sitiari, tashibihi na taashira katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* zilivyotumiwa kuwasilisha dhamira. Karanja ametumia Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo kuonyesha namna tamathali hizi za usemi zilivyotumiwa na mwandishi kufikisha dhamira kwa hadhira yake teule. Nadharia hii ilimwezesha kuhakiki viashiria vilivyotumiwa kuunda tamathali za usemi; sitiari, taashira na tashibihi katika *Sauti ya Dhiki* na kuvipa maana viashiria hivi. Utafiti huu unafanana na wetu kwa vile sawa na utafiti wetu unaonyesha namna ambavyo tamathali za usemi zimetumiwa na mwandishi kufanikisha dhamira. Aidha, sawa na utafiti wetu, umeongozwa na Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo. Tofauti ni kuwa utafiti wa Karanja unahusu diwani moja inayoshughulikia ushairi ilhali utafiti wetu umehakiki maandishi ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule yanayozungumzia ugonjwa wa UKIMWI.

Rotich (2018) ametafiti kuhusu simulizi za virusi vya UKIMWI zinavyodhihirika katika nyimbo za jamii za Kenya kibaadausasa. Utafiti wake ulibainisha na kujadili baadhi ya mikakati ya kibaadausasa iliyotumiwa katika nyimbo zilizoteuliwa na kuchanganuliwa. Aidha, ulifafanua jinsi simulizi ndogondogo zinazohusu VVU/UKIMWI zinavyojitokeza katika nyimbo zilizoteuliwa na kuchanganuliwa. Utafiti wa Rotich unakaribiana na wetu kwa maana yeye ameangalia namna ambavyo nyimbo zimetumika kukabiliana na UKIMWI sawa na utafiti wetu ambapo tumeangalia namna ambavyo maandishi teule yaliyotumika kwenye utafiti yametumika katika kupambana na ugonjwa wa UKIMWI. Hata hivyo utafiti wa Rotich unatofautiana na wetu kwa maana yeye ameangalia nyimbo za jamii za Kenya ilhali utafiti wetu umeangalia maandishi kutoka tanzu tatu za fasihi andishi ambazo ni: riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Watunzi wa nyimbo alizozitumia walitoka nchini Kenya tu ilhali baadhi ya waandishi wa kazi tulizozitumia katika utafiti wetu walitoka

Tanzania. Baada ya kuangalia tafiti zilizofanywa na watafiti tangulizi, tumefafanua nadharia iliyouongoza utafiti wetu katika sehemu inayofuata.

## **2.5 Msingi wa Kinadharia**

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo. Kulingana na malengo ya utafiti huu, Nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo inaonekana kuwa ya kufaa zaidi kutuongoza katika kuchunguza na kuchambua data. Nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo iliasisiwa na Buffon (1930). Kulingana na Buffon, mtindo ni mtu mwenyewe. Hii ina maana ya upekee wa mtu katika matumizi yake ya lugha ili kuwasilisha ujumbe wake. Miongoni mwa waasisi muhimu wa nadharia hii ni Coombes (1953). Akinukuliwa na Wambua (2001) anasema:

Mhakiki ni lazima azingatie vipengele vinavyofanya kazi fulani ili iwe ya kuvutia. Nia ya mtindo ni kuchunguza lugha na kaida zake kwa nia ya kutambua mbinu zilizotengwa kwa kazi fulani ya kijamii, kufafanua sababu ya vipengele fulani kutumiwa na vingine kuachwa.

Tukizingatia maelezo yaliyotolewa kwenye dondoo lililonukuliwa, ni wazi kuwa Nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo hujishughulisha na namna msanii alivyotumia lugha katika kuwasilisha ujumbe wake. Nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo ilimuelekeza mtafiti kuupata kwa wepesi ujumbe uliowasilishwa na waandishi mbalimbali wa kazi zilizotumiwa kwenye utafiti huu. Madai haya yanaungwa mkono na wataalamu kadhaa katika fasihi wakiwemo: Senkoro (1982), Mosha (2002) na Wamitila (2013). Wataalamu hawa wanakubali kuwa maana ya kazi ya fasihi hujikita katika mtindo alioutumia mwandishi katika matini husika.

Kihistoria, taaluma ya uchambuzi wa mitindo ilianza katika kipindi cha karne ya tano huko Ugiriki na Urumi kabla ya kuzaliwa kwa Masihi. Katika kipindi hiki, balagha au elimu ya usemaji inayohusu ufasaha wa kusema ilikuwa maarufu sana. Taaluma hii ilijumuisha seti za kanuni na mbinu zilizowawezesha walumbi na wahutubu

kuzungumza kwa ufasaha kwa kutumia lugha iliyopambwa kwa tamathali za usemi na taswira kwa lengo la kuleta mabadiliko katika maoni na fikra za hadhira.

Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo katika uchambuzi wa matini iliweka msisitizo wake katika nafasi ya ujumi wa lugha katika kazi za fasihi. Kwa maneno mengine, lugha ya fasihi iliangaliwa kuwa ilitumia ujumi katika kueneza fikra au ujumbe. Ujumi huu ulidhihirishwa katika matumizi ya lugha kisanaa kwa lengo la kuumba wazo na kulisambaza kwa hadhira kwa namna ivutiayo kupitia upeo wa matumizi ya lugha ya kawaida.

Kwa hiyo, wachambuzi wa kazi za fasihi waliofuata mwelekeo wa Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo katika uchambuzi wa matini walielekeza jitihada zao za kifasihi katika vipengele kama vile aina ya lugha iliyotumika kulipamba au kulirembesha jambo fulani kama lilivyowasilishwa katika kazi ya fasihi inayohusika. Umuhimu ulielekezwa katika uteuzi na upangaji wa kisanaa wa maneno katika kazi ya fasihi, huu ni uendelezaji na ukuzaji wa imani kuwa matumizi maalum ya lugha ni vazi la wazo au fikra.

Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo huhusisha maelezo ya kiisimu ili kuweza kufafanua dhana zake za msingi katika fasihi. Leech (1969) anaeleza kwamba uhakiki wa mtindo huhusu uchanganuzi wa vipengele vya fasihi na pia vya isimu. Kwa maoni yake, hakuna kipengele mojawapo kati ya fasihi na isimu ambacho kinaweza kusimama pweke na kujifafanua kikamilifu. Hii ni ishara kwamba Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo hutumia maelezo ya isimu na fasihi katika kufafanua matini mbalimbali. Hii ina maana kuwa kila tunapohakiki mtindo katika mkabala wa kifasihi hatuwezi kupuuza matumizi ya vipengele vya kiisimu pia. Nadharia hii basi hujihusisha na uchunguzi wa kinachosemwa (ujumbe) na kinavyosemwa (mtindo).

Indangalasi (1988) anaunga mkono maelezo ya Leech (k.h.j) anaposema kuwa nadharia hii hujihusisha na jinsi lugha inavyotumika kuleta mvuto kisanaa. Mhimili huu ulitufaa katika kuchanganua mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI kwenye kazi teule za fasihi andishi. Leech (k.h.j) anaeleza kuwa lengo la Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo ni kuchunguza lugha na kanuni zake ili kubainisha mbinu zilizotengewa kazi fulani ya kijamii. Leech anaonekana kusesitiza kuwa Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo hudhamiria kufanikisha uchunguzi wa kina wa matumizi ya lugha katika fasihi.

Mihimili ya nadharia hii inahusisha yafuatayo; kwanza, mtindo wa kazi ya fasihi ndio hutumiwa na msanii kuwasilisha ujumbe wake. Mhimili huu ulitumiwa kufafanulia mitindo ya uandishi katika kazi teule za fasihi andishi. Pili, upo uwiano baina ya ujumbe na lugha katika kazi ya kifasihi na vipengele hivi viwili haviwezi kutenganishwa.

Tatu, lugha ndicho chombo tekelezi kinachosaidia kueleweka kwa ujumbe uliodhamiriwa na mwandishi. Maoni haya yanaungwa mkono na Tunner (1973) anaposema kuwa uteuzi wa maneno si huru na msanii hulazimika kuwa makini ili kazi yake ikubalike na walengwa au hadhira yake. Mihimili hii ilitusaidia kuangalia namna vipengele vya mtindo vinavyosaidia na kuathiri uelewaji wa dhamira.

Nne, mwandishi hutumia lugha kiufundi na athari za ujumi haziwezi kutenganishwa na matumizi ya kisanaa katika kazi yake. Maoni haya yanaungwa mkono na Simpson (2004) anayedai kuwa Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo husisitiza wazo kuwa kila kazi ya fasihi ina ubunifu fulani ambao ukichanganuliwa kwa undani husaidia uelewekaji wa undani wa matini za fasihi. Pamoja na maoni haya ni yale ya Champman (1982) anayeelekea kuafikiana na Leech (k.h.j) anapodai kuwa fasihi

haiwezi kujadiliwa pasipo kuzingatia kwamba ina matumizi maalum ya lugha. Mhimili huu ulituwezesha kuchanganua tamathali za usemi zilizotumika katika kazi teule za fasihi andishi.

Mtafiti aliteua nadharia hii kutokana na mhimili wa mawazo wa kumuongoza kuchambua vipengele mbalimbali vya lugha na hatimaye kumwezesha kuibua dhima mbalimbali za kimtindo katika maandishi teule ya fasihi andishi. Nadharia hii aidha ilitumiwa kwa kuzingatia kwamba kila mtunzi wa kazi za fasihi huwa na upekee wake unaoweza kumtofautisha na watunzi wengine hata kama wataandika utanzu mmoja na katika kipindi kimoja. Nadharia hii ilifaa kubainisha upekee wa kimtindo baina ya watunzi wa kazi zilizoshughulikiwa katika utafiti huu.

Agu (2008) anasema kwamba uchunguzi wa kimtindo unajumlisha uchunguzi wa sintaksia, uteuzi wa maneno, nahau, taswira na mengineyo. Anaeleza kuwa kiwango cha kisintaksia kinahusisha miundo ya sentensi, uteuzi wa maneno na jinsi msanii anavyoyapanga ili kufanikisha malengo ya kisanii. Uhakiki wa kimtindo pia unahusisha matumizi ya tamathali za usemi. Kulingana na Agu, lugha ya aina hii hutumiwa ili kuipa kazi iliyoandikwa uzuri, kuweza kutumia maneno machache ipasavyo na kupata uzito wa maudhui. Maelezo ya wananadharia hawa yanafaa katika kutupa mwelekeo ili kuweza kuchanganua mtindo katika maandishi teule ya fasihi andishi.

Leech na Short (1981) wameainisha viwango vya kushughulikiwa katika mtazamo wa kifasihi na ambao mtafiti ameegemea katika utafiti huu. Kwanza ni kiwango cha kileksia ambapo aina mbalimbali za maneno huchunguzwa. Maneno yanayochunguzwa ni pamoja na; nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi na kadhalika. Pili, kiwango cha kisarufi ambapo aina za sentensi, uchangamano wa sentensi, na aina

za virai hushughulikiwa. Tatu, ni kiwango cha kisemantiki ambapo tamathali za usemi kama vile jazanda, tashbihi, tashhisi na kadhalika hushughulikiwa. Nne, ni mshikamano na mwingiliano wa kimuktadha ambapo dhana za kimtindo huchunguzwa katika mwingiliano wao. Mtafiti alihusisha kiwango cha pili, tatu na nne katika utafiti huu. Kiwango cha pili na cha tatu vilimsaidia mtafiti kuhakiki mbinu za usimulizi na vilevile kuonyesha mchango wa tamathali za usemi kwenye ufahamu wa ujumbe katika maandishi teule ya fasihi andishi. Kiwango cha nne kilimwongoza mtafiti kuchunguza jinsi vipengele mbalimbali vya mtindo vinavyoingiliana ili kujenga mtindo katika maandishi ya fasihi andishi yaliyoteuliwa.

Wamitila (2008) akiunga mkono maelezo ya Leech na Short (k.h.j) anafafanua vipengele vya kimsingi ambavyo huchunguzwa katika kazi ya fasihi kwa mwelekeo wa Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo. Vipengele alivyotaja ni: tamathali za usemi, uteuzi wa sarufi, muwala, mshikamano, mazungumzo na mbinu za uwasilishaji wa mawazo huku akivihusisha vyote na mtindo. Vipengele vilivyofaidi utafiti huu ni: tamathali za usemi, sarufi na mbinu za uwasilishaji usemi.

Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Leech (1969), mihimili ya nadharia hii ilitusaidia kuchunguza mtindo na uwasilishaji wa dhamira za UKIMWI katika maandishi teule ya fasihi andishi na kufikia malengo ya utafiti huu ambayo ni: Kuchanganua mitindo tofauti ya uwasilishi ilivyotumika kuibua suala la UKIMWI katika kazi teule za fasihi andishi, kujadili dhamira mbalimbali zinazowasilishwa kwenye kazi teule za fasihi andishi kuhusu UKIMWI na kufafanua dhima ya mtindo katika uwasilishaji wa dhamira na kutathmini mchango wa kazi teule za fasihi andishi katika kukabiliana na janga la UKIMWI.

Kwa ujumla, utafiti huu ulitumia vipengele vilivyofafanuliwa na wanamitindo waliotajwa kwa kuwa wametoa mchango ulioimarisha uelewaji wa nadharia ya utafiti huu. Vipengele hivyo viliuwekea utafiti msingi madhubuti na kuupa mwelekeo uliozingatiwa katika kuafikia azma kuu ya utafiti huu.

Kwa muhtasari, Nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo hutumiwa kurejelea mkabala wa uchanganuzi wa matini za kifasihi kwa kuchunguza mtindo kwa njia ya kisayansi, yenye nidhamu na taratibu za kitaaluma; na huweza kuelezwa kama nadharia iliyo katikati ya isimu na fasihi. Kimsingi, nadharia hii ina mwelekeo wa kifani na inadhamiriwa kuchunguza mtindo wa kinachosemwa (maudhui) na jinsi kinavyosemwa (fani). Nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo ilimwezesha mtafiti kuchanganua data iliyodondolewa kwenye maandishi teule yaliyotumika kwenye utafiti.

## **2.6 Hitimisho**

Sura hii imeangalia mapitio ya maandishi kwa kuhakiki yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Maandishi yaliyopitiwa yalikusiana na suala kuu la utafiti ambalo ni “uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika kazi teule za fasihi: Kielelezo cha tanzu za fasihi andishi.” Nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo ambayo imesheheni mihimili inayochukuana vyema na suala la utafiti ilishughulikiwa kwa kina. Aidha, katika uhakiki huo tumeangalia dhana ya mtindo katika kazi za fasihi, matumizi ya lugha na tamathali za usemi pamoja na kueleza dhana ya dhamira katika kazi za fasihi. Sura inayofuata imezungumzia mbinu zilizotumika katika utafiti huu.



## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.0 Utangulizi**

Sura iliyotangulia iliangalia mapitio ya maandishi, kuhakiki yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti na kuelezea kuhusu nadharia iliyoongoza utafiti. Katika utafiti huu, kuna suala na malengo ya utafiti yanayofaa kushughulikiwa kupitia kwa ukusanyaji wa data, uchambuzi na uandishi wa matokeo ya utafiti. Sura hii imeshughulikia mbinu za utafiti, muundo wa utafiti, eneo la utafiti na uteuzi wa sampuli. Aidha, imewasilisha mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa katika utafiti. Sehemu inayofuata inajadili mbinu hizo za utafiti.

#### **3.1 Mbinu za Utafiti**

Utafiti huu umezingatia mbinu mbalimbali ambazo zimeteuliwa na mtafiti ili kumwezesha kukusanya data. Kothari (2008) anaeleza kwamba mbinu za utafiti ni uti wa mgongo wa utafiti wa kitaaluma. Kwa kuzingatia wazo hilo, sura hii imewasilisha mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti. Mbinu ya maktabani ilitumika ili kupata data kulingana na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule. Mbali na maandishi teule yaliyotumika, maandishi mengine ya fasihi yalisomwa ili kumuongoza mtafiti katika kuiweka kazi ya utafiti katika mkabala unaofaa.

#### **3.2 Muundo wa Utafiti**

Muundo wa utafiti ni ramani inayochorwa kuonyesha sura nzima ya utafiti inavyopaswa kuanzia ukusanyaji wa data mpaka uandishi wa tasnifu nzima (Kothari, 2008; Babbie, 1999; Yin, 1994). Kuna aina mbalimbali za miundo ya utafiti na katika utafiti huu tumeongozwa na ule wa uchunguzi kifani. Uchunguzi kifani ni aina ya muundo wa utafiti, ambao humpa mtafiti uhuru wa kuteua jambo moja mahususi

ambalo atalichunguza kwa undani na kulitolea mahitimisho mwafaka (Robson, 2007; Creswell, 2009). Uchunguzi kifani ni umbo la utafiti ambapo mtafiti huteua eneo au kitu maalum ambacho kitashughulikiwa na kuwezesha kupatikana kwa data za utafiti zilizokusudiwa.

Good (1966) anaeleza kwamba, uchunguzi kifani ni mbinu nzuri ya utafiti kwa sababu ni ya uhakika kwani inamwezesha mtafiti kupata taarifa muhimu na sahihi kwa kutumia muda na gharama ndogo ikilinganishwa na mbinu nyingine. Aidha, uchunguzi kifani humwezesha mtafiti kuuelewa muktadha mzima wa jambo analolitafiti na hivyo kuwa rahisi kwake kukamilisha malengo ya utafiti wake. Kothari (2009) anasema kwamba mbinu ya uchunguzi kifani humsaidia mtafiti kujibu maswali kama vile nini? kwa nini? kwa sababu gani? kwa namna gani? Utafiti huu wa uchunguzi kifani ulitufaa kwa vile ulituwezesha kuhakiki kwa kina maandishi yote yaliyoteuliwa yanayozungumzia suala la UKIMWI.

Katika utafiti huu maandishi teule ya fasihi andishi kuhusu UKIMWI ndiyo msingi wa uchunguzi kifani kwa maana maandishi hayo ni sehemu ndogo ya kazi nyingi za fasihi andishi ambazo zimeandikwa. Creswell (2009) anaeleza kwamba, uchunguzi kifani ni mbinu nzuri ya kumwelekeza mtafiti kukusanya na kupata data anazohitaji kwenye utafiti wake.

Katika utafiti huu, vitabu vilivyoteuliwa vimewasilisha ujumbe wake vikitumia mitindo tofauti ya uandishi. Baada ya kusoma vitabu teule, nilidondoa vifungu mahsusni kwa kuvirekodi kwenye shajara maalum. Hatimaye, niliichanganua data kwa kubainisha namna matumizi ya lugha na tamathali za usemi zinavyojitokeza na zinavyotumika kuibua dhamira katika maandishi teule. Aidha, niliifafanua dhima ya

mtindo katika uwasilishi wa dhamira na kutathmini mchango wa maandishi kwenye tanzu teule za fasihi andishi katika kukabiliana na janga la UKIMWI nchini Kenya.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika maktaba. Mtafiti alipitia maandishi mbalimbali yakiwemo majarida, vitabu, makala na mitandao ya mawasiliano ili kupata maelezo muhimu kuhusiana na mada ya utafiti. Isitoshe, mtafiti alichanganua vitabu vifuatavyo kwa kina ili kupata data faafu ya utafiti huu: Mkufya (2005), *Ua la Faraja*, Omar (2007), *Kala Tufaha*, Matundura (2008), *Sitaki Iwe Siri*, Momanyi, *Pendo katika Shari*, Jalala (2004), *Giza*, Reynolds (2006), *Orodha*, Medical Aid Foundation. (2010), *Kilio Chetu*, Iribemwangi (2007), *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, Kitula na Kobia (2007), *Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine* na Mohamed na Walibora (2010), *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine*. Aidha, tulirejelea makala na maandishi mbalimbali kuhusiana na Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo tuliyozingatia kutuongoza katika utafiti huu.

Tumerejelea pia makala na tasnifu anuwai zilizoandikwa kuhusu Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo katika kazi za fasihi. Pamoja na hayo, tumekita utafiti huu kwenye mitandao ya kiakademia ili kupata yaliyoandikwa kuhusiana na mada ya utafiti na nadharia iliyotuongoza katika utafiti huu. Katika utafiti huu wa maktabani, maelezo ya ziada yalipatikana katika vitabu, makala, majarida, tasnifu, tovuti na wavuti. Young (1984) anaeleza upataji wa data iliyoandikwa kama mbinu ya kukusanyia data mezani bila kuwatafuta watafitiwa na kuwahoji ama kuwasaili. Data hii hukusanywa kutoka kwa machapisho ambayo yanahusiana na mada ya utafiti husika.

### 3.4 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli katika utafiti huu ni wa kimakusudi. Kazi teule za fasihi andishi ya Kiswahili zimeteuliwa kwa vile kutokana na uchunguzi wa awali alioufanya mtafiti, zimeshughulikia suala la UKIMWI kwa kiwango kikubwa. Katika utafiti wowote ule, pana haja ya kuiteua sampuli ya kutumika ya kumwezesha mtafiti kuzua data ya kutumika. Babbie (1999) anaeleza sampuli kuwa kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka kundi kubwa la watafitiwa linalotoa data za kuwakilisha kundi zima. Mtafiti alizingatia maoni haya katika uteuzi wa sampuli.

Mtafiti aliteua riwaya nne, tamthilia tatu na diwani tatu za hadithi fupi. Kazi zenyewe ni: Mkufya (2005), *Ua la Faraja*, Omar (2007), *Kala Tufaha*, Matundura (2008), *Sitaki Iwe Siri*, Momanyi (2008), *Pendo katika Shari*, Jalala (2004), *Giza*, Reynolds (2006), *Orodha*, Medical Aid Foundation (2010), *Kilio Chetu*, Iribemwangi (2007), *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, Walibora na Mohamed (2010), *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine* na King'ei na Kobia (2007) (Wahariri), *Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine*. Mihimili ya Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo iliongoza mtafiti kupata data inayohusiana na malengo ya utafiti. Uteuzi wa sampuli kimaksudi ulifaa utafiti huu katika kuonyesha namna waandishi katika tanzu tofauti za fasihi andishi ya Kiswahili walivyowasilisha suala la UKIMWI.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Katika utafiti huu, data ilikusanywa kutoka riwaya nne, tamthilia tatu na hadithi fupi sita kutoka kwa diwani tatu za hadithi fupi. Mtafiti alivisoma vitabu hivi kwa kina kisha akatenga na kuandika hoja zote muhimu kuhusiana na utafiti huu katika daftari maalum la kukusanyia data kwa ajili ya kufanyiwa uchambuzi. Kimsingi, mtafiti alitumia mbinu ya uchanganuzi wa matini katika ukusanyaji wa data.

### 3.6 Uchambuzi wa Data

Uchanganuzi wa matini ni mbinu ambayo inampa mtafiti fursa ya kusoma maandishi husika kwa utulivu, umakini na uzingativu kisha akaweza kubaini data ambazo zinasaidia kujibu maswali ya utafiti wake kama anavyosema Leininger (1985). Katika uchanganuzi, mtafiti alipopata kifungu kilichohusiana na mada ya utafiti alikiandika katika shajara maalumu na kisha kuendelea tena kusoma kazi nyingine. Kwa kufanya hivyo, mtafiti aliweza kudondoa na kunukuu vifungu mbalimbali kwa ajili ya kuvitumia baadaye katika uchambuzi wa data.

Katika sura za uchanganuzi wa data kwenye utafiti huu, yapo madondoo kadhaa ambayo yametumiwa na mtafiti katika kujenga ama kushadidia hoja fulani kwa minajili ya kuyaafiki malengo ya utafiti. Madondoo hayo yalikusanywa katika kipindi cha ukusanyaji wa data. Kothari (2008) anaeleza kwamba mbinu ya uchanganuzi wa matini ni nzuri na haipotezi muda katika ukusanyaji wa data. Mbinu hii ni faafu kwenye utafiti hususan mtafiti anapomakinika na kusoma maandishi husika kwa vile huwa rahisi kumpatia data mwafaka kwa minajili ya utafiti wake.

Taylor na Bogdan (1984) na Bogdan na Biklen (1992) wanaeleza kwamba uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itamwezesha mtafiti kujibu maswali ya utafiti. Jambo hili limeweza kufanyika kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini. Mbinu hii humruhusu mtafiti kusoma kazi za fasihi andishi kwa minajili ya kuelewa maudhui, falsafa, mtazamo, fani na dhamira. Baada ya kusoma kazi husika na kufahamu yaliyomo, mtafiti hutumia njia ya maelezo katika kuzichambua data hizo na kuzifanya rahisi kueleweka kwa msomaji. Uchambuzi wa data za utafiti huu ulifanywa kwa namna ifuatayo: Hatua ya kwanza ilikuwa ni kupanga data iliyokusanywa kulingana na malengo mahsusuni ya utafiti.

Hatua ya pili ikawa ni kuunda mada kuu na mada ndogondogo kwa kila lengo mahususi la utafiti. Lengo kuu la kuunda mada kuu na ndogondogo lilikuwa ni kurahisisha kazi ya uchambuzi wa data. Uundwaji wa mada hizo pia ulimwongoza mtafiti katika kuzingatia mambo ya msingi ya kuchambua bila kupoteza muda kuchambua mambo yasiyohitajika. Hatua ya tatu ilikuwa ni kuchambua data kwa kuzidondoa na kuzitolea maelezo yanayohusiana na mada ya utafiti. Uchambuzi ulianza kwa kudondoa vifungu kutoka katika kazi teule za fasihi andishi ya Kiswahili na kuvitolea ufafanuzi kimaelezo.

### **3.7 Uwasilishaji wa Data**

Katika utafiti huu, data iliyokusanywa imewasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo haya yalizingatia; mitindo tofauti ya uwasilishi wa UKIMWI, dhamira kwenye kazi teule za fasihi kuhusu UKIMWI, dhima ya mtindo katika uwasilishi wa dhamira na mchango wa kazi za fasihi andishi katika kukabiliana na janga la UKIMWI. Uwasilishaji wa data ulifanywa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia teule iliyouongoza utafiti.

### **3.8 Masuala ya Etikeli**

Katika kazi hii, mtafiti alijikita katika matini teule za kubuni kulingana na malengo ya utafiti. Kazi teule zilizotumika katika utafiti huu zimejadiliwa kama zilizojitenga na waandishi husika. Aidha wahusika waliotumiwa katika kazi hii ni wa kubuni na hivyo mtafiti hakutumia majina halisi ya watu wanaofahamika katika jamii ambao wameathirika na ugonjwa wa UKIMWI. Maadili au itikeli ni neno pana linalorejelea kuheshimu taratibu, miiko, mila na desturi zinazoongoza maisha au shughuli fulani katika jamii kama anavyosema Kumar (1999). Utafiti kama yalivyo mambo mbalimbali katika jamii una miiko yake ambayo inapaswa kuzingatiwa. Utafiti huu

umefanywa kwa kuzingatia miiko yote ya utafiti. Madondoo yote yanayojitokeza katika utafiti huu yamefanywa kwa usahihi na yote yamedondolewa katika kazi zilizoteuliwa na si vinginevyo.

### **3.9 Hitimisho**

Sura hii imewasilisha mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti zilizosaidia kuyashughulikia malengo ya utafiti na kuwezesha kukamilika kwa suala kuu la utafiti. Mbinu zilizoshughulikiwa ni pamoja na; ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa matini, uchambuzi wa data na uwasilishaji wa data. Sura inayofuata inachambua na kuwasilisha data iliyokusanywa kuhusiana na malengo mahsusi ya utafiti huu.

## SURA YA NNE

### MITINDO YA KUWASILISHA DHAMIRA ZA UKIMWI

#### 4.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imezungumzia mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Sura hii imewasilisha data iliyodondolewa na kuchanganuliwa. Uchanganuzi na uwasilishi wa data katika sehemu hii uliongozwa na lengo la kwanza la utafiti huu ambalo ni: kuchanganua namna mitindo tofautitofauti ya uwasilishi imetumika kuibua suala la UKIMWI katika kazi teule za fasihi andishi. Baadhi ya kazi zilizotumika ni; *Ua la Faraja* (Mkufya, 2005), *Pendo katika Shari* (Matundura, 2008), *Giza* (Jalala, 2004), na *Kala Tufaha* (Omar, 2007) miongoni mwa nyingine. Katika sura hii, tumebainisha na kuchanganua mbinu za lugha na tamathali za usemi kama vile: tashibih, taswira, methali, sitiari, kuchanganya ndimi na nyingine zilizotumiwa na waandishi wa riwaya, tamthilia na hadithi fupi teule kuibua suala la UKIMWI. Sehemu inayofuata inawasilisha uchanganuzi huo.

#### 4.1 Matumizi ya Mbinu za Lugha na Tamathali za Usemi

Lugha hutumika katika kazi yoyote ya fasihi kubeba dhamira, migogoro na ujumbe tofauti kulingana na azma ya mtunzi wa kazi husika. Kipengele cha lugha ni muhimu sana kwani ndicho kinachotofautisha fasihi na sanaa nyingine kama vile uchoraji au uchongaji. Senkoro (2011) anasema kwamba tunapoangalia matumizi ya lugha tunazingatia vipengele vifuatavyo: Misemo, methali, tamathali za semi na lugha za wahusika hasa lahaja zao. Maoni yanayokaribiana na haya lakini yanayotofautiana kwa kiwango fulani yanatolewa na Wamitila (2008) anayesema kuwa, zipo mbinu nyingine ambazo ni muhimu katika uchanganuzi wa matumizi ya lugha ambazo si



tamathali za usemi. Kwa maoni yake, mbinu hizi ni pamoja na: takriri, kuchanganya na kuhamisha ndimi, tanakali za sauti, usambamba na maswali ya balagha.

Tamathali za usemi pamoja na uainishaji wake ni dhana iliyoshughulikiwa na wataalam mbalimbali. Wataalamu maarufu waliushughulikia uainishaji wake ni pamoja na Holman (1960), Kuhenga (1977), Mbatiah (2001) na Senkoro (2011). Wataalam hawa wote wanakubaliana kuwa tamathali za usemi ni ukiushi wa kimaksudi katika lugha ya kawaida katika fasihi. Hii ina maana kuwa waandishi wa fasihi huchukua lugha ya kawaida na kuifinyanga upya ili kuzalisha maumbo mapya katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii.

Katika sehemu hii, tumechunguza kwa kina baadhi ya mbinu za lugha na tamathali za usemi na kisha kuonyesha zilivyotumiwa na wasanii wa maandishi teule ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi kuwasilisha ujumbe kuhusu UKIMWI. Kulingana na utafiti huu, tumebaini na kujadili baadhi ya mbinu za lugha na tamathali za usemi zinazojitokeza katika riwaya teule zilizotumiwa.

Katika utafiti huu, tumezifadili mbinu za lugha na tamathali za usemi kwa pamoja kwa maana kuna mwingiliano mkubwa sana baina yake. Mbinu zilizotumiwa na wasanii katika riwaya teule ni kama zilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo la 4:1.

**Jedwali la 4.1: Mdafao wa utokeaji wa mbinu za lugha na tamathali za usemi katika riwaya teule.**

Na.	Mbinu za Lugha na Tamathali za Usemi	Ua la Faraja	Kala Tufaha	Pendo katika Shari	Sitaki Iwe Siri
1	Tashbihi	56	27	34	41
2	Kuchanganya ndimi	19	6	15	2
3	Methali	12	15	6	8
4	Taswira	14	11	0	6
5	Misemo/nahau	11	34	18	4
6	Mdokezo	09	08	10	0
7	Sitiari	22	02	0	0
8	Jazanda	0	03	0	0
9	Tashhisi	09	0	03	04
10	Balagha	7	6	0	0
11	Utohozi	10	0	0	0
12	Tasfida	08	0	0	0
13	Wimbo/ushairi	6	3	0	3
14	Mbinu rejeshi	4	4	0	0
15	Tanakali za sauti	2	5	0	0
16	Takriri	4	0	0	0
17	Tabaini	02	06	0	0
18	Kejeli	02	03	03	0
19	Barua	2	1	0	1
20	Lafudhi	1	0	1	0
	Jumla	200	134	90	69

**Chanzo: Data za Utafiti**

**4.1.1 Mjadala wa mbinu za lugha na tamathali za usemi**

Jedwali la 4:1 limetoa muhtasari wa mitindo ya lugha inayotumiwa na wasanii wa riwaya nne teule kujadili suala la UKIMWI. Inajitokeza wazi kutokana na utafiti huu kwamba waandishi wa riwaya za *Ua la Faraja* na *Kala Tufaha* wametumia mbinu nyingi zaidi ikilinganishwa na waandishi wa riwaya za *Pendo katika Shari* na *Sitaki Iwe Siri*. Mwandishi wa riwaya ya *Ua la Faraja* ametumia mbinu 200, wa *Kala Tufaha* akatumia mbinu 134, wa *Pendo katika Shari* akatumia mbinu 90 na wa *Sitaki Iwe Siri* akatumia mbinu 69. Kutokana na jedwali 4.1 wasanii wote wa kazi zilizoteuliwa katika utafiti huu, wametumia kwa kiwango kikubwa mbinu zifuatazo katika kuliibua suala la UKIMWI: Tashbihi, kuchanganya ndimi, methali, taswira, misemo, mdokezo na sitiari. Mbinu zingine zilizosalia kama vile jazanda, tashhisi,

balagha, utohozi na tasfida zilitumiwa na baadhi ya wasanii katika kuliwasilisha suala la UKIMWI. Katika sehemu inayofuata tutajadili baadhi ya mbinu zinazoelekea kutumiwa kwa kiwango kikubwa na wasanii katika kuliibua suala la UKIMWI. Mbinu ya kwanza tutakayoijadili ni tashbihi.

#### **4.1.2 Tashbihi**

Tashbihi ni kati ya tamathali za usemi ambazo hutumiwa na wasanii mbalimbali kuwasilisha ujumbe wao. Senkoro (1993) anaeleza kwamba tashbihi ni tamathali ya usemi inayotoa mfano wa vitu unaojengwa kwa kulinganisha vitu viwili au zaidi kwa kutumia maneno ya ulinganishi ambayo ni pamoja na: kama, mithili ya na kadhalika. Kahigi (1995) anatoa ufafanuzi kuwa tashbihi ni usemi wa kimlinganisho utumiao maneno yafuatayo ya ulinganisho; kama, mithili ya, kama vile, kana kwamba na mengine. Kwa upande wake, Senkoro (2011) anafasili tashbihi kuwa ni tamathali ya usemi ambapo watu wawili au vitu viwili au zaidi hulinganishwa na watu au vitu vingine kwa kutumia maneno kama vile; mithili ya, kama kwamba, mfano wa na mengine.

Ukichunguza fasili hizo utabaini kuwa wataalamu hao wanakubaliana kwa pamoja kuwa tashbihi hutumika kulinganisha vitu ama watu kwa kutumia maneno kama vile; mithili ya, kama vile, mithili ya, kama, mfano wa na kadhalika. Tashbihi ni tamathali ya usemi ambayo imetumiwa kwa kiwango cha juu sana ikilinganishwa na mbinu zingine katika kazi zote zilizotumiwa katika utafiti huu. Ni mbinu ambayo imetumiwa na waandishi wote wa riwaya teule zilizorejelewa katika utafiti huu.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, mwandishi ameitumia mbinu ya tashbihi pakubwa. Mfano mmoja unaotumiwa na mwandishi ni pale anaposema kuwa wanaume wote

walimtazama kwa shauku kama simba anavyokodolea pofu nyikani. Tamathali hii ya usemi imetumiwa katika muktadha ufuatao;

1. *Asha akapita. Kila aliyekumbwa na wimbi hilo la manukato hakuwezakujizuia kupandisha pumzi ili yamuingie sawasawa. Wanaume wote walimtazama kwa shauku kama simba anavyokodolea pofu nyikani. (Ua la Faraja, uk.10)*

Katika dondoo lililonukuliwa hapo juu, mwandishi analinganisha shauku ya wanaume na ile ya simba anavyotamani kumla pofu nyikani. Mwandishi anasema kuwa “*walimtazama kwa shauku kama simba anavyokodolea pofu nyikani.*” Kutokana na mavazi na maumbile yake, Asha aliwanasa wanaume waliokuwa pale. Msanii aidha anatueleza kwamba kila aliyekumbwa na wimbi hilo la manukato hakuweza kujizuia kupandisha pumzi yamuingie sawasawa. Hii ina maana kwamba mhusika Asha alikuwa anajipodoa sana kupita kiasi ili awanase wanaume. Alijipodoa hivyo kimaksudi ili awavutie na kuwanasa wanaume.

Manukato haya yaliwavutia sana wanaume na ndiyo sababu mwandishi anatueleza kuwa wengi wa wanaume walipandisha pumzi ili wayapate manukato hayo sawasawa. Asha aliwachochea wanaume kwa matembezi yake ambapo alikuwa akinengua viuno. Hali hii iliwafanya wanaume wantamani kwa shauku. Mwandishi anazidi kusema kuwa walimtazama kwa shauku kama simba anavyokodolea pofu nyikani. Asha alifanya hivyo maksudi ili kuwakoga wanaume waliokuwa pale. Asha alifahamu vyema saikolojia ya wanaume na alifanya hivi ili awanase wawe naye kwa uhusiano wa mapenzi. Asha ni kati ya wahusika ambao walitumia miili yao kama chambo cha kuwanasa wanaume wawapatie pesa. Mienendo kama hii ndiyo ilisababisha visa vya uasherati ambavyo vilichangia pakubwa katika kueneza ugonjwa wa UKIMWI katika maisha ya wahusika. Mienendo ya Asha iliwavutia wanaume wengi ambao walitamani kujihusisha naye kimapenzi.

Mwandishi wa riwaya ya **Ua la Faraja** pia ametumia tamathali ya usemi ya tashbihi pale anaposema kuwa; “tamaa ya mwili ilimjia na kumzoa kama wimbi kali la bahari na kuzidi kumsukuma kinyume cha matarajio yake.” Tamathali hii imetumika kama inavyoonyeshwa katika dondoo lifuatalo:

2. *Akamkabidhi lile shati. Omolo akalichukua na kwenda mpaka dirishani. Akalivaa. Alifungua mkanda wa suruali ili achomekee shati. Sasa alijisikia tamaa ya ajabu ya kufanya tendo, tendo alilolichukia na kulikataa. Alipojitahidi kuvaa nguo, ile tamaa ya mwili **ilimjia na kumzoa kama wimbi kali la bahari na kuzidi kumsukuma kinyume cha matarajio yake.** Queen alipomuona anahangaika, akacheka kicheko ambacho kilizidi kumsisimua Omolo (Ua la Faraja, uk. 52).*

Katika kifungu kilichodondolewa hapo juu, mhusika Queen alikuwa amemwalika Omolo kwake kwa matembezi. Kwa muda mrefu Queen alikuwa ametamani sana kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Omolo lakini Omolo hakuonyesha hisia zozote kwake. Msimamo wa kutotaka uhusiano wowote wa kimapenzi na Queen ulimfanya Queen atafute mbinu ambayo ingemasa Omolo.

Wakati wa matembezi ya Omolo, Queen alimfanyia ulaghai na kumwekea dawa ya kuisimua hisia zake kwenye kinywaji. Omolo alipokunywa tu kile kinywaji, hisia zake ziliamka na kupanda na akajihisi tofauti sana. Omolo alijisikia tamaa ya ajabu ya kufanya tendo alilolichukia na kulikataa. Mwandishi anatueleza kwamba, “**ile tamaa ya mwili ilimjia na kumzoa kama wimbi kali la bahari na kuzidi kumsukuma kinyume na matarajio yake.**” Omolo alilazimika kufanya kitendo cha ngono na Queen ndipo akatuliza hisia zake za ajabu. Ilibidi Omolo atende kitendo kilichokuwa kinyume cha dhamiri zake kwa sababu ya ujanja wa mhusika Queen.

Queen alikuwa mwanamke asherati na alitamani kwa muda mrefu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Omolo. Queen alifurahi sana wakati alipobaini kuwa mpango wake ulikuwa umefaulu. Tunaeleza kwamba Queen alipomuona Omolo anahangaika,

alicheka kicheko ambacho kilizidi kumsisimua Omolo. Mwandishi anapitisha ujumbe kwamba visa kama hivi ndivyo vilivyochangia pakubwa katika kueneza ugonjwa wa UKIMWI katika jamii. Mhusika Queen hatimaye aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Msanii anasema, **“sasa basi , hivi karibuni watu wamegundua kwamba ana dalili za ugonjwa wa UKIMWI”** (uk.126). Matendo yake ya uzinifu na wanaume tofautitofauti ndiyo yaliyochangia katika kufanya aathirike na ugonjwa wa UKIMWI.

Mfano mwingine wa tamathali ya tashbihi katika riwaya ya **Ua la Faraja** umetumiwa na mwandishi katika uwasilishaji wa dhamira pale ambapo anasema; **“mimi namuona kama shetani tu..”** Katika dondoo linalofuata, mfano huu unajitokeza vyema ambapo msanii anasema:

3. *Siyo kweli mjomba Omolo. Wewe hujui kiini cha yote. Mimi mwislamu, najua huo wajibu, na ni haki kwa Mzazi kusesitiza kwa watoto jambo la suala. Lakini siyo mzee Ngoma wa kuniambia hekima hiyo! Mimi namuona kama shetani tu... (Ua la Faraja, uk.119 -120).*

Katika dondoo lililo hapo juu, Omolo alikutana na Juma mtoto wa Ngoma wakizungumza kuhusu mabadiliko ya Ngoma ambaye sasa alikuwa ameuacha ulevi akiwaambia wanawe waende msikitini kuswali. Juma hakupokea kauli hii ya babake vyema akikumbuka mateso ambayo alikuwa amemfanyia mamake na ndio sababu anamlinganisha babake na shetani; yaani kitu kibaya cha kudhuru maisha ya mtu. Juma alikuwa mtoto wa Ngoma na alikuwa na chuki sana kwa babake Ngoma. Juma anasema, **“Mimi namuona kama shetani tu...”** matendo ya Ngoma yanafanya mwanawe amuone kama mtu mbaya sana. Ngoma aliipuuza na kuidharau jamii yake kwa muda mrefu. Alikataa kukidhi mahitaji ya jamii yake, jambo lililomsukuma mke wake kujiingiza katika biashara.

Kinaya kinajitokeza tunapofahamishwa kwamba Ngoma hakutaka hata mkewe kufanya hiyo biashara ndogo. Ngoma kwa muda mrefu sana alishiriki ulevi na kufanya uasherati na wanawake wengine nje ya ndoa yake. Haikuwa rahisi jamii ya Ngoma kukubali na kuamini kwamba alikuwa ameacha ulevi na anasa na kumrudia Mungu kwa vile kwa muda mrefu sana alishiriki ulevi na uasherati uliochangia kuenea kwa ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi anatueleza kuwa, **“siku ile aliposikia dhoruba ile ya habari kwamba kuna uwezekano kuwa baba amemwambukiza mama virusi vya UKIMWI, moyo wake ulipasuka kama bomu,” (uk.35).** Tabia ya Ngoma ilimfanya mwanawe Juma amchukie kupindukia. Juma alikiona kama kinaya kikubwa Ngoma kujifanya amebadilika na kumlazimisha mwanawe kwenda msikitini kuswali.

Katika riwaya ya **Kala Tufaha**, mwandishi pia ameshirikisha matumizi ya mbinu ya tashbihi. Mwandishi anatumia mbinu hii anaporejelea hali ya Kibibi alipotaka kujitoa uhai wake. Alikuwa amefukuzwa nyumbani na wazazi wake baada ya kugunduliwa kuwa alikuwa na ujauzito. Wazazi wake hawakutaka kuelezwa namna alivyopata ujauzito. Kibibi aliona maisha yalikuwa magumu kwake na hivyo akaamua kujitoa uhai. Mwandishi anasema;

4. *Mtoto wa watu alikaa kando ya barabara kwenye nyasi ili ashushe pumzi. Alitamani sana kuutua mzigo aliokuwa ameubeba lakini haikuyumkinika mara moja. Alikuwa mfano wa punda kihongwe mbeba mizigo aliyechoka kwenda; siku zote hudinda akahiari kufilia mbali kama kuendelea na safari (Kala Tufaha: uk. 5-6).*

Katika muktadha huu, mwandishi anayaangazia maisha ya Kibibi ambaye alikuwa amenajisiwa na Fumbwe kisha akampachika mimba. Kibibi alikuwa ametoroka kutoka kwa Fumbwe na alikuwa anajaribu kuavya mimba. Kibibi aidha alikuwa amefukuzwa na wazazi wake kutokana na mimba hiyo na ndipo akafanya uamuzi wa

kuiavya. Mimba aliyokuwa amebeba ndiyo inayolinganishwa na mzigo aliokuwa ameubeba.

Mwandishi anatumia kwamba Kibibi alitamani sana kuutua mzigo aliokuwa ameubeba lakini haikuyumkinika. Kibibi analinganishwa na punda kihongwe mbeba mzigo aliyechoka kwenda. Mtunzi anasema, *“alikuwa mfano wa punda kihongwe mbeba mizigo aliyechoka kwenda.”* Mwandishi anasema siku zote punda hudinda akahiari kufilia mbali kama kuendelea na safari. Katika kifungu hiki, Kibibi alikuwa amehiari kufilia mbali kwa kuiavya mimba. Maisha ya Kibibi yalikuwa kwenye njipanda kwa vile alijiona kama aliyechukiwa na kila mtu na akakosa hata upendo wa wazazi wake na ndiyo sababu alitamani kuutua mzigo aliubeba. Tabia ya uzinzi ya Fumbwe ndiyo iliyomletea ugonjwa wa UKIMWI hatimaye.

Mwandishi wa riwaya ya **Kala Tufaha** ametumia mifano zaidi ya tashbihi. Mfano mwingine aliotumia ni wakati ambapo Kibibi alikuwa amepania kwenda nje aende zake mbali na nyumba ya Fumbwe aliyolinganisha na jehanamu. Kibibi alikuwa amechoshwa na aina ya maisha aliyokuwa akiyaishi kwa Fumbwe. Mwandishi anasema:

5. *Si kupenda kwangu. Nimeghilibiwa na Shetani. Alisema Fumbwe katika hali ya kubembebeza. Kibibi hakutaka kusikia hili au lile. Alikuwa amepania kwenda zake nje; mbali na nyumba hiyo aliyoiona mithili ya jehanamu. Aliinuka na kuja alikokuwa Fumbwe. Akajibidiisha kumsukuma wala asiweze chochote (Kala Tufaha, uk. 68).*

Katika dondoo ambalo limenukuliwa, *“Alikuwa amepania kwenda zake nje; mbali na nyumba hiyo aliyoiona mithili ya jehanamu.”* Mwandishi anatumia kisa cha Fumbwe alipokuwa amemaliza kumtendea unyama Kibibi katika nyumba yake. Fumbwe alimnajisi Kibibi baada ya kumwekea dawa ya kumfanya alale kwenye



tufaha. Hili lilimwezesha Fumbwe atekeleze uhalifu wake pasipo kizuizi chochote. Matendo haya yalifanywa na Fumbwe alipobaki na Kibibi peke yake nyumbani baada ya mkewe kwenda mashambani. Fumbwe hasemi ukweli wakati anaposema kwamba haikuwa kupenda kwake na kuwa alighilibiwa na shetani. Hatuwezi kukubaliana na matamshi haya ya Fumbwe kwa maana alikuwa na mke aliyeishi naye. Hakuwa anaishi mbali na mke wake ndipo pengine useme kuwa alikuwa amemkosa na hivyo akaingiwa na hisia za mapenzi. Isitoshe, alifanya maksudi kitendo cha kumlaghai Kibibi kwa kumwekea dawa kwenye tufaha na hivyo hawezi akamsingizia shetani.

Kibibi alienenda kama aliyeshikwa na wazimu kwani hakuamini kwamba Fumbwe angefanya kitendo cha unyama kama hicho. Kitendo alichokifanya Fumbwe kilikuwa cha uhalifu, unyama na aibu kubwa kutoka kwa mtu wa cheo na hadhi yake katika jamii. Unyama uliofanyiwa Kibibi na Fumbwe ndio unaomfanya mwandishi amithilishe nyumba ya Fumbwe na jehanamu ambapo tunaamini mambo mabaya hufanyika. Kibibi alitamani kutoka katika jehanamu ya Fumbwe lakini mambo hayakuwa rahisi. Tabia ya uzunifu ya Fumbwe ilendelea hata ofisini kwake na hatimaye akaambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi wa riwaya ya **Kala Tufaha** aidha ametumia tashbihi pale ambapo Kibibi alikuwa ametembelea ofisi za utetezi wa haki za wanawake. Kibibi alikuwa na matumaini kuwa akitembelea afisi za kina mama watetezi, wangemsaidia katika kupigania haki yake. Katika tukio hili, Kibibi anapewa matumaini yaliyokosa mashiko. Mwandishi anasema;

6. *Usiwe na shaka. Alisema Bi Kidawa. Nitamwandikia huyo bwana barua kwanza. Atatubu kwa kukuchezea kama kikaragosi. Wajua wanaume wengi wanataka kuwachezea wasichana na hilo silikubali. Nipo hapa kutetea wanawake wenzangu (Kala Tufaha, uk. 99).*

Katika dondoo hili, baada ya Kibibi kutendewa unyama na Fumbwe, aliamua kuchukua hatua ili ulimwengu ujue madhila ambayo watoto wa kike huwa wanayapitia. Kibibi alitembelea afisi za watetezi wa kina mama ili kuwasilisha kesi yake. Ni katika muktadha huu ambapo mtetezi wa kina mama, Bi Kidawa akamuelezea Kibibi hatua ambayo angeichukua. Bi Kidawa alisema, “*Atatubu kwa kukuchezea kama kikaragosi.*” Alimueleza Kibibi kwamba Fumbwe atajutia makosa yake ili akome kuchezea wanawake kama vitu visivyokuwa na maana yoyote. Bi Kidawa anasema kwamba atamwandikia Fumbwe barua kwanza na kisha anamhakikishia Kibibi kwamba Fumbwe atatubu kwa kumchezea kama kikaragosi. Bi Kidawa alipaswa kuwa mtetezi wa wanawake wenzake lakini ukweli wa mambo ni kwamba hakufanya hivyo. Ni jambo la kusikitisha kwamba alihongwa na Fumbwe na hivyo hatimaye hakuonyesha ari kuu ya kutetea na kumpigania Kibibi ili apate haki yake. Fumbwe alitumia cheo chake na uwezo wake wa kifedha kunyamazisha kesi ya Kibibi. Ingawa hivyo, tabia yake ya uzinzi hatimaye ilifanya akaupata ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi wa riwaya ya **Pendo katika Shari** pia ameshirikisha matumizi ya tashbihi katika uwasilishaji wa ujumbe wake. Mfano wa kwanza ambapo mwandishi ametumia mbinu hii ni pale ambapo anasema; *lakini hawa walimpuuza na kumuona kama jongoo asiyeweza kupanda mtungi.* Tashbihi hii inajitokeza na kueleweka vyema katika dondoo lifuatalo mwandishi anaposema;

7. *Matano aliwashauri rafikize Sulubu na Makelele na kuwatahadharisha dhidi ya ugonjwa wa ukimwi uliokuwa ukiua watu kila uchao. **Lakini hawa walimpuuza na kumuona kama jongoo asiyeweza kupanda mtungi.** Walimsuta na kumwambia hajui maisha ni nini. Wewe wajitia ushamba bwana. Unajifanya mshago. Hujui maisha ni mafupi na ni lazima ule raha kwani karaha yaja (Pendo katika Shari, uk.13).*

Katika muktadha huu, Makelele na rafikiye Sulubu wanaupuuza ushauri wa rafiki yao Matano. Matano anawaonya kujiepusha na mienendo mibaya inayoweza kuwafanya waambukizwe ugonjwa wa UKIMWI lakini hao wanamlinganisha na mwanamume ambaye hana uwezo wa kufanya mapenzi na mwanamke. Mwandishi anasema, **“lakini hawa walimpuuza na kumuona kama jongoo asiyeweza kupanda mtungi.”** Jongoo asiyepanda mtungi ni usemi maarufu unaotumiwa kuwarejelea wanaume ambao hawakuwa na uwezo wa kufanya mapenzi na wanawake. Sulubu na rafikiye Makelele wanaona Matano kama mtu mwenye ushamba mwingi kwa vile waliamini mtu alistahili kula raha kwa vile maisha ni mafupi. Kwa mtazamo wao, waliona kwamba raha ingepatikana tu maishani mwao iwapo wangejihusisha katika kufanya mapenzi. Matendo ya wahusika hawa yalikuwa hatari kwa sababu ya maenezi ya ugonjwa wa UKIMWI ambao ulikuwa ukiwaua watu wengi. Isitoshe, Makelele na Sulubu walikuwa na wake na jamaa nyumbani na halingekuwa jambo la busara wao kujihusisha na kufanya mapenzi nje ya ndoa. Matano ambaye walimuona kuwa mshamba ndiye aliyekuwa na hekima kuwashinda kwa maana alijua namna ya kujitunza.

Mfano mwingine wa mbinu ya tashbihi uliotumika katika riwaya ya **Pendo katika Shari** unapatikana kwenye muktadha ambapo Sulubu alikuwa amedokezewa kwamba alikuwa na virusi vya UKIMWI. Mwandishi anatueleza namna ambavyo Sulubu alikuwa akilia mithili ya mtoto mdogo wakati alipobaini alikuwa na virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Mfano huu unaeleweka vyema katika dondoo lifuatalo mwandishi anaposema:

8. *Wakati huu Sulubu alikuwa akilia mithili ya mtoto mdogo, hasa alipofahamu sasa kuwa huenda ikawa yeye ndiye aliyesababisha vifo vya Rehema na wanawe. Isitoshe, huenda ndiye anayemuua Pendo taratibu. Haya yalimtia uchungu mno (Pendo katika Shari, uk. 51).*

Katika muktadha huu, Sulubu alikuwa amefika hospitalini ili kuchunguzwa au kupimwa hali yake ya afya. Rehema na mwanawe walikuwa wamefariki kutokana na maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI. Sulubu alipopimwa na daktari, ilithibitika kwamba alikuwa na virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Matokeo haya yalimletea uchungu mwingi kwa kukumbuka kuwa yeye ndiye aliyesababisha vifo vya Rehema na wanawe na kwa kuwa yeye ndiye aliyemuua Pendo. Hali hii ndiyo iliyomfanya alie kama mtoto mdogo kama anavyosema mwandishi. Mtunzi anasema, *“Wakati huu Sulubu alikuwa akilia mihili ya mtoto mdogo, hasa alipofahamu sasa kuwa huenda ikawa yeye ndiye aliyesababisha vifo vya Rehema na wanawe.”* Mwanzoni, Sulubu hakutaka kupimwa na hata kwenda hospitalini. Hakuamini kwamba tabia yake ya uzinifu ingemletea madhara ya maambukizi ya UKIMWI kwake na kwa jamaa yake. Sulubu alikuwa amefikia kiwango cha majuto japo Waswahili husema, msiba wa kujitakia hauna kilio. Ni kweli kwamba Sulubu alikuwa amepata msiba wa kujitakia kwa vile alipuuza ushauri ambao alipewa na rafikiye Matano kujiepusha na mienendo hatari ya uzinifu. Sulubu na rafikiye Makelele walimpuuzilia mbali Matano wakamlinganisha na jongoo asiyeweza kupanda mtungi.

Katika riwaya ya **Pendo katika Shari**, mwandishi ametumia tashbihi zaidi katika uwasilishaji wa ujumbe wake. Sulubu alijiona mwenye hatia kwa kusababisha mkewe kupata ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anasema; akisota na kukohoa mfululizo kama anayeugua pumu. Dalili alizoonyesha zilikuwa za ugonjwa wa UKIMWI. Mfano huu unajitokeza vyema zaidi katika dondoo linalofuata;

9. *Sulubu, alimtazama usoni na macho yao yakakutana. Sulubu huruma ilimvaa alipomwona mkewe akisota na kukohoa mfululizo kama anayeugua pumu. Aliangalia ile kamba aliyoishikilia kana kwamba alitaka impe jibu la matatizo yake (Pendo katika Shari, uk.54).*

Katika muktadha huu, Sulubu alikuwa anaugua ugonjwa wa UKIMWI ambao ulimfikisha pabaya. Mwandishi anasema, **“huruma ilimvaa Sulubu alipomwona mkewe akisota na kukohoa mfululizo kama anayeugua pumu.”** Sulubu alipatwa na huruma kwa vile ni yeye aliyemwambukiza mke wake ugonjwa wa UKIMWI uliomfanya akohoe bila kukoma. Kikohozi cha mfululizo bila kukoma aghalabu huhusishwa na baadhi ya dalili za ugonjwa wa UKIMWI. Kwa vile alikuwa ametamauka sana maishani alifikia kiwango cha kuutoa uhai wake akitumia kamba. Sulubu anakumbuka maovu yote aliyoifanyia jamii yake, akaaibika na akaona suluhu tu ni kujiondoa katika dunia hii. Sulubu aliamini kuwa kujitoa uhai ndiyo suluhu ya matatizo yake lakini ukweli ni kwamba si suluhu kamwe. Kitendo kama hiki cha kujitoa uhai huiachia jamii shida nyingi kuliko kuipatia suluhu ya matatizo. Tabia yake ya uzinifu ilikuwa imeiletea jamii yake maafa kwa kuwaambukiza ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi wa riwaya ya **Sitaki Iwe Siri** ametumia tashbihi kama tamathali ya usemi katika kuwasilisha ujumbe wake. Kuna mifano kadha wa kadha aliyoiteua katika kazi yake. Kwa mfano anasema “wanafunzi walifyatuka kama mishale ungedhani ni wanajeshi kwenye vita vya kwanza vya dunia.” Mfano huu unajitokeza na kueleweka kwenye dondoo linalofuata:

10. *Kwa kuwa mtu hakatai wito, hukataa aitiwalo, Musa naye alijipata akirudisha kitabu chake haraka mkobani na kukimbia kwenda eneo la pardi. Wanafunzi walifyatuka kama mishale ungedhani ni wanajeshi kwenye vita vya kwanza vya dunia (Sitaki Iwe Siri, uk.16).*

Katika muktadha huu, mwandishi ametumia tashbihi kuonyesha namna wanafunzi walivyokimbia mbio kama risasi kwenda kwa pardi ili wapate kuelezwa kile walichoitiwa. Mtunzi anasema kuwa, **“wanafunzi walifyatuka kama mishale ungedhani ni wanajeshi kwenye vita vya kwanza vya dunia.”** Tashbihi hii

imetumika kuonyesha ari na wepesi ambao wanafunzi walikuwa nao walipoitwa kwenye pardi. Chambilecho wahenga, mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo. Aidha mtu hakatai wito lakini hukataa aitiwalo. Mwalimu mkuu wa shule ya Hekima aliwakusanya wanafunzi pamoja kwa pardi ili awapatie tangazo kuhusu shindano la uandishi wa insha kuadhimisha siku ya UKIMWI duniani. Mwalimu aliwapa wanafunzi changamoto ili washiriki katika shindano hilo. Ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa umeiathiri sana jamii kwa njia hasi na hivyo serikali ilikuwa ikiadhimisha siku ya UKIMWI duniani kila mwaka.

Ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa umeiathiri sana jamii na ndiyo sababu Shirika la Afya Ulimwenguni lilikuwa limeandaa shindano la uandishi wa insha la kuadhimisha siku ya UKIMWI duniani. Mashindano kama haya yaliandaliwa kuwapa vijana nafasi ya kuyashiriki na pia kuwapa jukwaa la kufanya utafiti na kupata maelezo ya kutosha kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi wa riwaya ya **Sitaki Iwe Siri** ametumia mifano zaidi ya tashbihi katika uwasilishaji wake wa ujumbe. Katika muktadha mwingine ametumia mfano unaosema; *moyo wake ulidunda kama kengele ya kanisa*. Mfano huu unajitokeza na kueleweka vyema katika dondoo lifuatalo:

**11.** *Musa alionekana mwenye furaha baada ya kusikia tangazo hilo maalum. Moyo wake ulidunda kama kengele ya kanisa. Alihisi msukumo wa aina fulani ukimchochea kushiriki katika shindano hilo (Sitaki Iwe Siri, uk. 20).*

Baada ya tangazo lililofanywa na mwalimu mkuu, ni mwanafunzi Musa pekee kutoka shule nzima aliyechochewa kushiriki katika shindano lililoandaliwa kuadhimisha siku ya UKIMWI duniani. Shindano hilo lilikuwa limeandaliwa na Wizara ya Afya kwa ushirikiano na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO). Musa alikuwa na msukumo wa

ndani kwa ndani kushiriki katika hilo shindano na ndiyo maana moyo wake ulidunda sana kwa sauti iliyolinganishwa na kengele ya kanisa.

Mwandishi anatueleza kuwa Musa alionekana mwenye furaha baada ya kusikia tangazo hilo maalum kwa sababu alikuwa amepata fursa ya kufanya utafiti na kuulewa ugonjwa ambao nyanyake hakutaka hata kuutaja. Mtunzi anasema, “**Moyo wake ulidunda kama kengele ya kanisa**” kuwa na maana kuwa moyo wake ulipiga kwa sauti ya juu kabisa. Wazazi wa Musa walikufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI lakini nyanyake hakutaka kuwaeleza wajukuu wake ukweli wa mambo. Alitaka ibaki tu siri kwa vile ugonjwa wa UKIMWI ulihusishwa na aibu na mambo mengi ambayo jamii haikujivunia.

Mfano mwingine wa tashbihi uliotumiwa na mwandishi wa riwaya ya **Sitaki Iwe Siri** unatokea pale ambapo msanii anasema; **kila uchao, dhuluma hizo ziliukereza moyo wake kama msumeno**. Mhusika Yuri hakufurahishwa na tabia ya watu katika jamii yake waliokuwa na mtazamo hasi kwake kutokana na ugonjwa ambao alikuwa anaogua. Tashbihi hii inajitokeza vyema katika dondoo lifuatalo:

- 12.** *Dhahaka za watu hasa marafiki zake kuwa Yuri alikuwa amekwisha kazi na hata kutemewa mate zilimtesa sana. **Kila uchao, dhuluma hizo ziliukereza moyo wake kama msumeno ukatao mbele na nyuma.** Alipiga moyo konde kuyakomesha mateso hayo ima fa ima (Sitaki Iwe Siri, uk.49).*

Tashbihi iliyoonyeshwa hapo juu imetumika katika insha ambayo Musa aliandika kwenye shindano la kuadhimisha siku ya UKIMWI duniani. Katika insha hii, kuna mhusika aliyelitwa Yuri ambaye alipatwa na virusi vya UKIMWI. Jamii ilikuwa na mtazamo hasi sana kwa wale waliopatwa na ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi anasema, “**Kila uchao, dhahaka hizo ziliukereza moyo wake kama msumeno ukatao mbele na nyuma.**” Wanajamii walifanyia dhahaka mhusika Yuri kwa vile alikuwa

ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Jamii katika riwaya ya *Sitaki Iwe Siri* ilikuwa na mtazamo hasi kwa wale waliopata UKIMWI kwa vile iliamini kuwa mgonjwa aliyepata UKIMWI alikuwa sawa na yule aliyejikatia tiketi ya kwenda ahera au jehanamu.

Matendo na matamshi ya wanajamii kwa walioathirika na UKIMWI yaliwafanya watamauke sana maishani. Mhusika Yuri alighadhabishwa sana na matendo na dhihaka za watu, hali iliyomfanya kujinyonga kwa vile alichoka na dhihaka zilizokereza moyo wake kama msumeno ukatao mbele na nyuma. Insha ya Musa ilishinda katika shindano lililoandaliwa kuadhimisha siku ya UKIMWI duniani. Kupitia insha ya Musa, mwandishi anatoa ujumbe kwa jamii kwamba tusiwabague na kuwanyanyapaisha wagonjwa wa UKIMWI kwa vile wao hufikishwa mahali ambapo huhisi kuwa huwatakiwi na hivyo kujitoa uhai. Badala yake wanajamii wawapende na kuwakubali kwa kuuchukulia UKIMWI kama ugonjwa wowote wa kawaida.

Katika tamthilia ya **Orodha**, tashbihi imetumika katika sehemu tofautitofauti. Katika sehemu ya kumi na moja wakati wanakijiji walipokuwa wakizungumza, mbinu hii imetumika. Baadhi ya wanakijiji walikosa maadili na hivyo kujihusisha na matendo yaliyowaletea madhara hatimaye. Msanii anatueleza:

**13.** *Mwanakijiji wa 1: Ndiyo, yeye ni **kama punda wa kijiji** Mpe karoti na kila mtu anaweza kumpanda! (Orodha, uk.18).*

Tashbihi iliyotumika katika muktadha huu ni, “**kama punda wa kijiji.**” Tabia za Furaha zimelinganishwa na punda anayebeba mizigo mingi. Furaha alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume wengi na ndivyo ambavyo mwandishi anamlinganisha na punda ambaye anaweza kubebeshwa mizigo mingi mradi tu apewe karoti. Furaha amesawiriwa kama mhusika asiyetosheka na mwanamume mmoja. Matendo yake yaliwakirihi wanajamii wakati ambapo wakati mmoja alionekana



nyuma ya nyumba yao akifanya mapenzi na Salim. Kwa sababu ya tabia zake zilizokiuka maadili ya jamii yake, alikuwa kwa vinywa vya wanakijiji.

Katika dondoo lililotumiwa, mwandishi anatumia msemu “mpe karoti” na “kila mtu anaweza kumpanda” kuwa na maana kwamba Furaha angefanya mapenzi na yeyote yule mradi apewe pesa alizohitaji. Matokeo ya matendo yake yalikuwa kwamba aliupata ugonjwa wa UKIMWI. Katika uk.24, msanii kupitia kwa mama Furaha anasema, **“Furaha, inabidi nikwambie... daktari. anasema una... ugonjwa wa slim.”** Ugonjwa wa UKIMWI ulitajwa na wanajamii hawa kuwa ugonjwa wa “slim”. Hii ilitokana na madhara ya ugonjwa wenyewe uliomfanya mwathirika kukonda kupindukia. Furaha aliupata ugonjwa wa UKIMWI kutokana na tabia yake ya kushiriki mapenzi na wanaume wengi kupita kiasi.

Katika tamthilia ya **Orodha**, Furaha amesawiriwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Salim, Kitunda, Padri James na Ecko. Kilele cha tabia ya Furaha ya uzinifu yalikuwa maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI uliomletea mauti hatimaye. Katika sehemu ya kumi na tano, mwandishi wa tamthilia ya *Orodha* ametumia tashbihi katika maelekezo yaliyo kwa maandishi ya mlazo. Anatumia kuwa:

- 14.** *Taswira ya kumaliza sehemu ya chumba cha kulala inabaki imeganda. Wanakijiji ni kama mizuka inayopita taratibu kwenye sehemu hiyo – au wameganda katika mikao hadi inapokuwa zamu yao kuongea (Orodha, uk.25).*

Tashbihi iliyotumika katika dondoo hili ni **“Wanakijiji ni kama mizuka inayopita taratibu.”** Wanakijiji wamelinganishwa na mizuka. Wanakijiji walikuwa wanazungumzia maisha ya mhusika Furaha. Wanatoa maoni mbalimbali kuhusu ugonjwa wa UKIMWI ambao Furaha alipatwa nao. Wengine wanasema ugonjwa huo uliitwa ‘slim’ kwa vile aliyeambukizwa ugonjwa huo hukonda sana. Wanakijiji wengine walisema kwamba huenda Furaha alirogwa na mtu. Aidha kuna wale

wanakijiji walioamini kuwa mtu hupata ugonjwa wa UKIMWI akigusana na muathirika wa UKIMWI ilhali wengine waliamini kuwa mtu huupata UKIMWI anapolala chumba kimoja na yule aliyeathirika kwa ugonjwa huo.

Kutokana na mazungumzo yanayoendelea baina ya wanakijiji, ni bayana kuwa wanajamii hawana ufahamu wa kutosha kuhusu chanzo cha ugonjwa wa UKIMWI. Kila mmoja alikuwa na mtazamo na imani yake kuhusu chanzo cha ugonjwa huo. Hali hii ni hatari kwa maana ingewafanya wanajamii wengi waendeleo kuupata ugonjwa wa UKIMWI kwa maana hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu.

Tamathali ambayo imetumika kwa kiasi katika tamthilia ya **Kilio Chetu** ni tashbihi. Tumeshaeleza pale mwanzoni katika 4.2.2 kuwa tashbihi ni mbinu ya ulinganishi ambapo kitu kimoja huwa kinalinganishwa na kingine kwa matumizi ya maneno kama vile; Kwa mfano, mithili ya, sawa na, kama vile na mengineyo. Katika tamthilia ya *Kilio Chetu*, mtunzi ametumia mifano michache. Kwa mfano anasema:

**15. Wanapukutika kama majani ya kiangazi (Kilio Chetu, uk.1).**

Katika mfano huu, mtunzi analinganisha vifo vya watu vilivyokuwa vikitokea na majani yanavyopukutika kwa wingi sana. Wakati wa kiangazi, **majani huwa yanapukutika kwa wingi** kumaanisha kuwa watu walikuwa wakifariki kwa wingi kutokana na athari ya ugonjwa wa UKIMWI. Katika jamii inayozungumziwa, msanii anatueleza kuwa dubwana kubwa lilikuwa limeingia kisiwani na kuwaletea watu balaa.

Dubwana laweza kulinganishwa na ugonjwa wa UKIMWI ambao ulikuwa umeivamia jamii. Watu walitoka upele, wengine waliharisha, mara nywele kunyonyoka na vifo vikafuatia. Baada ya dalili hizi watu wengi sana walipoteza maisha yao hali ambayo

mwandishi analinganisha na kupukutika kama majani ya kiangazi. Wakati wa kiangazi majani mengi sana hupukutika na kupeperushwa na upepo kwa kiwango cha juu sana. Ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa umevamia jamii na kuwaangamiza watu kwa wingi sana.

Mtunzi wa tamthilia ya **Kilio Chetu** pia ametumia tashbihi katika ujenzi wa hadithi yake. Katika tamthilia hii, inabainika kwamba msanii hakushirikisha tamathali hii ya usemi kwa wingi sana ikilinganishwa na nyingine. Mazungumzo na mijadala mingi ilikuwa ikiendelea miongoni mwa wanajamii kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Katika dondoo linalofuata anasema:

- 16.** *Kakanyaga nyaya? Mbona wengine wanasema kafa kwa UKIMWI? Wewe nawe, unakuwa nyumanyuma kama koti? Mtu aliyekufa kwa kukanyaga nyaya maana yake kafa kwa UKIMWI (Kilio Chetu, uk.5).*

Katika muktadha huu, tashbihi iliyotumika ni “nyumanyuma kama koti.” Baba Joti anaitumia akimrejelea mke wake pale anapoonekana kutoelewa maana ya msamiati tofauti ambao ulitumiwa na wanajamii kuurejelea ugonjwa wa UKIMWI. Wanajamii walikuwa wameibuka na msamiati tofautitofauti kuurejelea ugonjwa wa UKIMWI.

Kukanyaga nyaya kunalinganishwa na mtu kuathirika na nyaya za stima au nguvu za umeme. Mtu anapokanyaga nyaya za stima, wakati mwingi hufariki kutokana na athari yake kwa vile huwa hatari sana kwa maisha ya mwanadamu. Katika dondoo lililotumika katika muktadha huu, mhusika ambaye ni mama Joti hakuelewa maana ya msemo huu na ndio maana bwanake anamrejelea kama anayebaki nyumanyuma kama koti. Hii ina maana kuwa mama Joti hakuwa na ufahamu mwema wa yale ambayo yalikuwa yakiendelea katika jamii hususan mjadala kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Mjadala ambao ulikuwa ukiendelea katika jamii hii ulikuwa unahusu ugonjwa wa UKIMWI. Msanii ametumia tashbihi, “**unakuwa nyumanyuma kama koti**” kuwa na

maana kwamba, wanajamii walikuwa wameibuka na msamiati mgeni katika kuujadili msamiati kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI.

Tamathali zingine za usemi ambazo zimeshirikishwa na mwandishi wa **Kilio Chetu** katika utunzi wake ni pamoja na nyimbo au korasi, takriri, balagha, tabaini, kuchanganya ndimi, methali na misemo miongoni mwa zingine. Ingawa hivyo tamathali ambazo zimetajwa mwisho zimetumika kwa asilimia ndogo sana katika tamthilia nzima.

Tamathali ya usemi ambayo imetumiwa pakubwa na mwandishi wa hadithi fupi ya **Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine** kuiwasilisha hadithi yake ni tashbihi. Kama ilivyoielezwa mwanzoni mwa sura hii, ni mbinu inayotumika kulinganisha kitu kimoja na kingine. Katika mazungumzo baina ya Anna na Wakesho kwenye hadithi ya tahadhari bandia, mwandishi ametumia tashbihi ifuatayo:

**17. *Wakesho najua u msiri kama kaburi au tuseme kama giza (Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine ( uk.1).***

Tashbihi iliyotumika katika dondoo hili ina maana kwamba Wakesho alikuwa na uwezo wa kuficha siri kabisa sawa na kaburi lifunikavyo maiti. Rafikiye Anna alikuwa anaomba kwamba kwa vile walikuwa marafiki wa chanda na pete, walipaswa kuwa wazi mmoja kwa mwingine lakini wasiwe wa kufichana siri. Katika muktadha huu, Wakesho anadhihirisha tabia yake ya usiri. Kuna mambo mengi ambayo yalikuwa yanapita katika mawazo yake. Mwanzoni alikuwa amepatwa na msiba wa kupoteza wazazi wake kwenye ajali barabarani hali iliyomfanya yeye na mpenzi wake Jimi kusitisha mipango yao ya harusi.

Msanii aidha anatueleza namna ambavyo Wakesho alikuwa amebakwa akiwa chuoni alipokuwa anatoka maktabani kusoma. Alipopimwa na daktari, alisemekana kuwa na

ugonjwa wa UKIMWI lakini hali hii haikuwa imethibithika. Kisaikolojia Wakesho alianza kusumbuka na kuathirika hata kiafya. Mambo hayo yote yalikuwa yanampitikia katika mawazo yake lakini hakuthubutu kamwe hata kumwambia rafikiye wa karibu Anna. Jamii kwa jumla ilikuwa inaogopa sana ugonjwa wa UKIMWI na haikutaka kuuzungumzia. Msanii ameitumia tashbihi, “**msiri kama kaburi**” kuibua mtazamo wa jamii kuhusu ugonjwa wa UKIMWI ambao haukuzungumziwa tu ovyoovyo hadharani.

Tashbihi nyingine ambayo mwandishi wa **Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine** ametumia kuwasilisha hadithi yake inarejelea hali ya afya ya Wakesho. Hali ya afya ya Wakesho ilikuwa imebadilika sana na hivyo anatumia tashbihi ili kutupa picha kamili ya hali halisi. Anatumia kuwa:

**18.** *Alikuwa amekonda taabani na **alionekana mwembamba kama ng'onda.** Wakesho aliinama na kuanza kutetemeka kwa nguvu na kuguna kama mtu aliyeshikwa na kifafa ghafla (**Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine( uk.2).***

Mwandishi anabainisha namna ambavyo Wakesho alikuwa amekonda kiasi kwamba miguu yake ilishindwa kuunyanyua uzani wake mdogo. Msanii anasema, “**alionekana mwembamba kama ng'onda.**” Wakesho alivurugwa na mawazo yake sana na hali hii ilimfanya aanze kukonda kwa maana alikuwa hata amepoteza hamu ya kula chakula. Hali ya Wakesho ilibadilika akaanza kutapika kitapishi cha maji huku macho yakianza kupiga wekundu na kutiririkwa na michirizi ya machozi. Hali yake ilikuwa imebadilika ikawa mbaya zaidi, ndiyo sababu mwandishi akatumia tashbihi hii. Kinaya kinachojitokeza ni kwamba hali aliyokuwa akipitia Wakesho ilikuwa tu ya kisaikolojia. Baada ya daktari wake mmoja kumpima na kusema alikuwa na ugonjwa wa UKIMWI bila kuthibitisha, Wakesho alianza kutatizika. Baadaye uchunguzi

ulipofanywa na madaktari wengine, ilibainika kuwa Wakesho hakuwa na ugonjwa wa UKIMWI.

Tashbihi “**alionekana mwembamba kama ng’onda**” imetumiwa na msanii kuonyesha namna ambavyo wagonjwa wa UKIMWI walikuwa wakiathirika vibaya. Mgonjwa wa UKIMWI aliishiwa nguvu na kudhoofika sana, ndiyo maana mtunzi akaulinganisha wembamba wake na ng’onda. Tashbihi iliyotumika katika muktadha huu imetumiwa na msanii kuibua athari ya ugonjwa wa UKIMWI kwa wale walioambukizwa ugonjwa huo. Mbinu zingine ambazo mwandishi wa hadithi hii ametumia kwa uchache sana ni pamoja na: kubadili au kuhamisha msimbo, tanakali za sauti, sitiari, mdokezo na balagha.

Mwandishi wa hadithi ya **Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine** ametumia sana tashbihi katika uwasilishaji wa ujumbe wake. Katika barua ya kwanza ambayo Francesca alimwandikia Vicky, alimuonyesha vile alivyowachezea wanaume kama tambara bovu. Katika hadithi hii, inabainika kuwa mhusika aliyejulikana kama Francesca alikuwa na wapenzi wengi wa kiume. Anaporejelea kipenzi chake cha mashambani, Francesca anasema:

**19.** *Laniambia sasa, jembe linalitumikia kweli, hela zinaingia kama mafuriko ya El nino! Wajua linavyoanza barua” kipenzi cha moyo wangu ...na kutamatisha kwa methali kwamba, “Akupendaye kwa dhati ya moyoni! (Alidhani Kapata na Hadithi nyingine, uk.85).*

Katika muktadha huu, Francesca anarejelea mpenzi wake wa mashambani anayemtaja kama “lile jiboy” langu la kijijini. Mwandishi anatuonyesha namna ambavyo mpenzi wa Francesca alikuwa akipambana na kazi ya kilimo na kupata pesa nyingi alizotumia Francesca. Alikuwa anapata pesa nyingi sana za kumtumia Francesca ndiyo maana akazilinganisha na mvua ya El nino! Hizo pesa alizipata kwa kutoa jasho la kufanya kazi ya kilimo. Mhusika Francesca hakuwa na mapenzi ya dhati kwa Ngufumali bali

lengo lake kuu lilikuwa kujipatia pesa kutoka kwake na kufaidika ingawa kwa upande mwingine, Ngufumali alikuwa na upendo wa ukweli kwake. Francesca alitumia mwili wake kama kitega uchumi cha kumpatia mapato bila kujua kwamba kulikuwa na hatari ya kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Hatimaye tunaelezwa kuwa alipatwa na ugonjwa wa UKIMWI.

Mtunzi wa mkusanyiko wa **Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine** ametumia tashbihi nyingine tunaporejelea barua ambayo Francesca alimwandikia Vicky. Tabia na matendo ya Francesca akiwa chuoni yalikuwa ya kuhofisha. Katika barua hii, Francesca anajitapa kwa ubingwa wake wa kuwanasa wanaume hapo chuoni.

Mwandishi anasema:

- 20.** *Sio kwamba nimejiachia sawa na bendera ya kupeperushwa na upepo, hasha. Miye mara nyingi **hujiona kama simba mawindoni**; nikimwona paa miye naye. Akiwa pundamilia, vilevile; sungura naye, hana bahati lau nitampiku kwa kasi (Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine uk.89).*

Katika muktadha huu, Francesca anaonyesha kwamba yeye hawezi kutosheka na mpenzi mmoja. Anatetea msimamo wake wa kuwa na wapenzi wengi kwa maana anaamini kuwa kila mmoja wao alikuwa na umuhimu sana katika maisha yake. Ingawa hivyo anajitetea kwamba hajajiachilia vile bendera ipeperushwavyo na upepo. Katika dondoo hili, Francesca anasema kuwa, “**miye mara nyingi hujiona kama simba mawindoni.**” Hii ina maana kwamba yeye alikuwa na mbinu na uwezo wa kuwanasa na kuwatumia wanaume sawa na simba afanyavyo wanyama wengine nyikani na mawindoni. Aidha, katika barua ambayo Francesca alimwandikia Vicky anamweleza kwamba japo hawakufanya vyema masomoni, walifaulu kuwanasa waume wa wengine. Mtunzi wa hadithi hii anazidi kuonyesha namna baadhi ya wanawake kama vile Francesca walivyotumia hila na ujanja kuwafanya wanaume

wawafuate kila wakati sawa na ambavyo mbwa hufuata harufu ya minofu ya nyama karamuni.

Tashbihi “**Hela zaingia kama mafuriko ya El nino**” uk.85 imetumiwa na mtunzi kuonyesha namna ambavyo baadhi ya wanaume walikuwa wakijibiidisha sana kufanya kazi ili kupata hela. Hela hizo zilitumika katika kufanya starehe ambazo zilichangia katika maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI. Mhusika Francesca ni kati ya wale walioambukizwa ugonjwa wa UKIMWI kutokana na tabia hiyo. Francesca anasema kuwa “mara nyingi hujiona kama simba mawindoni”. Msanii ametumia tashbihi hii kuonyesha tabia ya watu katika jamii waliojiona kuwa bingwa. Tabia hii iliwaitea madhara kwa maana twaelezwa kuwa mhusika Francesca alipatwa na UKIMWI. Katika uk.93, mtunzi anasema, “**sijui kama umewasambazia wangapi ya Rabi! Ole wao!**”. Vicky anathibitisha kuwa Francesca alikuwa na ugonjwa wa UKIMWI na alikuwa amewaambukiza watu wengi. Tamathali zingine za usemi zilizotumika katika hadithi hii ni pamoja na; kuchanganya ndimi, mdokezo, tabaini, sitiari na balagha.

Tamathali ya usemi ambayo imetumika pakubwa na mwandishi wa hadithi ya **Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine** kuwasilisha ujumbe wake ni tashbihi. Mhusika aliyejulikana kama Mwasame, maarufu kama Roho Safi alitamani kwa muda mrefu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Salome lakini hakufanikiwa. Salome aliamua kuolewa na Majoni katika maeneo ya Kambi Miwa. Katika sherehe ya harusi baina ya Salome na Majoni, msanii anaema:

21. *Alihudhuria kwa roho safi ili kusuluhia kaida na kawaida ya jumuiya ya Kambi Miwa. Ilibidi avumilie kama anayetwishwa makaa ya moto kichwani (Kiti cha Moyoni, uk. 80).*



Katika muktadha huu, ni kaida ya wakazi wa Kambi Miwa iliyomlazimu Mwasame kuihudhuria harusi hiyo jambo ambalo halikuwa rahisi kamwe. Ingawa Salome alikataa kuolewa na Mwasame, kaida ya wakazi wa Kambi Miwa ilimshurutisha aihudhurie harusi hiyo. Mwandishi anasema “alihudhuria kwa roho safi ili kusuluhia kaida na kawaida ya jumuiya ya Kambi Miwa.” Katika dondoo hili, Mwasame alihudhuria harusi ya Salome na Majoni lakini moyoni alikuwa anaungulika. Twaambiwa kwamba ilibidi Mwasame avumilie kama anayetwisha makaa ya moto kichwani. Hii ina maana kuwa Mwasame alikuwa na uchungu mwingi sana hasa alipokumbuka kuwa kipenzi chake cha rohoni kilikuwa kinaolewa na mtu mwingine.

Tabia ya uvumilivu ndiyo iliyomletea Mwasame shida hatimaye. Uvumilivu wake ulimfanya asubiri mpaka Majoni akafa kisha akamrithi Salome. Salome alikuwa ameshaambukizwa ugonjwa na Majoni na hivyo Mwasame pia akaupata ugonjwa wa UKIMWI uliochukua maisha yake.

Mwasame aliposikia tetesi kuwa Majoni alikuwa amemtoroka Salome, alianza kujipitishapitisha karibu ambapo Salome alikuwa akiishi. Mwasame alikuwa na matumaini kwamba huenda Salome akabadili nia yake akimuona akijipitisha karibu ikiwa kweli Majoni alikuwa amemtoroka. Katika dondoo lifuatalo tashbihi imetumika Salome anaposema:

**22.** *Unatafuta nini hapa?* “Nilikuwaa...aaa!” “Eeh! Nimekuona unapitapita hapa sijui mara ngapi... unatafuta nini? Kimya . **Unarandarandaje hapa kama mtu anayewashwa na upupu? (Kiti cha Moyoni, uk. 84).**

Mazungumzo haya yanaonyesha namna ambavyo Mwasame alikuwa bado anatamani kupata fursa ya kuufufua uhusiano wake na Salome. Mwasame anaonyesha kuwa alikuwa na upendo wa dhati kwa Salome kwa maana licha ya kukataliwa na kuolewa na Majoni, aliomba muujiza ufanyike ili apate kuunganika na kipenzi chake cha roho.

Kwa upande wake Salome hakuwa na haja na alizidi kumrushia Mwasame cheche za matusi. Salome anashangaa namna ambavyo Mwasame alikuwa anarandaranda kama mtu aliyekosa mwelekeo maishani. Msanii anasema, ***“Unarandarandaje hapa kama mtu anayewashwa na upupu?”*** Mtunzi ametumia tashbihi hii kuibua suala la UKIMWI. Tabia yake ya kurandaranda ilimfanya akajiingiza katika uhusiano wa kimapenzi na Salome aliyemuambukiza ugonjwa wa UKIMWI.

Baada ya kifo cha Majoni, Mwasame alianza kuishi na Salome na baada ya muda wakapata mtoto. Muda si muda, Salome pia alifariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Baada ya muda usio mrefu, Mwasame pia alianza kuugua kwa maana ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa umemvamia. Mwasame aliathirika vibaya na ugonjwa huo ukasababisha tumbo lake kutoa sauti za kelele zinazolinganishwa na mngurumo. Hatimaye, Mwasame pia aliaga dunia kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Katika hadithi hii ya *Roho Safi* iliyo katika diwani ya *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine*, mwandishi ameshirikisha tamathali za usemi na mbinu zingine ingawa hizi zinajitokeza kwenye sehemu ndogo katika hadithi. Tamathali za usemi na mbinu hizo ni pamoja na; taswira, tabaini, tanakali za sauti, mbinu rejeshi, uzungumzi nafsia, balagha, kuchanganya ndimi, sitiari, mdokezo, dhihaka, takriri na tashhisi.

Tamathali ya usemi ya tashbihi imetumika pakubwa na wasanii wa takriban kazi zote zilizoteuliwa kutumika katika utafiti huu isipokuwa tamthilia ya *Giza*. Katika kazi zote teule zilizotumiwa kwenye utafiti huu, mbinu ya tashbihi imewawezesha wasanii kuibua suala la UKIMWI. Jamii tofautitofauti zina mitazamo inayohitilafiana kuhusiana na suala la UKIMWI ambalo bado linaiathiri jamii kwa njia hasi. Mbinu ya tashbihi ni kati ya mbinu zilizotumiwa na wasanii mbalimbali kuliibua suala la UKIMWI. Katika sehemu inayofuata tunaichambua mbinu ya kuchanganya ndimi.

### 4.1.3 Kuchanganya ndimi

Kuchanganya ndimi ni mojawapo ya mbinu zinazotumiwa na watunzi wa kazi za kifasihi kuwasilisha ujumbe wao. Spolsky (1998), anaeleza kwamba kuchanganya ndimi kunahusu matumizi ya maneno ama sentensi zenye muundo ambao umevunja kaida za lugha husika. Hali hii inaweza kutegemea uwezo wa kumudu lugha aliyonayo mzungumzaji, mada inayojadiliwa, mazingira ya lugha tumizi, ujumbe unaokusudiwa kupitishwa pamoja na uhusiano wa wahusika. Wamitila (2003) anaeleza kwamba hii ni mbinu ambayo kwayo mwandishi anatumia lugha mbili au zaidi kwa kuchanganya. Anataja kwamba sababu kuu ni kuonyesha tofauti za wahusika katika matumizi ya lugha. Nakubaliana na mawazo ya Wamitila (k.h.j) ingawa wakati mwingine mbinu hii hutumika wakati ambapo mzungumzaji anakosa umilisi wa lugha mbili anazotumia.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, mwandishi ametumia mbinu hii katika sehemu nyingi. Kwanza kabisa, mbinu ya kuchanganya ndimi imetumiwa katika riwaya ya *Ua la Faraja* pale ambapo mhusika Queen alikuwa amekutana na Omolo. Mhusika Queen alikuwa amemwalika Omolo amtembelee nyumbani kwake. Kwa muda mrefu, Queen alikuwa ametamani kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Omolo bila mafanikio. Omolo alikuwa na msimamo thabiti kuhusu masuala ya uhusiano wa kimapenzi hususan na wahusika wa jinsia ya kike. Dondoo lililonukuliwa linajitokeza wakati ambapo Queen amefaulu kumshawishi Omolo amtembelee. Mwandishi anasema:

- 23.** *Polepole, Queen alinyata mpaka pale alipokuwa. Anachutuma huku ameshikilia glasi ya pombe iliyonywewa nusu, “Which are your favourites” alimuuliza kwa sauti ya kilevi, huku akiweka mkono wenye glasi ya pombe begani kwa Omolo. Hakuwa ametulia. Alikuwa anayumba kiasi...Queen alisema huku akichukua glasi ya Omolo. Akatia Duncan robo ya ile glasi, kisha akaenda kwenye friji na kuchukua juice aliyoiandaa rasmi kwa ajili ya Omolo toka asubuhi siku ile (Ua la Faraja, uk.50- 51).*

Katika dondoo hili, maneno “*which are your favourites na juice*” yamechanganywa na maneno ya Kiswahili. Queen amechanganya lugha katika sehemu hii kudhihirisha uwezo wake wa kumudu lugha. Aidha, amechanganya lugha kwa sababu ya uhusiano wake na Omolo. Queen alikuwa amempatia Omolo glasi ya pombe na aliongea na Omolo kwa sauti ya kilevi. Uhusiano ambao unajitokeza katika muktadha huu ni ule wa kimapenzi. Mhusika Queen alikuwa amemwalika Omolo kwake na alimtengenezea kinywaji spesheli cha “juice” alichochanganya na kile cha nanasi. Kwa muda mrefu, alikuwa ametamani kufanya mapenzi na Omolo ambaye hakutaka tangu mwanzoni. Alitia katika kinywaji hicho dawa za kusisimua hisia za mwanamume hali iliyomlazimu Omolo kufanya mapenzi na Queen. Mabadiliko ya hisia za Omolo yalimfurahisha sana Queen ambaye alifurahi sana wakati Omolo alipolazimika kufanya ngono naye ili kutuliza hisia zake.

Tabia ya mhusika Queen ya kujihusisha na mapenzi na wanaume wengi ndiyo hatimaye inayomletea ugonjwa wa UKIMWI. Katika uk.28 mtunzi anasema, “**yule mwanamke wako Queen aliyepata mkanda wa jeshi juzi alikuwa kwenye kliniki ya kifua kikuu, amekonda amengojea kufa tu.**” Jamii iliamini kuwa yeyote aliyepatwa na UKIMWI angefariki na hivyo Queen alipopata ugonjwa wa UKIMWI alikuwa anasubiri kifo tu.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, mhusika mwingine ambaye ametumiwa na mwandishi kuendeleza mbinu ya kuchanganya ndimi ni Asha. Asha alikuwa amepewa kazi na meneja wake kumtembeza Hastings kama msaidizi wake kwa muda wa juma moja. Mwanzoni, mawasiliano yalikuwa magumu kwani Asha hakuwa hodari katika kuongea Kiingereza.

Asha alipopewa jukumu la kuwa msaidizi wa Hastings, ilibidi ajifunze Kiingereza ili mawasiliano baina yao yaweze kufanikiwa. Walipoanza safari, ilibidi wawasiliane ndipo Asha amuelekeze vyema Hastings. Hatimaye safari ilianza kuchangamka na yule mtalii akamwambia hivi Asha:

**24. *You teach me Swahili, I teach you English, okay?*** Asha akaitikia kwa kichwa. Mtalii akatoa saa kama ya mwanariadha na kumwonyesha Asha akisema, **“Two hours Swahili, two hours English” (Ua la Faraja, uk. 85).**

Mbinu ya kuchanganya ndimi imetumika hapa ili kurahisisha mawasiliano baina ya Asha na mtalii Hastings ambapo kila mmoja hukuelewa vyema lugha aliyoomba kujifunza vyema. Hastings alisema, **“you teach me Swahili, I teach you English.”** Hii ina maana kwamba Hastings alitaka iwe kama biashara ya nipe nikupe. Yeye hakuelewa Swahili na kwa upande mwingine Asha hakuelewa Kiingereza. Hastings alipendekeza mafunzo ya kila lugha yawe ya saa mbilimbili. Katika muktadha huu, mbinu ya kuchanganya ndimi imetumika kwa lengo la kupitisha ujumbe kati ya Hastings na Asha. Aidha, mbinu hii imetumika kwa sababu ya uhusiano baina ya mtalii na msaidizi wake. Mbinu ya kuchanganya ndimi ilifanikisha mawasiliano baina ya wahusika hawa wawili ambao baadaye walijenga uhusiano wa kimapenzi kati yao. Tabia ya Asha kuhusiana na wanaume wengi ndiyo hatimaye ilisababisha akaambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

Uhusiano wa Hastings na Asha ulijengeka mpaka ukafikia kiwango ambapo Hastings alimuoa Asha. Ingawa Hastings alimuoa Asha, Asha hakudhihirisha maadili mema. Mtunzi anasema, **“Katika ndoa yao ile mtu na hawara wake walizua tabia ya kutembelea Dar es Salaam na mbuga za wanyama pori” (uk.92).** Dondoo hili lina maana kwamba licha ya kuolewa na Hastings, Asha aliendelea kuwa hawara. Tabia hii hatimaye ilimfanya akaathiriwa na ugonjwa wa UKIMWI.

Katika tamthilia ya **Giza**, mwandishi ametumia tamathali mbalimbali kuwasilisha ujumbe wake kuhusu UKIMWI. Tamathali ambayo imetumika pakubwa katika mchezo huu wa kuigiza ni kuchanganya ndimi. Hali hii huenda inatokea kwa kuwa wahusika wengi waliotumika katika maandishi haya ni wanafunzi wa vyuo vikuu walio na mazoea ya kuchanganya lugha. Katika mazungumzo baina ya wahusika Robby na Mona tunaona namna ambavyo mbinu ya kuchanganya ndimi imetumika. Mtunzi anasema:

**25. *Hii sweet nitakutumia message bye!* (Giza, uk. 5)**

Robby na Mona walikuwa marafiki na baada ya kukutana na kuagana, Robby anamueleza wanapoachana kuwa atamtumia ujumbe. Robby anadai kuwa alikuwa tayari kuacha kusomea digrii kwa vile hakutaka kumuacha Mona katika hali ya huzuni. Robby alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Davina ambaye alikuwa akiugua ugonjwa wa UKIMWI. Uhusiano wa kimapenzi umedhihirika katika dondoo lililonukuliwa wakati Robby anapomuaga Mona kwa kumuahidi kuwa angemtumia ujumbe. Msanii anasema, “*Hii sweet nitakutumia message bye!*” Msanii anatueleza kwamba, Mona alipogundua baadaye kuwa alikuwa na ugonjwa wa UKIMWI, aliamua kulipiza kisasi. Katika uk. 29, Mona anasema, “**Mbona nishawanasa wengi wanajigonga tu. Siachi vitu, mbona pia hawakunihurumia?**” Tabia ya Mona inaonyesha uchungu aliokuwa nao na kutamauka kwake maishani. Hivyo basi msanii ametumia uhusiano wake na Robby kuliibua suala la UKIMWI katika jamii.

Vilevile tunapoyazingatia mazungumzo baina ya Nuru na Mona katika riwaya ya **Giza**, tunaona matumizi ya mbinu ya kuchanganya ndimi. Wanafunzi wa chuo kikuu wanashiriki mazungumzo yao ambapo matumizi ya mbinu ya kuchanganya ndimi yanadhihirika. Mazungumzo mengi ya wanafunzi wa vyuo vikuu hurejelea suala la mapenzi. Mwandishi anasema:

26. *Wewe Nuru, eti Mai kaniambia kuwa Davina aliyekukuwa girlfriend wa Robby amefariki (Giza, uk.8).*

Katika muktadha huu Mona anatumia mbinu ya kuchanganya ndimi akimaanisha kuwa Davina aliyekuwa mpenzi wa Robby alikuwa ameaga dunia. Msanii anasema, “Davina aliyekuwa **girlfriend** wa Robby amefariki.” Mona ametumia mbinu ya kuchanganya ndimi kwa sababu ya uhusiano wake na Nuru. Wote walikuwa vijana na wanafunzi wa chuo kikuu. Vijana wengi siku hizi hususan wanafunzi wa vyuo vikuu huwa wanachanganya lugha katika mawasiliano yao. Wengi wa vijana hupenda kutumia sheng’ na wengine kutumia lugha ambayo haieleweki na wazazi wao au watu wa umri mkubwa kuwashinda. Kulingana na mazungumzo ya wahusika hawa, Davina alifariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Davina alikuwa rafiki wa Robby huku Robby naye akiwa rafiki wa Mona. Ikiwa Robby alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI, bila shaka Mona pia alikuwa ameambukizwa. Hivyo basi msanii amefaulu kutumia mbinu ya kuchanganya ndimi katika kuliibua suala la UKIMWI.

Katika mazungumzo baina ya Steve na Nuru, matumizi ya mbinu ya kuchanganya ndimi pia yanadhihirika. Ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa umeenea sana na ulikuwa unaathiri maisha ya wengi hususan vijana kwa njia hasi. Vijana wengi hawakuwa wanachukua tahadhari za kutosha na ndio maana wengi walikuwa wanaambukizwa viini vya ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi wa tamthilia ya **Giza** anataeleza:

27. *Nuru unatakiwa kuwa mwangalifu kwa maana utapata kichaa cha UKIMWI. Unawaza vile ambavyo havipo! Utashindwa kufanya mambo yako na UKIMWI usiupate na maisha yawe marefu na magumu. **Be careful** (Giza, uk.19).*

Katika muktadha huu, Nuru alikuwa anaonyesha hofu yake kuhusu namna ambavyo ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa unamaliza maisha ya watu. Alionyesha hofu yake kuwa huenda wapakoteza pesa ya elimu yao maana hawakujua hali zao. Vijana wengi na hasa wa vyuo vikuu hawakujua hali zao kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI.

Kutokana na kauli hii ndipo Steve akamueleza kwamba alipaswa kuwa mwangalifu asipate kichaa cha UKIMWI. Msanii anasema, **“Be careful.”** Uhusiano baina ya Steve na Nuru ulikuwa wa kimapenzi na ndio maana wakaitumia mbinu ya kuchanganya ndimi katika mazungumzo yao. Licha ya Steve kuonyesha kujitolea kwake kupambana na ugonjwa wa UKIMWI, anatumia hongo ili daktari asitoe majibu kamili ya hali yake kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Katika onyesho la tano mtunzi anasema, **“Anaonekana Steve akiongea na watu wa maabara anatoa pesa. Mtu wa maabara anazihesabu shilingi elfu arobaini”** (uk. 20). Unyama uliofanywa na Steve ulimletea Nuru asiye kuwa na hatia ugonjwa wa UKIMWI. Hali hii inatokana na sababu kuwa, Steve alifaulu kudanganya mpaka akamuoa Nuru ilhali alijua bayana kuwa alikuwa anaogua ugonjwa wa UKIMWI.

Katika **Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine**, mwandishi ameshirikisha tamathali mbalimbali za usemi katika uwasilishaji wake wa ujumbe kuhusu UKIMWI. Mbinu ya kwanza ambayo imetumika pakubwa katika hadithi hii ni ile ya kubadili msimbo. Hii ni mbinu ya utunzi ambapo mwandishi hubadili lugha anayoitumia katika maelezo na kuingiza matumizi ya lugha nyingine kwa mfululizo. Ikiwa mzungumzaji anatumia lugha ya Kiswahili, anafika wakati katika mazungumzo yake akaingiza matumizi ya lugha nyingine kama vile Kiingereza. Katika hali hii, anaweza kuchopeka sentensi moja kamilifu na kisha kuirejelea lugha aliyokuwa akiitumia awali. Katika *Hadithi ya Likizo ya Mauti*, mtunzi ametumia mbinu hii tunapoyaangalia mazungumzo, baina ya Mzee Gogo na kimada chake Ulimbo. Mwandishi anatumia:

- 28.** *Kwa nini unanipenda ilhali huko tayari kujitolea nafsi yako kwangu? Ama kweli, wamesema wazee kuwa, **You cannot eat your cake and have it! You see you want me but not to the extent of wanting to marry me... I think you have missed the point** (Likizo ya Mauti, uk.81).*



Katika muktadha huu, mwandishi ametumia mbinu ya kubadili msimbo wakati Ulimbo alikuwa anazungumza na kipenzi chake, Mzee Gogo. Alikuwa analalamika kwamba mzee hakuwa anataka kumuoa japo alidai kwamba alimpenda. Kupitia mhusika Ulimbo, mtunzi anasema, **“you cannot eat your cake and have it! You see you want me but not to the extent of wanting to marry me.”** Mbinu hii imetumika hapa ili Ulimbo ajionyeshe kwamba pia ni mtu ambaye amesoma. Anatumia Kiingereza ili apitishie ujumbe wake uliohusiana na suala la mapenzi.

Mzee Gogo anapojibu Ulimbo pia anabadili msimbo. Anasema, **“I think you have missed the point.”** Hii ina maana kwamba Mzee alikuwa anamkumbusha kimada wake kuwa alikuwa amekosea kwa maana alisema kuwa, uhusiano wowote wa kimapenzi haukustahili kuishia kwa ndoa. Anaendelea kusema kwamba hii ni *‘holiday’* yangu na wewe. Mzee alikumbusha Ulimbo kwamba ulikuwa wakati wao wa kufurahia wala si wakati wa kuanza kulaumiana.

Katika safari yao ya kwenda kujistarehesha, Mzee Gogo alibadili msimbo na kuchanganya ndimi mara kwa mara. Mzee Gogo alikuwa ameiacha jamaa yake nyumbani na alikuwa katika starehe zake na kimada wake. Alitaka kuonyesha kimada kuwa alikuwa mtu aliyesafiri sana katika miji na mataifa mbalimbali ulimwenguni.

Katika mazungumzo yao na Ulimbo, anasema:

**29.** *Si neno, Darling, mimi niko very familiar with these cities. Lakini nafikiri wamebadilisha route kidogo. Pengine nitakuelezea baadaye wapi tunapita. Seriously, I hope you are having a good time, Honey! (Likizo ya Mauti, uk.70).*

Mzee Gogo alitaka kuonyesha Ulimbo kwamba ni mtu ambaye amesoma na amesafiri sana katika nchi mbalimbali ulimwenguni. Mzee Gogo anasema, **“Darling, mimi niko very familiar with these cities.”** Mzee Gogo alitaka kuonyesha kimada wake kwamba alikuwa amesafiri katika maeneo na miji mbalimbali duniani. Aidha, Mzee Gogo

anabadili msimbo anaposema, **“Seriously, I hope you are having a good time.”** Mzee Gogo alipopeleka kimada wake likizoni, alikusudia kumfurahisha sana. Anatumaini kuwa kimada wake alikuwa anafurahia likizo yao na ndio maana anabadili msimbo anapowasiliana na Ulimbo. Alitaka kupitisha ujumbe fulani alipobadili msimbo na aidha alionyesha uhusiano wa kimapenzi uliokuwa baina yao. Uhusiano wa kimapenzi baina ya wawili hawa ulimletea mzee Gogo shida kwa maana tunaelezwa katika mwisho wa hadithi kuwa aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Mzee Gogo anajuta kwa kujihusisha na mapenzi na kimada wake. Msanii anasema, **“Nilidhani nimepata kumbe ndio nimepatikana. Kwa nini? Sikusikia la mwadhini ama la mteka maji”** (uk. 83). Ni kweli kuwa mzee Gogo alipuza ushauri wa yeyote yule lakini mwishowe matokeo yakawa mabaya sana kwake.

Mbinu ya kuchanganya ndimi imetumiwa na wasanii teule katika kuliweka wazi suala la UKIMWI. Katika utafiti huu imebainika kwamba sio watunzi wote walioitumia mbinu hii kuwasilisha ujumbe wao. Waandishi wa *Ua la Faraja, Kala Tufaha, Giza* na *Likizo ya Mauti* ndio waliotumia mbinu hii. Waandishi waliosalia wa *Kilio Chetu, Sitaki Iwe Siri, Kiti cha Moyoni, Alidhani Kapata, Pendo katika Shari* na *Orodha* hawakuishirikisha mbinu hii katika utunzi wao. Ingawa hivyo watunzi waliotumia mbinu hii walifanikiwa katika kuliibua suala la UKIMWI. Kutokana na mifano kadhaa iliyonukuliwa katika sehemu hii, mbinu ya kuchanganya ndimi aghalabu imetumika na wahusika kadha wa kadha kuendeleza mapenzi. Uhusiano wa kimapenzi unaofanyika baina ya wahusika kama vile wa mzee Gogo na Ulimbo hatimaye ulisababisha mzee Gogo akaambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Katika kuliweka wazi zaidi suala la UKIMWI, tumejadili nafasi ya methali katika kuliibua suala hili katika sehemu inayofuata.

#### 4.1.4 Methali

Methali ni aina ya usemi wa kimapokeo unaokubalika na jamii kuwa na ukweli fulani na unaotumika kufumbia ama kutolea mfano na huwa umebeba maana pana zaidi kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa. Senkoro (2011) anaielezea methali kuwa ni semi fupifupi zinazobeba uzoefu kuhusu maisha na hivyo kuadilisha na kuhekimisha jamii. Nyangwine na Masebo (2008) wanaielezea methali kuwa ni sehemu ya lugha ambayo inaweza kufananishwa na kiungo cha lugha na kitoweo cha lugha pia. Methali hutumiwa kwa kuyatafakari na kuyapima maisha, kufunzia na kutawalia jamii na mazingira ya binadamu. Methali hufafanua falsafa ya jamii na hekima ya wale wanaoitumia katika mazungumzo yao. Kutokana na maelezo ya waandishi ambao wameshatajwa, methali hutekeleza majukumu mengi lakini kimsingi twaweza kusema kwamba ni tungo za kimapokeo ambazo hubeba falsafa ya maisha ya jamii husika.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, mwandishi ametumia methali kadha wa kadha kupitisha ujumbe wake. Kwanza, mwandishi anatumia methali *maji ukiyavulia nguo ndipo uyakoge*. Katika mkahawa wa Malaika, Jose, maarufu kama Soksi aliingia akinadi biashara yake ya kuuza mipira au kondomu. Katika muktadha huo yafuatayo yalijiri:

**30.** *Mambo kwa soksi! Mambo kwa soksi! Maji uyavulie nguo ndipo uyakoge! Ulapo ndizi usiimenye ila ivishe ganda! Jambo la raha leo ni kuvishana magozi! (Ua la Faraja, uk.12)*

Katika muktadha huu, mtunzi anaitumia methali, “**maji uyavulie nguo ndipo uyakoge!**” kumaanisha kwamba watu walistahili kujitayarisha kabla ya kufanya mapenzi kwa sababu ya magonjwa hatari kama vile UKIMWI. Ilibidi wahusika kuva mipira ya kondomu ili kuzuia uwezekano wa maambukizi ya ugonjwa huu. Msanii kupitia kwa Jose anasisitiza, “**mambo kwa soksi! Mambo kwa soksi!**” akiwa na maana kwamba kitendo chochote cha ngono kilipaswa kufanywa kwa tahadhari kwa

kutumia mipira ya kondomu. Mwandishi anazidi kusema kuwa, “ulapo ndizi, usiimenye ila ivishe ganda.” Katika kifungu hiki, mtunzi analinganisha kitendo cha kufanya ngono na kula ndizi. Hii ndiyo sababu anasema kuwa kabla ya kufanya mapenzi, ilikuwa muhimu kuvaa mipira ya kiume ili kujikinga na magonjwa hatari. Mhusika Jose alikuwa anafanya biashara ya kuuza mipira ya kondomu karibu na Malaika Bar saa za jioni na usiku wakati maduka yote yalipokuwa yamefungwa. Jose alikuwa katika mstari wa mbele katika kuhamasisha wanajamii kuhusu kujikinga dhidi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI.

Vilevile mtunzi wa riwaya ya **Ua la Faraja** ametumia methali *majuto ni mjukuu, mwisho huja kinyume*. Msanii anaonyesha mabadiliko ambayo Ngoma aliyadhihirisha, ya kuanza kwenda msikitini kuswali kama ilivyo desturi ya Waislamu. Mabadiliko ya Ngoma yalionekana kama ya kinafikiki na sarakasi mbele ya jamii yake. Awali Ngoma alijihusisha na ulevi na uasherati na kuipuuza jamii yake kabisa. Mwandishi anasema:

**31.** *Kero ya ulevi ikawa imepungua nyumbani. Lakini kupungua kwake hakukumletea furaha Tabu, kwani hisia zake zilimpa ilani kwamba kulikuwa na kiini kichungu zaidi katika hayo mabadiliko ya tabia ya mumewe. Ijapokuwa hakuna aliyemfunulia mwenziwe moyo wake na kutoa dukuduku yake waziwazi, kwa kila mmoja kulikuwa na hofu. Hofu ilikuwa kwamba: **majuto ni mjukuu, mwisho huja kinyume (Ua la Faraja, uk.115-116).***

Mwandishi ametumia methali, “**majuto ni mjukuu, huja kinyume**” kurejelea matendo ya ulevi na uasherati wa mumewe Tabu. Japo Ngoma anaonyesha kwamba ameabadili mwenendo wa maisha yake wa kujihusisha na anasa, lakini mkewe anahofia kwamba tayari huenda makosa yalikuwa yamefanyika. Katika muktadha huu alimaanisha kwamba huenda tayari alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Licha ya Ngoma kuacha ulevi, kupatikana kwake hapo nyumbani kwake hakukumletea mkewe furaha yoyote. Hii inatokana na misingi ambayo Ngoma aliiwekea jamii yake. Kwa muda mrefu sana, Ngoma alijihusisha na ulevi na uasherati

na kuidharau sana familia yake. Alikuwa anafanya biashara ya matatu lakini pesa alizozipata hazikuifaidi jamaa yake kwa vyovyote vile. Tabu alilazimika kuanzisha biashara ndogo ili kuikimu familia lakini Ngoma hakutaka mkewe afanye biashara. Hali hii iliyafanya maisha ya Tabu na wanawe kuwa magumu sana na hivyo kuifanya jamii yake kuwa na uchungu. Mabadiliko yake yalitokea wakati ambapo Ngoma alikuwa tayari ameiwekea jamii yake kidonda ambacho hakingeweza kupona kwa haraka chambilecho wahenga, majuto ni mjukuu, huja baada ya kitendo. Mbinu hii imetumiwa na mtunzi kuibua suala la UKIMWI kwa maana Ngoma alifanya uamuzi wa kubadili maisha yake akiwa amechelewa. Anadhihirisha ukweli wa methali kuwa, majuto ni mjukuu huja baada ya kitendo.

Mwandishi wa **Ua la Faraja** aidha ametumia methali wakati tunaporejelea mazungumzo kati ya daktari Hans na Tabu. Tabu alikuwa anaomba daktari Hans aende azungumze na Omolo ili akubali kumuoa Grace. Tabu alikuwa amechunguza maisha ya Omolo na akamuona kama mtu aliyekomaa ambaye angekuwa mwanamume mwema. Ingawa hivyo, tabia na mazungumzo ya Omolo yalionyesha kwamba hakuwa tayari kuingia katika maisha ya ndoa. Mwandishi anasema;

**32.** *Kama unaweza, hebu mfanye yeye na mimi tuzoeane ili nimchunguze vizuri. Lakini kwa sasa, la muhimu ni kwamba Grace aepuke kufanya mapenzi naye. Hatujui pengine ni chui aliyevaa ngozi ya kondoo. Simba mwendapole ndiye mla nyama (Ua la Faraja, uk. 256- 257).*

Tabu alitaka Grace aolewe na Omolo lakini hakumfahamu vyema huyu Omolo na ndiyo maana alikuwa anamtuma Dkt. Hans aende azungumze na Omolo ili aelewe msimamo wake na yale ambayo alikuwa anapanga katika siku zake za usoni. Ni katika muktadha huu ambapo mwandishi anatumia methali mbili zilizoonyeshwa. Mtunzi anasema, “*Hatujui pengine ni chui aliyevaa ngozi ya kondoo. Simba mwendapole ndiye mla nyama.*” Methali ya kwanza inamaanisha kwamba huenda Omolo

amejificha tu kwa unyamavu wake lakini alikuwa mtovu wa maadili. Kuna watu katika jamii ambao wanaonekana kama waungwana lakini ukiwachunguza kwa undani, unaweza kupata kwamba wana tabia fulani mbaya ambayo wanaficha na wanakuwa kama chui wanaovalia ngozi ya kondoo. Omolo alikuwa anakaa peke yake na haikuwa rahisi kumuelewa sana na ndio maana Tabu akamuomba Dkt. Hans azungumze naye huku akifanya uchunguzi.

Methali ya pili ilitumiwa kumaanisha kwamba ule mwenendo wa Omolo wa kufanya mambo polepole ungefanya ayatende mambo kwa ufanisi, hususan uhusiano wake wa kimapenzi na Queen. Omolo alikuwa anayafanya mambo yake polepole. Kwa mfano, hakuwa tayari kuoja harakaharaka lakini tunaambiwa hatimaye kwamba aliweza kukubali kuoja Grace, dadake Tabu. Omolo alichukua tahadhari wakati alipofanya mapenzi na Queen kwa kutumia mipira au kondomu. Hatua hii ilimwezesha kuepuka kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Msanii anatufunza kuwa njia bora ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI ni kutumia mipira wakati ambapo tunajihusisha na mapenzi na watu wa jinsia tofauti.

Katika riwaya ya **Pendo katika Shari**, mwandishi ametumia mbinu ya methali kati ya mbinu zingine kuwasilisha ujumbe wake. Mhusika Pendo alienda hospitalini kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu kwa vile hali yake ya afya haikuwa nzuri. Katika hali hiyo na wakati huohuo, daktari alitaka kukutana na mumewe ili kumfanyia uchunguzi pia. Msanii anasema:

- 33.** *Hakutaka kumkabili Pendo na matokeo hayo. Kwa hivyo, akaamua kumpigia mumewe simu ili afike afisini mwake haraka iwezekanavyo. Daktari mbona sikuelewi? Mtoto amezidiwa au amefariki? Sulubu alitaka kujua analoitiwa. Sikiliza Sulubu, mtu hakatai wito, hukataa analoitiwa (Pendo katika Shari, uk. 21).*

Katika dondoo hili, Sulubu hakutaka kwenda kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu kwa vile alihofia kuwa na virusi vya UKIMWI. Hii ndiyo sababu daktari anampigia simu akimwambia kuwa, *“mtu hakatai wito bali anakataa analoitwa.”* Daktari alikuwa amegundua kuwa Pendo alikuwa na virusi vya UKIMWI na hivyo hakutaka kumkabidhi matokeo peke yake. Sulubu alikuwa na wasiwasi kuhusu hali yake ya afya na ndiyo sababu hakutaka kufanyiwa uchunguzi. Sulubu alijihusisha na ulevi pamoja na uasherati na akakataa kuwa mwaminifu katika maisha yake ya ndoa. Hali hii inamfanya kutaka kujua kile ambacho alikuwa akiitiwa hospitalini. Katika riwaya ya *Pendo Katika Shari*, msanii anatuonyesha madhara ambayo Sulubu aliiletea jamaa yake baada ya kukosa kuwa mwaminifu katika maisha yake ya ndoa. Hatimaye Sulubu aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi anasema, **“Tunajua unaugua UKIMWI, aliongeza Almasi”** (uk.59). Watoto wake walijua kuwa alikuwa anaugua ugonjwa wa UKIMWI na hivyo walikuwa tayari kumpa matumaini ya kuishi.

Mwandishi wa riwaya ya **Pendo katika Shari** aidha ametumia methali kufanikisha uandishi wa riwaya. Sulubu alikuwa anajihusisha katika uhusiano wa kimapenzi na mfanyakazi wake ofisini. Sulubu alikuwa na ujasiri hata wa kumleta nyumbani wakati ambapo mkewe alikuwa amelazwa hospitalini. Mwandishi anasema;

**34.** *Rehema ni mhazili wako, ni mfanyakazi wako afisini. Kwa nini unafanya usuhuba na mtumishi wako? Bwana, hii ni aibu sana! Mkeo alipokuwa hospitali Rehema aliamia kwako. Je, umemfukuza Pendo ili umfanye Rehema mkeo? Ha! Uzuri wa mkakasi, ndani kipande cha mti (Pendo katika Shari, uk.31).*

Methali *“uzuri wa mkakasi, ndani kipande cha mti”* imetumiwa na mhusika Matano akilalamika kuhusu tabia ya Sulubu wakati ambapo mke wake alikuwa mgonjwa. Alianza kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Rehema aliyekuwa mhazili wake na ndipo mwandishi analinganisha Sulubu na mkakasi ambao ndani kuna kipande cha mti. Inaweza kumaanisha kwamba mtu anaweza kuonekana tu mzuri kwa nje lakini

ndani awe ameoza kitabia. Matendo ambayo Sulubu alikuwa akiyafanya yalikuwa ya aibu kuu kwa maana hakujiheshimu na vilevile hakuheshimu mke wake wa ndoa. Ni utovu wa maadili ya kikazi kuwa na uhusiano wa kimapenzi na msichana mdogo, lakini Sulubu anaonekana kuyafanya pasipo aibu yoyote. Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba badala ya Sulubu kumshughulikia mke wake wakati ambapo alikuwa hospitalini, yeye anaona amepata fursa ya kufanya mapenzi na kipenzi chake Rehema. Kinacholeta uchungu zaidi ni pale ambapo Sulubu anamleta Rehema nyumbani ili wajistareheshe wakati ambapo Pendo alikuwa akiugua hospitalini. Ni kweli kwamba tabia ya ndani ya Sulubu ilikuwa imeoza na anaonyesha mfano wa mtu aliyekosa ubinadamu ndani mwake. Tabia ya Sulubu inachangia pakubwa kuibua suala la UKIMWI kwa maana hatimaye, Sulubu aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi wa riwaya ya **Sitaki Iwe Siri** ametumia methali katika kuwasilisha ujumbe anaposema kuwa, “**mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo.**” Wakati ambapo mtu au watu wanaitwa lazima kuwe na sababu maalum. Wanafunzi wa Shule ya Hekima waliitwa ghafla kwenye pardi na lazima kulikuwa na sababu mahsusi iliyofanya waitwe. Mfano huu umedhihirika vyema kimatumizi katika dondoo lifuatalo:

35. *Ilikuwa saa mbili kasorobo hivi. **Chambilecho Wahenga, mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo.** Kila mwanafunzi akiacha alichokuwa akifanya na kutimua mbiu kwenda kwenye eneo la pardi. **Kwa kuwa mtu hakatai wito, hukataa aitiwalo.** Musa naye alijipata akirudisha kitabu chake haraka mkobani na kukimbia kwenda eneo la pardi. Wanafunzi walifyatuka kama mishale ungedhani ni wanajeshi kwenye vita vya kwanza vya dunia (Sitaki Iwe Siri, uk.16).*

Methali ya “mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo” imetumika na mwandishi wa riwaya ya *Sitaki Iwe Siri* ili kuufanikisha ujumbe wake. Katika muktadha huu, methali hii ilitumika wakati ambapo wanafunzi wa Shule ya Hekima waliitwa na mwalimu wao mkuu kwenye pardi. Wanafunzi wa Shule ya Hekima walifyatuka mbiu kama mshale



kuelekea kwenye pardi kusikiza kile ambacho mwalimu wao mkuu alitaka kuwaambia. Alikuwa na tangazo maalum kuhusu mashindano ya kuandika insha kuadhimisha siku ya UKIMWI duniani.

Mwalimu mkuu wa shule ya Hekima alisomea wanafunzi wote tangazo hilo na kuwapa changamoto wajitose kwenye shindano hilo la kuandika insha. Ugonjwa wa UKIMWI umeiathiri jamii kwa njia hasi kwa muda mrefu na hivyo siku ya UKIMWI huadhimishwa kila mwaka. Siku ya UKIMWI huadhimishwa kote duniani na hutumika kama fursa ya kuielimisha na kuihamasisha jamii dhidi ya madhara ya ugonjwa huu. Njia mbalimbali hutumiwa katika kupitisha ujumbe kama vile mashairi, nyimbo, michezo ya kuigiza na hata uandishi wa insha. Wanafunzi wa shule ya Hekima walipoitwa kwenye pardi walipewa fursa ya kushiriki katika shindano la kuandika insha ya kuadhimisha siku ya UKIMWI duniani.

Katika riwaya ya **Sitaki Iwe Siri**, kuna matumizi zaidi ya methali yanayojitokeza. Baada ya kupewa changamoto na mwalimu mkuu wa shule ya Hekima kushiriki katika shindano la kuandika insha, Musa alikuwa katika harakati za kufanya utafiti kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Musa na wenzake walikuwa wametembelea hospitali ili kufanya utafiti huo. Msanii anatumia methali; kusafiri kwingi ndiko, kujua mengi. Methali hii imetumika katika dondoo linalofuata:

**36.** *Kwa muda huo wote, Musa, Haki na Ukwa walikuwa wamekaa macho kujionea tukio hilo na kulifuatilia hatua kwa hatua. Walishangazwa na jinsi mambo yalivyokuwa yanafanywa kule hospitalini. Kwa hakika, **hawakukosea wahenga waliposema kwamba, kusafiri kwingi ndiko kujua mengi.** Walikuwa tayari kujifunza mengi katika ziara yao ya hospitalini (**Sitaki Iwe Siri, uk.33**).*

Katika muktadha huu, mwandishi alitumia methali, “**kusafiri kwingi ndiko kujua mengi**” akiirejelea ziara ya Musa na wenzake kwenye hospitali. Musa alikuwa katika harakati za kufanya utafiti kuhusu ugonjwa wa UKIMWI ili aandike insha kwenye

shindano lililokuwa limetangazwa shuleni. Wakiwa hospitalini walijionea namna wanawake wajaawazito walivyoshughulikiwa na wagonjwa wengine kwa jumla. Katika harakati za kuhoji daktari kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, Musa aliona bango lililoandikwa UKIMWI SI UCHAWI. Musa na wenzake walijionea na kujifunza mengi hospitalini kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, chambilecho wahenga kusafiri kwingi kujua mengi. Mafunzo kuhusu UKIMWI hayangepatikana iwapo Musa na wenzake hawangesafiri kwenda hospitalini. Aidha, walianza kupata ufahamu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI ambao ulihifadhiwa kama siri na nyanya Mwalonga.

**Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine** ni mkusanyiko wa hadithi fupi kuhusu masuala mbalimbali. Miongoni mwa masuala ambayo yameshughulikiwa ni lile la UKIMWI. Katika hadithi ya “tahadhari bandia”, mwandishi ambaye ni Kitula King’ei ameliangazia suala la UKIMWI. Katika hadithi ya tahadhari bandia, mwandishi ametumia mbinu za lugha na tamathali kadha wa kadha za usemi japo zingine kwa uchache sana. Mbinu ambayo imetumika zaidi katika hadithi hii ni methali. Kama tulivyoeleza awali, methali ni fungu la maneno yaliyo na maana fiche. Kwanza kabisa mtunzi ametumia methali anaposema:

**37.** *Maradhi na usumbufu aliokuwa nao Wakesho ulisababishwa na matukio kadha yaliyomkumba ndani ya mwaka mmoja uliotangulia. Kama walivyonena wavyele, **Hapana msiba usiokuwa na mwenziwe.** Hiyo ni busara iliyokuwa na ukweli usiopingika kwani anayetarajia suluhu, sharti ajiandae kwa vita (**Likizo ya Mauti, uk. 2**).*

Methali “**Hapana msiba usiokuwa na mwenziwe**” imetumika kumrejelea mhusika Wakesho katika hadithi hii. Wakesho alikuwa amewapoteza wazazi wake kutokana na ajali ya barabara na wakati huohuo alikuwa na maradhi ambayo yalikuwa yanamsumbua. Hii ina maana kwamba mhusika huyu alikumbwa na misiba miwili mtawalia; msiba wa kuwapoteza wazazi na ule wa kupatwa na maradhi hatari. Matukio haya yote yalitukia katika kipindi cha mwaka mmoja. Katika dondoo hili,

mwandishi anaongeza kuwa yeyote anayetarajia suluhu, lazima ajiandae kwa vita. Chambilecho wahenga, amani haiji ila kwa ncha ya upanga.

Katika maisha ya mwanadamu, wakati mwingine shida au changamoto huwa zinafuatana na hii ndiyo hali ambayo ilimkumba mhusika Wakesho katika hadithi iliyoorejewa. Katika hadithi hii, kuna daktari mmoja aliyekiuka maadili ya kikazi na kutangaza hali ya afya ya Wakesho kabla ya kuthibitishwa na daktari mwingine. Tangazo hili lilimuathiri vibaya kwa njia hasi mhusika Wakesho aliyeamini kuwa alikuwa na ugonjwa wa UKIMWI. Ukweli ulipothibitishwa na daktari mwingine, ilibainika kuwa Wakesho hakupatikana na virusi vya ugonjwa wa UKIMWI.

Mtunzi wa hadithi ya “tahadhari bandia” pia ametumia methali kuyarejelea mapenzi ambayo Jimi alikuwa nayo kwa Wakesho. Msanii anatueleza kwamba licha ya tukio la tanzia lililotokea, Jimi alikuwa radhi kungoja hadi mwisho wa dahari. Wakesho alikuwa amepoteza wazazi wake kwenye ajali wakati ambapo Jimi na Wakesho walikuwa wanafanya mipango ya kuoana. Mwandishi anasema:

**38. *Akipenda chongo huita kengeza*** na pia kuwa, ***Kipendacho roho ni dawa.*** *Alikuwa yu radhi kungoja hadi mwisho wa dahari kusudi ampate Wakesho. Aliamini fika kuwa, ndoa hufungwa mbinguni na pia Hauchi hauchi, unakuja (Likizo ya Mauti, uk.3).*

Hii ina maana kwamba Jimi alikuwa na mapenzi ya dhati kwa Wakesho na alikuwa tayari kusubiri hadi wakati ambapo Wakesho angekuwa tayari kuolewa naye. Jimi na Wakesho waliamini kwamba ndoa hufungwa mbinguni na hivyo walikuwa tayari kusubiri mpaka ule wakati ambapo Mungu mwenyewe aliuteua. Mtunzi anasema, “*Akipenda chongo huita kengeza* na pia kuwa, ***Kipendacho roho ni dawa.***” Mwandishi anatueleza kuwa ikiwa mtu amependa mwingine, hawezi kuona dosari zozote ambazo mwenzake anazo. Wapenzi hawa wawili walikuwa tayari kungoja

mpaka ndoto yao itimie kwa maana asemavyo mwandishi hauchi hauchi unakuja. Wakesho aliumwa sana kwa vile alikimbiwa na marafiki zake wote walipogundua kuwa alikuwa na virusi vya UKIMWI. Wakesho anasema, “Nitawezaje kuukabili ulimwengu wakati ambapo hata Jimi mchumba wangu ameniasi kwa hatia ya jambo ambalo sikulisababisha?” Jimi na marafiki wengine wa Wakesho wanadhihirisha unafiki wa hali ya juu wanapomnyanyapaisha Wakesho. Matendo yao ni kinyume cha methali kipendacho roho ni dawa.

Katika hadithi ya **Likizo ya Mauti**, mwandishi anatuonyesha uhalifu ambao Wakesho alifanyiwa. Wakesho alivamiwa na wahalifu akitoka kusoma usiku na kunajisiwa. Uchunguzi ulikuwa bado unafanywa na mhalifu alikuwa bado hajatambuliwa. Alijilaumu na kuweka imani yake kwa ‘wapelelezi’ badala ya kumuachia Mungu shida zake. Mwandishi anasema:

**39.** *Alijilaumu kwa kuweka imani yake kwa wapelelezi hawa badala ya kumkabidhi Mungu Mweza wa shida zote za moyo wake. Ama kweli alisahau kuwa **bidii ya mja haiondoi kudura** (Likizo ya Mauti, uk.6).*

Methali “**bidii ya mja haiondoi kudura**” ina maana kwamba jitihada za mwanadamu haziwezi kuondoa kile ambacho Mungu amepanga katika maisha yetu. Methali hii imetumika kumrejelea mhusika Wakesho aliyesahau kwamba kile ambacho Mungu alikuwa amempangia ni tofauti sana na kile ambacho wanadamu walikuwa wanasema kumhusu. Aidha, mwandishi anatueleza kwamba tumkabidhi Mungu wetu mizigo yetu badala ya kuwategemea wanadamu. Katika maisha ya wanadamu, Mungu hupanga mambo mengi yafanyike na mwanadamu hana uwezo wala mamlaka ya kubadili chochote kilichopangwa na Mungu, chambilecho wahenga, jitihada haziwezi kuondoa kudura. Katika hadithi inayorejelewa, Wakesho alinajisiwa usiku akitoka kusoma. Katika macho ya wanadamu, ilikuwa wazi kuwa huenda Wakesho aliambukizwa virusi vya ugonjwa wa UKIMWI lakini hali ilikuwa tofauti kwa Wakesho. Matokeo

kamili yaliyothibitika yalipotolewa, ilibainika kwamba, Wakesho hakuambukizwa virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Chambilecho wahenga, bidii ya mja haiondoi kudura. Methali zingine ambazo mwandishi wa hadithi hii ametumia ni pamoja na; “Ibilisi wa mtu ni mtu”, ‘Ukistaajabu ya Musa, utayaona ya Firauni”, “Anayetarajia suluhu, sharti ajiandae kwa vita” na kadhalika.

Katika hadithi ya **Alidhani Kapata**, mwandishi ametumia methali kadha wa kadha kuwasilisha ujumbe wake. Katika barua ambayo Vicky alimwandikia Francesca, anaonyesha majuto kwa kutotia bidii masomoni wakati alipokuwa shuleni. Baadhi ya wanafunzi wakiwa shuleni huwa hawaweki bidii katika masomo yao na matokeo yake ni kwamba wao huanguka mitihani yao. Vicky anasema:

**40.** *Natamani lau ningelipata fursa ya kurudi huko chuoni-bila shaka ningelilakabiwa bookworm au pengine Vicky Mabuku! **Kweli majuto ni mjukuu!** Lau ningelijitahidi kweli, nikajua nilifuatia nini huko chuoni, ningelikuwa mwingine na pengine leo! (Alidhani Kapata, uk.87).*

Katika dondoo hili, Vicky anajuta kwa kutoweka bidii masomoni wakati alipokuwa bado anasoma. Vicky hajafanikiwa kupata kazi ambayo anaipenda kwa sababu ya kutofanya vyema katika masomo. Msanii anasema, “**Kweli majuto ni mjukuu!**” Vicky na wanafunzi wengine walipokuwa chuoni, hawakutia bidii masomoni ila walijihusisha tu na raha na starehe. Wanafunzi wanapokuwa shuleni, baadhi yao hupuza ushauri ambao hupewa na walimu au wakuu wao. Wengi wao hujihusisha na anasa na starehe za chuo na kusahau kuweka bidii kwenye masomo yao. Wanafunzi ambao hawaweki bidii masomoni bila shaka hufanya vibaya katika mitihani yao. Vicky ni mmojawapo wa wanafunzi wa sampuli hiyo ambao wamepata ugumu maishani kwa kukosa kutia bidii masomoni. Walipokuwa chuoni, walijihusisha zaidi na anasa na starehe ambazo ziliwaathiri wengine wao vibaya kwa kuwaambukiza

ugonjwa wa UKIMWI. Maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI yaliathiri pakubwa masomo ya baadhi ya wanafunzi ambao waliingilia mapenzi kwa pupa.

Mwandishi wa hadithi ya **Alidhani Kapata** aidha ametumia methali katika barua ya mwisho ambayo Vicky alimuandikia Francesca. Katika barua hii, msanii anatuonyesha kipindi cha majuto kwani mhusika Francesca ameambukizwa virusi vya UKIMWI kutokana na mienendo yake mibaya. Mhusika huyu alipuza mawaidha aliyokuwa anapewa na alijiona bingwa ambaye alikuwa na mbinu faafu za kuwanasa wanaume na kuwatumia kama tambara bovu. Mtunzi anasema:

**41.** *Usijeshangaa ukanunua blue moja, ukajikuta wajiumbua mbele ya Voltaire au hao Coakroach wako chuoni. **Pole dada; japo msiba wa kujitakia hauna kilio.** Hivi alikupa hela za kutosheleza matibabu? (Alidhani Kapata, uk.94).*

Katika barua hii, Vicky anamkumbusha Francesca matendo yake ya kustarehe na kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume wengi. Mtunzi anasema, “**Pole dada; japo msiba wa kujitakia hauna kilio.**” Katika hadithi hii, msanii amemsawiri mhusika Francesca kuwa mwanafunzi aliyeshiriki mapenzi na wanaume wengi. Francesca alikuwa akisema kuwa lazima mtu apate “*balanced diet*” ya wanaume na kwamba hicho ndicho kitu alichokuwa anapania maishani. Alikuwa na wapenzi wafuatao; Ngufumali, Voltaire na Cockroach wawili katika chuo kikuu. Uhusiano huu wa mapenzi na wanaume wengi ndio uliomletea shida. Chambilecho wahenga, msiba wa kujitakia hauna kilio. Methali hii imetumika kuwa na maana kwamba ugonjwa wa UKIMWI alioupata Francesca ulikuwa wa kujitakia kwa maana alijuhusisha kwa mienendo mibaya na kupuza ushauri aliopewa na Vicky. Methali zingine zilizotumika katika hadithi hii ni pamoja na: “Akili ni nywele, kila mtu ana zake” (uk. 90), “Usichokijua mja, ni sawa na paka mweusi kizani” (uk.92), “Mchele mmoja mapishi mengi” (uk.93) na “Umdhaniye ndiye, siye” (uk. 94).

Mbinu ya methali imetumiwa sana na mwandishi wa hadithi ya **Kiti cha Moyoni** kuwasilisha ujumbe wake. Mtunzi anatumia mbinu rejeshi, na kutupatia taswira ya mambo ambayo Mwasame alikuwa anakumbuka. Mwasame aliyekuwa pia anaitwa Roho Safi, alikataliwa na Salome na kuolewa na Majoni aliyetambulika kama lofa pale Kambi Miwa. Juhudi za Mwasame kuzidi kutafuta mapenzi ya Salome ziligonga mwamba kwa maana Salome alizidi kuonyesha madharau kwa Mwasame. Mwandishi anasema:

**42.** *Anakumbuka kujishaua kwa Salome na mabezo na mapuuza yake. Mwasame alitaka kumchukia, kumbeza, kumpuuza pia. **Dawa ya moto ni moto. Akupendaye mpende, mche asiyekupenda (Kiti cha Moyoni, uk.82).***

Mwasame anakumbuka vile ambavyo alidharauliwa na Salome ambaye sasa alikuwa anahitaji msaada wake. Alitaka pia kulipiza kisasi kwa kukataa kumsaidia kwa maana asemavyo mtunzi, **“Dawa ya moto ni moto. Akupendaye mpende, mche asiyekupenda.”** Salome alihitaji msaada wa Mwasame ili ampeleke Majoni hospitalini kwa vile alikuwa anaugua. Watu wote wa Kambi Miwa walikataa kumsaidia Salome lakini kinyume cha matarajio ya wengi, Mwasame alijitolea kumsaidia. Kwa hakika Mwasame alikuwa na upendo wa dhati kwa Salome na ndiyo maana alivumilia matusi yote kutoka kwake pasipo kukata tamaa. Muda ulivyopita ndivyo raghba ya Mwasame ilivyozidi kwa Salome. Mapenzi haya ya dhati ya Mwasame ndiyo yaliyomletea shida kwa maana baada ya kifo cha Majoni, Mwasame alimrithi Salome aliyekuwa ameambukizwa virusi vya UKIMWI. Methali **“akupendaye mpende, mche asiyekupenda”** imegeuzwa na Mwasame kwa maana licha ya Salome kuonyesha na kudhihirisha wazi kuwa hakumpenda, bado Mwasame alimpenda na alikuwa tayari kuendelea kumsaidia. Kutoachana na Salome kunaletoa Mwasame balaa kwa vile hatimaye aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI na kuaga dunia.

Katika mazungumzo baina ya Salome na Mwasame, kuna matumizi ya methali wakati ambapo Mwasame alikuwa anaelezea Salome habari ambazo alikuwa amezisikia kwamba Majoni alikuwa amemtoroka Salome. Mwasame alifuatilia kwa karibu sana matukio katika maisha ya Salome na Majoni. Mwasame alikuwa mwanamume tofauti sana na wanaume wengine. Kwa kawaida mwanamume akijaribu sana kumpenda mwanamke bila kufanikiwa, huwa anakata tamaa. Hali ilikuwa tofauti sana kwa mhusika huyu. Mwandishi anasema:

**43.** *Ni nini hiki nasikia kuhusu mume wako? Umesikia upepo na ujinga na udaku mtupu. Kunradhi bibiye! Unaniita bibiye, nimekuzalia nani? Samahani! Mwasame wewe pilipili usiyoila inakuwashia nini?* (Kiti cha Moyoni, uk. 84).

Salome ametumia methali “**pilipili usiyoila inakuwashia nini?**” kumfahamisha Mwasame kwamba mambo ambayo alikuwa akiyauliza kuhusu uhusiano baina ya Salome na Majoni hayakumhusu ndewe wala sikio. Alimuona Mwasame kama ambaye alikuwa anaingilia mambo ambayo hayakumhusu. Mwasame alikuwa amesikia kuwa lofa wa Salome alikuwa amemtoroka. Mwasame alikuwa na matumaini kuwa, baada ya lofa kumtoroka Salome, huenda Salome angelegeza msimamo wake na kumpenda tena Mwasame. Hali haikuwa hivyo na ndipo Salome akampigia Mwasame methali “pilipili usiyoila inakuwashia nini?” Katika dondoo hili, Mwasame alijilazimisha kujiingiza kwa mambo ambayo hayakumhusu. Alifuatilia maisha ya ndoa ya Majoni na Salome kwa vile hakuwa amekata tamaa kumpenda Salome. Majoni alipoenda Uganda, aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI ambao alikuja akamsambazia mkewe Salome. Majoni na mkewe walipokuwa wanaugua, ni Mwasame aliyewashughulikia. Baada ya kifo cha Majoni, Mwasame alitawala kwa kumrithi Salome aliyekuwa ameambukizwa virusi vya UKIMWI. Jamii yote ya Mwasame ilianguka kutokana na athari ya ugonjwa wa UKIMWI. Iwapo Mwasame



hangeyaingilia maisha ya Salome na Lofa wake, hangeambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

Katika sehemu hii, imejitokeza kwamba waandishi wa kazi zifuatazo ndio waliitumia mbinu ya methali kuwasilisha ujumbe wao kuusiana na UKIMWI: *Ua la Faraja, Kala Tufaha, Pendo katika Shari, Sitaki Iwe Siri, Likizo ya Mauti, Alidhani Kapata na Kiti cha Moyoni*. Kutokana na utafiti wetu, watunzi wa tamthilia za: *Orodha, Kilio Chetu* na *Giza* hawakushirikisha methali katika uwasilishi wa ujumbe wao. Licha ya kutumia methali kuliibua suala la UKIMWI katika kazi teule, watunzi tofautitofauti walitumia mbinu ya taswira katika kuliweka wazi zaidi suala hili ambalo limejadiliwa kwa kina katika sehemu inayofuata.

#### **4.1.5 Taswira**

Wataalam mbalimbali wameifafanua mbinu ya taswira katika kazi zao tofauti. Wafula na Ndung'u (1993) wanaeleza kwamba taswira ni mbinu ambayo huchora picha ya watu, vitu au mahali kwa kutumia ishara. Mdee na wenzake (2009) nao wanasema kwamba taswira ni picha ya mtu au kitu inayotokea katika fikra au akili za mtu anaposoma maelezo fulani. Madai hayo yanakaribiana na yale ya Njogu na Chimerah (1999) wanaosema kuwa taswira hutumika kuleta picha fulani akilini mwa msomaji. Msomaji anaweza kuona, kusikia, kupenda, kuchukizwa au kudharau kilichosawiriwa kutegemea nguvu za taswira zilizotumika. Masebo na Nyangwine (2008) wanaeleza taswira kuwa picha zinazojitokeza baada ya matumizi mbalimbali ya semi na ishara. Matumizi mazuri ya taswira na ishara hutegemea ufundi wa mwandishi wa kuweza kuchota mambo mbalimbali yanayomzunguka na jamii yake na kutoka katika historia na sehemu zingine za maisha azijuazo.

Katika kazi teule zilizotumika katika utafiti huu, waandishi mbalimbali wametumia mbinu ya taswira isipokuwa Momanyi (2008) aliyeandika riwaya ya **Pendo Katika Shari** ambaye hakushirikisha matumizi ya mbinu hii ya taswira. Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, mwandishi ameshirikisha matumizi ya taswira katika uwasilishaji wake wa ujumbe kuhusu UKIMWI. Mfano wa kwanza unajitokeza pale ambapo anatoa maelezo kuhusu mabadiliko ambayo Omolo alianza kuyahisi baada ya kinywaji cha *Duncan* kilichoandaliwa na Queen. Mwandishi anasema:

- 44.** *Akaka kwenye kochi akisoma kitabu na kumsubiri Queen alete shati lake avae, amalize kinywaji; aondoke. Alishangaa kuona hisia ngeni zinamjia. Damu yake ilisisimka. Kichwa kilikuwa kama kinavimba. Miguuni joto lilianza kupanda, alijisikia hamu ya kimwili ya ajabu imemwingia. Kwa kuwa hakuwa na mazoea ya kunywa pombe kali, akadhani hivyo ndivyo ulevi wa Duncan ulivyokuwa (Ua la Faraja, uk.51).*

Katika dondoo lililonukuliwa hapo juu, picha ya kimawazo inatujia tunapoziona hisia za Omolo zikibadilika baada ya kupewa kinywaji cha *Duncan* na Queen. Queen alitamani sana kufanya tendo la ngono na Omolo ambaye kwa muda mrefu hakutaka. Hivyo basi Queen alitumia mbinu ya kumwekea dawa za kuamsha hisia zake. Msanii anasema, “*Damu yake ilisisimka. Kichwa kilikuwa kama kinavimba. Miguuni joto lilianza kupanda, alijisikia hamu ya kimwili ya ajabu imemwingia. Kwa kuwa hakuwa na mazoea ya kunywa pombe kali, akadhani hivyo ndivyo ulevi wa Duncan ulivyokuwa.*” Omolo alishangaa kuona hisia ngeni zinamjia. Damu yake ilianza kukimbia kasi na kumsisimua. Alianza kuhisi joto miguuni na hata mwili mzima. Kwa mara ya kwanza katika maisha yake, Omolo alijihisi hamu ya ajabu ya kimwili imemwingia hali iliyompelekea Omolo kufanya mapenzi na Queen ili kutuliza hisia zake. Queen alifurahi sana kwa vile lengo lake lilikuwa limetimia. Msanii anatupa taswira kamili ya vile mambo yalivyokuwa mpaka Omolo akalazimika kufanya mapenzi na Queen. Tabia ya uasherati ya mhusika Queen hatimaye inamletea

maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Tunaelezwa katika riwaya kuwa, “**Mama mimi nina UKIMWI, alitamka Queen**” (uk. 168). Queen alikuwa mwanamke asherati na vitendo vyake vilichangia pakubwa katika kueneza ugonjwa wa UKIMWI katika jamii. Kwa vile Queen hakutaka kufa kifo cha aibu, aliamua kumeza vidonge kuzidi vinavyopendekezwa na daktari na hivyo akaaga dunia.

Mtunzi wa riwaya ya **Ua la Faraja** ametumia mifano mingi ya taswira katika kupitisha ujumbe wake. Tabia na mienendo ya mhusika Queen ilimletea madhara kwani hatimaye aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Mfano mwingine wa mbinu ya taswira unapatikana katika muktadha ambapo msanii anatoa maelezo ya namna ugonjwa wa UKIMWI umeathiri afya ya Queen. Mwandishi anasema:

**45. *Queen alikuwa amedhoofu sana. Mashavu yalikuwa yamebonyea, kifua kimesinyaa na ngozi yake ilikuwa imepauka na kuwa kavu kama mtu aliyekuwa kwenye mavumbi. Alikuwa amejitanda kanga safi, nyeupe zenye maua meusi. Kichwani alijifunga kitambaa, lakini nywele ambazo zilijitokeza pembeni mwa kitambaa zilikuwa zimelainika kama za mgonjwa wa utapia mlo (Ua la Faraja, uk.140).***

Katika dondoo lililonukuliwa, tunaona taswira ambapo mwandishi anatuonyesha madhara ya ugonjwa wa UKIMWI kwa afya ya mwathirika. Mtunzi anasema, “***Queen alikuwa amedhoofu sana. Mashavu yalikuwa yamebonyea, kifua kimesinyaa na ngozi yake ilikuwa imepauka na kuwa kavu kama mtu aliyekuwa kwenye mavumbi.***” Sura na siha ya mhusika Queen imebadilika pakubwa na kupitia taswira hii, mwandishi anamfanya msomaji awe na ufahamu wa mabadiliko ya afya ya mhusika anapopatwa na virusi vinavyosababisha ugonjwa huu. Mwandishi anasema kuwa, mashavu ya Queen yalikuwa yamebonyea, kifua kimesinyaa na ngozi yake ilikuwa kavu kama ya mtu aliyekuwa kwenye mavumbi. Msanii anaendelea kutufahamisha kuwa nywele ambazo zilijitokeza pembeni mwa kitambaa zilikuwa zimelainika kama za mgonjwa wa utapia mlo. Taswira iliyotolewa na mwandishi

inatufanya tuwe na picha halisi ya muathirika wa UKIMWI. Ni bayana kutokana na mfano huu kwamba msanii amefaulu kuliibua suala la UKIMWI kupitia taswira iliyotolewa.

Mwandishi wa riwaya ya **Kala Tufaha** vilevile ametumia mbinu ya taswira kwa kiwango kikubwa katika kupitisha ujumbe wake. Katika maelezo yake, anatoa taswira inayojitokeza kwenye usafiri katika magari ya umma. Kibibi alikuwa anatoka shuleni akielekea nyumbani baada ya kupokea matokeo ya mtihani wake wa shule za msingi.

Mfano wa kwanza unatumika pale ambapo anasema;

**46.** *Wenye gari hili walikuwa katika dunia yao tofauti. Hewa ndani ya gari ilikuwa na mchanganyiko wa harufu, kuanzia za wavuta sigara, wenye kunuka vikwapa, wenye majasho. Almuradi kukawa na uvundo moja kwa moja! Gari lilivyojaa kuandamana na harufu hiyo ilikuwa taabu kupumua. Zaidi ya hiyo dhiki ya harufu, kuna hao wasafiri kadhaa wa kiume waliojisukumiza kwa maksudi kwa wenzao wa kike (Kala Tufaha, uk.14).*

Mwandishi wa riwaya ya **Kala Tufaha** anatupatia taswira ya usafiri kwenye magari ya matatu. Mazingira ya usafiri kwa magari haya hayakuwa mazuri. Kibibi alikuwa anatoka shuleni ambapo alipata kuwa alifanya vyema katika mtihani wa shule za msingi. Hakuwa na furaha hata hivyo kwa vile alijua kwamba ndoto yake ya kuendelea na masomo ya shule ya upili ilikuwa imefika kikomo. Hili lilitokana na msimamo wa babake aliyekataa katakata kuruhusu mtoto wa kike kuendelea na masomo ya sekondari.

Tunaonyeshwa picha na harufu kwenye magari ambapo mwandishi anasema ilikuwa ya mchanganyiko. Kulikuwa na wavuta sigara, wenye kunuka vikwapa na wenye majasho. Ilikuwa vigumu kupumua kutokana na mazingira kama hayo. Licha ya harufu ya uvundo, msanii anatueleza kuwa, “*Zaidi ya hiyo dhiki ya harufu, kuna hao wasafiri kadhaa wa kiume waliojisukumiza kwa maksudi kwa wenzao wa kike.*”

Taswira hii inatupatia picha ya tabia za baadhi ya watu katika jamii. Tunapewa mfano wa wanaume ambao walijisukumiza kwa wenzao wa kike kimakusudi na huu ni mfano wa uozo unaoendelea katika jamii iliyotumiwa na mwandishi. Tabia hii ni ishara ya visa vya uasherati vinavyochangia kuendeleza ugonjwa wa UKIMWI katika jamii. Aidha tumepewa mfano wa utingo katika gari la usafiri wa umma ambaye alikuwa ameelekeza mikono yake maksudi kwa matiti ya Kibibi. Mwandishi anasema. **“Dada harakisha! Alifoka huku mikono kaelekeza kwenye matiti ya Kibibi.”** (uk.15). Huu ni mfano ambao unabainisha ambavyo uozo ulikuwa umejaa katika jamii iliyotumiwa na mtunzi. Uozo kama huu ndio uliochangia pakubwa katika kueneza virusi vya ugonjwa wa UKIMWI kwa maana matokeo ya matendo kama hayo ni kufanya ngono kiholela.

Mtunzi wa riwaya ya **Kala Tufaha** alishirikisha matumizi ya taswira katika sehemu zingine mbalimbali. Ametuonyesha makazi ya nyumba ya Fumbwe ambapo Kibibi alienda kufanya kazi ya uyaya. Kibibi alikuwa msichana mdogo ambaye alikuwa ametoka shule na baada ya babake kukataa kumpeleka katika shule ya sekondari, aliamua kumuachilia aende kwa Fumbwe kumsaidia mke wake kumtunza mtoto. Mwandishi anasema:

**47.** *Jumba hilo lilikuwa na uwanja mkubwa. Limezingirwa kwa ua wa zege. Kuuzunguka huo ua kwa upande wa ndani kulikuwa na miti iliyokuwa imehasiwa na kupogolewa ikasalia nadhifu. Uani hapakuwa na athari ya majani wala karatasi, ishara kwamba mazingira ya jumba hilo yalikuwa safi... majumba hayo yalikuwa na malango makubwa, nayo pia yalizungushiwa nyua za zege. **Kila jumba likawa na walinzi wa langoni. Kulikuwa na ulinzi wa kipekee katika mtaa huu, hivi kwamba hata panya hangeweza kuingia bila kugunduliwa!** (Kala Tufaha, uk.53).*

Jumba la Fumbwe lilikuwa kubwa mfano wa kasri. Lilikuwa na uwanja mkubwa na lilikuwa limezungushwa na ua wa zege. Kulikuwa na miti iliyolizunguka jumba hilo na kulikuwa na kila ishara kwamba lilikuwa safi. Msanii anatuchorea picha kuwa

majumba kama hayo yalikuwa na malango makubwa. Aidha, kulikuwa na ulinzi wa kipekee kwa maana kulikuwa na walinzi langoni. Mwandishi anasema kuwa kulikuwa na ulinzi wa kipekee katika mtaa huu hivi kwamba hata panya hangeweza kuingia bila kugunduliwa. Hii ina maana kwamba ulinzi ulikuwa wa kiwango cha juu sana.

Mwandishi anatupa picha ya kasri la Fumbwe ambapo Kibibi alifanyiwa unyama baadaye. Kibibi alikuwa amechukuliwa kutoka mashambani kwenda kusaidia mke wa Fumbwe kulea mtoto. Wazazi wa Kibibi walikataa kumpeleka kibibi katika shule ya upili lakini badala yake wakamruhusu kwenda kufanya kazi ya uyaya kwa Fumbwe ambako hatimaye alidhulumiwa kimapenzi na Fumbwe. Matendo ya Fumbwe ya kushiriki ngono na wasichana wadogo kama Kibibi ndiyo yalichangia pakubwa kuambukizwa kwake ugonjwa wa UKIMWI.

Katika riwaya ya **Sitaki Iwe Siri** msanii ametumia taswira kadha wa kadha kuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji. Mwandishi anatoa maelezo yake kuhusu ugonjwa uliowaua wazazi wa Musa. Ingawa hivyo, nyanya Mwalonga hakutaka ugonjwa huo ujulikane lakini alitaka ubakie siri. Hii ilitokana na mitazamo na misimamo ya jamii kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Jamii iliona kuwa yeyote aliyeambukizwa ugonjwa wa UKIMWI aliiletea aibu na fedheha kubwa. Msanii anasema:

**48.** *Nyanya alitumia raslimali nyingi kugharamia matibabu yao, lakini ndwele hiyo haikusikia dawa kutwa kucha, afya zao zilizidi kudhoofika. Wakakonda kama ng'onda na macho yao kuwaingia ndani. Mbavu zao zikaweza kuhesabika. Kafara nazo zikawa kazi bure. Hatimaye, nyanya alienda kwa waganga wa miti shamba, tanguri na hirizi (Sitaki Iwe Siri, uk.10).*

Katika dondoo lililotumiwa katika muktadha huu, mwandishi anatupatia taswira ya ugonjwa wa UKIMWI na namna ambavyo uliathiri jamii ya nyanya Mwalonga. Mwandishi anasema, “**wazazi wa Musa wakakonda kama ng'onda na macho yao**

**kuwaingia ndani.”** Anazidi kutuonyesha kwamba mbavu zao zikaweza kuhesabika kumaanisha kuwa walikuwa wamekonda sana. Tunapewa taswira ya athari za ugonjwa wa UKIMWI kwa mwathirika. Tunaonyeshwa namna nyanya Mwalonga alijaribu kadiri ya uwezo wake kutafuta matibabu kuokoa maisha ya wanawe lakini juhudi zake ziliambulia patupu. Alijaribu hata kutafuta msaada wa waganga wa miti shamba lakini juhudi zake zote ziligonga mwamba. Ugonjwa huu wa UKIMWI hatimaye uliwaua licha ya juhudi ambazo Mwalonga aliweka ili kuwaponya watoto wake. Alibaki na mayatima ambao alijaribu kwa uwezo wake kuwalea.

Isitoshe, mwandishi wa riwaya ya **Sitaki Iwe Siri** alishirikisha zaidi matumizi ya taswira katika barua ambayo Musa aliandika kwa ajili ya mashindano wakati wa kuiadhimisha siku ya UKIMWI ulimwenguni. Musa alikuwa mwanafunzi wa pekee kwa shule ya Hekima aliyejitokeza kushiriki katika shindano lililoandaliwa la uandishi wa insha. Kujitokeza kwa mwanafunzi Musa pekee kushiriki katika shindano lililotangazwa pia kunaonyesha kwamba jamii ilikuwa bado inauogopa ugonjwa wa UKIMWI na haikutaka kujihusisha na mambo yaliyouhusu. Mwandishi anasema;

**49.** *Watu walikuwa wamenong’ona kwamba maumbile ya Yuri yalikuwa yamebadilika si haba. Kioo kilimwambia ukweli. Mwili wake ulikuwa umekondeana. Macho yalikuwa yamemwingia ndani. Mitulinga ilikuwa inaonekana huku mwili wake mzima ukinyongo’nyea kama mkufu kwa sababu ya kuishiwa nguvu. Laiti ungalimwona Yuri akiwa na siha yake! (Sitaki Iwe Siri, uk.48).*

Katika dondoo lililonukuliwa, mwandishi anazidi kutuonyesha taswira ya ugonjwa wa UKIMWI na namna ambavyo ulikuwa unayaathiri maisha ya waathiriwa. Katika dondoo lililonukuliwa, mhusika aliyejulikana kama Yuri alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi akimrejelea Yuri anasema, *“Mwili wake ulikuwa umekondeana. Macho yalikuwa yamemwingia ndani. Mitulinga ilikuwa inaonekana huku mwili wake mzima ukinyongo’nyea kama mkufu kwa sababu ya*

*kuishiwa nguvu.*” Kwa ujumla, kilichokuwa kikitokea moja kwa moja ni siha ya mwathiriwa ambayo ilikuwa imebadilika sana. Mwathiriwa aghalabu alikuwa akikonda akikondeana kutokana na virusi vinavyosababisha UKIMWI. Mbinu ya taswira inayotumiwa na mwandishi inatupa picha halisi ya athari ya ugonjwa wa UKIMWI kwa maisha ya mhusika Yuri. Katika mwisho wa insha ya Musa, mhusika Yuri aliamua kujiua kutokana na unyanyapaa ambao alifanyiwa na jamii yake. Mwandishi anasema, **“Nimejiua kwa sababu ya Ukosefu wa Kinga Mwilini”** (uk.49). Mhusika Yuri anatueleza kuwa aliamua kutoa maisha yake ili awe funzo kwa wengine. Funzo ambalo alikuwa analiacha hata hivyo, halikuwa zuri kwa maana jamii haistahili kuamini kuwa mtu akiambukizwa ugonjwa wa UKIMWI anastahili kujinyonga. Maelezo haya ya Musa yalimwezesha kuibuka mshindi katika shindano la uandishi wa insha lililoandaliwa kuadhimisha siku ya UKIMWI duniani.

Katika riwaya ya **Sitaki Iwe Siri**, mfano mwingine wa matumizi ya mbinu ya taswira unatolewa na mwandishi wakati anapoelezea ushindi wa Musa kwenye shindano la uandishi wa insha. Wakati wa kutangaza matokeo ya uandishi wa insha, watu wengi sana walijitokeza kushuhudia. Mtunzi anasema:

**50.** *Musa alisimama kutoka mahala pake, akawa nusu anatembea nusu anakimbia. Wanafunzi na wazazi walimpungia Musa misitu ya mikono. Alipofika mbele ya jukwaa, wanahabari walikuwa wameshika nafasi zao. Miangaza kutoka kwenye kamera za wanahabari waliopiga picha ilionekana ikiwaka kama umeme. Kila mpiga picha alitaka kunasa picha nzuri ya Musa Matano (Sitaki Iwe Siri, uk.63).*

Katika dondoo hili, mwandishi anatuonyesha picha ya mazingira ya shule ya Hekima ambapo kijana Musa alikuwa ameibuka mshindi katika shindano la uandishi wa insha ya kuadhimisha siku ya UKIMWI duniani. Mtunzi anasema, **“Alipofika mbele ya jukwaa, wanahabari walikuwa wameshika nafasi zao. Miangaza kutoka kwenye kamera za wanahabari waliopiga picha ilionekana ikiwaka kama umeme. Kila**



*mpiga picha alitaka kunasa picha nzuri ya Musa Matano.*” Tunaambiwa kwamba kwa sababu ya furaha, Musa alikuwa nusu anatembea na nusu anakimbia. Wazazi na wanafunzi walimpungia Musa misitu ya mikono kumaanisha kwamba walikuwa wengi kupita kiasi. Aidha, miangaza kutoka kwa kamera za wanahabari waliopiga picha ilionekana ikiwaka kama umeme. Musa alifanya wazazi na walimu wajivunie ushindi huo kwa vile shule yake pia ilipata sifa na zawadi kemkem kutokana na insha bora aliyoandika. Insha ya Musa ilizidi kufichua mengi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI ambao uliogopwa na jamii. Kizazi cha kina Mwalonga hakikutaka kuuzungumzia ugonjwa huu na kilitaka kuuweka kama siri. Msimamo kama huu haungeisaidia jamii kwa maana ugonjwa wa UKIMWI ulihitaji maelezo na ufahamu zaidi ndipo jamii ielewe namna ya kukabiliana nao. Utafiti wa Musa ulileta mchango mkubwa wa kuwezesha ugonjwa wa UKIMWI kueleweka na wanajamii.

Katika utafiti wetu, tulibaini kuwa ni wasanii watatu pekee wa riwaya ya *Ua la Faraja, Kala Tufaha* na *Sitaki Iwe Siri* walioshirikisha pakubwa matumizi ya mbinu ya taswira. Waandishi wengine wa kazi za tamthilia na hadithi fupi teule zilizotumika katika utafiti huu hawakutumia mbinu hii kuwasilisha ujumbe wao. Licha ya taswira, utafiti wetu ulibaini misemo ikiwa kati ya mbinu zilizotumiwa na watunzi kuliibua suala la UKIMWI katika jamii. Mbinu ya misemo ndiyo tunayojadili katika sehemu inayofuata.

#### **4.1.6 Misemo**

Mbinu ya misemo imefafanuliwa na waandishi kadha wa kadha. Utafiti huu uliongozwa na ufafanuzi wa wasanii watatu. Wamitila (2003) anaifasili dhana ya misemo kwa kueleza kwamba ni neno lenye upana ambalo hutumiwa kuelezea kauli zinazoelezea ukweli fulani wa maisha. Nyangwine na Masebo (2008) wanaeleza kuwa

misemo hutumiwa kwa njia ya kupamba kazi ya fasihi na pia katika kuwaainisha wahusika na lugha zao. Waandishi hawa wanaongeza kuwa misemo hutumiwa na wasanii kutajirisha maelezo yao. Kwa ufupi, twaweza kusema kwamba misemo ni fungu la maneno linalofumbata maana kimapumbo ambayo imekusudiwa kutoa funzo katika jamii. Wasanii mbalimbali katika maandishi teule yaliyotumiwa katika utafiti huu wametumia misemo anuwai kupitisha ujumbe wao. Katika sehemu inayofuata, tutaangalia baadhi ya mifano na namna ilivyotumiwa na waandishi kupitisha ujumbe wao.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, mwandishi ametumia misemo kadha wa kadha kuwasilisha ujumbe wake. Mwandishi anaonyesha athari inayowapata wahusika ambao wanaambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Mfano mmoja wa msemu uliotumiwa ni, “*Sasa anasa zimemwegesha katikati ya miiba.*” Msemu huu umetumika kama inavyoonyeshwa katika dondoo linalofuata kurejelea mhusika Ngoma ambaye kitumbua chake sasa kilikuwa kimeingia mchanga. Mtunzi anasema:

**51.** *Kupanda mchongoma, kushuka ndio ngoma. Hoja hii ilimwandama Ngoma. Zamani alipopata pesa alidhani furaha ya maisha iko kwenye anasa hata kama akimkirahi mke wake. Sasa anasa zimemwegesha katikati ya miiba. Kila alipogusa akakuta panachoma. Alilala akiwaza, na usingizi ulimjia muda mrefu baada ya mke wake kulala (Ua la Faraja, uk.138).*

Mtunzi anasema, “*Sasa anasa zimemwegesha katikati ya miiba.*” Msemu huu umetumiwa na mwandishi kuirejelea hali ambayo Ngoma alikuwa ameifikisha jamii yake. Katika dondoo lililonukuliwa hapo juu, mwandishi anatumia msemu kurejelea matendo ya Ngoma akisema, “kupanda mchongoma, kushuka ndio ngoma.” Mtunzi ana maana kwamba kuanza jambo fulani maishani ni rahisi sana lakini kumaliza si rahisi. Ngoma alijihusisha katika anasa ambayo ilimsukuma kuingiza jamii yake katika lindi la mashaka.

Mwandishi anatumia sitiari ya miiba kuonyesha shida kubwa ambazo Ngoma alikuwa ameiletea jamii yake. Ngoma alipopata pesa, alizitumia kwa anasa tu za ulevi na uasherati na kusahau kabisa jukumu lake la kukidhi mahitaji ya jamii yake. Anasa zimesababisha Ngoma kumuambukiza mke wake Tabu ugonjwa wa UKIMWI. Hali hii imeiletea jamii yake majonzi makubwa yanayolinganishwa na miiba katika msemu uliotumiwa. Mtunzi wa riwaya ya *Ua la Faraja* anasema, anasa zimemwegesha katikati ya miiba. Hii ina maana kuwa starehe na anasa za Ngoma zimemuacha mahali pagumu na pachungu panapolinganishwa na miiba. Ugonjwa ambao chanzo chake kilikuwa Ngoma hatimaye ulimletea Tabu mauti pamoja na kuiachia jamii mateso makubwa sana.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, mwandishi ametumia misemo mingine anaporejelea maisha ya mhusika Queen ambaye alijiona amebadilika sana baada ya kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Ugonjwa wa UKIMWI ulisababisha mabadiliko makubwa sana katika maisha ya mwathiriwa na hali hii ilitokea kwa mhusika Queen ambaye alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Queen alijihusisha na mienendo hatari ya maisha ambapo alishiriki ngono na wanaume wengi kiholela. Queen alidhani kuwa alikuwa anastarehe na kuyafurahia maisha lakini hakujua kuwa angevuna kile ambacho alikuwa akipanda. Mwandishi anasema:

**52.** *Alipofika chumbani akavua nguo zote na kujifunga kanga. Kabla ya kujifunga akaukagua mwili wake uliodhoofu. Hivi ndiye mimi Queen, nimefika hali hii? Alijuliza. Unene wote uliomba umbile zuri ulikwishasinyaa, amekuwa mweusi, weusi usiovutia. **Ilikuwa kama nuru ya mwili wake imeingia giza.** Sehemu zake za siri zilitoa harufu kali kutokana na vidonda vilivyomshambulia nje na ndani (**Ua la Faraja, uk. 147- 148**).*

Mwandishi anatumia namna mhusika Queen alivyojiingiza katika anasa hali iliyosababisha afya yake kuzorota. Mtunzi anatumia kuwa, “**Ilikuwa kama nuru ya mwili wake imeingia giza.**” Unene wote uliomba umbile zuri ulikwishasinyaa,

amekuwa mweusi lakini weusi usiovutia. Rangi ya ngozi ilibadilika na kwa jumla, hali yake iliathirika vibaya. Queen aliuthamini sana mwili wake lakini sasa ulikuwa umeharibiwa na ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anatumia msembo kuwa “ilikuwa kama nuru ya mwili wake imeingia giza.”

Mwanzoni, Queen alikuwa mwanamke mrembo lakini mwenyewe akajiingiza katika maisha ya uzinzi na wanaume wengi. Alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na wahusika kama vile Ngoma ambao walikuwa na virusi vya UKIMWI. Tabia ya uasherati ilisababisha akaambukizwa ugonjwa wa UKIMWI ambao uliyavuruga maisha yake. Ugonjwa wa UKIMWI unaweza kulinganishwa na giza ambalo liliingia katika maisha ya Queen ambaye alitamauka na hatimaye kujitoka uhai. Queen alijiua kwa maana hakutaka kusemwa kuwa amekufa kifo cha aibu. Jamii iliyosawiriwa na mwandishi iliamini kuwa kifo kilichotokana na ugonjwa wa UKIMWI kilikuwa kifo cha aibu.

Katika riwaya ya **Kala Tufaha** msanii ametumia mbinu ya misemo kuwasilisha ujumbe wake kuhusu UKIMWI. Mwandishi amemsawiri mhusika Fumbwe akitekeleza kitendo cha unyama kwa msichana Kibibi. Fumbwe alimbaka Kibibi wakati mkewe alipokuwa ameenda mashambani. Hiki kilikuwa kitendo cha aibu ambacho Fumbwe alikitekeleza kwa msichana mdogo ambaye alikuwa anamsaidia mke wake kulea mtoto. Kitendo hiki kilifanyika katika nyumba ya Fumbwe. Katika dondoo linalofuata matumizi ya msembo yameonyeshwa:

- 53.** *Aliupitisha mkono wa kulia katika sehemu ya juu ya paja lake. Hapo akathibitikiwa na ukweli! Hapakuwa na kizuizi chochote. Vidole vyake vilipata unyevunyevu... alijihisi kuwa na mavune mithili ya mtu aliyekesha na kushinda kwenye kazi ya shokoa. Mara akapata maumivu makali katika eneo alilohofia! Papo hapo msichana wa wenyewe akapiga unyende na kukurupuka kutoka kitandani (Kala Tufaha, uk.66).*

Fumbwe alimpatia Kibibi tufaha alilowekea dawa ya kumfanya alale ndipo akapata fursa kumfanyia msichana wa wenyewe unyama. Kibibi alipopitisha mkono wa kulia katika sehemu ya juu ya paja lake, hakupata kizuizi chochote. Fumbwe alimtoa chupi na kumfanyia unyama kwa kumbaka. Alipata unyevunyevu katika sehemu zake za siri na hivyo akawa na hakika kwamba alikuwa ametendewa unyama. Alipoamka na kugundua kwamba ametendewa hayo maovu, alipiga kelele na kuruka kutoka kitandani. Mwandishi anasema, *“Papo hapo msichana wa wenyewe akapiga unyende na kukurupuka kutoka kitandani.”* Kelele aliyopiga iliwashtua sana majirani. Kibibi alipiga unyende alipogundua kuwa alikuwa ametendewa unyama na Fumbwe. Matendo ya Fumbwe yalikuwa ya kuchukiza na kughadhabisha. Uhusiano wa Fumbwe na mkewe haukuwa mzuri kwa maana Fumbwe alijiingiza katika visa vya ukosefu wa uaminifu katika maisha ya ndoa. Tabia na matendo haya hatimaye yalisababisha Fumbwe akaambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi wa riwaya ya **Kala Tufaha** aliitumia sana mbinu ya misemo pakubwa. Fumbwe anakumbuka vile alivyomchukua mke wake akampeleka kwa masomo na vile familia yao ilikuwa na umaskini mkubwa. Fumbwe alimsaidia mkewe, akabadilika maishani mwake na kupata kazi lakini analalamika kuwa mkewe alikuwa anajihusisha na mapenzi na wanaume wengine. Fumbwe mwenyewe aliyasema haya akisahau vituko ambavyo alikuwa akimfanyia mkewe. Anasema :

**54.** *Siku zote huzuni ilimtawala asione raha ya kuishi. Mke aliyemtwaakiwa hana chochote. Akimshughulikia kimasomo hadi yake kupata stashahada ya elimujamii. **Malipo yake kumla kivuli, tena nyumbani kwake. Ndiyo na yeye alikuwa na jicho la nje. Lakini mengi akiyafanyia nje. Pengine mara moja tu aliwahi kujisahau akafanyia nyumbani (Kala Tufaha, uk.176).***

Katika dondoo lililonukuliwa, mwandishi anasema, *“Malipo yake kumla kivuli, tena nyumbani kwake. Ndiyo na yeye alikuwa na jicho la nje.”* Mwandishi ametumia

misemo kumla kivuli na kuwa na jicho la nje. Mke wa Fumbwe pia aliamua kulipiza kisasi kwa matendo ya mumewe pale ambapo alijihusisha katika kufanya mapenzi na Inspekta Chongea. Fumbwe analalamika kuwa mkewe alikuwa akimla kivuli nyumbani kwake mwenyewe. Fumbwe mwenyewe anakiri kwamba alikuwa na jicho la nje, kumaanisha hakuwa mwaminifu katika maisha yake ya ndoa japo analalama kwamba mambo yake aliyafanyia nje isipokuwa mara moja tu wakati alipomnajisi Kibibi.

Mkewe Fumbwe alishuhudia visa vingi vya ukosefu wa uaminifu wa mumewe na akafikia kiwango ambapo aliamua kumla kivuli kwa kufanya mapenzi na Inspekta Chongea. Jamii ya Fumbwe inayotumiwa na msanii ni kati ya jamii zinazojihusisha katika matendo hatari. Tabia na mienendo ya Fumbwe ya kujiingiza katika uasherati inadhihirika zaidi alipoanza kushiriki katika kufanya mapenzi na wasichana wadogo hata ofisini mwake. Hakujua kwamba tabia hii ingeweza kuhatarisha maisha yake. Mwishowe anapata maradhi yanayomtatiza na kumkondesha sana. Mwandishi anasema, “Baada ya kuteseka na kuhangaishwa na ugonjwa usiokuwa na tiba, Fumbwe alikata kamba.” (uk.189). Maisha ya uzinifu ya Fumbwe na mkewe yalisababisha Fumbwe kupata ugonjwa wa UKIMWI ambao ulimua hatimaye.

Katika riwaya ya **Pendo katika Shari**, mwandishi pia ametumia misemo kuwasilisha ujumbe wake. Mhusika Sulubu anamtusi mkewe kwa vile alikuwa amemzalia watoto wa kike pekee. Sulubu anaonyesha wasiwasi kwa kuwa anaamini kwamba hangekuwa na mrithi iwapo hatapata mtoto wa kiume. Kuna mifano anuwai ambayo msanii ameiteua kumwezesha kupitisha ujumbe wake. Anasema:

- 55.** *Jambwe! Mke gani wewe unayenzalia majanajike tu hapa nyumbani! Alibweka. Mimi nitatiwa kundini vipi na wenzangu ikiwa sina mtoto wa kiume atakayenirithi? Alipumua kwa nguvu kisha akaendelea kufoka. Basi ikiwa unataka uamuzi ni huu. Toka na majike yako urudi kwenu.*

***Wewe unadhani nilitoa mahari uje unizalie virukanjia hapa? (Pendo katika Shari, uk. 6).***

Katika dondoo lililonukuliwa, Sulubu anazozana na mkewe kwa vile hakuwa amemzalia mtoto wa kiume. Sulubu anakashifu mkewe anaposema, “***Wewe unadhani nilitoa mahari uje unizalie virukanjia hapa?***” Analaumu mke wake kwa kumzalia majanajike tu. Anashangaa vipi angechukuliwa na wenzake ikiwa hakuwa na mtoto wa kiume. Sulubu anakosa utu kwa mke wake na watoto anapomfukuza akisema, “Toka na majike yako urudi kwenu.” Aidha, anamwambia mkewe kuwa hakutoa mahari ili aje amzalie virukanjia. Ni jambo la kusikitisha kwa Sulubu kuwaita watoto wake virukanjia, yaani wasichana wanaotembeatembea ovyoovyo wakijihusisha na uasherati. Jamii iliamini kwamba mtoto wa kiume ndiye aliyestahili kupewa urithi na hivyo Sulubu alikuwa na wasiwasi kwani hakubahatika kupata mtoto wa kiume.

Ingawa jamii ilikuwa na imani iliyotajwa kuhusu urithi, katiba ya Kenya sasa inaruhusu watoto wa kike kupewa urithi sawa na wenzao wa kiume. Sulubu alimlaumu mkewe kwa kumzalia watoto wa kike anaowaita majanajike na virukanjia. Aliwaona watoto wa kike kama watu ambao hawakuwa na thamani ila kujihusisha na masuala ya kutembeatembea tu. Sulubu hakufahamu kwamba uwezo wa kumpata mtoto wa kike ama kiume ulimtegemea yeye mwenyewe na mapenzi ya Mungu.

Katika riwaya ya **Pendo katika Shari**, Sulubu anaendeleza tabia ya ubabadume. Yeye aliona mwanamke kuwa kitu kisichokuwa na maana na faida maishani mwake. Sulubu alijipatia kibali cha kujihusisha na mapenzi nje ya ndoa kwa vile mkewe hakumzalia mtoto msichana. Tabia hii ndiyo iliyosababisha Sulubu kupata ugonjwa wa UKIMWI ulioiathri jamii yake vibaya kwa kusababisha vifo vya wake zake na kisha yeye mwenyewe. Mwandishi anatumaeleza kuwa, “Wanawe walipowasili nyumbani,

walifahamishwa juu ya kifo cha baba yao. Walilia na kusikitika, huku wakimsihi mama yao asikubali UKIMWI umpokonye uhai kama baba yao” (uk.60).

Katika muktadha mwingine katika riwaya ya **Pendo katika Shari**, mwandishi ametumia msemu pale ambapo Sulubu alikataa kumpeleka mke wake hospitalini wakati ambapo alikuwa akiugua. Sulubu alishuku hali yake ya afya na hivyo hakutaka ampeleke mkewe hospitalini apimwe ili ukweli kuhusu hali yake ya afya ufichuliwe. Sulubu alionyesha ukosefu wa utu wa kutoshughulika na hata kuyajali maisha ya mke wake. Msanii anasema:

**56.** *Walirudi na Sulubu lakini walipofika nyumbani, Rehema alikuwa katika dakika za mwisho duniani. Mama yake alijaribu kumsemesha lakini hakufumba jicho wala kufungua kinywa. Sulubu alipoulizwa na wakwe zake iwapo alijaribu kumpeleka mkewe hospitali aliwajibu kuwa, **dawa za hospitali hazikufua dafu** (Pendo katika Shari, uk.45).*

Katika dondoo lililonukuliwa msanii anatueleza kuhusu hali mbaya ya afya ya Rehema. Alikuwa katika dakika za mwisho hapa duniani kumaanisha kwamba alikuwa karibu kukata kamba. Rehema alisemeshwa lakini hakufumba jicho wala kufungua kinywa. Sulubu aliulizwa na wakwe zake iwapo alikuwa amepeleka Rehema hospitalini. Katika muktadha huu, Sulubu anawajibu wakwe zake kwa kutumia msemu kuwa, “ **dawa za hospitali hazikufua dafu.**” Alikuwa na maana kwamba alimpeleka mkewe hospitalini akatibiwa lakini dawa ambazo alipewa hazikufaulu kumponya mke wake. Kwa hakika Sulubu hakuwa anasema ukweli kwa maana hakuwahi kumpeleka mkewe hospitalini.

Sababu kuu iliyomfanya Sulubu kutompeleka mkewe hospitalini ni kwamba alishuku kuhusu hali yake ya afya. Sulubu alishiriki katika kufanya mapenzi kiholela na wanawake wengi nje ya ndoa na alihofia kuwa na ugonjwa wa UKIMWI. Aliona kuwa angempeleka mkewe hospitalini apimwe kisha apatikane na ugonjwa wa



UKIMWI, bila shaka ingejulikana kuwa ni yeye aliyemuambukiza ugonjwa huo. Hii ndiyo sababu alikuwa akidai kuwa dawa za hospitali hazikufua dafu. Kwa vile afya ya Rehema ilikuwa imezorota sana, aliaga dunia baada ya muda mfupi kutokana na athari ya ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anasema, “Usiku huo, Rehema aliaga dunia.” (uk.45).

Mwandishi wa riwaya hii ya **Pendo katika Shari** ametumia mfano mwingine wa msemo pale anaposema “**haya uyatima uliwakodolea macho.**” Ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa umeivamia jamaa ya Sulubu na ulikuwa unawaondoa mmoja baada ya mwingine kwa zamu. Chanzo cha maangamizi haya ni Sulubu aliyeuleta ugonjwa wa UKIMWI katika jamii yake. Mfano huu unadhihirika vyema katika dondoo linalofuata:

**57.** *Baadhi yao pia waliweza kukumbana uso kwa uso na janga hilo la ukimwi. Walimtazama Pendo kwa masikitiko, wakijua fika kwamba alikuwa anasubiri mauti. Waliwatazama wale wanawe na kutokwa na machozi, kwani **uyatima uliwakodolea macho (Pendo katika Shari, uk.60).***

Katika dondoo lililonukuliwa hapo juu, mwandishi anajaribu kutoa taswira ya hali ya kusikitisha ya jamaa ya Sulubu ambapo mke wake alikuwa karibu kuaga dunia kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi anasema, “**uyatima uliwakodolea macho.**” Mwandishi anaonyesha namna majirani walivyokuwa wanawasikitikia watoto katika jamii ya Sulubu kwani baada ya muda mfupi wangebaki mayatima. Walijua fika kwamba Pendo alikuwa anasubiri mauti. Hii inatokana na sababu kwamba Pendo alikuwa amengojea kifo tu kutokana na athari ya ugonjwa wa UKIMWI. Majirani waliwatazama wanawe Sulubu na kutokwa na machozi kwa maana walijua kwamba uyatima ulikuwa unawakodolea macho. Wanajamii walijua kwamba baada ya muda usiokuwa mrefu, Sulubu na Pendo wangeaga dunia na kuwaacha watoto wao mayatima. Jamii iliyotumiwa na mwandishi iliamini kwamba

mtu akipatwa na ugonjwa wa UKIMWI hatima yake ilikuwa mauti. Msemu huu umetumiwa na mtunzi wa riwaya ya *Pendo Katika Shari* katika kuliibua suala la UKIMWI.

Katika riwaya ya **Sitaki Iwe Siri**, mwandishi pia ameshirikisha mbinu ya misemo katika kuwasilisha ujumbe wake. Misemo kadha wa kadha imetumiwa kumwezesha kuwasilisha ujumbe wake. Mfano wa kwanza umetumiwa katika dondoo linalofuata linalorejelea hali ya afya ya Matano baada ya kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

Mtunzi anasema:

**58.** *Kutwa kucha, afya zao zilizidi kudhoofika. Wakakonda kama ng'onda na macho yao kuwaingia ndani. Mbavu zao zikaweza kuhesabika. Kafara nazo zikawa kazi bure. Hatimaye, nyanya alienda kwa waganga wa miti shamba, tanguri na hirizi (Sitaki Iwe Siri, uk.10).*

Mwandishi wa riwaya ya **Sitaki Iwe Siri** ametumia msemu, “**mbavu zao zikaweza kuhesabika.**” kuleta msisitizo wa hali ya afya ya Matano na mke wake ambayo ilikuwa imezorota sana. Taswira tunayoipata ni kwamba wahusika hawa walikuwa wamekonda sana. Msanii anasema kuwa macho yao yalikuwa yamewaingia ndani. Wahusika hawa walikuwa wamepatwa na ugonjwa wa UKIMWI uliowaathiri pakubwa na kuwasababisha wakonde namna ambavyo mwandishi ameeleza. Maradhi haya hatimaye yalisababisha kifo chao.

Nyanya Mwalonga alijua kwamba ni ugonjwa wa UKIMWI uliowaangamiza lakini hakutaka wajukuu wake wajue. Alitaka ibaki tu siri. Sababu kuu iliyofanya Mwalonga asitake kueleza wajukuu wake aina ya ugonjwa uliowaua wazazi wao ni kuwa, ugonjwa wa UKIMWI ulihusishwa na aibu na Mwalonga hakutaka wajukuu wake wajue kwamba wazazi wao walifariki kutokana na ugonjwa uliohusishwa na aibu katika jamii.

Katika tamthilia ya **Giza**, msanii vilevile ametumia misemo katika jitihada zake za kuwasilisha ujumbe wake kuhusu UKIMWI. Wahusika kadha wa kadha wamesawiriwa wakitumia misemo kwenye tamthilia. Misemo ni kati ya mbinu ambazo mtunzi wa tamthilia ya *Giza* ameshirikisha katika uwasilishaji wake wa ujumbe. Katika mazungumzo baina ya Nuru na Mona, msanii ameshirikisha matumizi ya msemu. Anataeleza:

**59.** *Nuru, we mzuri kama jina lako nadhani hata thamani yako ni kubwa kama jina lako lilivyo na thamani. (Kimya, Nuru hajibu, Mona aligundua kuwa alikuwa akiongea peke yake na Nuru alikuwa akilia.) Nuru: Vipi shoga mbona **unanikata utumbo mwenzio?** Umefikwa na nini? (**Giza, uk.6**).*

Katika muktadha huu, mtunzi ametumia msemu mbona “**unanikata utumbo mwenzio?**” Msemu huu umetumika kwa maana ya kuumiza. Mazungumzo yalikuwa yakiendelea baina ya Nuru na Mona lakini Mona aligundua kuwa alikuwa akiongea peke yake ilhali Nuru alikuwa analia. Mona aliona kuwa Nuru alikuwa anamuumiza kwa maana alikuwa analia bila kueleza kilichomfanya alie. Nuru alikuwa anapitikiwa na mawazo mengi kuhusu maisha yake, hali iliyomfanya alie. Aliona kuwa dunia ilikuwa imemfunika na giza hasa alipoizingatia hali yake ya afya ambayo ilikuwa hatarini. Nuru alikuwa ametamauka maishani na kuona maisha yakikosa maana kwake. Aligundua kuwa alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI na hivyo hakuona umuhimu wowote wa kuendelea kuishi. Aliona kama aliyekuwa akiteseka tu na masomo ya chuo kikuu. Hali hii ndiyo iliyomfanya Nuru asononeke maishani mwake bila kuzungumza.

Mwandishi wa tamthilia ya **Giza** aidha ametumia msemu wakati ambapo Nuru alikuwa anashiriki mazungumzo na Suzi. Suzi alikuwa anamsimulia Nuru kuhusu hali ngumu ya maisha aliyokuwa akiipitia hususan wakati ambapo mdogo wake alifariki

akiwa mikononi mwake. Jamii ya kina Suzi ilikuwa imeangamia kutokana na makali ya ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anasema:

**60.** *Sipendi kukumbuka siku hiyo, kwani nilimzoea mdogo wangu na aliniacha peke yangu kwenye dunia yenye giza... Mah! Pole Suzi! Duniani ni kufunga mkanda... (Giza, uk.15).*

Katika dondoo lililonukuliwa, mwandishi anatuonyesha changamoto za maisha ambazo Suzi amezipitia. Mdogo wa Suzi alidhoofika kutokana na ugonjwa wa UKIMWI na kisha akafariki licha ya jitihada ambazo Suzi alizifanya kuyaokoa maisha yake. Suzi aliachwa peke yake kwa jamii nzima na anatueleza kuwa hakutamani kukumbuka siku hiyo. Katika muktadha huu ndipo Nuru anatumia msemu duniani ni **“kufunga mkanda”** kumaanisha kuwa duniani ilibidi mtu ajikaze na kuvumilia maisha magumu na changamoto zinazowakumba waja. Suzi alikuwa ameachwa na wazazi wote na sasa mdogo wake aliyekuwa amebaki pia alimuacha. Hali iliyomkabili Suzi inaweza kuwa ngumu kwa mtu kuistahamili maishani hususan katika umri wa ujana. Suzi alikuwa amepitia hali ngumu katika maisha yake kwa maana mamake alipopimwa na kupatwa na virusi vya UKIMWI, mama aliyekuwa akimfanyia kazi alirusha mizigo yao nje na kuwafukuza baada ya kuwanyima mshahara. Walilazimika kwenda kukaa mitaani na watoto wengine ambako waliokota tu vyakula ambavyo walivitumia. Kwa hakika ilimbidi Suzi kufunga mkanda ndipo ayamudu maisha magumu aliyokuwa akiyapitia.

Aidha, mwandishi ametumia mbinu ya msemu katika mazungumzo yanayotokea baina ya Nuru na Mona. Katika jamii iliyorejelewa na mwandishi, ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa umeenea sana na hivyo kila juhudi zilikuwa zinafanywa kuihamasisha kuhusu madhara yake. Njia mojawapo ilikuwa kupitia kwa maandishi kwenye baadhi ya mavazi yaliyotumiwa na watu. Mtunzi anasema:

**61.** *Hai! (Anapita kijana amevaa fulana imeandikwa kwa herufi kubwa)*  
**UNARINGA UMEPIMA GIZA (Giza, uk.18).**

Katika muktadha huu, mwandishi ametumia msemu ‘unaringa umepima’ ambao umeandikwa kwenye fulana ambayo ilivaliwa na kijana fulani. Msemu huu umetumika ili kuwakumbusha wanajamii kupima ili kufahamu hali zao za afya kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anasema kwamba watu hawakupaswa kujivuna kabla ya kujua hali zao za afya. Kupitia kwa mhusika Nuru, mwandishi anathabiti kuwa thamani ya pesa na elimu ni bure iwapo watu hawatapimwa na kujua hali zao za afya. Mbinu zingine ambazo zimetumika na mwandishi wa tamthilia ya *Giza* ni pamoja na: takriri, sitiari, tanakali za sauti, methali, uzungumzi nafsia na nyimbo. Tamathali na mbinu hizi zimetumika japo kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na zile zilizojadiliwa.

Katika hadithi ya “tahadhari bandia,” mwandishi pia ameitumia mbinu ya misemo katika kuijenga hadithi yake. Wanafunzi wa chuo kinachorejelewa katika muktadha huu walikuwa wakivamiwa mara kwa mara na wahuni hususan wakati wa usiku. Wanafunzi walikuwa wamelalamikia usimamizi wa chuo kuhusu tatizo hili lakini hawakuwa wamelishughulikia. Mwandishi anathabiti kuwa katika hadithi kwamba:

**62.** *Juhudi zao za kuutanabaisha utawala wa chuo kuhusu tatizo hili*  
**ziliambulia patupu (Likizo ya Mauti, uk. 4).**

Msemu “**ziliambulia patupu**” umetumika kumaanisha hazikufanikiwa. Katika muktadha huu, wanafunzi wa chuo kinachorejelewa walikuwa wakiwasilisha malalamiko yao kwa usimamizi wake kuhusu visa vya uhalifu na ubakaji lakini usimamizi huo haukuchukua hatua yoyote. Visa vya ubakaji katika chuo kinachorejelewa vilichangia pakubwa katika kueneza virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Mmoja wa wanafunzi wa chuo kinachorejelewa kwa jina Wakesho alinajisiwa na alipopimwa alidhaniwa kuwa na ugonjwa wa UKIMWI. Hali hii

iliathiri kwa njia hasi mhusika huyu aliyetengwa na marafiki zake wa karibu sana. Aidha, alibaguliwa kufanya mtihani chuoni na vilevile kunyimwa nafasi ya kazi kwa kisingizio kuwa alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Hivyo basi juhudi za wanafunzi kukomesha visa vya ubakaji hazikuwa zimefanikiwa. Kwa maneno mengine, juhudi za wanafunzi hazikuzaa matunda yoyote kwani uhalifu ulizidi kufanyika chuoni.

Msemu mwingine ambao mtunzi wa hadithi ya “tahadhari bandia” ametumia unahusu matukio ambayo yalimkumba mhusika Wakesho. Mhusika huyu alikabiliwa na changamoto maishani kwani aliwapoteza wazazi wake wawili, hali iliyomfanya asimamishe mipango yake ya harusi na Jimi. Wakesho alidhaniwa kuwa na ugonjwa wa UKIMWI hali iliyoathiri pakubwa maisha yake kwa njia hasi. Msanii ametumia msemu ufuatao:

**63. *Yaliyogomelea msumari wa mwisho juu ya jeneza lake (Likizo ya Mauti, uk.4).***

Msemu “**Yaliyogomelea msumari wa mwisho juu ya jeneza lake,**” umetumika katika muktadha huu kurejelea shida ambazo Wakesho alikuwa anakabiliwa nazo. Msemu huu unapotumika huwa na maana kwamba mtu anapokuwa na shida, huenda zikatokea shida nyingi zaidi za kumfanya mhusika kutatizika kwa kiwango cha juu sana. Katika hadithi hii tunaambiwa kuwa, tayari Wakesho alikuwa amewapoteza wazazi, hali iliyoathiri mipango ya ndoa yake. Aidha, uchunguzi wa kimatibabu ulipofanywa, iligunduliwa kuwa alikuwa na virusi vya UKIMWI. Kauli kwamba Wakesho alikuwa na virusi vya UKIMWI ilikuwa sawa na kutangaza hukumu ya kifo dhidi yake. Jamii inayorejelewa na mwandishi ilikuwa na mtazamo hasi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI na yeyote aliyeambukizwa ugonjwa huo alikuwa sawa na yule aliyekata tikiti ya kuingia kaburini.

Msemu mwingine umetumiwa na mwandishi anapoyarejelea mawazo yaliyokuwa yanampitikia Wakesho. Changamoto nyingi zilikuwa zimemkabili na jambo hili linamfanya azame kwenye mawazo kwa maana alikuwa akisumbuliwa. Wakesho alikuwa amebakwa wakati alipokuwa ametoka kwenye maktaba. Isitoshe, uchunguzi wa Dkt. wa kwanza ulikuwa umemtangazia kuwa alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anatueleza:

**64.** *Wakesho hakujibu kwa muda mrefu na alionekana bado kapotea katika lindi lake la fikira akiwaza na kuwazua (Likizo ya Mauti, uk.6).*

Mwandishi anasema, “*alionekana bado kapotea katika lindi lake la fikira akiwaza na kuwazua.*” Mhusika Anna alikuwa anazungumza na Wakesho lakini Wakesho alikumbatia barua fulani aliyopewa bila kuifungua, lakini badala yake akazama katika mawazo mengi. Barua hiyo ilikuwa na majibu ya daktari kuhusu hali yake ya afya na hivyo alihofia maisha yake iwapo barua hiyo pia ingethibitisha kwamba alikuwa na virusi vya UKIMWI. Daktari wa kwanza alikosa kuzingatia maadili ya kazi na kutangaza kuwa Wakesho alikuwa na virusi vya UKIMWI bila kuthibitishwa na daktari wa pili. Mtunzi anasema, “I think she is postive” (uk.4). Tangazo hili lilimtia hofu sana mhusika Wakesho. Alipopata matokeo kutoka kwa daktari wa pili, Wakesho aliogopa kuifungua na badala yake akazama kwenye mawazo mengi.

Jamii inayorejelewa na mwandishi haikuwa imepewa mafunzo bora kuhusu ugonjwa wa UKIMWI na ndiyo sababu Wakesho alikuwa na uoga mwingi. Watu walio na virusi vya UKIMWI wakishughulikiwa vyema kwa matibabu na chakula, wanaweza kuishi maisha marefu kuliko inavyodhaniwa. Katika hadithi hii, kuna matumizi ya tamathali za usemi na mbinu za lugha japo zimetumika kwa kiwango cha chini sana. Mifano ya mbinu hizo ni pamoja na: methali, majazi, tanakali za sauti, tashbihi, mdokezo na sitiari.

Katika uwasilishaji wa hadithi yake, mwandishi wa hadithi ya **Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine** ametumia mbinu ya misemo. Katika barua ya kwanza ambayo Francesca anamwandikia Vicky, anamweleza namna ambavyo anastarehe na kuyafurahia maisha. Francesca aliishi maisha ya kutojali na kujiachilia kufanya mapenzi na wanaume tofautitofauti. Lengo lake kama anavyosema lilikuwa kujipatia fedha na pia kuwa na starehe maishani mwake. Mtunzi anasema:

**65.** *Miye falsafa yangu maishani, ni usimwamshe aliyelala, usije ukalala Mwenyewe naaamini kwamba, ulimwengu wa leo ni kutoka, ukaona, ukalenga, ukafuma. Basi! (Alidhani Kapata, uk.85).*

Francesca anaamini kwamba maishani mtu mwenyewe anapaswa kuwa macho na kufanya kile ambacho anaamini ni cha manufaa maishani bila ya kushughulika na wengine ambao kwa maoni yake wamelala. Mtunzi anasema, “*usimwamshe aliyelala, usije ukalala Mwenyewe.*” Anawachukulia wale ambao wamelala kama watu ambao hawajazinduka maishani. Anaamini kwamba hakuna haja ya kushughulika na wengine kwa maana angefanya hivyo anaamini angelala mwenyewe. Francesca aliamini kuwa alikuwa na mbinu na uwezo wa kustarehe na kuyafurahia maisha. Kwa maoni yake ilibidi mtu mwenyewe ajitokeze na kulenga kile ambacho alitaka kukipata maishani. Mwandishi anatuonyesha namna ambavyo Francesca alikuwa na wanaume kadhaa kama vile: Ngufumali, Coacroach wawili hapo chuoni miongoni mwa wengine. Mhusika huyu hakuyatilia maanani masomo lakini badala yake akawa anajihusisha katika uhusiano wa kimapenzi na wanaume wengi. Kilele cha yote ni kuwa, mhusika huyu aliambukizwa virusi vya ugonjwa wa UKIMWI.

Katika hadithi ya “tahadhari bandia,” mwandishi ametumia misemo katika barua ambayo Vicky alimwandikia Francesca kuhusu juhudi zake za kumnasa mume wa Vicky chuoni na kujihusisha naye kimapenzi. Francesca ni mhusika ambaye maadili yake yalikuwa yameporomoka na alikuwa anajihusisha katika uhusiano wa kimapenzi



na wanaume wengi. Tabia ya watu kama vile Francesca ilikuwa hatari sana katika enzi ambapo ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa ukiangamiza maisha ya wengi ambao walijihusisha na kufanya mapenzi kiholela. Anasema:

**66.** *Pole dada Francesca; ubaya sina, ila naomba ufahamu sio kila ng'ombe ana kupe umdandie mgongoni, kumdonoa!* (Alidhani Kapata, uk.91).

Mtunzi wa hadithi ya **Likizo ya Mauti** ametumia msemu, “*sio kila ng'ombe ana kupe umdandie mgongoni, kumdonoa!*” katika kuiwasilisha hadithi yake. Katika muktadha huu, Vicky alimweleza Francesca kwamba sio wanaume wote waliokuwa na pesa za bure za kuwapa wanawake. Anaongeza kwamba hakuwa na pesa ambazo zingendonolewa na wanawake wazizi waliolenga kujitajirisha wakitumia miili yao kama vitega uchumi. Alimfahamisha Francesca kwamba alilenga kupata pesa za bure kutoka kwa mume wa Vicky lakini haingewezekana. Aidha, katika barua ambayo Vicky alimwandikia Francesca, anamwonyesha namna mume wake alikuwa mtu wa maana na heshima kinyume cha alivyodhani Francesca. Vicky anaeleza mwenzake kuwa mume wake si kati ya wale “maprofesa wa shahada za mapenzi?” Mtunzi katika muktadha huu alimaanisha kwamba Francesca alikosea katika mawazo yake na kwamba hayakuwa ya ukweli hata kidogo. Vicky alishikilia kuwa Francesca alikuwa amekosea na hata kuambulia patupu kwa yale aliyomdhanika mume wa Vicky. Francesca ni mhusika aliyetumiwa na mwandishi kudhihirisha uozo uliokuwa katika jamii hususan miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Tabia yake ya uasherati ilimletea madhara kwa kuwa hatimaye aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi wa diwani ya **Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine** ametumia misemo kadha wa kadha kuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji. Katika hadithi ya “Roho Safi’, mbinu ya misemo ndiyo imetumika katika sehemu nyingi kupitisha ujumbe wa mwandishi. Kwenye hadithi, msichana Salome ambaye Mwasame au Roho Safi

alikuwa anamchumbia, aliolewa na Majoni. Harusi ilifanywa na hivyo ilibidi Mwasame ahudhurie kama ilivyo desturi ya wakazi wa Kambi Miwa. Mwandishi anatumia msemo katika dondoo linalofuata anaposema:

**67.** *Ingawa arusi ya Salome ilikuwa chanzo cha kero na hasira kwa Mwasame, **alipiga moyo konde** kuhudhuria kwa roho safi. Alihudhuria kwa roho safi ili kusuluhisha kaida na kawaida za jumuiya ya Kambi Miwa (**Kiti cha Moyoni, uk.80**).*

Katika dondoo lililotumika, Mwasame aliamua kuhudhuria arusi hiyo hata ingawa ndani mwake alikuwa na uchungu kwa maana Salome alikataa kuolewa naye na badala yake akachagua kuolewa na lofa Majoni. Msanii anasema, “**Mwasame alipiga moyo konde**” na kuihudhuria hiyo harusi. Si jambo lililo rahisi kwa mwanamume yeyote kufanya uamuzi na kitendo alichokifanya Mwasame. Hii ndiyo sababu msanii alisema kuwa alipiga moyo konde na akapata kuhudhuria hiyo harusi na hata kutoa zawadi yake kwa maharusi. Mhusika Mwasame alidhihirisha tabia ambazo hazingeweza kutoka kwa mwanamume yeyote wa kawaida. Mwasame alikuwa amempenda sana Salome lakini mwanzoni hakubahatika kumuoa.

Licha ya kutofanikiwa kumuoa Salome, Mwasame aliyafuatilia kwa karibu sana maisha ya Salome na Majoni. Majoni aliporejea kutoka Uganda, hali yake ya afya haikuwa nzuri. Alikuwa ameathirika na virusi vya ugonjwa wa UKIMWI ambavyo aliambukiza Salome baada ya kufanya mapenzi naye. Baada ya kifo cha Majoni, Mwasame alimrithi mjane mara moja na akafanya mapenzi naye. Matokeo yalikuwa kwamba, Mwasame pamoja na Salome wote waliangamia kwa sababu ya ugonjwa wa UKIMWI.

Maisha ya ndoa ya Majoni na Salome yalikabiliwa na changamoto muda mfupi baada ya kufanyika kwa harusi, hali iliyomfanya Salome kupigwa. Walipokutana na Salome,

Mwasame alitaka kujua sababu za zawadi yake kurudishwa. Mazungumzo yao hayakuisha vyema kwa vile Salome alimuonyesha Mwasame madharau aliposema:

**68.** *Aha! Unajifanya mjuaji, eeh! **Ila utaendelea kula mwande**, alitamka Salome kwa dharau. Salome alisonya na kukurupuka ghafla na kumwacha Mwasame kwenye mataa (Kiti cha Moyoni, uk. 82).*

Licha ya Salome kukataa kuolewa na Mwasame, aliweza kuhudhuria harusi ya Salome na Majoni na isitoshe akawapelekea zawadi. Mwasame alifuatilia kutaka kujua sababu za zawadi yake kukataliwa lakini Salome alijiona bora zaidi na hivyo alimdharau sana. Salome anasema, “**Ila utaendelea kula mwande.**” Matamshi haya yalitolewa na Salome kumlenga Mwasame akimaanisha kwamba angeendelea kupata shida maishani mwake. Kula mwande ni msemu unaotumiwa kwa maana ya kupata shida. Kinaya ni kwamba baada ya Salome kuanza kuugua, alihitaji msaada wa Mwasame. Mume wa Salome alipokuwa katika hali mbaya, alimuuliza Mwasame amsaidie kumpeleka hospitalini. Salome na Majoni walipougua, hakuna yeyote katika kijiji kizima aliyetaka kuwakaribia.

Mwandishi anasema kuwa Mwasame alizika aibu yake akajitolea mhanga kuwauguza wawili hao. Mwasame alijitolea kwa bidii sana kuuguza Salome na Majoni. Watu kijijini walikuwa wamekataa lakini kwa vile Mwasame alikuwa na roho safi, alijitolea kabisa kuwahudumia. Ingawa hivyo, wote waliangamia kutokana na athari ya ugonjwa wa UKIMWI.

Watunzi wote wa kazi zilizotumika katika utafiti huu waliishirikisha mbinu ya misemo katika kuuwasilisha ujumbe wao kuhusu UKIMWI, isipokuwa waandishi wa tamthilia za *Orodha* na *Kilio Chetu* ambao hawakuishirikisha mbinu ya misemo katika kupitisha ujumbe wao. Licha ya kutumia mbinu ya misemo kuwasilisha ujumbe

kuhusu UKIMWI, wasanii mbalimbali waliotumiwa katika utafiti huu walishirikisha matumizi ya mbinu ya mdokezo ambayo imeshughulikiwa katika sehemu inayofuata.

#### 4.1.7 Mdokezo

Katika sehemu iliyotangulia tumejadili mbinu ya misemo na namna ambavyo imetumiwa na wasanii mbalimbali kuwasilisha dhamira kuhusu UKIMWI. Katika sehemu hii, tutashughulikia mbinu ya mdokezo. Senkoro (2011) anaeleza kwamba mdokezo ni mtindo ambapo mwandishi hukatiza maneno au huacha kitu fulani bila kukitaja au maneno ambayo kwa kawaida ni wazi na huweza kujazwa kwa ubunifu wa msomaji. Sentensi za mdokezo humsaidia msomaji kujua hisia za mhusika fulani na hivyo kuweza kutabiri maudhui yanayowasilishwa kwake na mwandishi. Wasanii mbalimbali hutumia mtindo huu kwa kutimiza madhumuni mahsusi.

Katika utafiti wetu, mbinu ya mdokezo imetumiwa kwa kiwango fulani na wasanii wa maandishi teule yaliyotumika. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, mwandishi ameitumia mbinu hii katika baadhi ya sehemu za kazi yake. Katika mbinu hii, mzungumzaji hukatiza usemi akaachia msomaji akamilishe ili kupata maana ambayo mnenaji alilenga kuipitisha. Mfano wa kwanza umetumiwa na mwandishi katika mazungumzo kati ya mhusika Asha na Msafiri. Mtunzi anasema:

**69.** *Msafiri alikuwa amelewa, lakini alijitahidi kuongea kwa kupima kauli zake. Akauliza, wewe una mume? Hapana. Sipendi wanaume. Asha akajibu. Kwa nini? **Sipendi kuchungwa...sipendi utumwa (Ua la Faraja, uk.79).***

Katika dondoo hili, mbinu ya mdokezo imetumika na mwandishi ili kuwasilisha mawazo ya Asha. Asha ni mwanamke ambaye alipenda kukaa kwenye baa kwa madhumuni ya kuwanasa wanaume waliokuwa na pesa. Katika muktadha huu amekutana na mhusika aliyejulikana kama Msafiri. Msafiri alikuwa amelewa lakini alijaribu kuendeleza mazungumzo yake na Asha. Asha hakuwa na mume na

alipoulizwa na Msafiri sababu, akasema kwamba hapendi kuchungwa wala utumwa. Anasema, “*Sipendi kuchungwa...sipendi utumwa.*” Asha aliyaona maisha ya ndoa kama ya kifungo na utumwa. Hakutaka kuchungwa mara kwa mara na wanaume na anataka kuwa na maisha ambapo anafanya kila analotamani kufanya pasipo kizuizi chochote. Tabia ya Asha ilimfanya kufanya mapenzi na wanaume wengi kama vile Ngoma ambao walimuambukiza ugonjwa wa UKIMWI. Asha alipenda uhuru ndio maana anasema hapendi kuchungwa. Licha ya starehe za Asha, alilenga kuwapata wanaume ambao wangemtajirisha kifedha au kiuchumi. Wanaume wengi waliokuwa na mali walipenda kushiriki mapenzi na starehe ambazo zilichangia kuongezeka kwa visa vya maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi wa riwaya ya **Ua la Faraja** ametumia mifano kadha wa kadha ya mbinu ya mdokezo. Uhusiano kati ya Ngoma na familia yake ulikuwa umezorota sana kwa sababu ya tabia zake. Ilifikia kiwango ambapo alikosana na mwanawe Juma na hata kumkana kama mwanawe. Katika dondoo linalofuata, Grace na Omolo wanajaribu kumsihi Ngoma alegeze msimamo wake. Kuna matumizi ya mifano zaidi katika dondoo lifuatalo:

**70.** *Twajua Juma amekukosea...Grace alisema. Kosa kubwa...Ila wewe ni mzazi, sharti umsamehe... Omolo alishauri. Sisamehe! Juma siyo mwanangu. Sasa niambie bwana Omolo, utanisaidia kuuza hayo magari au hutanisaidia? (Ua la Faraja, uk.222).*

Katika dondoo lililonukuliwa hapo juu, mbinu ya mdokezo imetumiwa na mhusika Grace akimsihi Ngoma amsamehe mwanawe Juma. Grace anadokeza kwamba huenda Juma alikuwa amemkosea babake kwa njia nyingi kwa kufanya makosa mengi lakini inabidi Ngoma amsamehe mwanawe. Msanii anaitumia mbinu ya mdokezo anaposema, “*Kosa kubwa...Ila wewe ni mzazi, sharti umsamehe... Omolo alishauri.*”Juma alitofautiana na babake wakati alipokuwa akilazimishwa kwenda

mara kadhaa msikitini kuswali. Ilikuwa vigumu kwa Juma kutimiza hitaji hili hasa ikifahamika kwamba alilazimika kumsaidia mamake kununua bidhaa ambazo alikuwa anauza sokoni. Juma alifanya hivi mapema kabla ya kwenda shuleni. Ilibidi Juma amsaidie mamake kabla ya kwenda shule kwa maana Ngoma alikuwa ameidharau familia yake, licha ya kukataa kukimu mahitaji yake. Ngoma alikuwa akipata pesa nyingi zilizoishia katika ulevi na uasherati. Tabia hizi zilimfanya aambukizwe ugonjwa wa UKIMWI ambao alimsambazia mke wake. Shughuli ya kumsaidia mamake haingempa nafasi ya kwenda msikitini na isitoshe, hakumtarajia babake amwambie mambo ya kwenda msikitini kutokana na rekodi yake mbaya ya awali ya ulevi na uasherati. Omolo na Grace walikuwa katika harakati za kumsihi Ngoma amsamehe mwanawe Juma. Ngoma aliona ugumu sana kwa ushauri huu na akashikilia kwamba hawezi akamsamehe mwanawe Juma. Ngoma aliyasema haya ilhali afya yake ilikuwa ikiendelea kuzorota kila uchao.

Omolo alizidi kumshauri Juma aache tofauti zake na babake ili kuwe na uelewano baina yao. Awali Juma alikuwa ametofautiana na babake kufikia kiwango ambapo Ngoma alimkana na kumlaani mwanawe. Alipokuwa katika hali mbaya sana kwa sababu ya ugonjwa, alituma ujumbe wa kutaka kukutana na Juma. Mbinu ya mdokezo imetumika katika dondoo linalofuata:

**71.** *Huna sababu ya kutaka kufungua kesi. Maelewano mazuri baina yako na baba yako yanatosha. Amekuita, nenda ukasikilize alichokuitia. Yule mtu ni mgonjwa, hivi karibuni atakufa...(Ua la Faraja, uk.238).*

Katika muktadha huu, Omolo alikuwa anaongea na kijana Juma kuhusu mwaliko ambao alikuwa amepewa na babake Ngoma. Juma alikuwa amekataa mwaliko huo lakini Omolo anamshauri aende ili aone kile alichokuwa akiitiwa. Omolo anamsihi Juma awe na maelewano na babake badala ya kuanzisha kesi. Msanii anasema, “*Yule*

*mtu ni mgonjwa, hivi karibuni atakufa...*” Katika dondoo hili Omolo ana maana kuwa Ngoma alikuwa karibu kufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Ikiwa Ngoma angeaga dunia, basi Juma ndiye angekuwa mrithi wake. Juma alishauriwa kutoanza mizozo ya kesi na babake ila aende afanye maelewano naye. Kama kijana wa pekee wa mzee Ngoma, Juma ndiye alistahili kupokea urithi wa babake. Juma alishikilia msimamo mkali kutokana na tabia ambayo Ngoma alikuwa amedhihirisha kwa jamaa hususan kwa mamake. Licha ya kuidharau na kuipuuza, Ngoma alijihusisha na tabia ya uasherati na wanawake wengi kama vile Queen nje ya ndoa. Tabia hii ilimfanya Ngoma kumuambukiza mke wake Tabu ugonjwa wa UKIMWI. Kitendo hiki kilimtia Juma chuki na uchungu mkubwa sana kwa babake.

Mwandishi wa riwaya ya **Pendo katika Shari** vilevile ametumia mbinu ya mdokezo katika kuwasilisha ujumbe wake. Mumewe Pendo kwa jina Sulubu alikosa uaminifu katika maisha yake ya ndoa. Katika dondoo linalofuata, Pendo alikuwa mgonjwa na hivyo akalazwa hospitalini. Sulubu naye alitumia fursa hiyo kuendesha starehe zake kwa kuwaleta wanawake nyumbani ili kujihusisha nao katika mapenzi. Bi Sauda anasema:

**72.** *Ah! Pendo, singetaka mtengane na mumeo. Lakini yale ya kumleta hadi mwako nyumbani... nilisema potelea mbali nitakwambia. Leo hii huna budi kujua mbivu na mbichi dada. Bi Sauda alieleza. Usoni alionyesha huruma na machoni kajawa na tuhuma. Angalikuwa na njia angalimwauni Pendo (Pendo Katika Shari, uk.15).*

Katika dondoo hili, mbinu ya mdokezo imetumika pale ambapo Bi Sauda anamuelezea Pendo vituko ambavyo hufanywa na mumewe wakati yeye hayuko. Msanii anasema, “*Lakini yale ya kumleta hadi mwako nyumbani... nilisema potelea mbali nitakwambia.*” Bi. Sauda anasema kwamba Sulubu hufanya makosa mengi lakini lile la kuleta wanawake nyumbani kwake na kufanya nao mapenzi lilimkirihi sana na hangejizua kumueleza Pendo japo hakutaka watengane. Sauda alikuwa

akishuhudia visa na vituko vingi ambavyo vilikuwa vikifanywa na Sulubu. Aghalabu Sulubu aliyafanya haya yote wakati ambapo mkewe Tabu akiwa mbali. Sauda alimsikitikia Tabu kutokana na tabia ya uzinifu ya mumewe Sulubu. Sulubu ni kati ya wanaume waliokuwa wakiendeleza ubabadume ambao hawakuona mwanamke kama kitu cha maana machoni pao. Tabia hii ndiyo iliyosababisha akapata virusi vya ugonjwa wa UKIMWI.

Sulubu aliendeleza tabia yake ya uzinzi kwa kujihusisha na mapenzi na wanawake nje ya ndoa. Hii ni tabia ambayo Sulubu alikuwa akiifanya hadharani na kilele chake ni pale anapomleta mwanamke nyumbani kwake wakati ambapo Pendo alikuwa amelazwa hospitalini. Sulubu tangu mwanzo hakutaka kwenda hospitalini kupimwa kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Alikuwa akisumbuliwa na mawazo na hofu ya kuwa na virusi vya UKIMWI. Hali yake ilipozidi kudhoofika, aliamua kutembelea daktari ili amfanyie uchunguzi wa kimatibabu. Mbinu ya mdokezo katika riwaya ya *Pendo Katika Shari* imetumika katika kurejelea hali ambapo Sulubu alikuwa hospitalini. Msanii anasema:

**73.** *...wale madaktari wenziwe walimkabidhi vijitabu kadha ili akavisome na kuelewa vyema jinsi anavyopaswa kuishi. Sulubu alivitazama na kutikisa kichwa huku akitutuma, **No this cant be... Why me? Hii haiwezekani...?** Kisha machozi yakaanza kumtoka mfululizo (**Pendo katika Shari, uk.51**).*

Sulubu alipofanyiwa uchunguzi, ilipatikana kwamba alikuwa na virusi vya UKIMWI. Hakutaka kuyakubali matokeo ya uchunguzi huo na ndiyo sababu katika dondoo hili anasikika akisema, “*No this cant be... Why me? Hii haiwezekani...?*” Sulubu anakana kwamba haiwezekani kuwa yeye alikuwa amepatikana na virusi vinavyosababisha ugonjwa wa UKIMWI. Sulubu alikuwa katika hatua inayojulikana kama ya kukana kwa maana aliamini kuwa watu wengine waliweza kuambukizwa UKIMWI lakini si yeye. Madaktari walimpa ushauri na vitabu kadhaa ambavyo



alihitajika avisome ili vimsaidie afahamu namna ya kuishi na virusi vya UKIMWI. Sulubu aliendeleza vitendo vya uzinifu akisahau kuwa ugonjwa wa UKIMWI unaweza kumpata yeyote yule, awe tajiri au maskini; aliyesoma na asiyesoma.

Kutokana na mdafoa wa ujitokezaji kwenye jedwali 4:1 inaonekana kwamba kuna baadhi ya mbinu za lugha na tamathali za usemi zinazotumika zaidi na waandishi wa riwaya ikilinganishwa na zingine. Aidha, kuna waandishi wanaotumia mbinu nyingi zaidi kuwasilisha ujumbe wao ikilinganishwa na wengine. Kulingana na utafiti huu, mbinu zilizotumika kwa kiwango cha juu na waandishi kuwasilisha ujumbe wao ni: tashbihi, kuchanganya ndimi, methali, taswira, misemo na mdokezo. Mbinu ambazo hazikutumika kwa wingi na ambazo mdafoa wao wa ujitokezaji ni wa kiwango cha chini ni pamoja na: Balagha, wimbo/ushairi, barua, lafudhi miongoni mwa nyingine.

Aidha, waandishi wa riwaya za *Ua la Faraja* na *Kala Tufaha* ndio waliobobea zaidi katika matumizi ya mbinu za lugha na tamathali za usemi. Waandishi wa riwaya za *Pendo Katika Shari* na *Sitaki Iwe Siri* walitumia mbinu chache sana. Ukirejelea jedwali la 4:1, utagundua kwamba kuna baadhi ya mbinu kama vile balagha, nyimbo, tanakali za sauti, barua na lafudhi ambazo hazikutumiwa na waandishi hawa na kama zilitumika, basi zilitokea mara mojamoya tu.

Katika tamthilia ya **Orodha**, mwandishi ametumia mbinu mbalimbali za lugha na mojawapo ya mbinu ambayo imetumika na kutawala tamthilia hiyo ni mdokezo. Mbinu ya mdokezo imetumika pakubwa katika tamthilia ya **Orodha**. Mwandishi ametumia mbinu hii tunapoyazingatia mazungumzo ya Mama Furaha katika sehemu ya mwanzo wa tamthilia. Mwandishi anatumia:

**74.** *Mama Furaha: Yalikuwa maombi yake ya mwisho kabla ya kufa, kwamba niseme maneno machache... hakika, hutanikatalia hilo, Padri!... Asante (Akijiweka sawa)... Familia yangu... wanakijiji,*

*asanteni kwa kuhudhuria hii leo. Siku ya huzuni ya mazishi ya binti yangu mpendwa. Furaha... (Orodha, uk.2).*

Katika dondoo hili, mwandishi ametumia mbinu ya mdokezo kuashiria maneno yaliyokuwa katika barua iliyoandikwa na marehemu Furaha. Msanii anasema, *“Yalikuwa maombi yake ya mwisho kabla ya kufa, kwamba niseme maneno machache... hakika, hutanikatalia hilo, Padri!... Asante (Akijiweka sawa)... Familia yangu...* Mhusika Furaha aliandika orodha ambayo alitaka isomwe siku ya mazishi yake. Alitaka orodha hii isomwe ili jamii ifahamu kile kilichosababisha kifo chake, ndipo ichukue hatua za tahadhari. Katika tamthilia ya *Orodha*, msanii ameyasawiri maisha ya mhusika Furaha na kuonyesha namna ambavyo alikosa maadili mema katika jamii. Furaha alijiingiza katika maisha ya uasherati na alikuwa akiwabadilisha wanaume kama tambara bovu. Msanii anatuonyesha namna Furaha alivyokuwa na uhusiano wa kimapenzi na Ecko, Salim, Kitunda na Padri James.

Matokeo ya uhusiano wake wa kiholela ni kuwa aliambukizwa virusi vya UKIMWI. Kwa vile alikuwa na orodha ndefu ya wanaume, haikujulikana ni nani kati yao aliyemuambukiza ugonjwa wa UKIMWI. Orodha ambayo aliandika isomwe katika mazishi yake iliwatia hofu na kuwahangaisha sana wanaume wote waliokuwa na uhusiano wa kimapenzi naye. Padri James alikuwa kati ya wanaume ambao walihangaishwa sana na orodha ambayo Furaha aliandika akataka isomwe siku ya mazishi yake. Padri na wengine walidhani kuwa majina yao yangesomwa kwenye mazishi lakini badala yake sababu zinazosababisha UKIMWI zilisomwa kwa ujumla.

Katika sehemu ya tatu ya mchezo wa **Orodha**, mwandishi ametumia mbinu ya mdokezo anapowasilisha mazungumzo ya baba. Mhusika huyu alikuwa akilalamika kwa vile alikuwa akishughulika sana kufanya kazi shambani ili kuilisha jamaa yake lakini watoto wake hawakujali hata kumsaidia. Anadai kwamba watoto walikuwa tu

wanyonyaji tu kwani hawakutaka kufanya kazi zozote ila walimuachia yeye tu.

Anasema:

**75.** *Baba: Kweli! Haiwezekani! Kutwa ninafanya kazi kwa bidii kwenye ardhi yetu ili tuyalishe matumbo yetu... (akigutia). Mama Furaha, chakula changu kiko tayari! Karibu nitakufa njaa hali nyie mbu wadogo mwaionyonya damu yangu yote!(Orodha, uk.4).*

Katika dondoo lililo hapo juu, mhusika Baba alikuwa amechoshwa na tabia za watoto wake wa kike hususan Furaha. Anasema, “***Kweli! Haiwezekani! Kutwa ninafanya kazi kwa bidii kwenye ardhi yetu ili tuyalishe matumbo yetu...***” Baba anasema kuwa yeye alifanya kazi kwa bidii shambani ili kuwalisha wasiwe na njaa au upungufu wowote lakini watoto hawakuonyesha ishara ya kujali. Furaha aliyetarajiwa kutoa mwongozo kwa dada zake wadogo alijihusisha na wanaume. Baba alijibidiisha sana shambani ili kuhakikisha kwamba anailisha familia lakini juhudi zake hazikutambuliwa na jamii yake. Furaha hakuwa kielelezo kwa wenzake wadogo lakini badala yake aliamua kuishi maisha ya raha mustarehe ambayo hatimaye yalimletea balaa ya kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

Katika sehemu ya kumi na nane, mwandishi ametumia tena mbinu ya mdokezo tunapoyaangalia mazungumzo ya Mama Furaha. Padri alikuwa akiongea na mama Furaha akimsihi asiisome orodha ambayo Furaha alitaka isomwe siku ya mazishi yake. Padri alikuwa anadai kuwa kusoma orodha hiyo kungevuruga sherehe ya mazishi ya Furaha. Mwandishi anatueleza:

**76.** *Mama Furaha: Nisingependa ufanye hivyo, iwapo hutajali, Padri: Furaha alitaka isomwe na kusikiwa kwa mara ya kwanza kwenye mazishi. Hata sisi hatujaisoma... (Orodha, uk.36).*

Katika muktadha huu, Mama Furaha anazungumza na Padri kuhusu siku ya mazishi ya Furaha. Mama Furaha alikuwa anamueleza Padri kwamba kuna orodha ambayo iliandikwa na marehemu ambayo wao wenyewe hawakuwa wameiona au kuisoma.

Anasema, “*Hata sisi hatujaisoma...*” Yalikuwa mapenzi ya marehemu kwamba orodha ile ifunguliwe na kusomwa kwa mara ya mwanzo kabisa kwenye siku ya mazishi. Orodha iliyoandikwa ilipaswa kutumiwa kama funzo kwa jamii ili wajue ni kitu gani kilichomuua Furaha. Kauli hii ilimtia tumbo joto Padri ambaye pia alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Furaha. Padri aliamini kuwa orodha ya majina ya wanaume waliokuwa na uhusiano wa kimapenzi na marehemu ndiyo ambayo ingesomwa. Padri alisumbuliwa kwa sababu hakujua vile hali ingekuwa iwapo jina lake lingesomwa miongoni mwa mengine. Yeye alistahili kutoa ushauri wa kiroho kwa waumini lakini inasikitisha kwamba hata yeye alijihusisha na suala la mapenzi na Furaha.

Jamii inayosawiriwa na msanii ilikuwa imeoza kimaadili kwa maana Furaha alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume zaidi ya watano. Tabia hii ndiyo iliyochangia pakubwa katika kumfanya Furaha aambukizwe virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Mbinu ya mdokezo pia imetumika katika sehemu zingine za tamthilia. Hii ni mifano michahe tu lakini katika tamthilia nzima mbinu ya mdokezo imetumika pakubwa kumwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake hususan kuhusu UKIMWI.

Mwandishi wa tamthilia ya **Kilio Chetu** ameshirikisha matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha. Mbinu ambayo imetumika kwa kiwango kikubwa kuliko zingine ni mdokezo. Tulishaeleza pale mwanzo katika sehemu ya kwanza ya sura hii kwamba mdokezo ni mtindo ambapo mwandishi hukatiza maneno ambayo kawaida ni wazi na huweza kujazwa kwa ubunifu wa msomaji. Mwandishi wa tamthilia ya *Kilio Chetu* ametumia mbinu hii akirejelea namna watu katika jamii inayozungumziwa wameathirika vibaya na ugonjwa wa UKIMWI. Katika dondoo lifuatalo mtunzi anasema:

**77.** *Watu walitoka upele, wengine waliharisha, mara nywele kunyonyeka na vifo kufuatia. Watu walipukutika, wakupukutika, kama majani ya kiangazi. Wakapukutika... (Kilio Chetu, uk.1).*

Katika muktadha huu mwandishi ametumia mbinu ya mdokezo kubainisha athari na madhara ya ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi anasema, “*Watu walipukutika, wakupukutika, kama majani ya kiangazi. Wakapukutika...*” Mwandishi ameonyesha baadhi ya dalili za ugonjwa wa UKIMWI ambazo zilisababisha waathirika kufariki kwa kiwango kikubwa sana. Ugonjwa wa UKIMWI uliwaua watu wengi sana ndio sababu mtunzi anatoa ulinganisho na kupukutika kwa majani wakati wa kiangazi. Ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa na dalili nyingi na baadhi ya dalili ambazo msanii amezitaja ni kutoka upele, kuharisha na nywele kunyonyeka. Ugonjwa wa UKIMWI uliivamia jamii iliyorejelewa vibaya kwani ulisababisha mauaji ya watu wengi sana. Msanii analinganisha vifo vilivyokuwa vikitokea kutokana na athari ya UKIMWI na kupukutika kwa majani wakati wa kiangazi.

Jamii inayorejelewa katika tamthilia ya **Kilio Chetu** ilikuwa imefungwa na kaida za kitamaduni za Kiafrika. Katika utamaduni wa Kiafrika uliozingatiwa, iliaminika kuwa ilikuwa mwiko kwa wazazi kuzungumza na watoto wao kuhusu masuala ya mapenzi na ngono. Tamaduni kama hizi zimepotoka na hazina nafasi katika ulimwengu wa sasa. Mtunzi wa tamthilia ya *Kilo Chetu* pia ametumia mbinu hii ya mdokezo katika dondoo lifuatalo. Anasema:

**78.** *Na toka lini jamii yetu ikaruhusu kukalishana kitako na vitoto ukivieleza habari ya ngono? Mie nikae hapa nafungua kinywa changu (Anaigiza): Sasa wanangu mfanye hivi... na vile na vile mimba itatokea... uchuro huo! (Kilio chetu, uk.12).*

Katika dondoo hili, mhusika Mama Suzi ametumia mbinu ya mdokezo katika uzungumzi wake. Yeye na Baba Joti wanapinga kabisa mtazamo wa jamii ya sasa wa kuwapa mafunzo watoto kuhusu masuala ya ngono. Mwandishi anasema, “*Sasa*

*wanangu mfanye hivi... na vile na vile mimba itatokea... uchuro huo!”* Mama Suzi haoni namna ambavyo anaweza kuketi chini na mtoto wake wazungumzie kuhusu ngono na kile ambacho kinaweza kufanyika iwapo mtoto wake wa kike angekuwa amepachikwa mimba. Analiona kama jambo la aibu yeye kukaa na mtoto wake wa kike au kiume kuzungumzia suala la ngono ama mapenzi. Wanalinganisha kitendo kama hicho na tabia ya uchuro. Msimamo wa kizazi kinachotajwa ndio unaochangia pakubwa kuharibika kwa vijana. Ikiwa wazazi hawatakuwa huru kutoa ushauri kwa watoto wao, ni nani basi atalichukua jukumu hili?

Hali kama hii ndiyo inayowafanya vijana kujiamulia wenyewe na kujihusisha na matendo maovu kwa sababu ya kukosa mwelekeo na ushauri mwema. Mbinu hii imetumika pakubwa na mtunzi wa tamthilia ya *Kilio Chetu* kuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji. Katika sehemu hii, tumeangalia namna ambavyo mbinu ya mdokezo imetumiwa na waandishi mbalimbali kupitisha ujumbe wao. Kiwango cha matumizi ya mbinu hii hutofautiana kutoka msanii mmoja hadi mwingine. Katika sehemu inayofuata tumeangalia nafasi ya mbinu ya sitiari katika kuliibua suala la UKIMWI kupitia kazi teule zilizotumika katika utafiti huu.

#### **4.1.8 Sitiari**

Katika sehemu iliyotangulia, tuliangalia namna wasanii tofauti wametumia mbinu ya mdokezo kuwasilisha ujumbe wao kuhusu UKIMWI. Katika sehemu hii, tutashughulikia mbinu ya sitiari. Mulokozi (2002) anaeleza kwamba sitiari ni mbinu inayotumika kuumba picha fulani au inayoamsha mwitikio fulani kutoka kwa hadhira. Hii ni tamathali ya usemi ambayo hulinganisha watu na vitu vingine kana kwamba ni sawa. Katika mbinu hii kuna uhamishaji wa maana kutoka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine.

Katika tamthilia ya **Kilio Chetu**, mwandishi ametumia tamathali ya usemi ya sitiari kuwasilisha ujumbe wake. Kusudi la kutumia mbinu hii ni kutoa ulinganishi wa vitu au mambo mbalimbali kutoka kwa mazingira yanayofahamika. Janga la UKIMWI lilikuwa limeivamia sana jamii inayorejelewa na hivyo msanii anatumia mbinu ya sitiari ili wanajamii waone uzito wa tatizo linalowakabili. Katika tamthilia, msanii ametumia mfano wa dubwana ambacho ni kiumbe kikubwa sana kufanya ulinganishi.

Mwandishi anasema katika dondoo lifuatalo kuwa:

**79.** *Kulikuweko matajiri na kulikuwepo na maskini. Watu waliishi kwa furaha. Punde dubwana kubwa likakiingilia kisiwa kile na kukawa kutafutana. (Aigiza) **Dubwana likaleta balaa kisiwani. Kila aliyeguswa na dubwana alidhurika. Watu walitoka upele, wengine waliharishwa, mara nywele kunyonyoka na vifo vikafuatia (Kilio Chetu, uk.1).***

Katika dondoo lililonukuliwa hapo juu, mtunzi ametumia ulinganishi au sitiari ya dubwana. Anasema, “***Dubwana likaleta balaa kisiwani. Kila aliyeguswa na dubwana alidhurika. Watu walitoka upele, wengine waliharishwa, mara nywele kunyonyoka na vifo vikafuatia.***” Tunafahamu kuwa dubwana ni kiumbe kikubwa sana kinachonasibishwa na jitu. Katika muktadha huu, dubwana limelinganishwa na ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi anaonyesha namna ugonjwa huu unavyoathiri maisha ya watu kwa kuwaua. Vifo vingi vimetokea katika kisiwa kilichotajwa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Katika kisiwa kinachorejelewa kulikuwa watu wa tabaka mbalimbali, maskini kwa matajiri. Mwandishi anasema kuwa dubwana lilileta balaa kisiwani na halikubagua kati ya maskini na tajiri. Hii ina maana kuwa ugonjwa wa UKIMWI ulipoingia katika kisiwa kinachorejelewa, ulisababisha balaa na madhara makubwa kwa kila mtu. Mwandishi anasema kwamba yeyote aliyeupata ugonjwa wa UKIMWI alidhurika vibaya sana. Baadhi ya ishara zilizotokea baada ya watu kudhurika na

dubwana hili ni pamoja na; kutoka upele, kuhasiriwa, kunyonyoka kwa nywele na kadhalika. Kilele cha yote ni vifo vingi vilivyotokea kwa wahasiriwa wote wa ugonjwa wa UKIMWI. Sitiari ya dubwana imetumiwa vyema na msanii wa tamthilia husika ili kuliibua suala la UKIMWI.

Katika tamthilia ya **Kilio Chetu**, mwandishi aidha ameshirikisha sitiari anuwai katika uwasilishaji wake wa ujumbe. Baadhi ya sitiari zifuatazo zimetumika wakati ambapo Joti alijihusisha katika kufanya ngono na Suzi. Vijana wa chuo kikuu walikosa maadili mema na hivyo wakajingiza katika visa vya kufanya mapenzi kiholela. Tabia hii ya ukosefu wa maadili mema iliwadhuru baadhi yao kiasi cha kutopata faida ya masomo ya chuo kikuu. Mwandishi anasema:

**80.** *Ulitumia kondomu? Shiti wewe. Nini kondomu bwana. **Pekupeku tu.** (Kwa dharau) Unaweza **kula pipi na ganda lake** wewe? Sasa tuone basi. Leo mtoto kanitolea nje kabisa tena mkali pilipili si kitu (**Kilio Chetu, uk.19**).*

Katika muktadha huu kuna matumizi ya sitiari mbili. Sitiari ya kwanza ni **pekupeku** ambapo mhusika Joti alifanya mapenzi na Suzi bila kinga. Hakuvaa mpira au kondomu wakati ambapo alikuwa anajamiana na Suzi. Kutokana na maongezi ya Joti, ulikuwa ujinga au upumbavu mtupu kutumia mpira au kondomu. Vijana wengi waliamini kuwa mtu hangeweza kufurahia ngono iwapo alitumia kinga kwa maana wao wanaamini kuwa mpira ni kama kizuizi cha kuwatenganisha. Hali kama hii ndiyo inayochangia maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa.

Aidha katika dondoo hili, mtunzi ametumia sitiari '**kula pipi na ganda lake**'. Mwandishi anamaanisha kufanya mapenzi ukitumia mpira unaolinganishwa na ganda la pipi. Mhusika Joti anasema kuwa hawezi akafanya mapenzi akiwa amevaa mpira au pipi kwa vile hangefurahia. Analinganisha na ulaji wa peremende au pipi ambapo mtu hawezi kuupata utamu wa peremende iwapo ataila pamoja na ganda. Matendo haya ya



Joti kufanya mapenzi na wasichana wengi bila kinga ndiyo yaliyosababisha akapatwa na ugonjwa wa UKIMWI na hatimaye akafariki. Baadhi ya watu katika jamii hawachukui tahadhari kutumia mipira au kondomu wakifanya ngono kwa kisingizio kuwa wakifanya hivyo hawatafurahia tendo la ngono. Hali kama hii ndiyo huchangia maambukizi na maenezi mengi ya ugonjwa wa UKIMWI.

Katika tamthilia ya **Orodha**, msanii aidha ameshirikisha matumizi ya mbinu ya sitiari katika uwasilishaji wa dhamira zake kuhusu UKIMWI. Katika matumizi ya mbinu hii, ujumbe huwa unafumbwa na inabidi msomaji atafakari ndipo apate maana inayorejelewa na mwandishi. Katika tamthilia ya *Orodha*, wahusika mbalimbali wametumiwa na mtunzi kuwasilisha ujumbe kuhusu UKIMWI. Mwandishi ametumia sitiari ya mbu katika dondoo lifuatalo. Anasema:

**81.** *Baba... Mama Furaha, chakula changu kiko tayari! Karibu nitakufa njaa hali nyie mbu wadogo mwainyonya damu yangu yote! (Orodha, uk.4).*

Katika dondoo hili, mwandishi anasema, “*Karibu nitakufa njaa hali nyie mbu wadogo mwainyonya damu yangu yote!*” Baba anawalinganisha wasichana wake na ‘mbu’. Mbu hufyonza damu ya wanadamu na hivyo Baba anawalinganisha kwa maana hawakuleta manufaa yeyote katika jamii. Badala yake, wasichana kama Furaha walijihusisha na uhusiano wa mapenzi jambo ambalo linamfanya apate virusi vya UKIMWI. Furaha anaweza kulinganishwa na mbu kwa maana hakuleta faida kwa jamii ila hasara kwani alipopata ugonjwa wa UKIMWI, walianza kumshughulikia kwa upande wa matibabu. Furaha hakutosheka na mwanamume mmoja bali alifurahia kuwa na wanaume wengi. Ni kweli anavyosema babake Furaha kwa sababu baada ya Furaha kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI, jamii ilitumia pesa nyingi

kumshughulikia kimatibabu na hivyo badala ya kuiletea jamii faida alikuwa kama mbu ambaye alikuwa anaifyonza damu yao na hivyo kuwapa hasara.

Katika sehemu ya tano ya tamthilia ya **Orodha**, mwandishi pia ametumia ‘ua’ kama sitiari. Ua ni sehemu ya mti inayonawiri sana mti unapochanua na kutoa maua yake. Aghalabu, urembo wa wasichana huwa unalinganishwa na ‘ua’. Urembo huo hata hivyo huwa haudumu milele kwani, baada ya muda huwa unapungua sawa na ambavyo ua katika mti hunyauka. Katika dondoo linalofuata, Bwana Ecko anamlinganisha Furaha na ‘ua’. Mwandishi anatueleza:

**82.** *Bw Ecko: Tafadhali mpenzi niite... (Anambusu mkono wake) Chaka! Nani ambaye hajapata kuliona ua hili zuri likizungukazunguka kijijini! Umenenepa mno, mpenzi... na katika sehemu zote zinazostahili! (Furaha anasifiwa na amefurahi) (Orodha, uk.6).*

Katika dondoo hili, Ecko anatumia sitiari ya ‘ua’ kumrejelea mhusika Furaha. Mtunzi anasema, “*Nani ambaye hajapata kuliona ua hili zuri likizungukazunguka kijijini!*”

Bw. Ecko anampa Furaha sifa kutokana na urembo aliokuwa nao. Ecko anasema kuwa Furaha alikuwa amenenepa katika sehemu zote zinazostahili. Mary na Furaha walikuwa wametoroka nyumbani kwenda kukutana na wanaume usiku. Ecko alikuwa anausifu uzuri wa Furaha ndipo alipomlinganisha na uzuri wa ua. Ecko ni mfano wa wanaume ambao wanatumia uwezo wao wa kiuchumi kuwashawishi wasichana wadogo kufanya mapenzi naye. Furaha alipewa sifa za uongo na Ecko zilizomfurahisha sana. Furaha alijihusisha katika mapenzi na wanaume wengi waliomzidi umri kwa umbali na hali hii ndiyo iliyochangia yeye hatimaye kuambukizwa virusi vya ugonjwa wa UKIMWI na mwishowe kifo chake. Kwa ujumla, mwandishi wa tamthilia ya *Orodha* hakushirikisha matumizi mengi ya tamathali za usemi ila alitumia lugha ya kawaida. Mbinu zingine ambazo zilitumiwa japo kwa kiwango kidogo sana ni pamoja na tabaini, utohozi na taswira.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, mtunzi ameshirikisha matumizi mbalimbali ya sitiari. Ngoma ni kati ya wanaume ambao maadili yao katika jamii yalikuwa yameporomoka sana. Mhusika huyu alikuwa na mke na watoto katika jamii yake lakini alishiriki tabia ya ulevi na uasherati kwa fujo. Matendo haya yalifanywa bila kuijali jamii. Tabia ya Ngoma iliundekeza ubabadume ambapo mume hakumthamini mke wake ila alimuona tu kama chombo cha kutumiwa. Katika dondoo linalofuata, msanii alithibitisha kauli hii anaposema:

**83.** *Nani akutake wewe na hali umeshakokoteza mbegu za umeme mji mzima? (Ua la Faraja, uk. 76).*

Mhusika Chiku aliyasema maneno haya akiwa na Omolo kwenye baa wakati Ngoma alipokuja kuwakaribia. Sitiari iliyotumika katika dondoo hili ni, *“umeshakokoteza mbegu za umeme mji mzima?”* Msanii anatumia sitiari ya kukokoteza mbegu za umeme mji mzima kuwa na maana kwamba Ngoma alikuwa na virusi vya UKIMWI na alikuwa akivisambaza katika mji wote.

Ngoma alijihusisha katika kufanya ngono na wanawake wengi kama vile Queen na tabia hii ikachangia katika kumfanya aambukizwe virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Chiku aliyasema maneno haya kwa maana alielewa tabia ya uzinifu ya Ngoma ambayo ilikuwa imeletea watu wengi madhara katika jamii. Ngoma alikataa kuishughulikia jamii yake na badala yake akajiingiza katika ulevi wa kupindukia na kufanya mapenzi kiholela na wanawake wengi. Ngoma alimuambukiza mke wake asiyekuwa na hatia ugonjwa mbaya wa UKIMWI uliosababisha kifo chake. Ngoma naye baadaye aliathirika na UKIMWI na mwishowe akaaga dunia.

Kwa ujumla katika sura hii, mbinu mbalimbali zimeonyeshwa kama zilivyotumiwa na wasanii kuwasilisha dhamira zao kuhusu UKIMWI. Pamoja na mbinu zilizotajwa, utafiti huu ulibaini kwamba watunzi kadha walitofautiana katika mbinu

walizopendelea kutumia ikilinganishwa na wengine. Kwa mfano, Matundura (2008) katika riwaya ya *Sitaki Iwe Siri* alitumia kwa wingi sana tashbihi na methali kupitisha ujumbe wake. Mkufya (2005) katika riwaya ya *Ua la Faraja* alitumia pakubwa mbinu ya tashbihi ikifuatwa na sitiari. Omar (2007) katika riwaya ya *Kala Tufaha* alitumia pakubwa misemo na nahau ikifuatwa na tashbihi ilhali Momanyi (2008) alishirikisha matumizi ya tashbihi ikifuatwa na misemo katika uwasilishaji wake wa ujumbe. Mwandishi wa tamthilia ya *Kilio Chetu* alishirikisha zaidi matumizi ya mbinu ya mdokezo ikifuatwa na sitiari. Jilala (2004) katika tamthilia ya *Giza* naye alishirikisha zaidi matumizi ya mbinu ya kuchanganya ndimi ikifuatwa na balagha.

#### **4.2 Hitimisho**

Sura hii imehakiki kwa kina mitindo ya uandishi iliyotumika katika maandishi teule ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Katika sura hii imebainika kwamba mbinu za lugha na tamathali za usemi zifuatazo ndizo zilizotumiwa na waandishi takriban wote kwa wingi kuwasilisha ujumbe wao kuhusu UKIMWI. Mbinu hizo ni pamoja na: tashbihi, kuchanganya ndimi/kubadili msimbo, methali, taswira, misemo, mdokezo na sitiari. Mbinu zilizotumiwa na wasanii mbalimbali zimewawezesha kuwasilisha dhamira za UKIMWI katika kazi teule zilizotumika katika utafiti huu. Sura hii aidha imebaini upekee wa waandishi katika utunzi wa kazi zao za kisanii. Sura inayofuata imejadili dhamira kwenye maandishi teule yaliyotumika katika utafiti huu.

## SURA YA TANO

### DHAMIRA KATIKA MAANDISHI TEULE KUHUSU UKIMWI

#### 5.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilihakiki mitindo ya uandishi iliyotumika katika maandishi teule ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Sura hiyo iliweza kubainisha mbinu za lugha na tamathali za usemi zinazotumiwa kwa wingi na waandishi wengi kama vile tashbihi, kuchanganya ndimi, methali, taswira, misemo, mdokezo na sitiari. Aidha, sura hiyo ilionyesha upekee wa wasanii katika utunzi wa kazi zao. Katika sura hii, tumejadili na kubainisha dhamira mbalimbali zinazowasilishwa kwenye kazi teule za fasihi andishi kuhusu UKIMWI. Miongoni mwa dhamira hizo ni; kuporomoka kwa maadili ya jamii, unyanyapaa, utamaushi, dhuluma dhidi ya wanawake, usiri kuhusu UKIMWI, athari ya UKIMWI na ukosefu wa uwajibikaji.

#### 5.1 Kuporomoka kwa Maadili ya Jamii

Kila jamii huwa na kaida, desturi na maadili yanayoiongoza katika shughuli zake za kila siku. Maadili hayo huwa yamekubalika katika jamii na hivyo mwanajamii yeyote akifanya kinyume chake huwa amekiuka maadili hayo. Waandishi tofauti wa kazi zilizotumika kwenye utafiti huu wameangazia suala la kuporomoka kwa maadili ya jamii. Mwandishi wa riwaya ya *Ua la Faraja* ameangazia suala hili anapojadili tabia ya uasherati miongoni mwa wanajamii. Uasherati ni kitendo cha kufanya ngono kiholela na wahusika kadha wa kadha hali inayokiuka maadili ya jamii. Kitendo hiki kwa mujibu wa mwandishi wa riwaya hii kinachangia pakubwa maenezi ya ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi anaonyesha jinsi jamii inayozungumziwa ilijhusisha na matendo yaliyoendeleza uasherati katika jamii. Mwandishi anasema:

- 84.** *Asha aliingia, alikuwa pekee yake. Watu walimkodolea macho. Katika miaka ile ulikuwa msimu wa wanaume kupenda wanawake wanene, wenye matako makubwa na kifua kilichojaa maziwa. Asha alikuwa na kila sifa ya umbile hilo. Mwili wake mnene wenye matako yaliyojaa ulijiweka vizuri kwenye nguo ile ya aina yake. Alipotembea, matako yakiangukiana kwa utepetepe huku yakitingisika kwa mdundo na mwendo wake. Alijijua alivyo na alifanya kila jitihada kuwaonyesha wanaume waliotazama umbile lake (Ua la Faraja, uk.9-10).*

Kutokana na dondoo lililo hapo juu, inabainika kwamba jamii hii ilikuwa imeoza kimaadili. Mtunzi anasema, ulikuwa msimu wa **“wanaume kupenda wanawake wanene, wenye matako makubwa na kifua kilichojaa maziwa.”** Hii ina maana kwamba fikra za wanaume katika jamii inayozungumziwa zilikuwa tu kuhusu masuala ya wanawake na ngono. Matendo yanayoonyeshwa na mhusika Asha yalikusudiwa kuwanasa wanaume ili wajihusishe na uasherati. Mwandishi anasema kuwa, **“alipotembea, matako yakiangukiana kwa utepetepe huku yakitingisika kwa mdundo na mwendo wake. Alijijua alivyo na alifanya kila jitihada kuwaonyesha wanaume waliotazama umbile lake.”** Asha aliyafanya haya yote kimaksudu kwa maana alijua wanaume walikuwa wamemuangalia.

Kupitia kwa mfano uliotolewa katika dondoo lililotumika hapo juu, jamii inayorejelewa katika maandishi ya *Ua la Faraja* imeoza kimaadili. Matendo kama haya yalichangia pakubwa katika kusambaza ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi aidha anatuonyesha kuwa jamii inayozungumziwa ilipenda sana kufanya ngono. Kuna wahusika Pendo na Chiku wanaosema kuwa iwapo mtu anaogopa magonjwa basi aache kufanya ngono. Hii ina maana kwamba watu walipaswa kufanya ngono pasipo uoga wowote. Kulingana na Pendo na Chiku, watu walistahili kufanya ngono pasipo kinga yoyote. Mtunzi anasema:

- 85.** *Pendo na Chiku wakamshambulia, na wewe Yakobo unampa kichwa azidi kutupigia kelele! Mtu kama aogopa magonjwa achana na ngono! Ya nini kuvalishana mipira? (Ua la Faraja, uk.12).*

Inasikitisha kwamba wahusika Pendo na Chiku wanataka watu wajiingize katika mapenzi au kufanya ngono pasipo kinga. Pendo na Chiku wanasema, “*Mtu kama aogopa magonjwa achana na ngono! Ya nini kovalishana mipira?!*” Wahusika hawa hawakufurahishwa na tabia ya Jose ambaye alikuwa akifanya biashara ya kuuza kondomu. Wanadai kuwa Jose alikuwa akiwapigia kelele alipokuwa ananadi biashara yake. Kwa maoni yao, watu hawawezi kufurahia tendo la ndoa iwapo watatumia mipira. Wanamlaumu Yakobo kwa kununua mipira ya kondomu kwa maana waliamini alisaidia kufanya Jose azidi kuwa na kichwa kwa kuwapigia kelele zaidi. Wahusika hawa wanakashifu Jose na wengine wanaojihusisha katika biashara ya kuuza mipira au kondomu. Matendo kama haya ndiyo yanayoendeleza ugonjwa wa UKIMWI katika jamii. Kulingana na Pendo na Chiku, kama mtu anaogopa magonjwa inapaswa aachane na ngono. Hawakuona haja ya watu kovalishana mipira. Ni vigumu kufahamu nia ya wahusika hawa kwa maana walionunua mipira hawakuwa wanafanya tendo la ngono nao. Matendo ya Chiku na Pendo ya kutaka watu wafanye ngono pasipo kinga yanathibitisha kuporomoka kwa maadili ya jamii inayorejelewa.

Mwandishi aidha anaiendeleza dhamira yake kwa maana kwenye sinema na miziki yote ya Kiafrika, matendo ya mapenzi na ngono ndiyo yanayoshabikiwa. Mhusika Jose ni kati ya watu wachache ambao hawakufurahishwa na tabia hii na alipendekeza kwamba ilipaswa kupigwa vita. Inasikitisha kwamba sinema na miziki yoyote ya Kiafrika haikupitisha ujumbe mwingine muhimu zaidi ila matendo ya mapenzi na ngono. Si ajabu kwamba raia wengi kutoka kwa mataifa ya Kiafrika wameathirika zaidi na ugonjwa wa UKIMWI. Anasema:

**86.** *Mimi naona ni busara zaidi kupiga vita tabia ya watu kushabikia ngono. Kwenye sinema, kwenye miziki yote ya Kiafrika, kila Mahali ni hamasa ya ngono. Muziki umekosa maana zaidi ya kunengua na*

***kuonyesha uhodari wa viuno vya ngono. Pigeni vita ushabiki na sanaa ya kushabikia ngono (Ua la Faraja, uk.13).***

Jamii hii ilifurahia sana kunywa pombe na kujihusisha na masuala ya kucheza dansi na kufanya mapenzi. Jamii inayorejelewa imeshabikia sana ngono. Tabia ya kunengua na kuonyesha uhodari wa viuno vya ngono ilisheheni popote ambapo muziki uliandaliwa. Mtunzi anasema, “***Muziki umekosa maana zaidi ya kunengua na kuonyesha uhodari wa viuno vya ngono. Pigeni vita ushabiki na sanaa ya kushabikia ngono.***” Inajitokeza kwamba jamii hii ilipenda sana kuandaa muziki wa Kiafrika ambapo wanawake walionyesha uhodari wao wa kunengua viuno. Baada ya densi kama hizi kuandaliwa kilele chake kilikuwa kwamba watu walijihusisha katika kufanya ngono kiholela bila kinga. Matendo haya yaliendeleza uasherati na hivyo basi kueneza UKIMWI katika jamii husika. Tabia na matendo yaliyotajwa yalikuwa yanaihujumu jamii kimaadili, ndiyo maana mwandishi kupitia mhusika Jose anaona kwamba ni vyema watu wajitokeze kupinga na kupiga vita tabia ya kushabikia ngono.

Ngoma ni mhusika mwingine ambaye ametumiwa na mwandishi kuendeleza dhamira ya kuporomoka kwa maadili ya jamii. Mara kwa mara alishiriki ulevi kwenye baa na kufanya ngono na wanawake kadha wa kadha. Mara kwa mara aliingia kwake akijikokota akiwa na harufu ya marashi, ishara kwamba alikuwa ameshiriki ngono na wanawake nje ya ndoa. Tabia na matendo yake ya uzinifu yanafichuliwa na mkewe Tabu pale anaposema:

**87. *Kila siku nimekuonya; Acha! Hukunisikia. Ulijiona rijali sana kuvamia kila mzoga wa kike uliokuta. Sasa umeniletea gonjwa. Eti tujadiliane! Nijadiliane na mtu ambaye hata sasa ananuka harufu za uasherati...? (Ua la Faraja, uk.27).***

Tabu ambaye ni mkewe Ngoma amekereka na ana uchungu mwingi kutokana na tabia ya mumewe ya uasherati. Tabu anamkashifu Ngoma akisema, “***Ulijiona rijali sana kuvamia kila mzoga wa kike uliokuta.***” Mwandishi ana maana kwamba Ngoma



hakupisha mwanamke yeyote aliyevalia sketi. Alijifanya jogoo na kufanya ngono na kila mwanamke aliyekutana naye. Tabia ya Ngoma ya kujiachilia bure imeiletea jamii yake madhara. Tabu anasema kuwa Ngoma alikuwa amemletea ugonjwa na hakuona sababu yoyote ya kukaa chini na kujadiliana naye. Katika muktadha huu, mwandishi anaonyesha namna ambavyo mhusika Ngoma ameendeleza uasherati kwa kutokuwa mwaminifu katika maisha yake ya ndoa. Matendo ya Ngoma yalimkasirisha mkewe Tabu mpaka akafika kiwango cha kuondoka na kurudi kwao nyumbani. Watu kama vile Ngoma katika jamii ndio wanaoendeleza kuvunjika kwa asasi ya ndoa na kuporomoka kwa maadili ya jamii.

Dhamira ya kuporomoka kwa maadili ya jamii inazidi kubainishwa na mwandishi wa riwaya ya **Ua la Faraja** pale anapowamulika wahudumu kwenye baa. Wahudumu walikuwa na tabia ya kuwashawishi wateja wao kufanya mapenzi nao. Lengo lao lilikuwa kununuliwa pombe na kupewa pesa za matumizi huku wakiachilia miili yao kama malipo. Wahudumu hawa walitumia miili yao kama vitega uchumi. Mwandishi anasema:

**88.** *Sauti zao zilijaa mzaha na ukorofi wa kike kwa mwanamume. Macho yalimtaazama huku kope zikipepesa kwa ishara ya kushawishi. Sauti zao za pamoja zilikuwa na mkwaruzo kidogo na wororo wenye kuamsha hisia za kiume (Ua la Faraja, uk.4).*

Matendo kama haya yaliwanasa wanaume wakajikuta wamejiingiza katika visa vya uasherati hali ambayo ilichangia kuendeleza ugonjwa wa UKIMWI katika jamii. Katika dondoo lililonukuliwa, mwandishi anasema kuwa, “**sauti zao zilikuwa za kuwachokoza wanaume kwa maana zilikuwa na mkwaruzo kidogo na wororo wenye kuamsha hisia za kiume.**” Macho yao yalitazama mwanamume huku kope zikipepesa kwa ishara ya kushawishi. Huu ni ushahidi wa kutosha kwamba wahudumu

hawa kwenye baa walikuwa na nia ya kuwashawishi wanaume wajihusishe nao katika masuala ya mapenzi.

Lengo kuu la wahudumu kama hawa lilikuwa kwamba walitarajia kupata pesa kutoka kwa wateja wao waliowashawishi. Walikuwa wanauza miili yao ili wajipatie pesa. Tabia hii imeenea sana katika jamii yetu ambapo unawakuta wasichana wadogo wenye umri wa kwenda shule wameacha masomo na wamejiingiza katika biashara hii mbaya. Baadhi yao utawakuta wamesimama barabarani katika vituo vikuu wakingojea madereva wa kuendesha malori ya kwenda masafa marefu wanaoaminika kuwa na pesa nyingi za kuharibu. Matokeo ya tabia kama hii ni kuendeleza uasherati unaochangia pakubwa kueneza ugonjwa wa UKIMWI katika jamii. Aidha, mwandishi anatuonyesha kwamba ndoa ambapo wahusika hawakuishi pamoja zilikuwa na hatari ya kukabiliwa na maambukizi ya UKIMWI kwa vile aghalabu mume na mke huingiwa na shauku ya kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mtu wa jinsia tofauti. Mwandishi anasema:

**89.** *Mtu wiki mbili mpaka tatu, unamuacha mke anaganda kwa baridi na wanaume tupo, tubaki kumkodolea macho tu? ... unadhani mimi mjinga? Sisi hatucheleweshi ngoma miguuni kaka! Ukipata uwanja funga mabao uondoke. Usiku kucha umelala kwa mwanamke unangoja nini? (Ua la Faraja, uk. 9).*

Katika dondoo lililo hapo juu, inadhihirika kuwa uhusiano wa kimapenzi ulikuwa ukiendelea baina ya wake na waume ambao hawakuwa wanaishi pamoja kama mume na mke. Hali kama hii ilichangia pakubwa maambukizi na maenezi ya ugonjwa wa UKIMWI. Katika muktadha huu, wanaume waliamini kuwa mwanamke hangeweza kuachwa akiganda kwa baridi ilhali wanaume wengine walikuwepo. Wanaume wanaamini kuwa hawawezi kumkodolea tu mwanamke macho lakini watahakikisha kwamba wanafanya mapenzi naye. Inajitokeza pia kwenye dondoo hili kuwa mwanamume hakuhitaji kulala usiku wote kwa mwanamke lakini alipaswa tu kutumia

muda mfupi uliopatikana kutimiza lengo lake. Mwandishi anasema, “*Sisi hatucheleweshi ngoma miguuni kaka! Ukipata uwanja funga mabao uondoke. Usiku kucha umelala kwa mwanamke unangoja nini?*” Kutokana na mjadala huu, inaonekana kwamba wanaume hawakuheshimu ndoa za wengine na tabia kama hii inahatarisha ndoa za watu ambao hawakuishi pamoja. Mfano huu ni ishara tosha ya kuporomoka kwa maadili ya jamii. Mwandishi ametumia wahusika kama vile Asha na Msafiri kupitisha ujumbe kuhusu kuporomoka kwa maadili ya jamii.

Mwandishi wa riwaya ya **Ua la Faraja** anawasawiri wanawake kuwa katika mstari wa mbele katika kuendeleza uasherati. Anaonyesha namna baadhi yao walikuwa na ujasiri wa kuwakabili wanaume na kuwataka wafanye mapenzi nao. Zamani katika jamii nyingi za Kiafrika, lilikuwa jukumu la mwanamume kumtongoza na kumshawishi msichana. Katika jamii ya sasa, mambo yamebadilika ambapo baadhi ya wanawake ndio wanaokuwa mstari wa mbele katika kutongoza wanaume. Katika dondoo linalofuata msanii anasema:

**90.** *Mima alivua nguo. Omolo akazidi kushangaa, Mima alimvua suruali. Alipovua nguo ya ndani ndipo aliposhikwa na mshangao mkubwa... nilikuwa nakutaka. Nilivutiwa nawe tufanye mapenzi (Ua la Faraja, uk.21).*

Ujasiri wa wahusika wa kike katika riwaya ya *Ua La Faraja* unashangaza. Mima alivua suruali ya Omolo na jambo hili lilimshangaza sana Omolo. Alimvua nguo ya ndani na kumwambia Omolo kuwa alikuwa anamtaka. Mtunzi anasema, “... *nilikuwa nakutaka. Nilivutiwa nawe tufanye mapenzi.*” Mima anamueleza Omolo kuwa alikuwa amevutiwa naye na alitaka wafanye mapenzi naye. Huu ni ujasiri wa kipekee unaoendelezwa na mhusika wa jinsia ya kike. Matendo kama ya mhusika Mima tunayatarajia yafanywe na wanaume lakini katika jamii iliyotumiwa na mwandishi ni kinaya kuwa wanawake ndio wanaoendaendeleza. Mima anasawiriwa kuiendeleza

dhamira ya mwandishi pale ambapo anataka Omolo afanye mapenzi naye kwa lazima kwa vile anadai alikuwa amempenda. Wahusika wengine wa kike katika riwaya wanaoendeleza tabia iliyotajwa ni Pendo na Chiku ambao wanachochea na kuamsha hisia za Ngoma ili awe na uhusiano wa kimapenzi nao. Hivyo basi kwa ujumla mwandishi anatuonyesha kuwa majira yamebadilika ambapo wanawake ndio wanakuwa mstari wa mbele kushawishi wanaume wafanye ngono nao. Hii ni ithibati kuwa jamii zetu zimeporomoka kimaadili.

Mwandishi anazidi kuonyesha namna wahusika wa jinsia ya kike wanavyomsaidia kufanikisha dhamira yake ya kuporomoka kwa maadili ya jamii. Mhusika Chiku anaonekana kughadhabishwa na tabia ya Omolo ya kutokuwa na haja na wanawake. Chiku ni miongoni mwa wahusika wa jinsia ya kike ambao walitamani sana kujihusisha katika masuala ya mapenzi na ngono kama wangepata wanaume wengi wa kushabikia mambo hayo. Mhusika Omolo aliyekuwa akilengwa, hata hivyo hakuwa na haja ya uhusiano na matendo kama hayo. Vitendo vya wahusika kama vile Chiku ndivyo vinavyoendeleza dhamira ya mwandishi ya kuporomoka kwa maadili ya jamii.

Mhusika Pendo aidha amesawiriwa na mwandishi wa riwaya ya *Ua la Faraja* akiendeleza dhamira ya kuporomoka kwa maadili ya jamii kutokana na matendo yake. Alipokutana na Omolo, alimsemesha kwa sauti ya kilevi, lakini yenye kubembeleza na kuonyesha hamu zake za kimwili. Alimsongea Omolo na akataka ampe busu lakini Omolo akasonga mbali. Haya ni matendo ya kushangaza hasa kutoka kwa jinsia ya kike. Pendo anadhihirisha matendo yanayoendeleza tabia ya uasherati, hali inayoendeleza dhamira ya mwandishi. Katika muktadha huu, Pendo alitaka kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mhusika Omolo kwa lazima lakini Omolo akakataa. Tabia ya Pendo pia inachangia katika kuendeleza dhamira ya mwandishi.

Wahusika wengine wa kike ambao wamesawiriwa na mwandishi kuiendeleza dhamira yake ni kama vile Asha. Asha alitumia maumbile yake kuwashawishi wanaume wampatie pesa baada ya kujihusisha nao kimapenzi na kingono. Mhusika Asha alikuwa na tamaa ya pesa na aliutumia mwili wake vibaya ili apate pesa nyingi. Inaonekana kwamba Asha alijihusisha kimapenzi na wanaume wengi akiwa na lengo la kutoshelezwa kihisia na kifedha. Tabia ya uzinzi ya wahusika kama hawa ndiyo inayoendeleza dhamira ya mwandishi ya kuporomoka kwa maadili ya jamii. Mwishoni mwa riwaya ya *Ua la Faraja*, mhusika Asha ni kati ya wahusika wengine ambao wameambukizwa na virusi vya ugonjwa wa UKIMWI.

Aidha, mhusika Asha alijiingiza katika uhusiano wa kimapenzi na Mzungu Hastings mpaka ikafikia wakati wakaoana. Asha alipewa mali nyingi na Hastings lakini kutokana na mienendo yake, hatimaye Asha aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI na kufariki baada ya kujihusisha kwa matendo ya uzinzi. Mali aliyoachiwa na Mzungu haikumfaidi kwa maana alifariki baada ya muda mfupi. Asha ni miongoni mwa wahusika wanaotumiwa na mwandishi kuiendeleza dhamira yake.

Mwandishi wa riwaya ya **Ua la Faraja** anazidi kuonyesha namna dhamira ya kuporomoka kwa maadili ya jamii inavyoendelezwa katika kazi yake. Anaonyesha namna Ngoma anavyoshuku uhusiano wake na mhusika Queen. Queen alikuwa kati ya wanawake asherati waliojitokeza kuhakikisha kuwa wameambukiza watu wengine virusi vya UKIMWI. Mwandishi anasema:

**91.** *Yawezekana Queen ameniambukiza? Nitaliepukaje janga hili? Kwa nini nilifanya uzinzi? Hivi ni kweli huu ndio mwanzo wangu wa kuelekea kaburini? (Ua la Faraja, uk.30)*

Ngoma anaanza kuwa na shaka kuhusu hali yake ya afya akikumbuka uhusiano wake wa kimapenzi na Queen. Msanii anasema, “*Yawezekana Queen ameniambukiza?...*

*Hivi ni kweli huu ndio mwanzo wangu wa kuelekea kaburini?*” Usemi wa Ngoma unaonyesha kwamba anajuta kwa matendo yake ya kujihusisha kimapenzi na mhusika Queen. Inasemekana kwamba mhusika Queen alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI na hivyo Ngoma alihofia kuwa huenda yeye pia alikuwa ameathirika. Ngoma anahofia kuwa huenda huo ukawa mwanzo wake wa kuelekea kaburini. Msanii anasema, “*Yawezekana Queen ameniambukiza.*” Ngoma anajutia matendo yake lakini mwenyewe alipuza ushauri aliopewa mwanzoni na hata lalama ambazo mkewe alikuwa akimtolea. Chambilecho wahenga, majuto ni mjukuu, huja baada ya kitendo. Matendo ya Ngoma na Queen ndiyo kati ya yale yanayotumiwa na mwandishi kuiendeleza dhamira yake ya kuporomoka kwa maadili ya jamii.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, mwandishi aidha anazidi kuiendeleza dhamira yake kuhusu kuporomoka kwa maadili ya jamii anaposawiri matendo ya mhusika Queen ambayo anamfanyia mhusika Omolo. Queen alitamani sana awe na uhusiano wa kimapenzi na Omolo lakini kwa muda mrefu sana, hakufanikiwa. Omolo hakuwa na haja na uhusiano kama huu hususan na mhusika wa jinsia ya kike. Queen alifanya njama siku moja alipomwalika kwake na kumwekea dawa ya kumsisimua kihisia katika kinywaji alichompa, hali iliyomlazimu Omolo kufanya ngono naye. Mwandishi anasema:

**92. *Na siku ile ikawa ya kwanza kwa Omolo kulifurahia tendo lile akiwa katika utu uzima wake...* (Ua la Faraja, uk. 52).**

Matendo kama haya ya mhusika Queen ndiyo yanayotumiwa na mwandishi kuiendeleza dhamira yake. Vitendo vya Queen vilidhihirisha utovu wa maadili na ni watu kama hawa katika jamii wanaoendeleza tabia ya uzinzi ambayo kilele chake aghalabu huwa maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI.

Dhamira ya kuporomoka kwa maadili ya jamii imeangaziwa pakubwa katika tamthilia ya **Orodha**. Mwandishi anatueleza kuhusu wahusika Mary na Furaha na namna wanavyotoroka usiku kwenda kufanya mapenzi na wanaume. Wasichana hawa walitoroka usiku kwenda kukutana na wanaume ili wajihusishe katika mapenzi. Furaha anatumia vitisho kumtia woga mdogo wake ili asitambue siri yake ya kutoroka nyumbani usiku akienda baa. Tabia ya Mary na Furaha ya kuoza kwao kimaadili inadhihirishwa katika kisa cha kutoroka nyumbani.

Wasichana hawa walikazana kutafuta wanaume wawanunulie pombe, wawape pesa na kufanya nao ngono. Matendo haya yanaporomosha maadili ya kijamii. Katika tamthilia ya *Orodha*, mwandishi anatueleza namna vijana wa kike wanavyojiuza ili wapate pesa na vifaa vingine vya matumizi. Mwandishi akimtumia mhusika Mary anatueleza kwamba:

**93.** *Mary: (Akimvuta Furaha kando). Nimekwambia hawa vijana ni burudani... hata yule mshamba Juma. Sikia, pata burudani na kuwa mwema. Kwa Ecko. Anaweza kukununulia vitu vingi sana! Unadhani wasichana wadogo kijijini hapa wanapataje viatu vipya, magauni na mabegi mapya mapya ili wapendeze... wapendeze kiasi cha kuwavutia vijana wazuri wa kiume! (Orodha, uk. 8)*

Vijana wadogo wa kike waliitumia miili yao kujiuza ili wapate pesa ya kukidhi mahitaji yao ya kimsingi. Msanii anasema, “*Anaweza kukununulia vitu vingi sana! Unadhani wasichana wadogo kijijini hapa wanapataje viatu vipya, magauni na mabegi mapya mapya ili wapendeze... wapendeze kiasi cha kuwavutia vijana wazuri wa kiume!*” Mary anaelezea rafikiye Furaha kwamba akiwa mwema kwa Ecko, anaweza kumnunulia vitu vingi sana. Anamfahamisha kwamba wasichana wote katika kijiji chao hupata viatu, magauni na mabegi mapya kutoka kwa hawa wazee. Anasema kuwa wasichana wanawatumia wazee kuwafadhili ili waweze kuwapendeza vijana wa kiume. Kwa upande mwingine, wazee wenye mali kama vile Ecko, walitumia uwezo

wao wa kiuchumi kufanya mapenzi na wasichana wadogo. Matendo haya yote yanaonyesha kuporomoka kwa maadili ya kijamii. Aidha, ni matendo ya sampuli hii yanayoendeleza maenezi ya ugonjwa wa UKIMWI. Msichana Furaha aliambukizwa UKIMWI kutokana na tabia yake ya uzinzi.

Katika tamthilia ya **Orodha**, maadili ya jamii yameporomoka sana ambapo wanaume wengi walijihusisha katika ngono na msichana mmoja aitwaye Furaha. Furaha anajihusisha katika uhusiano wa kimapenzi na wazee pamoja na vijana. Ni kinaya kwamba Padri aliyetarajiwa kutoa mwongozo wa kiroho kuhusu masuala ya kijamii ni mnafiki. Padri James anafanya mapenzi na msichana Furaha aliyetaka usaidizi kwake. Mwandishi anatueleza:

**94.** *Padri James: ... Kwa watu hawa, mimi ndiye Padri wao... lakini mimi pia ni mwanadamu! Nafanya kila niwezalo kufanya ... na bado, kwangu yaelekea kwamba alikwishabikiriwa, kwa hiyo ingelela tofauti gani? Nilidhani hata ningeliweza kumliwaza? Lakini mtu, lazima awe mwangalifu... katika jumuiya ndogo namna hii... taarifa husafiri... wakati wote... kitu fulani huropokwa (Orodha, uk. 10).*

Kutokana na dondoo lilo hapo juu, msanii anatuonyesha uozo uliojaa katika jamii. Tunamtarajia Padri James awe kielelezo katika jamii kwa kuwaongoza watu kufanya mapenzi ya Mungu lakini yuko katika mstari wa mbele katika kujihusisha na masuala ya ngono akidai kwamba yeye pia ni mwanadamu. Msanii anasema, “:... **Kwa watu hawa, mimi ndiye Padri wao... lakini mimi pia ni mwanadamu! Nafanya kila niwezalo kufanya ... na bado, kwangu yaelekea kwamba alikwishabikiriwa, kwa hiyo ingelela tofauti gani?**” Anadai kwamba kwa vile Furaha alikuwa amevunjwa ubikira wake, hakuona makosa yeye kufanya mapenzi naye. Kulingana na Padri kwa vile Furaha alikuwa ameshavunja ubikira wake hakuona tofauti ambayo ingetokea yeye pia akifanya mapenzi naye. Ni jambo la kusikitisha sana kwa maana iwapo viongozi wa kidini kama vile padri James watawaza na kutenda vile alivyotenda, ni



nani sasa atatoa mwelekeo na mwongozo wa kimaadili kwa jamii? Matendo haya yanamtia hofu sana kiasi kwamba wakati mama Furaha alipotaka kusoma orodha ambayo Furaha aliagiza isomwe wakati wa mazishi yake, alikuwa na upinzani mkubwa akidai kuwa angeharibu mazishi hayo.

Mwandishi wa tamthilia ya **Orodha** anazidi kubainisha dhamira yake ya kuporomoka kwa maadili ya jamii pale anapotuonyesha namna ambavyo wanaume watano: Salim, Ecko, Padri James, Kitunda na Juma wamejihusisha katika kufanya mapenzi na msichana Furaha. Kitendo hiki kinatambulika wakati ambapo wahusika waliotajwa walikuwa na wasiwasi mkuu Furaha alipoagiza orodha isomwe wakati wa mazishi yake. Wahusika hawa waliamini kuwa orodha iliyopaswa kusomwa ni ya majina ya wanaume wote ambao Furaha amefanya ngono nao. Tabia na mienendo ya wahusika waliotajwa inadhihirisha namna ambavyo maadili ya jamii husika yameporomoka sana.

Katika tamthilia ya **Kilio Chetu**, mwandishi anatuonyesha namna ambavyo jamii imeoza kimaadili hususan miongoni mwa vijana. Katika jamii hii, vijana wanajihusisha na mapenzi kiholela. Watoto wadogo sana wanasawiriwa kujihusisha na masuala ya ngono. Mtunzi anatuieleza kuwa mtoto Fausta wa darasa la tano alikufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Msanii anatoa kilio kuwa baadhi ya wazazi wenyewe wamechangia katika kuporomoka kwa maadili ya wanao. Anasema:

95. *Mimi nawashangaa hata wale akina mama...Unawakuta wamekaa na watoto wao wanaangalia picha za matusi... (Anacheka)... Shoga, watu tumechanganyikiwa. Tumeibomoa ghala imara ya kuhifadhi maadili yetu. Ghala tuliyojenga kwa miti yetu ya asili. Na sasa tunatukuza ghala iliyojengwa kwa miti dhafu ya kijenzi. Miti inayougua kama mabua. Miti ambayo haipatikani kwa urahisi hapa kwetu (Kilio Chetu, uk.8).*

Msanii anatuonyesha namna ambavyo kina mama ambao hata wamesoma wanavyojiendeleza. Anasema kwamba baadhi ya kina mama hawajiendeshi kama kielelezo kwa watoto wao. Katika dondoo lililo hapo juu anatumia kuwa, **“utawakuta kina mama hao wamekaa na watoto wao wakiangalia picha za matusi.”** Ikiwa wazazi wanakaa na watoto wakitazama picha mbaya za matusi kama vile za watu wakifanya ngono, tunawatarajia vipi watoto wasiyatende hayo wanayoyaona?

Mwandishi analalama kuwa jamii imebomoa ghala imara la kuhifadhi maadili yetu. Anaendelea kuhoji kuwa sasa tunatukuza ghala lililojengwa kwa miti dhaifu ya kijenzi. Katika muktadha huu, ni bayana kuwa ni wazazi na hasa kina mama ndio wanaowasaidia watoto kupotoka. Wazazi wanakaa na watoto wao kutazama picha za watu wakifanya ngono. Ni vigumu kwa mtoto aliyekaa na mzazi kuangalia picha kama hizo kuona kuwa ni makosa kufanya kile kinachoonyeshwa kwenye picha.

Aidha, mtunzi anazidi kulalamikia utamaduni wetu wa jadi ambao umepuuzwa kwa kuukaribisha utamaduni wa kigeni. Anasema, ***“Tumeibomoa ghala imara ya kuhifadhi maadili yetu. Ghala tuliyojenga kwa miti yetu ya asili. Na sasa tunatukuza ghala iliyojengwa kwa miti dhaifu ya kijenzi.”*** Utamaduni wa jadi ulizingatia maadili mema na vijana walipewa mafunzo na mwelekeo mwema maishani mwao. Kwa upande mwingine, utamaduni wa kigeni kwa kiwango kikubwa umechangia katika kuporomoka kwa maadili ya jamii kwa maana kuna maovu mengi ambayo utamaduni wa kigeni unatukuza.

Aidha, mwandishi anatuonyesha namna watoto wa kike wanavyotumia vidonge vya kuzuia wasipate mimba na hivyo kushiriki ngono kiholela wakiwa bado na umri mdogo. Wazazi wa mhusika Suzi wanagundua kuwa mtoto wao si malaika vile

walivyodhania. Wameshtushwa na tukio ambapo Suzi anapatikana na vidonge vya kumzuia asipate mimba. Hii ina maana kuwa mtoto huyu alikuwa akijihusisha na mapenzi kabla ya ndoa. Mwandishi aidha anatupatia takwimu za namna watoto wa darasa la tatu na la nne walivyopata mimba. Kwa kweli, huu ni umri mdogo sana. Hili ni jambo la kutia shaka kwa sababu takwimu hizi zinafichua kwamba watoto hawa hawajayingatia masomo shuleni bali wanajihusisha na masuala yanayohusu ngono.

Mwandishi anasema:

**96. *Haya angalia mwaka wa 1991 watoto 38 darasa la tatu walipata mimba; mwaka huo huo watoto 230 wa darasa la nne walipata mimba. Najua nikikutajia darasa la pili huwezi kuamini (Kilio Chetu, uk.15).***

Takwimu zinazoonyeshwa katika dondoo lililo hapo juu zinahofisha. Twaambiwa na msanii kuwa, **“Katika mwaka wa 1991, idadi ya watoto 38 wa darasa la tatu walipata mimba. Aidha wakati uo huo, watoto 230 wa darasa la nne walipata mimba.”** Takwimu hizi zinaonyesha uozo uliokithiri katika shule zetu na jamii kwa jumla. Hii ina maana kuwa watoto wa umri mdogo sana wanajihusisha na masuala ya ngono. Ikiwa hali itaendelea vile ilivyoonyeshwa katika takwimu hizi, kuna hatari kubwa kwa watoto wa jinsia ya kike kutokamilisha masomo yao. Ikiwa wanafunzi wa darasa la tatu wanajihusisha na vitendo vya uzinifu hivi, sembuse wale wa madarasa ya juu, shule za upili na vyo vikiu? Hatari kubwa zaidi ni ile ya kupata magonjwa ya zinaa na UKIMWI. Kauli hii inashadidiwa na mwandishi anapotuonyesha namna watoto wa shule walivyofanya mapenzi bila hofu yoyote. Aidha mapenzi haya waliyafanya bila kinga yoyote.

Mwandishi anazidi kumulika wazo hili la uozo wa jamii pale anapotuonyesha namna vijana wa shule walivyopenda kuangalia video, picha na magazeti kuhusu ngono. Athari ya utamaduni wa kigeni ndiyo iliyochangia kwa kiwango fulani tabia ya aina

hii. Tabia na mienendo ya aina hii iliwachochea kujihusisha na masuala ya mapenzi na kufanya ngono kiholela. Mwandishi anafichua haya anaposema:

**97.** *Leo si ndio siku ya picha ya 'X'? Umesahau?... Aa toa ushamba wewe. Hujui mkanda wa video wa ngono? Mambo ya mapenzi.*”Vijana wanajidai kwamba nchi yao ni ya demokrasia na hiyo wanajiamulia kila walipendalo. Vijana wanasema, Siyo zamani akina mama utasikia: Vibaya kuangalia magazeti ya mapicha ya uchi mtaota... Sinema za 'X' ni kwa wakubwa tu siku hizi tunaangalia vyote, nani anaota (**Kilio Chetu, uk.20**).

Kutokana na dondoo lililo hapo juu, vijana katika jamii hii wanaangalia video na picha zinazohusu ngono na hali kama hii inaathiri mawazo yao. Msanii anasema, “*Hujui mkanda wa video wa ngono? Mambo ya mapenzi.*” Vijana walikuwa na ratiba ya picha za video ambazo walitazamia kuziangalia kila siku. Wanaulizana kuhusu mkanda wa video wa ngono na mapenzi. Inasikitisha kuwa mambo haya ndiyo yaliyotawala fikra zao. Vijana wanazidi kujidai kuwa kwa vile kulikuwa na demokrasia katika nchi yao, walikuwa na uhuru wa kujiamulia lolote walilolipenda. Wanafurahia vile jamii ilivyokuwa imebadilika kwa maana kwa wakati wao hakuna ambaye angewazuia kuangalia video kwa misingi ya umri wao. Aidha, hakuna atakayewakataza kuangalia picha mbaya za watu wakiwa uchi.

Mabadiliko haya ya kijamii yamechangia pakubwa katika kuporomoka kwa maadili miongoni mwa vijana hususan watoto walio katika umri wa kwenda shule. Matokeo ni kwamba vijana hawa hujaribu kuweka katika matendo yale ambayo wamejifunza na kuyaona, jambo linalochangia wao kujihusisha katika vitendo vinavyokiuka maadili ya jamii. Vilevile inaonekana kwamba katika jamii iliyorejelewa katika utafiti huu, hakuna ambaye aliwajibika kuwakataza vijana hao kuangalia picha na magazeti ambayo yaliwafaa watu wa umri wa zaidi ya miaka kumi na minane. Matendo haya

hatimaye yalisababisha wengi wao kupata mimba za mapema na kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

Isitoshe, katika tamthilia ya **Kilio Chetu**, mwandishi anatuonyesha namna ambavyo vijana takriban wote shuleni wana wapenzi na hata hutumia wakati wa ‘Tuition’ kujiingiza katika masuala ya mapenzi. Tunaonyeshwa namna baadhi ya vijana kama vile Joti na Jumbe walivyomlaumu Mwarami kwa kutokuwa na mpenzi. Wanamtisha kumuondoa katika kundi lao iwapo ataendelea kuwa na tabia ambayo wanaiita ya ushamba. Wanamkashifu mwenzao kwa kudai kwamba aliogopa wasichana. Mawazo na tabia kama hii huendeleza uozo wa maadili kwa jamii miongoni mwa vijana. Aidha, ni ithibati tosha ya kuporomoka kwa maadili ya vijana katika taasisi zetu za elimu.

Aidha, mwandishi anatuonyesha namna ambavyo wasichana katika jamii hii walikuwa wakipata mimba na kuziavya. Mhusika Suzi alipopata mimba alieleza rafikiye Anna kuwa alipanga kuitoa lakini akakatazwa. Anna alipomweleza kuwa angetoa angefariki, anampa mifano ya wale ambao walitoa mimba lakini hawakufariki.

Mwandishi anasema:

- 98.** *ANNA: Utakufa Suzi, umeishafanya kosa kwa nini ufanye kosa lingine? SUZI: Mbona Salma alitoa mimba na wala hajafa? ANNA: Sawa hajafa, hiyo ni kudra ya Mwenyezi Mungu, lakini unajuaje kama yeye ni mzima? Je, kama ameharibu kizazi kwa kutoa mimba? Wewe unasema Salma huyo mmoja, mimi ninawafahamu watu wanne waliokufa kwa kutoa mimba. Suzi, ni hatari usitoe rafiki yangu (Kilio Chetu, uk. 32-33).*

Mifano iliyotolewa kwenye dondoo lililo hapo juu ni ithibati ya kutosha kuwa vijana wengi sana walikuwa wakijihusisha na masuala ya ngono bila kinga. Matokeo ya kutotumia kinga yalikuwa kwamba waliishia kupata mimba na ugonjwa wa UKIMWI. Katika dondoo lililonukuliwa inabainika kwamba mazoea na tabia ya kuavya mimba

miongoni mwa vijana wa shule haikuwa ngeni. Msanii anasema, “*Mbona Salma alitoa mimba na wala hajafa?... Wewe unasema Salma huyo mmoja, mimi ninawafahamu watu wanne waliokufa kwa kutoa mimba.*” Wengi wao walikuwa wanajihusisha katika tabia hii mbaya ya mauaji ya watoto wasio na hatia.

Ingawa baadhi ya wasichana walikuwa wakinusurika wakiavya mimba, msanii pia anatufichulia kwamba wengi wao pia walikuwa wanapoteza maisha yao. Ugunduzi kama huu miongoni mwa watoto wa shule unahofisha hasa ikifahamika kwamba vijana ndio viongozi na wazazi wa kesho. Jamii inapaswa kusimama imara na itumie asasi mbalimbali husika kuhamasisha vijana ili wadumishe tabia na mwenendo bora katika jamii. Hatua hii inaweza kuokoa kizazi cha sasa ambacho kiko katika hatari ya kuangamia.

Mwandishi wa hadithi ya **Likizo ya Mauti** anaangazia ukosefu wa uaminifu katika ndoa na athari zake. Mzee Gogo amesawiriwa kujihusisha na mapenzi nje ya ndoa licha ya kuwa na familia yake. Mzee Gogo alifanya mapenzi na msichana mdogo sana aliyekuwa na umri kama wa bintiye. Mtunzi anatueleza:

**99.** *Hili si jambo la kufanyia mzaha kwani unajua kwamba tayari ninayo familia yangu wala sio dhamira yangu kuvunja nadhiri niliyoiweka katika ndoa yangu. Kwani kuwa wapenzi ni sharti kwanza tuoane?*  
(**Likizo ya Mauti, uk.81**)

Ni bayana kutoka kwa dondoo hili kwamba Gogo alikuwa na familia. Mtunzi anasema, “*tayari ninayo familia yangu wala sio dhamira yangu kuvunja nadhiri niliyoiweka katika ndoa yangu.*” Ni kinaya anaposema hayuko tayari kuvunja nadhiri aliyoiweka ilhali tayari ashaivunja nadhiri hiyo. Gogo anajihusisha kimapenzi na msichana aitwaye Ulimbo. Aliamua kupanda ndege na kimada wake na kumpeleka likizo ya muda katika mji wa Tujisake. Walienda kuishi katika hoteli kuu ya Anasa International iliyokuwa jengo la orofa sitini. Mzee Gogo na kimada wake walifanya

kila aina ya starehe. Mwandishi anatuonyesha kila aina ya starehe ambayo walifanya. Anasema, wapenzi hao walijitoma kidimbwini kuogelea na aidha waliandaliwa kila aina ya vyakula, matunda na vinywaji kunako maji ya matunda hadi mivinyo mikali na mitamu. Waliogelea pamoja huku wakishikana na mara nyingine wakisimama na kukumbatiana kwa mikogo na madaha. Gogo na kimada wake walistarehe na kuyafurahia maisha huku Gogo akiwa ameiacha familia yake nyumbani. Alikuwa radhi kugharamika pakubwa ili kufurahisha kimada wake huku akiisahau familia yake.

Mwandishi anatueleza kwamba Mzee Gogo alifanya mapenzi na msichana mdogo sana. Gogo ni mfano wa wazee, maarufu kama ‘**sponsor**’ wanaotumia ushawishi wao na uwezo wa kiuchumi kuwahadaa na kuwalaghai wasichana wadogo. Msanii anafichua kwamba:

**100.** *Mzee Gogo alichelea kutiwa mbaroni kwa kufanya mapenzi na msichana ambaye umri wake haukuwa halali. Hata hivyo alisahau kwamba ingawa aliweza kuuhepa mkono wa sheria na macho ya wanajamii wengine, kunalo moja lililomponyoka... Alighafilika asikumbuke kuwa ziraili jipya lililozuka kivyake likawashinda hata vigogo wa sayansi na maarifa lilikuwa tayari mawindoni kila mahali na kila wakati! (Likizo ya Mauti, uk.82)*

Mzee Gogo alihofia kutiwa mbaroni kwa kufanya mapenzi na msichana ambaye umri wake haukuwa halali. Msanii anasema, “.... *Mzee Gogo alichelea kutiwa mbaroni kwa kufanya mapenzi na msichana ambaye umri wake haukuwa halali.*” Mzee Gogo alisahau kwamba, ingawa aliweza kuuhepa mkono wa sheria na macho ya wanajamii, hangeweza kuepuka ziraili jipya lililozuka kivyake na hata kuwashinda vigogo wa sayansi na maarifa. Ziraili hilo la UKIMWI lilikuwa tayari mawindoni kutafuta wateja kila mahali na kila wakati. Mwandishi anatuonyesha matunda ambayo Mzee Gogo aliyavuna baada ya starehe zake za muda. Mzee Gogo alikimbia balaa na kwenda kujitosa kwenye beluwa. Hali ya afya ya Mzee Gogo ilibadilika baada ya

muda na akashauriwa kumwendea daktari mshauri ili apewe mawaidha ya kuweza kuivumilia na kuimudu hali yake ya sasa.

Baada ya starehe na anasa zote na Ulimbo, Mzee Gogo alipata maradhi ya UKIMWI. Baada ya haya yote kufanyika, Mzee Gogo anaanza kujuta. Mwandishi anatueleza kuwa mzee Gogo alidhani kuwa alikuwa amepata kumbe ndiye aliyekuwa amepatikana. Anajuta kwa kutosikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Majuto ni mjukuu, huja baada ya kitendo. Mzee Gogo anajuta kwa kupuuza ushauri aliopewa. Chambilecho wahenga, maji yakimwagika hayazoleki. Mzee Gogo alipitia hali ngumu sana ya maisha baada ya starehe zake zote na kimada wake. Mwandishi anatupa taswira ya namna ugonjwa wa UKIMWI ulivyomla Mzee Gogo mbichimbichi. Haya yote yalifanyika kutokana na uhusiano wa kimapenzi wa Mzee Gogo na kimada wake Ulimbo.

Katika hadithi ya **Likizo ya Mauti**, mwandishi anatuonyesha namna furaha iliyotazamiwa kupatikana na Mzee Gogo ilivyogeuka kuwa mauti. Mwanzoni safarini walinusurika kifo baada ya ndege waliyosafiria kunusurika kupata ajali. Isitoshe, baada ya kunusurika Mzee Gogo anaambukizwa ugonjwa wa UKIMWI unaomletea maumivu na hatimaye maangamizi. Mwandishi anatuonya tuwe waaminifu katika maisha ya ndoa ndipo tuepuke kuletea jamii madhila kama alivyofanya Mzee Gogo.

Katika hadithi ya **Alidhani Kapata**, mwandishi anasawiri wahusika kadha wa kadha wanaoendeleza dhamira ya ukosefu wa maadili mema katika jamii. Mhusika ambaye ametumika pakubwa kuendeleza dhamira hii ni Francesca. Francesca ana uhusiano wa kimapenzi na Voltaire ambaye anatuambia kwamba ni mume wa watu. Anasema:

**101.** *Lakini shoga, pana tatizo sugu; darling wangu, mume wa watu! Hilo jike linaloninyima hewa kupumua, aibu kamishna wa polisi-kitengo*



***cha ujasusi! Lakini kwa sasa, sioni haja ya kumsukuma Voltaire hadi ukingoni; anifaa kweli (Alidhani Kapata, uk.86).***

Francesca amechukua mume wa wenyewe na anajidai kwamba pale chuoni pao hata wahadhiri walikuwa wanastahi kwa namna ambavyo alikuwa anajipamba. Mwandishi anasema, “***darling wangu , mume wa watu! Hilo jike linaloninyima hewa kupumua, aibu kamishna wa polisi-kitengo cha ujasusi!***” Ni bayana kwamba Francesca alifanya urafiki na Voltaire ili ampe pesa ambazo alitumia pale chuoni kujipamba na kujistarehesha. Mhusika Francesca anazidi kuendeleza dhamira ya ukosefu wa maadili mema kwa maana licha ya kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Voltaire aliyekuwa mume wa watu, alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Ngufumali.

Francesca anamtumia Ngufumali kama chombo tu cha kumfadhili kifedha lakini ukweli ni kuwa hakuwa na hisia za mapenzi ya dhati kwake. Anasema kuwa hangemuacha Ngufumali kwa maana alikuwa akimtumia pesa za kununulia kijiredio na za matumizi mengine. Haya yanathibitika anapomdunisha Ngufumali katika usemi wake anapomrejelea kama “***lile jiboy la kijijini.***” Licha ya Ngufumali, Francesca alijihusisha kimapenzi na vijana wawili wa chuo kikuu waliojulikana kama “cockroach”. Tabia hii ni ya kushangaza hasa inapofanywa na mwanafunzi wa chuo kikuu anayepaswa kuwa anayashughulikia masomo yake. Katika barua ambayo Vicky alimwandikia Francesca mwandishi anasema:

**102. *France, waniliza nduguyo hapa! yaani, zaidi ya kuwa huna fadhila kuwa Ngufumali unatembea na Voltaire mume wa watu, bado na hao cockroach unao tena wawili? Ndio tuseme washindana na nani au nini vile bibi? (Alidhani Kapata, uk.88)***

Inasikitisha kuwa Francesca Pondamali akiwa mwanafunzi wa chuo kikuu alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume wengi. Mtunzi anasema, “***zaidi ya kuwa huna fadhila kuwa Ngufumali unatembea na Voltaire mume wa watu, bado na hao cockroach unao tena wawili?***” Licha ya Ngufumali ambaye hauthamini, Francesca

alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Voltaire aliyekuwa mume wa watu na “cockroach” wawili wa chuo kikuu. Matokeo ya sarakasi zake yalikuwa kwamba aliambukizwa virusi vya UKIMWI. Tabia na mienendo mibaya inayokiuka maadili ya jamii ndiyo iliyosababisha Francesca kuambukizwa virusi vya UKIMWI. Alitumia mwili wake kama kitega uchumi cha kumwezesha kupata pesa kutoka kwa wanaume.

Francesca ni kiwakilishi cha watu katika jamii wasiotosheka na ambao wanataka kuonyesha ubingwa katika kuyafanya mambo fulani. Kama mwanafunzi wa chuo kikuu, mhusika huyu alikosa mwelekeo maishani na kujiingiza katika mambo ambayo hayangemletea faida yoyote ila hasara na maangamizi. Francesca alikuwa na wapenzi wengi kupita kiasi na ndiyo sababu akaambukizwa virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anatukumbusha kuwa ukosefu wa maadili mema katika jamii unaambatana na madhara yake. Licha ya ukosefu wa maadili mema katika jamii, waandishi wa kazi teule zilizotumika katika utafiti huu wamejadili dhamira ya unyanyapaa ambayo tumeishughulikia katika sehemu inayofuata.

## **5.2 Unyanyapaa**

Unyanyapaa unaweza kufafanuliwa kuwa ni chuki, mitazamo hasi na dhuluma wanayofanyiwa wanaougua maradhi ya UKIMWI. Matokeo yake ni kutengwa na familia, wanarika na jamii kwa jumla, kutohudumiwa vyema katika vituo vya afya, mazingira ya shuleni, kunyimwa haki, kuathirika kimawazo, ambayo ni mambo yanayochangia pakubwa katika kutinga hatua za matibabu. Mwandishi wa riwaya ya *Ua la Faraja* anaiendeleza dhamira hii kwa kuwatumia wahusika kadha wa kadha. Zito na Rajabu katika mazungumzo yao kwenye baa wanaudhihirisha unyanyapaa. Mwandishi anasema:

**103.** *Hapana, namsikitikia mke wake Ngoma. Yule mama ni mstaarabu sana. Ingawaje mumewe ni mlevi wa kutupwa, yeye anawalea wanawe*

*kwa adabu kwelikweli. Sasa ukiambiwa pengine Ngoma kamhukumu kifo (Ua la Faraja, uk.15).*

Katika dondoo lililo hapo juu, hata kama haijajulikana iwapo Ngoma alitumia mpira wakati wa kufanya mapenzi, tayari inaonekana kwamba kitendo alichomfanyia Tabu ni sawa na kumhukumu kifo. Msanii anasema, “*Sasa ukiambiwa pengine Ngoma kamhukumu kifo.*” Zito na Rajabu wanamsikitikia mke wa Ngoma kwa maana wanaamini kuwa anaenda kufariki baada ya muda mfupi. Wanamuona Tabu kama mama mwenye ustaarabu lakini mumewe ndiye wa kulaumiwa kwa maana wanajua kuwa alikuwa amemuambukiza Tabu ugonjwa wa UKIMWI. Kauli hii ni ya kuuendeleza unyanyapaa kwani mtu anapopata UKIMWI sio tiketi ya moja kwa moja ya mauti. Aidha, Ngoma hajafanyiwa uchunguzi wa kimatibabu kubaini iwapo ana virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Matendo ya kumhurumia Tabu hata kabla ya Ngoma kupimwa na kuthibitisha kuwa ana virusi vya UKIMWI yanaendeleza unyanyapaa.

Katika mazungumzo ya Tabu ambaye ni mkewe Ngoma, tunaiona dhamira ya unyanyapaa ikiendelezwa. Kulingana na maoni ya Tabu, maambukizi ya UKIMWI ni sawa na hukumu ya kifo. Tabu anamlalamikia Ngoma akimuuliza sababu zilizomfanya amhukumu kifo kwa kumuambukiza ugonjwa wa UKIMWI. Tabu ana uchungu mwingi sana dhidi ya mumewe Ngoma. Anaona kwamba Ngoma alikuwa amemtendea unyama wa hali ya juu ambapo amemuambukiza ugonjwa ambao kwa maoni yake, hatima yake ni kifo. Katika muktadha huu, kauli na usemi wa Tabu unauendeleza unyanyapaa katika jamii hali inayowakosesha amani waathiriwa wa ugonjwa wa UKIMWI.

Mazungumzo yanayofanywa na Tabu akiwa na mwanawe yanaonyesha mtazamo wa jamii husika dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI. Tabu alipokutana na mwanawe, hali ya

huzuni na majonzi iliwaingia ikifahamika kwamba baada ya muda mfupi hawangekuwa pamoja. Jamii hii ilikosa kufahamu kuwa kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI hakukuwa mwisho wa maisha. Mwandishi anasema:

**104.** *Tabu alianza kulia kwa uchungu mwingi. Kwa kawaida ya mila za kwao, ilikuwa aibu kubwa kwa mama na mwanawe wa kiume kujadili mambo ya namna ile wote machozi yalizidi kuwatoka, kila mmoja akitafakari na kulia kwa nafsi yake. **Lakini kiini cha kilio chao kilikuwa ugonjwa wenye sifa mbaya, kashfa, aibu, laana na udaku wa kila aina na mateso makubwa ya nafsi za wadhurika (Ua la Faraja, uk.38).***

Tabu na mwanawe Juma wanalia kwa uchungu mkubwa kwa maana wanafahamu kwamba ugonjwa alioupata Tabu ungemletea fedheha kubwa kilele chake kikiwa ni kifo. Mtunzi anasema, “***Lakini kiini cha kilio chao kilikuwa ugonjwa wenye sifa mbaya, kashfa, aibu, laana na udaku wa kila aina na mateso makubwa ya nafsi za wadhurika.*** Kutokana na dondoo lililonukuliwa hapo juu, jamii inauchukulia ugonjwa huu kuwa wenye sifa mbaya, kashfa, aibu, laana na udaku wa kila aina. Jamii inayorejelewa na msanii ilikosa kufahamu kuwa ugonjwa ni ugonjwa. Aidha, inategemea namna ambavyo mtu alikuwa ameupata ugonjwa husika. Katika muktadha huu, ni bayana kuwa Tabu aliupata ugonjwa wa UKIMWI pasipo kukusudia. Mumewe Ngoma ndiye aliyejihusisha na uasherati akaupata UKIMWI ndipo akamuambukiza mkewe asiyekuwa na hatia.

Kwa kweli, jamii inayorejelewa hapa inachangia pakubwa katika kuuendeleza unyanyapaa miongoni mwa waathiriwa wa ugonjwa wa UKIMWI. Badala ya kuanza kumlaumu na kumkashifu mwathiriwa wa UKIMWI, ingekuwa bora jamii ichunguze ili ipate uhakika kuhusu chanzo cha maambukizi hayo. Katika hali zingine, mtu anaweza kupata UKIMWI kutokana na utepetevu wa madaktari kwa kupewa damu iliyo na virusi tayari au kutumia kifaa kama vile sindano ambacho kina virusi vya

UKIMWI. Hata hivyo, jamii haipaswi kumhukumu mgonjwa wa UKIMWI kwa maana ugonjwa wowote ule unaweza ukasababisha kifo cha mwathiriwa.

Kwenye riwaya ya **Ua la Faraja**, msanii amemsawiri mhusika Queen kama mmoja wa wahusika ambao wametumiwa na mwandishi kuiendeleza dhamira ya unyanyapaa. Mhusika huyu anahoji maana ya maisha na sababu ya watu kuishi. Queen ni mfano wa watu katika jamii ambao hutamauka sana wanapokabiliwa na shida au changamoto maishani mwao. Katika dondoo lifuatalo, mwandishi anasema:

**105.** *Kama yapo waliyosimulia Wakristo, basi ataishia kwenye moto milele. Lakini kama hadithi ya mbinguni na pepo ni uongo, mtu atakwenda wapi akifa? Ni kweli watu wakifa wanaisha na kupotea hivi hivi? Kuna umuhimu gani basi wa kuwepo kwa watu duniani? (Ua la Faraja, uk.68)*

Kutokana na dondoo hili, ni wazi kwamba Queen ametamauka na kukata tamaa ya maisha. Anasema, “*Ni kweli watu wakifa wanaisha na kupotea hivi hivi? Kuna umuhimu gani basi wa kuwepo kwa watu duniani?*” Queen alishindwa kukabiliana na unyanyapaa uliozingira maradhi ya UKIMWI. Afya yake ilizidi kuzorota na baada ya miezi mitatu, jeraha waliloliita mkanda wa jeshi lilipona baada ya matibabu ya muda mrefu hospitalini lakini sasa kifua kikuu ndicho kilichomsumbua.

Msanii anatufichulia kuwa, mhusika Queen alifika kiwango ambapo hakuona haja ya kutumia dawa za kupunguza makali. Katika mazungumzo yao, Omolo anamsihi asikate tamaa ya kuishi hadi dakika ya mwisho. Mazungumzo ya Queen na Omolo yanaonyesha kuwa alikuwa amemngoja tu mamake na kisha ajitoe uhai wake kwa kujinyonga. Queen hakuona tofauti kati ya kuishi miaka hamsini na mia moja, au yule anayekufa leo na yule aliyeishi siku chache au siku nyingi. Mawazo ya utamaushi yanazidi kusesitizwa na mwandishi kupitia kwa mhusika Queen.

Mhusika Queen kwa hakika alikuwa amekata tamaa katika maisha yake. Mamake Queen alipoletwa na Omolo, Queen alimkabidhi wosia wake. Baada ya kukamilika kwa wosia, aliandaa karamu ndogo waliyoisherehekea na mamake na kisha usiku huo akameza vidonge zaidi vya usingizi vilivyosababisha kifo chake. Queen alikuwa mdhanaishi na hivyo ndivyo alivyomaliza maisha yake. Queen amejitoa uhai wake kwa maana aliamini kuwa jamii haingemsamehe kwa maovu aliyoyafanya. Aidha hakutaka wanajamii waendeleo kumuonea huruma na yeye mwenyewe kuaibika kwa kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi ameiwasilisha dhamira yake ya unyanyapaa katika tamthilia ya **Giza**. Kupitia kwa mhusika Suzi, mwandishi anatuonyesha namna jamii ilivyokuwa ikiwatenga na kuwadhulumu wale walioonekana kuugua maradhi ya UKIMWI. Tabia na matendo kama haya ndiyo yaliyowaathri kwa njia hasi wale walioambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Kwa sababu ya unyanyapaa, watu kama hawa hawakuishi kwa muda mrefu. Mwandishi anasema:

**106.** *SUZI: Mdogo wangu alianza kuugua. Yule mama alivyoona hivyo alitufukuza... Hakutusaidia. Nilitumia pesa zangu kumhudumia. Alipopimwa alikutwa na virusi vya UKIMWI. Mama alitufukuza na akaturushia mizigo yetu nje na mshahara akininyima (Giza, uk.14-15).*

Mwajiri wa Suzi na dadake anaendeleza unyanyapaa kwa maana punde tu alipoona dalili za ugonjwa wa UKIMWI, aliwafukuza. Mtunzi anasema, “*Yule mama alivyoona hivyo alitufukuza... Mama alitufukuza na akaturushia mizigo yetu nje na mshahara akininyima.*” Mwajiri wa kina Suzi aliwafukuza kwa maana alitambua kuwa ugonjwa ambao dadake Suzi alikuwa akiugua ulikuwa UKIMWI.

Jamii inayorejelewa na msanii ilikuwa na mtazamo hasi kuhusu ugonjwa huu. Iliaminika kwamba yeyote aliyeupata ugonjwa wa UKIMWI alijihusisha na uzinzi na

uasherati. Mtazamo huu uliifanya jamii iuone na kuuchukulia ugonjwa huu kama wa aibu na fedheha kubwa kwa mwathiriwa. Isitoshe, mwajiri wa Suzi alionyesha ukatili wa kiwango cha juu aliporusha mizigo yao nje na kukataa kuwalipa mshahara. Huu ni ukatili uliopita mipaka. Matendo haya kwa jumla yanaendeleza unyanyapaa katika jamii.

Wahusika mbalimbali katika jamii hii waliendeleza unyanyapaa. Kupitia kwa mhusika Suzi, mwandishi anazidi kuendeleza dhamira yake ya unyanyapaa. Suzi alipokuwa hospitalini, hakushughulikiwa inavyopaswa kama mgonjwa yeyote yule kwa kuwa alikuwa anaogua UKIMWI. Inasikitisha kuwa hata madaktari na wahudumu wengine hospitalini waliendeleza unyanyapaa. Mtunzi anatufichulia kuwa:

**107.** *SUZI: Ndipo nilipoishi, kule kihazarani nilifukuzwa eti maiti ilileta nuksi. (Mara Suzi anashindwa kuzungumza, anakohoa sana, anatajika mfululizo. Nuru anaenda kumwita Nesi, lakini anakuta Nesi anakunywa chai hajibu kitu, Nuru anaporudi anamkuta Suzi macho yameangalia juu) Giza aa gizaaaa (...)* (Giza, uk.16)

Kabla ya Suzi kufariki akiwa kule kihazarani alifukuzwa na kuitwa kama maiti aliyeleta nuksi. Mtunzi anasema, “*kule kihazarani nilifukuzwa eti maiti ilileta nuksi... Nuru anaenda kumwita Nesi, lakini anakuta Nesi anakunywa chai hajibu kitu.*” Inasikitisha kuwa wahudumu hospitalini wanawaita wagonjwa wanaogua UKIMWI kama maiti wanaotembea. Hii inamaanisha kuwa tayari walikuwa wamejua hatima ya mgonjwa husika. Hii ndiyo sababu Nesi alipoitwa kwenda kumhudumia Suzi alipokuwa katika hali mahututi, hakujali ila tu aliendelea kunywa chai yake. Alijua tu kwamba mgonjwa aliyeitiwa alikuwa anaogua ugonjwa wa UKIMWI na hivyo hakustahili kumhudumia. Unyanyapaa huu ndio ulioathiri sana maisha ya wagonjwa wa UKIMWI na kuchangia sana wao kufa haraka.

Ni kinaya kuwa wahudumu hospitalini, wakiwemo manesi na madaktari ndio wanaouendeleza unyanyapaa. Hawa ni wataalamu ambao jamii inawategemea kwa kutibu wagonjwa na hivyo inasikitisha sana wao pia kuhusika katika kuuendeleza unyanyapaa katika jamii. Hata kama wataalamu hawa wanajua kuwa mgonjwa yu karibu kufa, taaluma yao hairuhusu waseme ukweli huo ila waendeleo kumpa matumaini ya kuishi.

Mazungumzo kati ya Nuru na Mona yanatuonyesha namna mwandishi anavyozidi kuushadidia ujumbe wake mkuu kuhusu unyanyapaa. Kupitia kwa wahusika hawa, madaktari na manesi hawakumjali mtoto kwa maana alikuwa anaogua UKIMWI. Wahudumu hao walimtenga na kukataa kumtibu mtoto kwa vile alikuwa anaogua UKIMWI. Inabainika wazi kwamba madaktari na manesi waliwatesa wagonjwa wa UKIMWI na hawakuwa tayari kuwahudumia. Mwandishi anasema kwamba huenda walihitaji kuhongwa kwa maana walikosa maadili ya kazi. Matendo ya kuwatenga wagonjwa wa UKIMWI yaliyoendelezwa na watu waliostahili kuwapa msaada yalichangia pakubwa katika kuangamiza kwa haraka maisha ya waathirika wa UKIMWI.

Mwandishi anawasawiri madaktari kama watu walioendeleza unyanyapaa. Badala ya madaktari kuwa katika mstari wa mbele kuwahudumia wagonjwa, wao ndio walikuwa tayari sana kuwapiga vita. Katika jamii iliyotumiwa na mwandishi, inaonekana kwamba madaktari walihitaji kuhongwa kwanza kabla ya kuhudumia wagonjwa wa UKIMWI. Msanii anasema:

**108.** *Daktari: Wagonjwa hawa wanasumbua sana inapaswa wakae nyumbani tu. (anamgeukia Nuru) Una hela za kununulia maji ya dripu? (Giza, uk. 36)*



Ni kinaya daktari kusema mgonjwa anamsumbua na anastahili kukaa nyumbani badala ya kumhudumia. Madaktari katika jamii hii walikosa maadili ya kazi kwa sababu ya ufisadi. Mwandishi anasema, “*Una hela za kununulia maji ya dripu?*” Tamaa ya pesa inawafanya madaktari kuuendeleza unyanyapaa dhidi ya wagonjwa ambao ni waathirika wa UKIMWI. Wahusika waliotajwa katika sehemu hii wanaendeleza unyanyapaa katika tamthilia. Waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI wanatengwa badala ya kuonyeshwa mapenzi na hali hii ndiyo inayochangia wengi wao kukata tamaa na kufariki haraka punde tu wanapogunduliwa kuwa na virusi vya ugonjwa wa UKIMWI.

Aidha kupitia mhusika Mona, mwandishi anaiendeleza dhamira yake ya unyanyapaa. Mwanzoni mwa onyesho la tisa katika tamthilia ya *Giza*, Mona anaonyesha kutamauka akisema kuwa yeye alikuwa amesubiri kifo tu kwa vile alikuwa anaugua ugonjwa wa UKIMWI. Badala ya jamii kumpa matumaini ya kuishi akiwa na ugonjwa huo, inauendeleza unyanyapaa. Msanii anasema:

**109.** MONA: *Huku, majungu tupu. Watu wote wananifahamu na jinsi ninavyougua. Siendi tena. Nuru bye (Nuru anaenda kwake anamkuta Steve anagaragara, anatapika ovyo) (Giza, uk.34).*

Katika dondoo hili, Mona anatueleza kwamba watu walifahamu ya kuwa yeye alikuwa anaugua ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi anasema, “*Watu wote wananifahamu na jinsi ninavyougua. Siendi tena.*” Ufahamu huu ulimfanya asiwe na ujasiri wa kutembea mahali popote. Huenda hali hii ilitokana na mtazamo ambao jamii ilikuwa nao kuhusu waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI. Ugonjwa wa UKIMWI ulihusishwa na aibu, fedheha na mwathirika alionekana kama mtu muovu na mzinifu katika jamii.

Aidha, ugonjwa huu wa UKIMWI ulichukuliwa kama laana katika jamii inayorejelewa. Mtazamo huu ulimfanya Mona akose uhuru wa kutangamana na wengine kwa maana hakutaka wanajamii wamuone na kumchukulia kwa njia hasi. Ukweli ni kwamba jamii iliwatenga waathirika wote wa UKIMWI na hali hii iliendeleza sana unyanyapaa. Wagonjwa wa UKIMWI walipaswa kuonyeshwa upendo, kupewa matibabu, chakula bora na kupewa matumaini ya kuishi maisha kama watu wanaougua ugonjwa wowote ule.

Katika tamthilia ya **Orodha**, mwandishi ameitaja dhamira ya unyanyapaa katika sehemu mbalimbali. Mhusika Furaha anatueleza namna dada zake walitoroka chumba alichokuwa akilala wakahamia chumba kingine. Inasikitisha kuwa watu katika jamii iliyotumiwa na mwandishi huwatoroka wale walioambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi anatueleza kuwa:

**110.** *Salim:... Oh, wakati huu wadogo wako wanalala wapi? Furaha: Niliposhikwa na ugonjwa, wakahamia chumba kingine. Usiku nilikuwa nikiwasumbua!” (Orodha, uk.28)*

Dada zake Furaha waliendeleza dhamira ya unyanyapaa walipomtoroka Furaha. Msanii anatueleza kuwa, “*Niliposhikwa na ugonjwa, wakahamia chumba kingine. Usiku nilikuwa nikiwasumbua!*” Dada zake Furaha walitoroka na kuhamia chumba kingine kwa vile alikuwa anaugua ugonjwa wa UKIMWI. Furaha anasema kuwa walitoroka kwa vile alikuwa anawasumbua na huenda pia walitoroka kwa kuhofia kwamba angewaambukiza ugonjwa huo. Ugonjwa wa UKIMWI ulihusishwa na mambo mabaya katika jamii na ndiyo maana wadogo wa Furaha waliweza kumtoroka. Kitendo walichokifanya kinamtenga Furaha na hivyo kuundeleza unyanyapaa.

Isitoshe, katika tamthilia ya **Orodha**, ni kinaya kuwa hata mamake Furaha anaiendeleza dhamira ya unyanyapaa. Iwapo mama mzazi anamuogopa mwanawe, ni

nani atakayemkaribia? Mama Furaha anajiunga na kundi la watu wengine katika kuogopa na kujitenga na waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI. Huu ni unyanyapaa ambao unapaswa kupigwa vita kwa vyovyote vile. Unyanyapaa ndio huwafanya waathirika kufariki haraka kwa maana wao hujihisi kutengwa kabisa na wanajamii.

Katika hadithi fupi ya “tahadhari bandia”, mtunzi amesawiri hali inayowakumba waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI. Ingawa Wakesho alidhaniwa tu kuwa na ugonjwa wa UKIMWI, jamii ilimtenga na kumdhulumu kihisia. Mwandishi anatueleza kwamba Wakesho alikatazwa kufanya mtihani baada ya kutoka hospitalini. Ingawa Wakesho alikuwa na uwezo wa kufanya mtihani baada ya kutoka hospitalini, hakuruhusiwa. Mwandishi anatueleza :

**111. *Ingawa alikuwa na nguvu na uwezo wa kuifanya mitihani hiyo, Wakesho hakuruhusiwa na alihisi ubaguzi na unyama katika uamuzi huo (Likizo ya Mauti, uk.4).***

Juhudi za Wakesho za kusihhi utawala wa chuo kumruhusu kuufanya mtihani hazikuambulia chochote. Unyanyapaa unaendelezwa kwa kuwa msanii anasema, *“Wakesho hakuruhusiwa na alihisi ubaguzi na unyama katika uamuzi huo.”* Sababu ya kumzuia Wakesho asifanye mtihani haikueleweka kwa maana mwenyewe alijihisi angeufanya mtihani ule bila tatizo. Kwa vile alidhaniwa kuugua ugonjwa wa UKIMWI, alitengwa na kutoruhusiwa kufanya mtihani. Huu ni ubaguzi wa kiwango cha juu na hatutarajii taasisi za elimu kuuendeleza unyanyapaa kwa wanafunzi wake. Tunahitaji taasisi ya elimu na mafunzo kama ilivyotajwa katika tamthilia kuchangia katika kuhamasisha jamii kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Tunatarajia walimu wawe na ufahamu zaidi na kuisaidia jamii kuelewa zaidi ugonjwa wa UKIMWI lakini hali ni kinyume cha matarajio ya wengi. Taasisi hii ndiyo inayojiunga na nyingine zinazohusika katika kuuendeleza unyanyapaa miongoni mwa wanajamii.

Jamii na hata marafiki wa Wakesho walimuambaa kama wanavyoliambaa jini au shetani walipogundua kwamba alikuwa amepatwa na virusi vya UKIMWI. Hata mchumba wake wa karibu aitwaye Jimi alimtenga. Mambo haya yote yanafanyika hata kabla ya kuthibitisha kuwa Wakesho alikuwa na ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anasema:

**112. *Kinachoniuma zaidi sio maradhi haya ya UKIMWI ikiwa ndiyo hatima yangu ya maisha lakini ni kule kukimbiwa na marafiki na wenzangu wote kwa umoja wao. Nitawezaje kuukabili ulimwengu wakati ambapo hata Jimi, mchumba wangu ameniasi kwa hatia ya jambo ambalo sikulisababisha? Huu ni unyama kamili. Hiki ndicho kilele cha unafiki wa binadamu (Likizo ya Mauti, uk.5).***

Kutokana na dondoo lililo hapo juu, msanii anatuonyesha mtazamo ambao jamii ilikuwa nao kuhusu waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi anasema, *“Kinachoniuma zaidi sio maradhi haya ya UKIMWI ikiwa ndiyo hatima yangu ya maisha lakini ni kule kukimbiwa na marafiki na wenzangu wote kwa umoja wao. Nitawezaje kuukabili ulimwengu wakati ambapo hata Jimi, mchumba wangu ameniasi kwa hatia ya jambo ambalo sikulisababisha?”* Wakesho hatatiziki na ugonjwa wa UKIMWI lakini kile kitendo cha kukimbiwa na marafiki zake kwa pamoja. Wakesho aliyekuwa na marafiki wengi anabaki katika hali ya upweke kwa vile ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Ni jambo la kusikitisha sana kwa sababu hata mchumba wake Jimi alikuwa amemuasi kwa vile alimhusisha na ugonjwa wa UKIMWI. Wakesho anahoji kwamba hata ugonjwa wa UKIMWI anaosingiziwa hakuusababisha mwenyewe.

Kwa kweli huu ni unyama wa kiwango cha juu sana. Jamii iliyotajwa katika hadithi hii ina mtazamo hasi kwa waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI. Mtazamo kama huu na matendo ya ubaguzi ndiyo yanayowafanya waathirika kutatizika kisaikolojia na kisha kufa kwa haraka. Waathirika hao huhisi wamekataliwa na kila mtu katika

ulimwengu huu na hivyo huona bora wafe kuliko kuishi katika ulimwengu uliojaa unafiki na usaliti.

Katika **Likizo ya Mauti**, mwandishi anazidi kuibainisha dhamira yake kuhusu unyanyapaa anapotuelezea kuhusu nafasi ya kazi ambayo Wakesho aliikosa kwa sababu ya hali yake ya afya. Baadhi ya mashirika ya serikali na yasiyokuwa ya kiserikali yalikuwa yakiwanyima watu kazi walipogundua kwamba mhusika alikuwa mwathiriwa wa ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anatumia:

**113.** *Alivutiwa na barua mbili tu katika furushi zima. Moja ilitoka katika shirika moja la kijamii lililoitwa, Bright Future Limited ambamo Wakesho alikuwa amepeleka maombi ya kazi. Barua yenyewe ilikuwa na mistari miwili tu na ilisema; 'Haya ni kuhusu maombi yako ya kazi katika shirika hili. Kutokana na hali yako ya sasa, shirika hili haliwezi kukuajiri ingawa umetimiza masharti yanayotakiwa (Likizo ya Mauti, uk.5).*

Wakesho alikuwa amepeleka maombi ya kazi kwenye mashirika mbalimbali lakini majibu aliyoyapokea yalikuwa ya kutamausha. Msanii anasema kwamba barua yenyewe ilikuwa na mistari miwili tu iliyosema kuwa, “**kutokana na hali yako ya sasa, shirika haliwezi kukuajiri ingawa umetimiza masharti yanayotakiwa.**”

Wakesho alidhaniwa tu kuwa na ugonjwa wa UKIMWI lakini anabaguliwa hata kwa nafasi ya kazi ambayo alikuwa amehitimu kuipata. Huu ni ubaguzi na unyanyapaa wa hali ya juu unaokiuka haki za kibinadamu.

Ni makosa makubwa sana kumnyima mtu nafasi ya kazi kutokana na hali yake ya afya. Wakesho alilia kwikwi na uchungu kwani alihisi ulimwengu ulikuwa umemfanyia njama kumfungia milango ya ufanisi maishani mwake. Wasanii mbalimbali wameonyesha namna ambavyo unyanyapaa uliyaathiri maisha ya waathiriwa wa UKIMWI. Licha ya unyanyapaa unaojitokeza katika maandishi teule yaliyotumiwa katika utafiti huu, wasanii pia wameliangazia suala la dhuluma dhidi ya

wanawake. Dhamira ya dhuluma dhidi ya wanawake ndiyo imeshughulikiwa kwa kina katika sehemu inayofuata.

### 5.3 Dhuluma Dhidi ya Wanawake

Dhuluma dhidi ya wanawake yaweza kufafanuliwa kama ugandamizaji ambao watu wa jinsia ya kike hufanyiwa hususan na wanaume. Unyanyasaji huu aghalabu umejikita katika misingi ya taasubi za kiume ambapo mwanamke anachukuliwa kama chombo cha kutumiwa tu na mwanamume. Katika riwaya ya **Kala Tufaha**, mwandishi anaonyesha namna ambavyo mtoto wa kike anadhulumiwa kwa kunyimwa nafasi ya kuendelea na masomo katika shule ya upili.

Mhusika anayeitwa Kibibi alifanya vizuri katika mtihani wa darasa la nane akaibuka wa kwanza katika tarafa lakini babake alikataa katakata kumruhusu aendelee na masomo ya sekondari. Mzee Selemani alithamini masomo ya mtoto wa kiume na kudharau masomo ya mtoto wa kike. Kibibi anajiuliza maswali yafuatayo:

**114. *Mbona Imu hakupita vizuri na baba alimtafutia shule ya upili. Kwa nini anayathamini sana masomo ya kakangu na kunitekeleza mimi? Kama kuzaliwa msichana, nilitaka mimi?***” aliwaza huku akilengwalengwa na machozi (**Kala Tufaha, uk.15**).

Ni kinaya kwamba mtoto Imu ambaye alikuwa mbumbumbu katika masomo anatafutiwa shule aendelee na masomo ya sekondari ilhali Kibibi aliyeibuka wa kwanza katika tarafa ananyimwa nafasi ya kuendelea na masomo. Kibibi anasema, ***“Mbona Imu hakupita vizuri na baba alimtafutia shule ya upili. Kwa nini anayathamini sana masomo ya kakangu na kunitekeleza mimi? Kama kuzaliwa msichana, nilitaka mimi?”*** Ni uchungu mkubwa Kibibi kunyimwa nafasi ya kuendelea na masomo kwa misingi ya jinsia. Inasikitisha sana kuangamiza ndoto ya Kibibi ya kuwa daktari kwa sababu alizaliwa msichana. Mwalimu Selemani Chai

alikuwa na uwezo wa kugharamia elimu ya wanawe wote wawili ila hakuafikiana na wazo la kumsomesha mtoto wa kike hadi upeo wa elimu.

Mzee Selemani alikuwa na mtazamo hasi kuhusu masomo ya mtoto wa kike. Aliamini kwamba hawakufunzwa mambo mazuri shuleni ila kufundishwa kwenda tuputupu au kwenda uchi. Kwa maoni yake, mavazi waliyonayo wasichana yanaviiacha viungo vingi zaidi wazi kuliko vile vinavyosetiriwa. Mtindo wa mavazi wa wasichana walioenda shuleni ndio ambao unatamausha Mzee Selemani mpaka akakataa kumsomesha mtoto wa kike. Aliamini kwamba Kibibi, sawa na wasichana wengine angeuchukua mtindo huo wa mavazi angepelekwa shuleni. Selemani aliamini kwamba mtindo huo wa mavazi ungewafanya wajingize katika uasherati uliokuwa chanzo cha maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI. Msimamo wa mzee Selemani ni wa kidhalimu kwa maana alisahau kwamba watu huwa wanatofautiana na huenda Kibibi hangechukua mtindo wa mavazi wa wasichana wengine.

Mzee Selemani alidhani kwamba kuruhusu msichana kuendelea na masomo ni sawa na kukaribisha ukahaba kwenye boma. Mzee aliamini kuwa hakukuwa na chochote kizuri shuleni ila kujihusisha na matendo ambayo yalikiuka maadili ya jamii. Anatoa mfano wa Chaurembo bintiye Mosi ambaye alikosa maadili mema baada ya kutoka shuleni. Kwa jumla Mzee Selemani alikuwa na mtazamo hasi kwa masomo ya watoto wa kike na hali hii iliendeleza dhamira ya dhuluma dhidi ya wanawake kwa vile aliruhusu Imu ambaye hakufanya vyema kuendelea na masomo kwa vile alikuwa mwanamume.

Katika riwaya hii vilevile, mwandishi anaonyesha namna ambavyo wanawake hawana usemi wowote mbele ya waume wao. Aidha, wanawake wanasawiriwa kama watu ambao wanajidunisha wenyewe mbele za waume wao. Kibibi alihitaji mamake

amtetee mbele ya babake ili aendelee na masomo lakini juhudi hizo zikaambulia patupu. Mwandishi anasema:

**115.** *Hana sutua yoyote mbele ya mumewe, mwalimu Selemani Chai. Yeye mwanamke, akisema atakayemsikiliza ni nani? Baba mtu ashakata kauli masomo ya Kibibi ndio basi. Bi Habiba tangu hapo hajawahi kumwinulia mumewe ulimi (Kala Tufaha, uk.17).*

Katika jamii inayorejelewa katika riwaya ya *Kala Tufaha*, mwanamke hakuwa na usemi wowote mbele ya mwanamume. Msanii anasema, “yeye mwanamke akisema atakayemsikiliza ni nani?... Bi Habiba tangu hapo hajawahi kumwinulia mumewe ulimi.” Hii ina maana kuwa Selemani hangesikia chochote ambacho mkewe angesema kuhusiana na jambo lolote katika jamii. Katika jamii hii, mwanamume akikata shauri kuhusu jambo fulani, mwanamke hakuruhusiwa kusema wala kutenda kinyume. Katika muktadha huu, mzee Selemani alikuwa ameshakata kauli kwamba Kibibi hangeendelea na masomo na hakuna ambacho kingebadili msimamo wake. Hivyo basi, juhudi za Kibibi kumtumia mamake kumsihi Selemani abadili msimamo wake mkali kuhusu masomo ya Kibibi hazingezalisha matunda yoyote.

Ni dhuluma kuu kumnyima mwanamke nafasi ya kunena na kutoa maoni na maamuzi kuhusu masuala ya kijamii. Ili jamii yoyote ipate kuendelea vizuri, pana haja ya nafasi ya wazazi wote katika jamii kutambulika. Enzi ambapo mume pekee ndiye aliyepaswa kufanya maamuzi kwa kila kitu zilipitwa na wakati. Mwanamke anapaswa kutambuliwa katika jamii na malezi bora kwa watoto yanahitaji mchango wa wazazi wote sawa na maamuzi yoyote yanayofanywa yanayoiathiri jamii.

Dhuluma nyingine inayodokezwa na mwandishi ni kuwa Mzee Selemani badala ya kumruhusu Kibibi aendelee na masomo, alikuwa na njama ya kumwoza kwa lazima katika umri huo mdogo. Selemani anamuona bintiye kama kitega uchumi na ndiyo



maana anapanga kumuoza katika umri huo mdogo. Huu ni unyanyasaji wa hali ya juu ambapo haki za kibinadamu zinanyimwa. Mtunzi anatumia:

**116. *Mwalimu Selemani ameshapanga na rafiki yake huyo wa hapo mferejini kuhusu ndoa ya watoto wao wawili. Kitinda mimba wa mzee Majembe yuafanya kazi Uarabuni. Atakuja likizo nyumbani baada ya miaka miwili. Pengine hapo kutakuwa na mpango wa posa au hata ndoa yenyewe. Kibibi hayajui haya lakini mama mtu keshambiwa na kuonywa kutomwarifu. Aila ya majembe, wote hawana habari ila huyo mzee mwenye nyumba (Kala Tufaha, uk.20).***

Mzee Selemani na rafikiye Majembe wanafanya mpango kwa siri kuhusu ndoa ya watoto wao wawili. Mtunzi anasema, “*Mwalimu Selemani ameshapanga na rafiki yake huyo wa hapo mferejini kuhusu ndoa ya watoto wao wawili.*” Mpango na maamuzi ya ndoa yanafanywa pasipo kuwahusisha watoto wenyewe. Hii ni aina ya dhuluma kwa maana si vyema kulazimisha mtu kuoa au kuolewa na mwingine bila idhini wala mapenzi yake. Mamake Kibibi pekee ndiye aliyejua kuhusu mpango huu lakini alionywa kutomwarifu mtu yeyote kuuhusu.

Mzee Selemani na Majembe waliona watoto wao kama vyombo vya kuchezeza tu. Baada ya kunyimwa nafasi ya kuendelea na masomo, Kibibi anachukuliwa kama kitega uchumi. Jamii ilimngandamiza sana mtoto wa kike. Baadhi ya wanawake waliyaachilia mbali masomo ya shule za msingi. Wengine wao waliyaachia masomo katika darasa la tatu na kuolewa. Wanawake wengine hawakulikaribia jengo la shule na kama walienda chuoni hawakuhitimisha msahafu. Katika jamii inayorejelewa hapa iliainika kuwa mahali pa mwanamke ni jikoni.

Mtazamo wa jamii ulikuwa kwamba hata mwanamke asome afike wapi, mwisho hurudi katika twaa ya mumewe. Jamii hii iliamini katika kumdhibiti mtoto wa kike ambaye hakuwa na usemi wowote maana iliainika kwamba mahali pake ni jikoni. Kwa upande mwingine, wanawake wenyewe yaelekea hawakuona umuhimu wa

masomo. Baadhi yao hawakuona faida ya mwanamke kusoma kwa vile mwishowe huolewa na mume na kuwa mke nyumbani. Kujidharau huku kwa mke kunampa mwanamume fursa ya kumchezea na kumdhulumu. Kupitia kwa mhusika Kimini, mwandishi anasema kwamba, mtoto awe msichana au mvulana, anapaswa kuhimizwa kuendelea na masomo.

Mfano mwingine wa dhuluma ambao mwandishi anautumia ni ule wa kuruhusu Kibibi kwenda kwa Fumbwe kufanya kazi ya uyaya. Wazazi wa Kibibi wako huru kuruhusu binti wao kwenda kufanya kazi ya kulea mtoto lakini hawakubali kumruhusu Kibibi aendelee na masomo yake ya shule ya upili. Dhuluma kuu ya kimapenzi ilifanywa wakati ambapo Fumbwe alimnyemelea Kibibi akitumia hila na ujanja mpaka akambaka. Msanii anasema:

**117.** .... *Alishuku kulikuwa na jambo lililotendeka ambalo si la kawaida. Alivuta fikra kujaribu kukumbuka mambo. Hakupata lolote la maana kwa wakati ule. Aliupitisha mkono wake wa kulia katika sehemu ya juu ya paja lake. Hapo akathibitika na ukweli! Hapakuwa na kizuizi chochote. Vidole vyake vilipata unyenyekevu. Kibibi aliingiwa na kiwewe (Kala Tufaha, uk. 65-66).*

Mkewe Fumbwe alikuwa ameelekea sehemu za mashambani kuona wazazi, akamuacha mumewe nyumbani pamoja na Kibibi. Fumbwe aliona amepata fursa ya kipekee kutimiza lile ambalo lilikuwa moyoni mwake kwa muda. Fumbwe alimwekea dawa ya kumfanya Kibibi alale kwenye tufaha kisha akamfanyia unyama alipokuwa amelala. Mtunzi anasema, “*Aliupitisha mkono wake wa kulia katika sehemu ya juu ya paja lake. Hapo akathibitika na ukweli! Hapakuwa na kizuizi chochote. Vidole vyake vilipata unyenyekevu.*” Hii ni dhuluma kubwa ya unyanyasaji wa kimapenzi anayoitekeleza Fumbwe ikitarajiwa kwamba alipaswa kumchukua Kibibi kama mtoto wake. Matendo ya Fumbwe ya unyama yaliendeleza uovu uliosababisha maenezi ya ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi anadhihirisha dhuluma dhidi ya wanawake pale ambapo Kibibi alitafuta msaada wa polisi baada ya kitendo kile cha unyama. Kibibi aliripoti kisa chake katika kituo cha polisi lakini kinaya ni kwamba msimamizi mkuu wa kituo hicho cha ujasusi alikuwa Fumbwe mwenyewe. Askari ambao Kibibi aliwaelezea kisa chake, walitetemeka tu walipoona Fumbwe akiwasili. Hatimaye kesi yenyewe ilifikishwa kwa Fumbwe ambaye alikuwa mshtakiwa. Kesi hiyo haikuenda popote na hivyo Kibibi akadhulumiwa. Baada ya tukio hilo la unyama, Fumbwe alimwagiza askari langoni kutomruhusu Kibibi kutoka hadi pale ambapo angewaarifu. Kibibi aliwekewa vikwazo ili tukio hilo la unyama lisije likatambulika.

Mwandishi wa riwaya ya **Kala Tufaha** anazidi kutuonyesha namna utingo anavyomfanyia mtoto wa kike dhuluma ya kimapenzi. Katika usafiri wa umma, kuna tabia mbaya ambayo hutokea wakati mwingine. Baadhi ya utingo hushika sehemu ya matiti ya wanawake kwa kisingizio cha kufanya kazi yao. Kibibi alipokuwa akisafiri kutoka shuleni kuangalia matokeo ya mtihani, utingo alimfanyia kitendo hiki cha utovu wa heshima. Mwandishi anaonyesha namna watoto wa kike wanavyochezewa kama vyombo vya mapenzi.

Tabia ya kushikashika mtu wa jinsia tofauti hadharani ni utovu wa adabu na dhuluma ya hali ya juu. Sehemu ya matiti ni nyeti sana kwa mtoto wa kike na haipaswi mtu yeyote kuishikashika kiholela. Matendo kama haya yanaendeleza dhuluma kubwa ya kimapenzi dhidi ya mtoto wa kike. Haya ni matendo ya uzinifu yaliyochangia pakubwa katika kusambaza ugonjwa wa UKIMWI. Katika riwaya ya *Kala Tufaha* mwandishi anazidi kudhihirisha dhuluma dhidi ya mtoto wa kike pale anapotuelezea kuhusu kufukuzwa nyumbani kwa Kibibi licha ya magumu aliyoyapitia maishani. Mwandishi anasema:

**118. *Sitaki kabisa kukuona kwangu. Izara uliyotushushia inatutosha. Nasema nyumba yangu hii uione paa na moshi (Kala Tufaha, uk.19).***

Wazazi wa Kibibi hawakutaka kumpatia nafasi ajieleze vile hali ilivyokuwa lakini waliamua kumfukuza nyumbani pasipo kumjali na kuijali hali yake. Mzee Selemani anasema, “*Sitaki kabisa kukuona kwangu. Izara uliyotushushia inatutosha. Nasema nyumba yangu hii uione paa na moshi.*” Kibibi alikuwa ametendewa unyama na Fumbwe alipombaka na matokeo yakawa kwamba alishika mimba. Unyanyasaji na mateso ambayo Kibibi aliyapokea kwa Fumbwe yalimfanya atoroke arudi nyumbani kwa wazazi. Chambilecho wahenga, ng’ombe akivunjika guu malishoni hujikokota zizini kusaidiwa. Hali ilikuwa kinyume sana katika maisha ya Kibibi. Alitoroka kwa Fumbwe akarudi nyumbani akiwa na matarajio kuwa angekaribishwa na kusaidiwa wakati alipokuwa anapitia hali ngumu maishani.

Kinyume cha matarajio yake, Kibibi alifukuzwa kama mbwa koko na wazazi wake. Babake alimwambia kuwa alikuwa amewaaibisha sana na akaamrisha kuiona nyumba yao paa. Kwa kweli huu ulikuwa ni unyanyasaji wa hali ya juu sana. Wazazi wa Kibibi hawakutaka kumsikiliza wala kumpa wakati kuwaeleza kilichofanyika. Walimuona mwana wao kama mkosaji na hivyo kuamuru awaondokee mara moja. Swali ni kwamba, wazazi hawa walitarajia mtoto aende wapi ilhali wao ndio waliokuwa chanzo cha haya yote yaliyomfika Kibibi? Kama wangempeleka shuleni wangeiepuka aibu waliyodai alikuwa amewaletea.

Kibibi alijaribu akatembelea ofisi za watetezi wa haki za binadamu na pia wakuu wa serikali. Lengo lake lilikuwa kusaidiwa kumchukulia Fumbwe hatua kutokana na kitendo chake cha unyama alichomfanyia Kibibi. Kibibi alidhulumiwa kwa maana hata vyombo vya serikali alivyotarajia kumsaidia, havikuweza. Mwandishi anasema:

**119.** *Sijui kahongwa au nini! Mpaka lini wanawake tutabaki kwenye dhiki hii? Wangapi waliotendwa kama mimi? Wakienda kwenye vyombo vya sheria wanakumbana na waume? (Kala Tufaha, uk.100)*

Juhudi za Kibibi kupeleka kesi kwenye ofisi za Jumuiya ya Wanasheria Wanawake hazikumfaa kwa vile hakusaidiwa. Wanawake watetezi aliotarajia wamsaidie walihongwa na hivyo hawakumpa Kibibi msaada wowote. Matendo ya wahusika kama Fumbwe yasipokomeshwa ndiyo yanaweza kuchangia kusambaza ugonjwa wa UKIMWI katika jamii. Msanii anasema, “*Sijui kahongwa au nini! Mpaka lini wanawake tutabaki kwenye dhiki hii? Wangapi waliotendwa kama mimi?*” Fumbwe alitumia cheo chake na uwezo wake kiuchumi kuharibu ushahidi na kuhonga wote waliohusika na kesi ya Kibibi na hivyo ikakosa kuleta matokeo ya kumsaidia Kibibi. Fumbwe aliagiza vibaraka wake waende pale Kibibi alipokuwa akiishi wamtishe ili aogope na aachane na kesi hiyo. Aliagiza kwamba wakili wa Kibibi aidha alistahili kutishwa ili aachane na azma yake ya kumtetea Kibibi. Fumbwe alifanya juu chini kuhakikisha kwamba Kibibi hafanikiwi kwa vyovyote vile katika juhudi zake za kutafuta haki. Licha ya kumdhulumu Kibibi kwa kumbaka, bado Fumbwe analemaza kila juhudi zinazofanywa na Kibibi kupigania haki yake.

Mtunzi wa riwaya ya **Kala Tufaha** anazidi kuonyesha namna jamii ilivyomdhulumu mtoto wa kike. Kibibi alipokuwa akifanya biashara katika jiji, alihangaishwa na askari wa manispaa ambao walitaka rushwa kutoka kwake au kumtaka kimapenzi. Tabia ya askari wa manispaa kutaka kufanya ngono na mwanamke yeyote yule waliyempata ilichangia katika kueneza ugonjwa wa UKIMWI katika jamii. Matendo haya yote yanaendeleza dhuluma dhidi ya mwanamke. Mwandishi anasema:

**120.** *Dhiki zaidi ni hao askari wa manispaa; wasipotaka rushwa wanamtaka yeye (Kala Tufaha, uk.132).*

Kibibi alipokuwa anaishi na Ma' Asha, aliamua kufanya biashara ya uchuuzi ndipo apate pesa za matumizi yake na mtoto aliyezaliwa. Alikumbana na changamoto katika harakati zake za kufanya biashara ya uchuuzi. Mwandishi anasema, “*Dhiki zaidi ni hao askari wa manispaa; wasipotaka rushwa wanamtaka yeye.*” Licha ya biashara yake ndogo ya uchuuzi, Kibibi alihangaishwa na askari wa manispaa. Kwa jumla, mwandishi anaonyesha namna jamii ilivyokuwa ikiwanyanyasa watoto wa kike. Dhuluma inafanywa kwa watoto wa kike lakini hakuna njia ambayo wanaweza kuitumia ili kutetea na kupigania haki yao. Ni masikitiko kwamba mtoto wa kike anadhulumiwa kutoka kila sehemu ya maisha yake. Biashara ya uchuuzi aliyofanya ilikuwa ndogo sana lakini bado askari wa manispaa walitaka awahonge. Huu ni unyanyasaji kwa maana Kibibi alifanya hiyo biashara ili awe na uwezo wa kulisha mwanawe.

Katika riwaya ya **Pendo katika Shari**, mwandishi anaonyesha dhuluma inayofanywa dhidi ya wanawake wakati anaposawiri Sulubu akimpiga mkewe. Sulubu ni kati ya wanaume katika jamii walioendeleza taasubi ya kiume. Sulubu alikosa uhusiano mwema na mke wake kutokana na matendo yake ya uovu. Mtunzi anatuelezea:

**121.** *Kila wakati macho yalikuwa utosini akimtamani mwanamke yeyote aliyepita mbele yake. Tabia hiyo ilimfanya mkewe kumtoroka kwani alikuwa anampiga kila mara na kumfukuza ili aweze kustarehe na warembo aliowabadilisha kama nguo (Pendo Katika Shari, uk.12).*

Licha ya udhalimu wa kumpiga mkewe, Sulubu hakuiheshimu ndoa yake kamwe kwa maana alikuwa akistarehe na warembo ainaaina bila aibu yoyote. Twaelezwa kuwa, “*Kila wakati macho yalikuwa utosini akimtamani mwanamke yeyote aliyepita mbele yake. Tabia hiyo ilimfanya mkewe kumtoroka kwani alikuwa anampiga kila mara na kumfukuza ili aweze kustarehe na warembo aliowabadilisha kama nguo.*” Hii ina maana kwamba Sulubu alikuwa na tamaa kubwa ya kufanya mapenzi na

wanawake wengine nje ya ndoa. Twafahamishwa kwamba tabia hiyo ilimfanya mkewe kumtoroka kwani alikuwa anampiga mara kwa mara ili apate fursa na uhuru wa kuwabadilisha wanawake vile alivyopenda. Matendo haya ni ya dhuluma kwa maana yaelekea Sulubu alikuwa akiyafanya bila kujali hisia za mkewe. Sulubu alimdhulumu mkewe kwa kumpiga, aidha kwa kukosa uaminifu katika maisha yake ya ndoa. Matendo ya Sulubu ya kuwabadilisha wanawake kama nguo yalimfanya akaambukizwa ugonjwa wa UKIMWI aliousambaza kwa mkewe baadaye.

Katika riwaya ya **Pendo katika Shari**, mwandishi anaisawiri ndoa ya Sulubu na Pendo kuwa kifungo cha dhuluma. Pendo anaamua kutembelea jirani yake Sauda ili amueleze chanzo cha dhuluma katika ndoa yake. Pendo alihisi kwamba kulikuwa na tatizo kubwa katika maisha yake ya ndoa. Mwandishi anasema:

**122. *Ijapokuwa Sulubu ana umati wa wasichana wanaohiari awabadilishe kama nguo, yupo mmoja kati yao ambaye amemganda kama funza... unajua anakoishi msichana huyo? Pendo alimuuliza huku akiukubali ukweli huo wa mambo. Sijui mwenzangu kama ningalijua, ningalikuwa nishamtia adabu mimi mwenyewe bila usaidizi wako. Lakini mbona hujaniambia haya yote Sauda! Ah! Pendo, singetaka mtengane na mumeo...lakini ya kumleta hadi mwako nyumbani... nilisema potelea mbali nitakwambia. Leo hii huna budi kujua mbivu na mbichi dada (Pendo katika Shari, uk.14-15).***

Kutokana na dondoo lililo hapo juu, ni bayana kuwa Sulubu alikuwa na umati au mlolongo wa wasichana waliotamani awabadilishe kama nguo. Sulubu alikuwa akijihusisha kimapenzi na wasichana wengi wasiohesabika. Sauda ambaye ni jirani wa Sulubu alikuwa akishuhudia visa na visanga ambavyo Sulubu alikuwa akifanya lakini alichelea kumuarifu Pendo wasije wakafarakana na kutengana. Mwandishi anasema, ***“Ijapokuwa Sulubu ana umati wa wasichana wanaohiari awabadilishe kama nguo, yupo mmoja kati yao ambaye amemganda kama funza... lakini ya kumleta hadi mwako nyumbani... nilisema potelea mbali nitakwambia.”*** Sulubu alifikia wakati ambapo aliamua kumleta nyumbani msichana mmoja ambaye alikuwa amemganda

kama funza. Tukio hili lilimkasirisha Sauda mpaka akaamua kumfahamisha Pendo vituko ambavyo Sulubu alikuwa akimfanyia. Sulubu anadhihirisha dhuluma kwa mkewe pale ambapo anakosa kuheshimu kitanda chake cha ndoa. Hana aibu kuwaleta wanawake wengine na kulala nao kitandani nyumbani kwake pasi na mkewe kujua. Tukio hili linamsononesha Pendo anayelia kwa uchungu wakati anafahamishwa na jirani yake Sauda kuhusu kilichokuwa kikiendelea nyumbani kwake. Licha ya Sulubu kumtesa mkewe kisaikolojia, aidha alimuambukiza ugonjwa wa UKIMWI kutokana na tabia yake iliyooza.

Isitoshe, katika riwaya ya **Pendo katika Shari**, mtunzi anadhihirisha dhamira ya dhuluma wakati ambapo Sulubu alimkataza mkewe kufanya biashara ilhali hakuwa anampatia pesa za matumizi. Sulubu hakuwa anakidhi mahitaji ya jamii yake lakini ni kinaya kuwa hakutaka mkewe afanye biashara. Je, alitaka jamii yake ijikimu vipi?

Mwandishi anasema:

**123.** *Sulubu naye alizidi kukaza kamba ya uhasama baina yake na mkewe. Pesa zake zikawa adimu kupatikana kama alivyokuwa yeye. **Kamwe hakutaka mkewe aanzishe biashara ya aina yoyote ili kuyakimu baadhi ya mahitaji yake. Kila alipomwomba mumewe pesa za chakula, nguo au hata za matibabu ya mtoto wao mchanga, Sulubu alimtilia huku akimtolea kule. Aidha, alizidisha ujeuri akawa haambiliki hasemezeki (Pendo katika Shari, uk.15-16).***

Sulubu aliendeleza uhasama baina yake na mkewe. Msanii anatumia kuwa pesa zake zilikuwa adimu kupatikana kama alivyokuwa mwenyewe. Hakuwa anatoa pesa kushughulikia mahitaji ya jamii, aidha hakuwa akipatikana kwake kwa urahisi. Licha ya kumnyima mkewe pesa za matumizi pale nyumbani, Sulubu hakutaka mkewe ajihusishe na biashara ya aina yoyote. Mtunzi anasema, “***Kamwe hakutaka mkewe aanzishe biashara ya aina yoyote ili kuyakimu baadhi ya mahitaji yake. Kila alipomwomba mumewe pesa za chakula, nguo au hata za matibabu ya mtoto wao mchanga, Sulubu alimtilia huku akimtolea kule.***” Hakuthubutu kutoa pesa za



chakula, matibabu na hata nguo za mtoto wao mdogo. Sulubu hakutaka mkewe ashiriki katika biashara, lakini kwa upande mwingine alikataa kumpatia pesa za matumizi ya mahitaji ya kimsingi pale nyumbani. Je, alitaka mkewe aishi kwa njia ipi? Kwa kweli, hii ni dhuluma ya kiwango cha juu sana.

Ili kujikimu kimaisha, Pendo alikaidi masharti ya mumewe na akajenga kibanda ambapo alifanya biashara iliyomsaidia kujikimu. Sulubu kupitia wakala wake Zito, alitekeleza kitendo chake cha udhalimu kwa kuteketeza kibanda cha mkewe na mali yote iliyokuwa ndani. Alimpa shilingi mia mbili akamwambia akanunue petroli na kuteketeza kabisa kibanda cha mkewe Pendo. Zito alifanya kama alivyoambiwa, na baada ya kukiteketeza kibanda usiku huo, alienda kuonana na tajiri wake mahali walipopanga kukutana, kisha akapewa ujira wake.

Kitendo kilichofanywa na Sulubu ni cha kikatili. Kitendo hiki kilimfanya Pendo kulia kwa uchungu sana pamoja na mtoto wake mchanga. Sulubu alikuwa amekataa kuiwajibikia jamii yake kwa kuipatia mahitaji ya kimsingi na ndiye huyo anayehusika katika kuhujumu juhudi anazofanya mkewe kupata pesa za matumizi. Sulubu alitumia pesa zake kwa wanawake warembo aliobadilisha kama nguo usiku na mchana. Licha ya Sulubu kuharibu mali ya jamii, aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI ulioiathiri jamii yake kwa njia hasi.

Mwandishi anaonyesha kwamba, baada ya kuchoma kibanda cha Pendo, Sulubu hakuwa na msamaha wowote ila anazidi kumkashifu na kumkejeli mke wake. Sulubu alimkashifu mkewe akisema kuwa alijenga kibanda karibu na barabara ili mwanamume mpita njia aweze kumsabahi, aidha awahi kufurahi na kupasua vicheko. Alidai kuwa mkewe alikuwa anafanya uzinzi na wanaume wengine. Kwa kweli Sulubu alionyesha udhalimu wa hali ya juu kwa mkewe. Licha ya kuteketeza kibanda

chake na kukataa kumpatia pesa za matumizi, anaendelea kumrushia cheche za matusi akitukana pia mtoto wake anayemwita kitoto ambacho anasema hakiwezi kulinganishwa na sayari ya Zuhura.

Dhamira ya dhuluma inaangaziwa zaidi katika riwaya ya **Pendo katika Shari** tunapozidi kuyarejelea matendo ya Sulubu. Twaelezwa na mwandishi kwamba Sulubu alitupa vitu vya nyumba yake nje pamoja na kuwafukuza wanawe kutoka nyumbani kwake ilipobainika kwamba Pendo alikuwa na virusi vya UKIMWI. Mwandishi anasema:

**124.** *Walimpa Pendo ushauri kuhusu hali yake hiyo kisha Pendo akawaza na kuelekea nyumbani. Alipokaribia nyumba yake, alipata mshtuko mwingine. Vitu vyake vyote vilikuwa vimetupwa nje, wakiwemo wanawe ambao walijiketia pale nje kwa huzuni. Walipomwona mama yao, walimkimbilia, kila mmoja akiwa na kisa kumweleza. Alikuwa na watu wengine wawili wakatoa vitu vyote. Almasi alianza, alikuwa amekasirika sana. Alitutukana na kutufukuza sote nje. Tatu alipomuuliza mbona anatoa vitu vyetu nje, alimpiga kofi na kumrusha nje... Tatu alilia sana (Pendo katika Shari, uk.25).*

Katika dondoo lililo hapo juu, Pendo alikuwa ameenda hospitalini ili apewe ushauri kuhusu hali yake ya kupatwa na ugonjwa wa UKIMWI. Pendo alipokuwa anarudi nyumbani, alipata mshtuko wa maisha yake alipopata vitu vyake vya nyumba pamoja na wanawe wametupwa nje. Aliwakuta watoto wamejiketia pale nje kwa huzuni na masikitiko. Msanii anasema, “*Vitu vyake vyote vilikuwa vimetupwa nje, wakiwemo wanawe ambao walijiketia pale nje kwa huzuni... Tatu alipomuuliza mbona anatoa vitu vyetu nje, alimpiga kofi na kumrusha nje... Tatu alilia sana.*” Walimueleza mama yao vile baba yao alifika nyumbani akiwa amekasirika na kuanza moja kwa moja kurusha vitu nje na kuwaamuru pia watoke. Aliwatukana na hata kumpiga Tatu kofi alipojaribu kumuuliza sababu iliyofanya atende vile alivyotenda. Pendo alihitaji kuhimizwa na kupewa matumaini ya kuishi kutokana na hali yake lakini alichokipata kutoka kwa mumewe Sulubu kilikuwa cha masikitiko makuu. Sulubu aliidhulumu

sana familia yake ambayo haikuwa na hatia. Kitendo cha kuifukuza jamii yake yote kwa sababu ya ugonjwa kweli ni cha kikatili.

Katika riwaya ya **Pendo Katika Shari**, mwandishi anaendeleza dhamira ya dhuluma dhidi ya wanawake anapotuonyesha namna Sulubu aliuza kipande cha shamba na kutumia pesa hizo wazazi wa Rehema kama mahari. Baada ya mahari, Sulubu alimwoa Rehema ilhali watoto wake mwenyewe walikuwa wakiteseka kutokana na ukosefu wa karo. Watoto wake walifukuzwa kutoka shuleni kutokana na ukosefu wa karo. Uchunguzi ulipofanywa, iligunduliwa kwamba Pendo alikuwa ameambukizwa virusi vya UKIMWI. Mwenendo wake wa kuwa na wapenzi wengi na kufanya ngono kiholela ulisababisha amwambukize mkewe Pendo virusi vya UKIMWI. Pendo aliugua pamoja na kitoto chake kilichotangulia kufariki. Pendo alipozidi kuugua Sulubu alikataa kumpeleka hospitalini na hatimaye akaaga dunia. Mwandishi anasema:

**125.** *Walirudi na Sulubu lakini walipofika nyumbani, Rehema alikuwa katika dakika zake za mwisho duniani. Mama yake alijaribu kumsemesha lakini hakumfumbua jicho wala kufungua kinywa. **Sulubu alipoulizwa na wakwe zake iwapo alijaribu kumpeleka mkewe hospitali, aliwajibu kuwa dawa za hospitali hazikufua dafu.** Usiku huo, Rehema aliaga dunia. Bi Kibibi hakuweza kustahimili. Alipiga ukwenzi mkali uliofanya majirani kumiminika nyumbani kwa Sulubu. Walimpata Sulubu akilia kama mtoto mdogo (**Pendo katika Shari, uk.45**).*

Sulubu alikataa kumpeleka Rehema hospitalini hali iliyomwathiri mpaka akaaga dunia kwa maana alikuwa na virusi vya UKIMWI. Mwandishi anasema, “**Sulubu alipoulizwa na wakwe zake iwapo alijaribu kumpeleka mkewe hospitalini, aliwajibu kuwa dawa za hospitali hazikufua dafu.**” Huu ulikuwa udanganyifu kwa maana Sulubu hakujaribu kamwe kumpeleka mkewe hospitalini. Kilio cha Sulubu wakati Rehema alipoaga dunia kilikuwa kama machozi ya mamba. Yeye ndiye aliyekuwa chanzo cha mauti ya mkewe Rehema. Kama hangejikusisha katika vitendo

vya uzinzi na wanawake wengi, hangeambukizwa virusi vya ugonjwa wa UKIMWI ambavyo alimsambazia mke wake. Chanzo cha kifo cha Rehema hakikuwa kingine ila matendo maovu ya uzinifu ya Sulubu. Huu ni udhalimu ambao Sulubu aliudhihirisha kwa jamii yake.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, mwandishi ameshughulikia pia dhamira ya dhuluma. Dhuluma ni unyanyasaji na ugandamizaji wa haki za mtu. Katika riwaya hii, tunamuona mhusika Ngoma akiidhulumu jamii yake. Ngoma aliyaingilia maisha ya anasa na starehe na kusahau wajibu wake kama mume wa jamii yake. Hakuwa anayakidhi mahitaji ya jamaa yake ila alitafuta tu visingizio kuinyanyasa jamaa yake.

Mtunzi anasema:

**126.** *Siku aliyompatia kazi Grace, Omolo alishtushwa na kauli za bwana Ngoma wakati alipokuwa anazozana na mkewe. Ngoma alikuwa anafoka akiuliza sababu na mbinu iliyotumika kumwomba Omolo msaada wa ajira hiyo... Amekusaidia wewe kama nani? (Ua la Faraja, uk.18)*

Matamshi ya Ngoma yanamdhulumu na kumdhalilisha mkewe Tabu. Ngoma hakuamini kuwa Tabu angeomba tu usaidizi kutoka kwa Omolo kwa roho safi. Msanii anasema, “*Ngoma alikuwa anatoka akiuliza sababu na mbinu iliyotumika kumwomba Omolo msaada wa ajira hiyo. Amekusaidia wewe kama nani?*” Kwake aliona kuwa huenda kulikuwa na uhusiano wa kimapenzi kati ya Omolo na mkewe ndipo akakubali kumsaidia. Ngoma alikuwa akiuliza sababu na mbinu iliyotumika kumwomba Omolo msaada wa ajira hiyo na alitaka kujua alisaidiwa kama nani. Kwa hakika, huu ni udhalimu ambapo Ngoma hakuamini kwamba mkewe Tabu angeweza kufanikiwa kutekeleza jukumu kama hilo muhimu. Kwa vile yeye alikuwa anajihusisha mara kwa mara katika uhusiano na wanawake wengine nje ya ndoa, alidhani mkewe pia alikuwa na tabia kama hiyo.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, Ngoma aliiendeleza dhamira ya dhuluma kwa vile licha ya utajiri na mali nyingi aliyokuwa nayo, jamii yake iliishi maisha ya umaskini. Utajiri wake haukuifaa aila yake ila uliwafaa wanawake wengine nje ya ndoa. Matendo ya Ngoma ya kufanya ngono na wanawake wengi nje ya ndoa ulisababisha akaambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Msanii anasema:

**127. *Juma alimchukia baba yake kwa kutomjali mamake na kumsababisha ajishughulisha na biashara ya kupika vitumbua na chapati, kuuza genge la mboga ili apate pesa za kujinunulia mahitaji yake. Ngoma alikuwa tajiri. Sasa Juma alijiuliza; kama baba yake ana pesa nyingi za kulewa pombe, kwa nini mama yake anaishi maisha ya kimaskini? (Ua la Faraja, uk.34)***

Tabia ya Ngoma ya kutojishughulisha na mahitaji ya jamii yake ilimfanya mwanawe Juma kumchukia. Mtunzi anasema, “*Juma alimchukia baba yake kwa kutomjali mamake na kumsababisha ajishughulisha na biashara ya kupika vitumbua na chapati, kuuza genge la mboga ili apate pesa za kujinunulia mahitaji yake*”. Katika dondoo hili inaonekana kuwa, Tabu alilazimika kufanya biashara ndogondogo ili kukidhi mahitaji ya jamii. Tabu alilazimika kufanya biashara ya kupika vitumbua na chapati, kuuza genge la mboga ili apate pesa za kujinunulia mahitaji yake. Ngoma alikataa kimaksudi kuisaidia familia yake kwa vile tunaelezwa kuwa alikuwa mtu tajiri. Juma alifahamu kuwa Ngoma alikuwa na kipato kizuri lakini hakuijali familia yake. Pesa zake ziliishia kwenye pombe na wanawake nje ya ndoa, jambo lililomkasirisha sana Juma na mamake. Tabia ya Ngoma ya ulevi na uasherati ilisababisha akapata ugonjwa wa UKIMWI. Kama Ngoma angetumia utajiri wake kuisaidia familia yake, hangeutumia ovyo mpaka akapata UKIMWI aliosambaza kwa mkewe wake.

Ukosefu wa uwajibikaji wa Ngoma kama mume na baba ya watoto unaonyesha namna alivyoamua kuidhulumu jamaa yake kimaksudi. Mhusika Ngoma hakuonyesha

upendo wowote kwa familia yake. Kwa mfano, anamfokea Juma wakati ambapo alichelewa kutoka shuleni na akamlazimisha kwenda kuswali kabla ya kwenda shuleni. Tukio hili lilifanyika baada ya Ngoma kujifanya amebadilika kwa kuacha pombe na wanawake na kumrudia Mungu. Ngoma alimlazimisha mwanawe Juma kwenda msikitini mara tatu kwa siku bila ya kuyazingatia mengine ambayo alikuwa anayatekeleza. Dhamira ya dhuluma inajitokeza katika muktadha huu kwa vile Ngoma hakutaka Tabu aendeleo na biashara yake iliyomsaidia kukidhi mahitaji ya jamii. Aidha, Juma alilazimishwa kwenda kuswali mara kadhaa kwa siku pasipo kuzingatia kwamba suala la imani lilitokana na uamuzi wa mtu binafsi na wala si la kulazimishwa.

Ngoma alizidi kudhihirisha udhalimu wake kwa jamii yake. Tabu alivumilia vituko na visanga vyote vya maisha ya uzinifu wa Ngoma. Licha ya uvumilivu wote ambao Tabu alionyesha, twaelezwa na msanii kwamba Ngoma alimpa talaka mkewe Tabu. Matendo ya Ngoma na mizozano baina yake na mkewe yalichangia pakubwa katika kutolewa kwa talaka. Sababu kuu iliyosababisha talaka ambayo Ngoma alitoa ni kwamba, Tabu aliirudia dini yake ya awali ya Ukristo na kuuacha Uislamu. Kitendo hiki kilimkasirisha Ngoma sana. Ngoma alisahau kuwa kuna uhuru wa kuabudu na huwezi kulazimisha mtu kuingia dini ambayo imani yake haijaikubali. Uamuzi wa kutoa talaka kwa misingi ya imani ni wa kidhalimu na unapaswa kukemewa na kulaaniwa. Talaka hii ilikuwa inadhulumu Tabu kwani ililenga kumtenga Tabu na urithi wa mali ya Ngoma wakati ukitimia.

Aidha, Ngoma anazidi kudhihirisha udhalimu wake kwa jamaa yake wakati ambapo anamlaani mwanawe Juma. Pamoja na kumlaani Juma, Ngoma anamkana mwanawe na kutangaza kwamba amemwondoa kwenye orodha ya wanawe. Matendo na

matamshi kama haya, yote kutoka kwa baba mzazi ni ya kusikitisha. Licha ya tofauti zilizotokea baina ya Ngoma na mwanawe Juma, hangefikia kiwango cha kumlaani na kumkana mwanawe. Juma alikuwa na uchungu kwa Ngoma kwa vile alikuwa anamtesa mamake kwa kutomjali na kwa kumwambukiza ugonjwa wa UKIMWI.

Mhusika Juma anaona kwamba babake Ngoma amemdhulumu sana mamake. Kwa maoni ya Juma, matendo ya Ngoma aliyofanyia mamake yalikuwa ya kikatili. Licha ya ya kumdhulumu mkewe kisaikolojia, alimuambukiza ugonjwa wa UKIMWI uliomtatiza sana. Ngoma alipodai amebadilika na kuyaacha matendo yake ya kale, alitaka kuilazimisha jamaa yake kufanya mambo vile yeye alivyotaka. Kitendo cha kulazimisha Juma aende msikitini kila mara hakikumfurahisha Juma aliyekataa katakata kuzingatia maagizo aliyopewa na Ngoma. Hili pamoja na mengine yakasababisha Ngoma kumkana na kumlaani mwanawe. Kitendo hiki ni cha kidhalimu kwa maana utangamano katika jamii yoyote unahitaji mashauriano na wala si amri na vitisho. Kwa hakika, matendo ya Ngoma kwa jamii yake yalikuwa ya kusikitisha kwa vile hakujali wala kuishughulikia ilivyopasa lakini badala yake aliiletea dhiki kuu.

Katika sehemu hii, tumehakiki suala la dhuluma dhidi ya wanawake na namna linavyowasilishwa na wasanii mbalimbali katika kazi zao. Tumeona kwamba wanawake wanadhulumiwa katika jamii hali inayofanya baadhi yao kuathirika na ugonjwa wa UKIMWI. Matendo yanayofanyika na baadhi ya wahusika ni ya kugandamiza na yananyima baadhi yao haki za kimsingi za kibinadamu. Katika sehemu inayofuata, tumechunguza suala la utamaushi.

## 5.4 Utamaushi

Njogu na Wafula (2007) wanasema kwamba utamaushi au udhanaishi ni falsafa kuhusu dhana ya maisha. Ni falsafa inayohusiana na utamaushi unaotokana na neno “kutamauka”. Kutamauka ni kutokuwa na furaha au kutokuwa na tamaa kwa kuhisi kukosa matumaini katika maisha. Utamaushi ni tendo la kukata tamaa maishani kwa kuona kuwa maisha hayana maana tena kwa mhusika.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, tunaonyeshwa namna ambavyo wahusika kadhaa wametamauka maishani mwao. Mhusika mmoja ambaye mwandishi anamsawiri ni Omolo. Kwa muda mrefu sana Omolo aliishi maisha ya upweke na kwa kipindi kirefu sana aliishi bila kuo. Aidha, mhusika huyu hakufurahia kuwa na uhusiano wa kimapenzi na watu wa jinsia ya kike ambao alikuwa akiwaambaa. Omolo alifikia wakati ambapo alikuwa anajiuliza maswali mengi sana kuhusu maana ya maisha.

Mwandishi anasema:

**128.** *Omolo alipenda kujiuliza swali hili akimaanisha; faida ya maisha ni nini? Kwa nini mtu ahangaike kufanya kazi ili apate pesa, akishazipata azitumie ziiishe? Kuna manufaa gani au raha gani ya ajabu iliyowafanya watu wayahangaikie maisha? Alishangaa kwa nini hata yule mwenye maisha ya shida anapougua na kukaribia kifo hafurahi kwisha kwa shida zake akifa bali huhangaika kujitibu ili apone aendelee na shida zake (Ua la Faraja, uk.23).*

Msanii akitumia mbinu ya uzungumzi nafsia, anaonyesha namna Omolo alivyokuwa akijiuliza maswali fulani maishani mwake. Omolo alitaka kujua faida ya maisha ni nini. Mtunzi anasema, “*faida ya maisha ni nini? Kwa nini mtu ahangaike kufanya kazi ili apate pesa, akishazipata azitumie ziiishe?*” Omolo alitaka kujua manufaa au raha gani ya ajabu inayowafanya watu kuyahangaikia maisha. Kwa maoni ya Omolo watu hujishughulisha sana maishani kutafuta pesa kwa kufanya biashara, kujishughulisha na kilimo, kusoma, kufanya kazi ya kuajiriwa na wengine kuwaibia watu. Watu hawa wote hupata pesa na kuzitumia mpaka zikaisha.



Mhusika huyu anahoji ikiwa kuna faida yoyote maishani kufanya mambo haya yote siku nenda siku rudi. Isitoshe, anashangazwa na tabia ya wanadamu kwa maana hata wale walio na shida wanapokuwa wagonjwa, hushughulika watibiwe wapone badala ya kujiachilia wafe ili waepukane na shida za ulimwengu. Msanii anasema, *“Alishangaa kwa nini hata yule mwenye maisha ya shida anapougua na kukaribia kifo hafurahi kwisha kwa shida zake akifa bali huhangaika kujitibu ili apona aendelee na shida zake.”* Mtazamo wa Omolo maishani ni kwamba, mtu anapokuwa na shida au magonjwa anastahili kufurahi kwa maana akifariki basi shida zake zitakuwa zimemalizika. Mwandishi anaonyesha baadhi ya watu maishani kama vile Omolo ambao hawaoni faida yoyote ya kuishi na hivyo kuiendeleza dhamira yake ya utamaushi. Maisha hayana faida au maana yoyote kwa watu kama hawa.

Mhusika mwingine aliyetumiwa pakubwa na mwandishi katika riwaya ya **Ua la Faraja** kuendeleza dhamira ya utamaushi alikuwa Queen. Queen aliugua kwa muda mrefu mpaka akafikia kiwango ambapo alikuwa amekata tamaa. Hakuona faida ya maisha. Akiwa na rafikiye Omolo, walishikilia msimamo wao kuhusu udhanaishi. Mtazamo wake ulikuwa kwamba kuwepo katika ulimwengu huu hakukuwa na maana kamwe. Aliichukia fahari yote aliyokuwa nayo huko nyuma, ambayo sasa ilikuwa inaelekea ukingoni. Mhusika Queen alishangaa kwa nini afanye juhudi katika maisha kisha baada ya kufanikiwa afe. Yeye alishindwa kukabiliana na ukweli huu kuwa alikuwa na maradhi ya UKIMWI. Kwake UKIMWI ulikuwa kifo. Hakuelewa kwamba hata ukiugua UKIMWI, kulikuwa na njia ya kuyarefusha maisha kwa kutumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI. Mhusika Queen alitamauka maishani. Anasema:

**129.** *Adhabu gani hii? Alisema mwenyewe huku akila. Kweli aliyaona maisha ni adhabu: kuzaliwa, kuyaonja na kisha kunyang'anywa na kifo! Raha zote hazikuwa na maana tena. Zimepotea kwenye*

***kumbukumbu yake. Kilichokuwemo kichwani mwake ni yale mawazo ya kuukaribia mwisho wake (Ua la Faraja, uk.68).***

Mhusika huyu anaendeleza dhamira ya mwandishi ya utamaushi kwani aliyaona maisha kama adhabu. Anakumbuka vile alivyong'ang'ana na masomo shuleni na chuoni na vile alivyong'ang'ana na kazi. Anaona ulimwengu ukikosa huruma kwa maana mtu huzaliwa, akayaonja maisha na kisha kifo humchukua au humnyang'anya. Queen anatumieza kwamba, ***“Kweli aliyaona maisha ni adhabu: kuzaliwa, kuyaonja na kisha kunyang'anywa na kifo! Raha zote hazikuwa na maana tena. Zimepotea kwenye kumbukumbu yake. Kilichokuwemo kichwani mwake ni yale mawazo ya kuukaribia mwisho wake.”*** Anakumbuka raha na starehe zote ambazo alifanya ambazo hazikuwa na maana tena kwa vile kilichomtawala na kumshughulisha wakati huo ni mawazo ya kuukaribia mwisho wa maisha yake ulimwenguni.

Ukweli kuwa Queen alikuwa afe ndio ulioyatawala maisha yake. Alishindwa kukabiliana na unyanyapaa uliozingira maradhi ya UKIMWI. Afya yake ilizidi kuzorota na baada ya miezi mitatu, jeraha waliloliita mkanda wa jeshi lilipona baada ya matibabu ya muda mrefu hospitalini lakini sasa kifua kikuu ndicho kilichomsumbua. Aidha, mhusika Queen alifikia kiwango ambapo hakuona haja ya kutumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI. Hakuona tofauti kati ya kuishi miaka hamsini na mia moja, au yule anayekufa leo na yule aliyeishi siku chache au siku nyingi. Queen alikuwa amekata tamaa hakika katika maisha yake.

Mamake Queen alipoletwa na Omolo, Queen alimkabidhi wosia wake. Baada ya kukamilika kwa wosia, aliandaa karamu ndogo waliyosherehekea na mamake kisha usiku huo akameza vidonge zaidi vya usingizi vilivyosababisha kifo chake. Queen alikuwa mdhanaishi na hivyo ndivyo alivyomaliza maisha yake. Afya yake ilikuwa imedhoofika sana kutokana na athari ya ugonjwa wa UKIMWI. Ni kweli kwamba

Queen hakuona maana ya maisha na hali ya kuendelea kuwatatiza watu wengine hususan mamake na hivyo akaamua kuyaondoa maisha yake katika ulimwengu huu. Queen aliona angekufa kifo cha aibu kutokana na ugonjwa wa UKIMWI na hivyo akaamua kujitoa uhai mapema. Queen alijitoa uhai kwa kutamauka kabisa maishani mwake.

Dhamira ya utamaushi aidha imewasilishwa na mwandishi wa tamthilia ya **Giza**. Kuna wahusika kadha wa kadha ambao wametumika na mwandishi kuwasilisha dhamira hii. Mhusika wa kwanza ambaye mwandishi amemtumia ni Nuru. Nuru amesawiriwa kuwa mhusika asiyeona manufaa ya masomo na hata maisha. Mwandishi anasema:

**130.** *Nuru: Nasoma ili iweje? Sioni sababu ya kusoma kwani sitapata nafasi ya kufaidi matunda ya mateso shuleni. Hata wazazi wangu walionizaa na kunigharamia maisha yangu hawatapata nafasi ya kufurahia matunda ya kazi yao bali wataambulia huzuni na mateso pamoja na majuto yasiyoisha (anainua macho na kutazama juu) Nini maana ya maisha? Eti ninasoma nipate digrii ya nini? Mbona naona giza tu! Giza! Giza! Aah! Sioni mbele niendako wala nyuma nitokako (Giza, uk.7).*

Katika dondoo lililionukuliwa , mhusika Nuru anaugua moyoni mwake hasa akifikiria ufupi wa maisha yake. Ameanza kuhisi kuwa huenda asiishi kwa muda mrefu kutokana na hatari ya kuangamizwa na ugonjwa wa UKIMWI. Anasema, “*Sioni sababu ya kusoma kwani sitapata nafasi ya kufaidi matunda ya mateso shuleni. Hata wazazi wangu walionizaa na kunigharamia maisha yangu hawatapata nafasi ya kufurahia matunda ya kazi yao bali wataambulia huzuni na mateso pamoja na majuto yasiyoisha.*” Hii ndiyo sababu anasema kuwa haoni umuhimu wowote wa kusoma kwani hataonja faida ya jasho lake. Aidha, wazazi wake hawatafurahia juhudi zao za kugharamia masomo yake. Anaona kwamba badala ya wazazi wake kufurahia

matunda ya jasho lao kwa kujinyima kwa sababu yake, wataambulia huzuni na mateso pamoja na majuto yasiyoisha.

Katika muktadha huu, Nuru anajuta kwa kuwa hakuona maana ya maisha na masomo yake. Nuru aliyaona maisha kama yasiyokuwa na faida yoyote kwake. Aidha, hakuona umuhimu wa kusoma apate digrii ambayo anaona kuwa haingekuwa na manufaa yoyote maishani mwake. Kwa jumla, Nuru anaonyesha kwamba hakukuwa na haja ya watu kung'ang'ana na kushughulika na vitu vya ulimwengu kwa maana mwishowe watakufa na kuviacha vikiwa havijawafaidi. Hii ndiyo sababu anaonyesha kutamauka kwake maishani. Ni kweli kwamba Nuru hatimaye alikufa kutokana na athari ya ugonjwa wa UKIMWI.

Katika muktadha mwingine, baada ya kusoma ujumbe uliokuwa kwenye fulana ya kijana: **UNARINGA UMEPIMA GIZA!**, Nuru anaanza kuwa na mtazamo tofauti kuhusu maisha yake. Kupitia kwa mhusika Nuru, mwandishi anaonyesha hali ya utamaushi wa watu katika jamii ambao hawakujua hali zao za afya. Anasema thamani ya pesa na elimu kwao ni bure kwa maana huenda tayari walikuwa wameambukizwa virusi vya UKIMWI. Katika sehemu nyingine ya tamthilia, mhusika Nuru anaelekea kumlaumu Mungu kwa kumuuliza sababu ya kuruhusu waja kuteseka. Anauliza sababu ya Mungu kuumba watu tu ili wahangaika na maisha ya dunia. Katika onyesho la kumi anasema, **“Mungu anapenda sisi tuteseke? Hana huruma? Alituumba ili iweje?”** (uk. 40) Mazungumzo na maswali haya yote yanathibitisha kuwa Nuru alikuwa ametamauka na hakuona namna ambavyo angeendelea kuishi katika dunia hii. Baada ya mumewe Steve kufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI, Nuru hatimaye pia alimfuata kwa kifo kilichotokana na ugonjwa wa UKIMWI.

Mhusika mwingine ambaye ametumika na mtunzi wa tamthilia ya **Giza** kuendeleza dhamira ya utamaushi ni Robby. Robby ni mhusika ambaye alipenda raha na starehe maishani. Alijihusisha na maisha hatari hasa katika enzi ambapo ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa umeenea na kuwa hatari sana kwa maisha ya wanadamu. Msanii anatueleza kwamba ulifika wakati maishani mwake ambapo alianza kujutia aina ya maisha ambayo alikuwa akiyaishi. Mtunzi anatueleza:

**131.** *Robby: Davina! Davina! Kweli amekufa! Lakini... sina hakika. Nakumbuka rafiki yangu Kapu alionionya juu ya mapenzi yangu na Davina, sikumsikiliza. Sasa nitakufa. Nitakufa vibaya eti wanasema hata Mmh! Kitu inakatika. Basi zangu zimekwisha. Niache chuo. Nikasubiri kifo. Kufa kibudu, kifo cha majuto. Robby mie hata sijaishi bado. Eeh niliishi lini? Sitakuwa na familia wala kazi, sitayaona maisha. Maisha ambayo kila mtu huyapitia. Nasoma ili iweje? Nasogeza siku? Maskini baba na mama yangu! Wangejua (Giza, uk.10).*

Katika dondoo hili, Robby anaona kwamba maisha yake yatakatika hivi punde. Anasema, “*Sasa nitakufa. Nitakufa vibaya eti wanasema hata Mmh!*” Anajuta kuhusu mapenzi yake na Davina aliyokatazwa na rafikiye Kapu lakini akapuuza akidhani rafikiye hakumtaka mema lakini alitaka kumkosesha raha zake za dunia. Mapenzi hayo yalimletea baa maishani kwani aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Anazidi kusema, “*Niache chuo. Nikasubiri kifo. Kufa kibudu, kifo cha majuto.*”

Robby alianza kujuta kwamba anaenda kuacha kusoma kwenye chuo na kusubiri kufa kibudu kwa kifo alichokiona ni cha cha majuto. Anajuta kuwa alikuwa bado kijana na hakuwa ameishi ulimwenguni vya kutosha. Anasema, “*Sitakuwa na familia wala kazi, sitayaona maisha... Nasoma ili iweje?*” Mhusika huyu anajuta kwamba hatafanikiwa kuwa na familia katika maisha yake na hatayaonja na kuyaona maisha ya mtu anapokuwa na familia. Anajuta kwamba hatafanikiwa kuyaishi maisha ambayo kila mtu huyapitia akiwa duniani. Hakuona haja ya kusoma kwani aliamini kuwa alikuwa anasogeza siku tu huku akisubiri kifo. Anawasikitikia wazazi wake kwa kuwa

hawataweza kufaidi jasho la kazi yao ya malezi. Jamii hii iliamini kuwa kupata UKIMWI ilikuwa sawa na kujikatia tiketi ya moja kwa moja kwenda ahera. Kwa sababu hiyo, Robby alitamauka sana akaona kwamba hataendelea kuishi amalize kusoma ili afurahie kazi na awe na jamii. Kwa maoni yake, alichosubiri tu kilikuwa kifo chake. Kwa hakika huu ni utamaushi kwa maana kwake maisha yalikuwa yamekosa maana.

Mwandishi pia anasawiri mhusika Suzi akiendeleza dhamira ya utamaushi. Anatueleza maisha magumu ya Suzi na namna anavyokabiliana nayo. Suzi anatueleza alivyopoteza watu wa karibu sana katika maisha yake. Mateso na vifo vya mamake na dadake mdogo vilimtamausha sana. Mwandishi anasema:

**132. SUZI: *Wasamaria walinisaidia kumzika. Na maisha yangu tangu siku hiyo yakabadilika nikawa sitafuti tena chakula, cha nini? Namtafutia nani? Basi nikaanza kuugua sana na kila siku nilikunywa asprini (Giza, uk.16).***

Vifo vya watu wa karibu sana kuanzia mamake na mdogo wake Suzi viliyaathiri kwa njia hasi maisha yake. Anasema, “*Na maisha yangu tangu siku hiyo yakabadilika nikawa sitafuti tena chakula, cha nini? Namtafutia nani? Basi nikaanza kuugua sana na kila siku nilikunywa asprini.*” Suzi anakumbuka kifo katili cha marehemu mamake aliyenyongwa na babake wa kambo. Anakumbuka vile alibakwa na babake wa kambo. Dadake mdogo naye alikufa akiwa mikononi mwake. Suzi anasema kuwa baada ya vifo hivyo, hakuona wa kutafutia chakula na hivyo kumaanisha kwamba yeye hakuwa anakula. Alianza kuugua sana kwa maana upele ulikuwa umemharibu, alikuwa anakohoa sana na pia alikuwa amedhoofika mwili. Alikuwa akiugua ila hakupata matibabu bora kwa maana anatueleza kuwa alikuwa akinywa asprini kila siku. Suzi alikuwa ameathirika vibaya na ugonjwa wa UKIMWI ambao ulikuwa unamla polepole. Suzi alifikia kiwango ambapo alikuwa amekata tamaa maishani.

Hali hii ilimsukuma Suzi na baada ya muda mfupi mwandishi anatumia kuwa Suzi pia alifariki.

Mhusika Mona katika tamthilia ya **Giza** ametumika pakubwa katika kuendeleza dhamira ya uatamushi. Ni mhusika ambaye alitambua kuwa amekaribia kufariki na hivyo akaamua kufanya mambo kwa namna ya kulipiza kisasi. Mona ni kati ya watu ambao wakipata shida husema kuwa hawawezi kufa peke yao. Kupitia kwa mhusika huyu, mwandishi anatumia yale ambayo Mona alifanya. Anasema:

**133. MONA: *Najua naenda kufa (anawaza) hivi kweli huu ni UKIMWI? Mbona Robby alikufa kwa ajali ya gari? (Giza, uk.26)***

Katika dondoo lililonukuliwa hapo juu, Mona tayari alikuwa anajua kuwa alikuwa njiani kuelekea ahera kwa maana alikuwa amepata virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Anasema, “**Najua naenda kufa (anawaza) hivi kweli huu ni UKIMWI?**” Hata hivyo, bado anatumia kwa nini mpenzi wake Robby alikufa kutokana na ajali ya barabarani. Hakuona kuwa Robby alijirusha barabarani agongwe na gari ili ijulikane kuwa kifo chake kilitokana na ajali na wala si ugonjwa wa UKIMWI. Ukweli ni kuwa Robby alikuwa ameambukizwa virusi vya UKIMWI. Katika sehemu nyingine ya tamthilia hii, sehemu ya onyesho la nane, mwandishi anasema, “**Hata mimi ningewaachia, mali ni nini ikiwa tayari nina UKIMWI? Hata nikizichukua napeleka ugomvi kwetu, nikifa nao wazigombanie.**” Mona hakuona umuhimu wa kuwa na mali ilhali tayari alikuwa na virusi vya UKIMWI. Hakuona haja ya kung`ang`nia mali kwa maana haingemfaidi yeye kama mtu binafsi. Kilele cha utamaushi wa Mona kinaonekana wakati alipogundua alikuwa na virusi vya UKIMWI. Aliamua kutomkataa mwanamume yeyote aliyetaka kufanya mapenzi naye. Alitumia ngono kama kitega-uchumi kilichomwezesha kupata pesa ambazo alisema

alitumia kununua dawa za kumwongeza siku. Matendo haya ni ishara ya kutosha kuwa mhusika huyu kweli alikuwa ametamauka.

Katika tamthilia ya **Giza** kwa ujumla, mwandishi anatueleza kuwa jamii iliyozungumziwa iliamini kuwa mtu anapopata UKIMWI basi huo ndio mwisho wake. Kutokana na mtazamo huu, ni wazi kuwa jamii hii ilikosa elimu na mafunzo ya kutosha kuwaeleza watu kwamba kupata UKIMWI sio mwisho wa maisha. Hii ndiyo sababu kila mhusika aliyepata UKIMWI katika tamthilia hii alitamauka kwa maana alijua kuwa bila shaka anazihesabu tu siku zake katika dunia hii. Katika sehemu hii, msanii ametuonyesha namna wahusika mbalimbali walivyotamuka maishani na kukosa matumaini maishani. Katika sehemu inayofuata, tutajadili namna ambavyo jamii imelishughulikia suala la usiri kuhusu ugonjwa wa UKIMWI.

### **5.5 Usiri Kuhusu Ugonjwa wa UKIMWI**

Jamii mbalimbali ziliukabili ugonjwa wa UKIMWI kwa mitazamo iliyohitilafiana. Baadhi ya jamii hazikutaka kuuzungumzia ugonjwa wa UKIMWI kwa uwazi. Mwandishi wa riwaya ya **Sitaki Iwe Siri** anayamulika masuala ya jamii yanayoghubika ugonjwa wa UKIMWI. Kwa muda mrefu, ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa unawaua watu lakini jamii haikutaka kuuzungumzia kwa uwazi. UKIMWI ulitangazwa kuwa janga na Rais Daniel Arap Moi wa Kenya mwaka wa 1999. Hii ilitokana na idadi kubwa ya vifo, uyatima na gharama kubwa kwa serikali ya kutibu waliougua. Maradhi haya mwanzoni yalizungumziwa kwa sauti ya chini lakini sasa yakaanza kutangazwa.

Katika riwaya ya **Sitaki Iwe Siri**, mwandishi anaonyesha kuwa ugonjwa wa UKIMWI ulidhaniwa kusababishwa na uchawi au uganga. Mtazamo kama huu ulishikiliwa na baadhi ya watu ambao hawakutaka kujua ukweli kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Kwa



vile baadhi ya jamii ziliunasibisha na uganga au uchawi, jamii nyingi ziliuogopa ugonjwa wa UKIMWI na hazikutaka kuuzungumzia hadharani. Mwandishi anasema:

**134.** *Vifo hivyo vilikuwa vimeutia kovu moyo wake. Yusufu na mke wake waliugua kwa muda mrefu sana na hatimaye kusalimu amri. Nyanya alitumia rasilimali nyingi kugharamia matibabu yao, lakini ndwele hiyo haikusikia dawa. Kutwa kucha, afya zao zilizidi kudhoofika. Wakakonda kama ng'onda na macho yao kuwaingia ndani. Mbavu zao zikaweza kuhesabika. Kafara nazo zikawa kazi bure. Hatimaye, nyanya alienda kwa waganga wa mitishamba, tunguri na hirizi (Sitaki Iwe Siri, uk.10).*

Nyanya Mwalonga alijaribu kwa kila hali kuyaokoa maisha ya mwanawe Yusufu Matano na mkewe Honorata Matano lakini hakufanikiwa. Alitumia fedha nyingi na hata mwishoni kuamini kwamba watoto wake walikuwa wamerogwa lakini hata juhudi zake za kuenda kwa waganga hazikufua dafu. Mtunzi anasema, “*Hatimaye, nyanya alienda kwa waganga wa mitishamba, tunguri na hirizi*”. Haya yote aliyafanya kwa maana aliamini kwamba chanzo cha ugonjwa wa UKIMWI kilikuwa uchawi na uganga. Wajukuu wa nyanya Mwalonga walitaka kujua kilichowaua wazazi wao mpaka wakabaki mayatima. Nyanya yao alikuwa anawapa jibu kwamba ni maradhi yaliyowaua bila kuwaambia ni maradhi ya aina gani.

Katika miaka ya mwanzo, walikubali maelezo hayo kwa sababu ya utoto. Lakini miaka kumi baadaye walitaka nyanya awaambie jina halisi la ugonjwa ambao uliwaua wazazi wao. Nyanya Mwalonga alipata taabu sana kujibu swali hili. Ugumu ulitokana na msimamo wa jamii kuhusu maradhi yaliyowaua wazazi wa wajukuu wake. Maradhi yenyewe yalichukuliwa kuwa ni laana kubwa kwa jamii. Kila aliyegua maradhi haya alianza kuepukwa kama mgonjwa wa ukoma. Akaogopwa jinsi yanavyoogopwa mauti. Akabaguliwa na jamii. Maradhi yenyewe yakachukuliwa kuwa ni muhuri wa mauti kwa kila aliyekumbwa na mkosi wa kuambukizwa. Kutokana na misimamo hii ya jamii kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, nyanya aliamua

kuuficha au kuusitiri ugonjwa kwa wajukuu wake. Katika riwaya, nyanya aliapa kuwa **“Nataka iwe siri.”** Aliapa kuhifadhi moyoni mwake siri kuhusu aina ya maradhi yaliyowaua wazazi wa wajukuu zake.

Wizara ya Afya kwa ushirikiano na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) iliandaa shindano la uandishi wa insha kuhusu UKIMWI kwa wanafunzi wa shule za msingi nchini. Hii ilikuwa njia moja ya kuadhimisha siku ya UKIMWI ulimwenguni. Wanafunzi walipewa changamoto ya kushiriki katika shindano hili na kijana Musa akawa mwanafunzi wa pekee aliyeamua kushiriki katika shindano hili. Musa alikuwa mjukuu wa Mwalonga ambaye alipoteza wazazi kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Katika juhudi zake za utafiti, Musa alipata maelezo kutoka kwa mkutubi wa maktaba kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anasema:

**135.** *Ah... ni mada nzuri sana. UKIMWI ni miongoni mwa masuala ibuka katika jamii zetu za ulimwengu wa sasa. **Suala la UKIMWI halijazungumziwa na kuwekwa wazi katika jamii. Kwa sababu ya ugonjwa huu kuchukuliwa kuwa ni mwiko** (Sitaki Iwe Siri, uk.24).*

Mkutubi wa maktaba ya shule ya Hekima pia anathibitisha msimamo ambao jamii ilikuwa nao kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Anasema, **“Suala la UKIMWI halijazungumziwa na kuwekwa wazi katika jamii. Kwa sababu ya ugonjwa huu kuchukuliwa kuwa ni mwiko.”** Ugonjwa huu ulichukuliwa kuwa mwiko na haukustahili kuzungumziwa hadharani na watu katika jamii. Mhusika Musa alianza kufanya utafiti kuhusu mada yake. Alitembelea maktaba mbalimbali na hata alipanga kutembelea hospitali. Musa aliomba nyanya ruhusa kwenda katika hospitali ya wilaya ya Kericho kuzungumza na daktari ili kutafuta habari mbalimbali kuhusu maradhi ya UKIMWI kwa minajili ya uandishi wake wa insha. Nyanya Mwalonga alianza kuwa na shaka aliposikia ombi la Musa. Mwandishi anasema:

**136.** *Nyanya alihangaishwa sana na habari hiyo. “Siri ambayo nimekuwa nikiweka jinsi kaburi linavyohifadhi siri hatimaye itajulikana!” Nyanya aliwaza huku akikubali ombi la Musa (Sitaki Iwe Siri, uk.28).*

Nyanya alianza kuwa na shaka kuhusu juhudi za utafiti ambao Juma alikuwa ameweka. Nyanya alianza kuhisi kuwa huenda siri yake ambayo alikuwa ameweka kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI ikafichuliwa. Msanii anasema, “*Nyanya alihangaishwa sana na habari hiyo. Siri ambayo nimekuwa nikiweka jinsi kaburi linavyohifadhi siri hatimaye itajulikana!*” Nyanya aliposikia neno UKIMWI likitajwa, moyo wake ulianza kwenda kasi. Akamkazia Musa macho yaliyojaa imani huku machozi yakimlengalenga. Alikumbuka jinsi maradhi hayo yali vyowaua wazazi wa wajukuu zake. Alikuwa ameweka siri sababu ya vifo vya wazazi wa akina Musa lakini siri hufichuliwa na muda. Miaka kumi baadaye, Musa alikuwa anafichua ukweli huo kwa kuandika insha yenye mada, “Sitaki Iwe Siri”, ingawa kwa hakika hakujua ukweli huo.

Dhamira ya mtunzi wa riwaya **Sitaki Iwe Siri** aidha inajitokeza kupitia kwa insha ambayo Musa aliiandika kwa ajili ya shindano la kuadhimisha siku ya UKIMWI duniani. Shindano lilikuwa limetangazwa shuleni na Musa akawa mwanafunzi wa pekee aliyejitokeza kulishiriki. Utungo wenyewe unamhusu mhusika Yuri Matata ambaye anajipata kunaswa kwenye utando wa maradhi ya UKIMWI. Yuri anaepukwa na marafiki zake wote pindi afya yake inapoanza kuzorota. Mwandishi huyu chipukizi anatuchorea kiwakilishi halisi cha matukio ya jamii yetu ambayo huwabagua wagonjwa wa UKIMWI. Anatoa kilio kwamba wakati ulikuwa umefika ambapo hakutaka maradhi ya UKIMWI kuwekwa kama siri.

Ingawa mhusika mkuu kwenye insha hii anajiua, kifo chake ni mwamko mpya katika vita dhidi ya UKIMWI. Aliacha ujumbe kwenye kijikaratasi uliosema kwamba ‘**sitaki**

**iwe siri.**’ Anasema wazi kuwa amejua kwa sababu ya Ukosefu wa Kinga Mwilini. Anasema kuwa ingawa ameyakatiza maisha yake, anataka yawe funzo kwa wengine. Insha iliyoandikwa na Musa inapitisha ujumbe mzito kwamba, kufa kutokana na maradhi ya UKIMWI si jambo linalopaswa kuwa siri. Maradhi haya ni ugonjwa kama ugonjwa mwingine wowote ule. Nyanya Mwalonga alijaribu sana kuficha siri kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Anakiri kwamba alikuwa amewaficha wajukuu wake kuhusu aina ya ugonjwa uliowaua wazazi wao. Anasema:

**137. *Ni sadfa kwamba siri mliyoghubika kwa miaka mingi ili wajukuu zangu wasijue imefichuliwa. Wajukuu wangu hawa ni mayatima. Wazazi wao walifariki kutokana na maradhi ya UKIMWI, nao wakabaki mikononi mwangu. Waliponiuliza kilichowaua wazazi wao niliwajibu kuwa ni maradhi. Walipotaka kujua ni maradhi yepi, nilidinda kuwaambia. Nilitaka iwe siri lakini sasa Musa huyu ameandika insha ya ushindi – Sitaki Iwe Siri. Hii ni hatua muhimu katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI...(Sitaki Iwe Siri, uk. 66).***

Nyanya Mwalonga anakiri kuwa alikuwa amewaficha wajukuu wake siri kuhusu kifo cha wazazi wao kwa miaka mingi. Anasema kwamba ni sadfa sasa siri hiyo ilikuwa imefichuliwa na mmoja wa wale ambao alikuwa anaficha. Mtunzi anasema, “*Ni sadfa kwamba siri mliyoghubika kwa miaka mingi ili wajukuu zangu wasijue imefichuliwa. Wajukuu wangu hawa ni mayatima. Wazazi wao walifariki kutokana na maradhi ya UKIMWI, nao wakabaki mikononi mwangu. Waliponiuliza kilichowaua wazazi wao niliwajibu kuwa ni maradhi. Walipotaka kujua ni maradhi yepi, nilidinda kuwaambia.* Mwalonga sasa anakiri kwamba wazazi wa wajukuu wake walikufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Anakiri kuwa alikuwa akiwaficha kila walipomuuliza kilichowaua wazazi wao. Alikuwa akiwaambia tu ni ugonjwa bila kusema ni ugonjwa gani. Anasema kuwa hakuwaambia kwa maana alitaka ugonjwa huo ubaki kuwa siri. Hali hii ilitokana na mtazamo wa jamii kwa ujumla ambapo ugonjwa wa UKIMWI ulichukuliwa kuwa wa laana, aibu, mkosi na hivyo watu wengi hawakutaka kujihusisha nao. Kwa jumla, mwandishi anadhamiria kutufahamisha

kwamba wakati ulikuwa umepita ambapo ugonjwa wa UKIMWI ulistahili kubaki siri. Lazima kuwe na uwazi kuhusu ugonjwa huu ndipo watu wauielewe vyema ili wachukue hatua za tahadhari kuzuia maambukizi yake.

Katika tamthilia ya **Orodha**, mwandishi anatumia kwamba watu katika jamii hawataki kusema ukweli kuhusu chanzo cha kifo. Watu katika jamii hupenda kuyataja magonjwa mengine tofauti kuwa chanzo cha vifo wala si ugonjwa wa UKIMWI. Jamii ilikuwa na mtazamo hasi kwa vifo vilivyotokana na UKIMWI kwa maana vilihusishwa na aibu na laana. Hivyo basi katika jamii iliyotumiwa na mwandishi, hata mtu akifa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI, watu wa jamii husika hawakuwa huru kuutangaza ugonjwa halisi uliosababisha kifo. Katika tamthilia ya *Orodha*, mwandishi anatumia kwamba:

**138.** *Mama Furaha: Kama waweza kuendelea... (Anasubiri hadi watu wote wanapokuwa makini)... Baadhi ya watu kijijini wanasema Furaha alikufa kwa Malaria; kuna wengine wanasema alikufa kwa kifua kikuu, baadhi wanasema kwamba amerogwa. Lakini minong`ono mliyosikia hapa kijijini ni ukweli... binti yangu amekufa... kwa UKIMWI (Orodha, uk.3).*

Katika dondoo lililo hapo juu, jamii haikutaka kuwa wazi kuhusu watu katika jamii ambao walikufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Baada ya Furaha kufariki, baadhi ya wanakijiji walisema kuwa alikufa kutokana na magonjwa mbalimbali. Msanii anasema, "... *Baadhi ya watu kijijini wanasema Furaha alikufa kwa Malaria; kuna wengine wanasema alikufa kwa kifua kikuu, baadhi wanasema kwamba amerogwa. Lakini minong`ono mliyosikia hapa kijijini ni ukweli... binti yangu amekufa... kwa UKIMWI.* Jamii iliyotumiwa na mwandishi haikufurahishwa na usemi wa mama Furaha alipobaini wazi kuwa bintiye alikufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Mama Furaha ni kati ya watu katika jamii wanaotumiwa na mwandishi kuvunja ukimya na usiri kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Yeye alikuwa wazi kuhusu

kilichomuua bintiye ili waliojihusisha na Furaha katika mapenzi pia wajue kwamba chuma chao ki motoni. Watu walishikwa na hofu pamoja na mihemko ya manung'uniko baada ya mama Furaha kutoa hotuba yake kwenye siku ya mazishi. Hata Padri James hakutaka ukweli usemwe akitaja shughuli ya mazishi kuwa takatifu. Ni kinaya kwa Padri James kusema haya ilhali tunamtarajia kuwa katika mstari wa mbele kueleza watu ukweli kuhusu ugonjwa wa UKIMWI.

Jamii iliyotumiwa na mwandishi katika tamthilia ya **Orodha** iliamini kuwa ugonjwa wa UKIMWI ulitokana na urogi. Wanakijiji waliamini kwamba, mhusika Furaha aliogwa na mtu wala si kuupata ugonjwa wa UKIMWI. Watu waliamini kwamba ugonjwa wa UKIMWI haukutokana na uhusiano wa kingono kati ya mume na mke. Imani kama hii miongoni mwa wanakijiji ni hatari sana kwani inaweza kuchangia katika kueneza ugonjwa wa UKIMWI.

Baadhi ya wanakijiji waliamini kuwa mtu anaweza kuupata ugonjwa wa UKIMWI kwa kugusana tu na mwathirika wa ugonjwa huo. Wanakijiji wengine waliamini kuwa mtu huambukizwa ugonjwa wa UKIMWI anapolala chumba kimoja na mwathiriwa wa UKIMWI. Mawazo haya yote ni potovu na yanaonyesha ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu ugonjwa wa UKIMWI katika jamii. Jamii inayorejelewa na mwandishi aidha iliamini kuwa mtu akifanya mapenzi na bikira, bila shaka atapata tiba ya ugonjwa wa UKIMWI. Haya yote ni mawazo potovu yanayohimiza watu katika jamii kuzidi kujihusisha na mapenzi kiholela. Matokeo ya matendo kama haya ni maambukizi makubwa ya ugonjwa wa UKIMWI katika jamii husika.

Mwandishi wa tamthilia ya **Kilio Chetu** anaisawiri jamii ikikataa kuzungumzia ugonjwa wa UKIMWI kwa kudai kuwa dini na mila hazikuruhusu ugonjwa huu uzungumziwe kwa uwazi. Dini inastahili kuwa katika mstari wa mbele kuuzungumzia

ugonjwa wa UKIMWI ili kuihamasisha jamii na ni kinaya katika jamii inayozungumziwa hapa kwamba dini inatenda kinyume, kwa maana Padri James anajihusisha kufanya ngono na mhusika Furaha. Ili jamii ipate kujiepusha na ugonjwa wa UKIMWI, ilitahili kupewa mafunzo ya kutosha kuuhusu ndipo ijue namna ya kukabiliana nao. Mtunzi anasema:

**139. *Wakabandika mabango kupeana tahadhari, lakini watoto wakateketea kwa kukosa habari zozote za kuwaokoa. Wakubwa kukwepa lawama wakajitetea. Mwiko kuzungumzia mambo haya kwa watoto. Dini inakataza, Oh! Mila haziruhusu (Kilio Chetu, uk.2).***

Kutokana na dondoo lililo hapo juu, jamii iliweka mabango na tahadhari kila mahali kuhusu ugonjwa wa UKIMWI lakini ikakosa kutoa elimu na mafunzo kuhusu ugonjwa wenyewe. Mwandishi anasema, “*Wakabandika mabango kupeana tahadhari, lakini watoto wakateketea kwa kukosa habari zozote za kuwaokoa. Wakubwa kukwepa lawama wakajitetea. Mwiko kuzungumzia mambo haya kwa watoto. Dini inakataza, Oh! Mila haziruhusu*”. Katika muktadha huu, jamii inayorejelewa hapa ilihifadhi ugonjwa huu kama siri ikiwa na kisingizio kuwa dini na mila haziruhusu ujadiliwe hadharani. Watu wakubwa katika jamii walikwepa lawama wakajitetea kuwa utamaduni wao haukuwaruhusu kuzungumzia ugonjwa wa UKIMWI. Kutokana na msimamo huu, jamii na hasa watoto waliangamia kwa kukosa elimu kuhusu UKIMWI.

Jamii iliweka mabango na kutoa tahadhari kuhusu ugonjwa wa UKIMWI bila mafunzo ya kufanya wauelewe ugonjwa wenyewe. Hayo mabango hayangefaa chochote iwapo hayangeambatana na mafunzo na uhamasishaji. Kwa sababu ya ukosefu wa elimu, mwandishi anatueleza kuwa watoto waliendelea kudhoofika kwa kukosa elimu ya jinsia; huku dubwana au ugonjwa wa UKIMWI ukiendelea kuwaangamiza. Jamii iliona kuwa kuwapa watoto hasa wasichana habari kuhusu

ngono ndio kuwaharibu zaidi. Baadhi ya wanajamii walidhani kwamba watoto wangepata elimu hii, wangekuwa na ufahamu zaidi wa kujihusisha na masuala ya ngono. Baadhi ya wanajamii waliona kuwa kumpa mtoto wa kike elimu kuhusu UKIMWI ni sawa na kumfundisha umalaya.

Ingawa hivyo, msimamo wa mwandishi ni kuwa elimu inalenga kuwaonyesha watoto madhara ya kufanya ngono kabla ya wakati wake, yaani ndoa. Mwandishi anapendekeza vijana wapewe elimu ya familia, ikiwemo ya jinsia. Watoto waambiwe wazi juu ya mambo yanayohusiana na mapenzi na hatima yake. Mtazamo wa jadi haukuruhusu watoto wafunzwe kuhusu ngono. Mtazamo na msimamo wa jamii inayozungumziwa umepitwa na wakati kwa maana watoto wanapokosa elimu ndipo wanapojipata kwenye madhara kama vile magonjwa na mimba zisizotakikana. Msanii anasisitiza kuhusu elimu akisema kuwa watoto wanafaa wajazwe elimu ili waone uchafu na hatari ya kufanya ngono kiholela. Mwandishi anatuonyesha mhusika Mkuu Suzi akijuta kwamba kama angepata elimu mapema, hangepata madhara ya ugonjwa wa UKIMWI. Ni vyema basi mtoto aelimishwe kuhusu madhara makubwa ya kufanya ngono kabla ya wakati wake. Akielimishwa kwa upana hawezi kuthubutu kuyafanya mambo ambayo huenda yakahatarisha afya na maisha yake.

Wazazi hawakuwa radhi kuachana na utamaduni wa kale wa kuweka ukuta baina yao na watoto katika kujadili mambo kuhusiana na ngono. Inasikitisha kwamba kizazi hiki kinaangamia kwa sababu kimewekwa gizani kuhusiana na elimu inayohusiana na masuala ya ngono. Hofu ya wazazi haikuwasaidia watoto bali ilichangia katika kuwaingiza katika madhara makuu ya kuambukizwa na ugonjwa wa UKIMWI.

Katika hadithi ya **Kiti cha Moyoni**, mwandishi alidhamiria kutuonyesha namna ambavyo jamii inazidi kuathirika na kuangamia kwa kukosa elimu na ufahamu wa



kutosha kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anaanza kwa kutuonyesha namna ambavyo mhusika Salome aliathirika baada ya mumewe kutoroka kwenda Uganda na kurudi baada ya miaka mitano. Mtunzi anatueleza kuwa Majoni alimuoia mwanamke Mgisu ambaye yaelekea alikuwa na virusi vya UKIMWI. Baada ya Majoni kurudi nyumbani, tayari alionekana kuwa na virusi vya UKIMWI. Twaelezwa:

**140.** *Majoni amerudi. Alikuwa akitembea mwendo wa kinyonga. Amenyongea. Ni mkondefu na mwenye macho yaliyojizika kwenye uso uliosawijika... Gurudumu la afya ya Majoni lilikuwa limetobokea Mbale. **Kohoakohoa zake zilikuwa mwanzo zinaeleweka kwa maana watu wakikohoa tangu hapo. Watu hukohoa kisha kikohozi kikaisha. Lakini kikohozi chake kikawa hakiishi naye akawa hana siha, hana udole...watu wakaanza kusema labda mwenzetu amekanyaga waya (Kiti cha Moyoni, uk.86).***

Msanii anatupatia taswira ya afya ya Majoni aliporejea kutoka Uganda. Anatueleza kuwa alikuwa akitembea kwa mwendo wa kinyonga, mkondefu na macho yalikuwa yamejizika kwenye uso uliosawijika. Anasema kwamba gurudumu la afya ya Majoni lilikuwa limetoboka kumaanisha kuwa alikuwa ameanza kuathirika kiafya na kuwa mgonjwa. Alikuwa na kikohozi kisichoisha na ikasemekana kuwa alikuwa amekanyaga waya au ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anatueleza kuwa, *“Kohoakohoa zake zilikuwa mwanzo zinaeleweka kwa maana watu wakikohoa tangu hapo. Watu hukohoa kisha kikohozi kikaisha. Lakini kikohozi chake kikawa hakiishi naye akawa hana siha, hana udole...watu wakaanza kusema labda mwenzetu amekanyaga waya.”*

Ni wazi kutokana na maelezo haya kwamba Majoni alikuwa ameambukizwa virusi vya UKIMWI. Licha ya dalili za UKIMWI ambazo Majoni alikuwa nazo tangu kurejea kutoka Uganda, Salome alikubali wakafanya naye mapenzi. Hii ina maana kuwa Salome alikosa elimu na ufahamu kuhusu UKIMWI. Kama angefahamu kuwa Majoni alikuwa na dalili za UKIMWI, hangekubali kumruhusu afanye mapenzi naye.

Majoni kwa upande wake hakuwajibika kwa maana hangefanya mapenzi na mkewe bila kinga iwapo alijua kuwa alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Jamii ambayo imetumiwa na mwandishi inaangamia kwa kukosa ufahamu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Matokeo yakawa Salome kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi pia anamsawiri mhusika Mwasame kuwa mtu ambaye alikosa elimu na ufahamu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Licha ya kushuhudia kifo cha Majoni, alipata fursa ya kuuendeleza uhusiano wake na kipenzi chake cha roho Salome. Yeye ndiye aliyekuwa mtu wa karibu sana aliyeshuhudia Majoni akiugua na kumsaidia kumpeleka hospitalini. Mwasame ndiye aliyekuwa katika nafasi bora kutambua aina ya ugonjwa ambao Majoni alikuwa nao lakini inasikitisha kwamba hakuelewa chochote.

Mwandishi anatueleza:

**141.** *Yote Mwasame anayakumbuka. Anakumbuka kwamba hata nyasi ilikuwa haijaota kwenye kaburi la lofa kabla majasho hayaajaanza kummwagika kumtafuta mtoto wa kwanza-wake yeye Mwasame na malkia wa moyo wake. Pamoja na dhoofuhali ya malkia, wakampata mtoto mvulana... lakini baada ya vikohozi visivyokwisha na kuendesha tena, malkia na Petro makao yao ni viungulima viwili vilivyosimama uani, kila mmoja na msalaba alioutengeneza Mwasame kwa nguvu zake haba kwa roho safi (Kiti cha Moyoni, uk.88).*

Twaelezwa kuwa haikuchukua muda baada ya kifo cha Majoni kwa Mwasame kujiingiza katika uhusiano wa kimapenzi na Salome. Msanii anasema nyasi ilikuwa haijaota kwenye kaburi la lofa Majoni kabla majasho kummwagika Mwasame kumtafuta mtoto wa kwanza na Salome. Msanii anatueleza kuwa, “*Pamoja na dhoofuhali ya malkia, wakampata mtoto mvulana... lakini baada ya vikohozi visivyokwisha na kuendesha tena, malkia na Petro makao yao ni viungulima viwili vilivyosimama uani, kila mmoja na msalaba alioutengeneza Mwasame kwa nguvu zake haba kwa roho safi.*” Licha ya dalili za ugonjwa wa UKIMWI zilizokuwa zinaonekana, waliweza kumpata mtoto mvulana waliyemuita Petro. Kwa sababu

mtoto alizaliwa akiwa na virusi vya UKIMWI, alifariki baada ya kipindi kifupi na akazikwa. Katika muktadha huu, ni bayana kuwa Mwasame alikosa elimu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI na ndiyo sababu akaanza moja kwa moja kufanya mapenzi na Salome bila kuchukua tahadhari zozote.

Mwasame alishuhudia vifo vya Salome na mtoto wake huku afya yake ikizidi kudhoofika. Baada ya muda, Mwasame alifariki. Mwandishi anatuonyesha kuwa, kuna watu katika jamii ambao wanaangamia kutokana na ukosefu wa elimu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Licha ya ukosefu wa elimu na usiri ambao baadhi ya jamii zimeuwekea ugonjwa wa UKIMWI, wasanii aidha wameonyesha madhara yanayosababishwa na ugonjwa wa UKIMWI. Mjadala huo unajitokeza katika sehemu inayofuata inayozungumzia athari ya ugonjwa wa UKIMWI katika jamii.

## **5.6 Athari ya UKIMWI**

Ugonjwa wa UKIMWI umeiathiri jamii kwa njia mbalimbali. Jamii tofauti zimesawiriwa zikipoteza wapendwa wao na hivyo kuathirika sana kisaikolojia na hata kiuchumi. Baadhi ya kina mama wanabaki wajane huku watoto wakiwa mayatima. Mwandishi wa tamthilia ya **Giza** amesawiri maisha ya wahusika mbalimbali na ameonyesha namna ambavyo ugonjwa wa UKIMWI umezima ndoto katika maisha yao. Mwandishi anatupa taswira ya jamii ambapo ugonjwa wa UKIMWI umeangamiza maisha ya watu wengi. Kupitia mhusika Kichaa, mwandishi anatueleza kuwa, ugonjwa wa UKIMWI umeivamia jamii na kusababisha vifo vya watu wengi sana. Mtunzi anasema kuwa GIZA limetawala akiwa na maana kwamba ugonjwa wa UKIMWI umesambaa sana na kupoteza maisha ya watu. Athari ya ugonjwa huu inadhihirishwa msanii anapotupatia mfano wa mhusika Davina tunayeambiwa alifariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi anasema:

**142.** *Davina alikuwa mpenzi wa afisa wa usalama Mori. Mori alifariki yapita miaka minne. Alikufa kwa UKIMWI na kwa vile Davina kaishi miaka minne zaidi basi watu wanaamini Mori hakufa kwa UKIMWI. Jambo usilolijua ni sawa na usiku wa kiza. Vipi hawa watu waliaminiana! (Anamgeukia Mona, anamtazama kwa jicho la huruma, machozi yanamtoka anasema) Mona niambie Steve yuko wapi? (Giza, uk. 9)*

Jamii inayozungumziwa katika maandishi haya ilikosa ufahamu wa kutosha kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Baada ya kifo cha Mori, Davina aliishi miaka minne zaidi na watu wakaamini kwamba Davina hakufariki kutokana na maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anatueleza, “*Davina alikuwa mpenzi wa afisa wa usalama Mori. Mori alifariki yapita miaka minne. Alikufa kwa UKIMWI na kwa vile Davina kaishi miaka minne zaidi basi watu wanaamini Mori hakufa kwa UKIMWI.*” Haya ni mawazo potovu kwa kuwa virusi vya UKIMWI vinaweza kuishi kwa mwili wa mwathirika hata kwa muda wa miaka kumi au zaidi. Mawazo ya kudhani kuwa Mori hakufariki kutokana na UKIMWI ndiyo yaliyowafanya baadhi ya wanajamii kujihusisha na mapenzi na Davina na hivyo kuangamia baadaye kutokana na makali ya ugonjwa wa UKIMWI. Katika jamii nyingi, matukio kama haya hutokea kwa maana hata watu wakifariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI, utakuta kuwa wengine wanaanza kujihusisha nao kimapenzi wakikana kuwa vifo vilivyotokea havikutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Matendo kama haya ndiyo yanayochangia pakubwa maenezi na maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI.

Aidha, ni bayana kuwa wanajamii wanaorejelewa hawakuwa wanatumia mipira au kondomu wakati ambapo walikuwa wanafanya mapenzi. Mapenzi yaliyofanywa bila kinga ndiyo yaliyochangia pakubwa kuenea kwa ugonjwa wa UKIMWI kwa haraka na kusababisha vifo. Katika muktadha huu, wale wote waliofanya ngono na Davina pamoja na Mona waliangamia kutokana na ugonjwa wa UKIMWI.

Katika tamthilia ya **Giza**, mtunzi anasawiri maisha ya mhusika Robby na namna anavyoendeleza dhamira ya athari ya ugonjwa wa UKIMWI. Robby alijihusisha katika mapenzi na Davina hata baada ya kugundua kuwa Davina alifariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Robby anajirusha barabarani na kugongwa na gari ili kuuficha ulimwengu kuhusu chanzo cha kifo chake. Alifahamu fika kuwa angefariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI na hivyo akaamua kujitoa uhai mapema. Mwandishi anasema:

**143. *Sasa nitakufa. Nitakufa vibaya eti wanasema hata Mmh!...Robby anataka kuvuka barabara mara gari linakuja kwa kasi linamgonga Robby anaanguka chini, huku povu likimtoka kinywani. Watu wanahisi kuwa amekufa kwa shinikizo la damu ...Robby huyooo! Zake ziliishia hapo. Hakuweza kujua ukweli wa kifo cha Davina. Waliobaki nyuma pia wako gizani. Hivyo ndivyo giza lilivyotanda kila kona ya maisha (Giza, uk.10-11).***

Robby aliamua kuzima Nuru ya maisha yake alipogundua kuwa Davina alikufa kutokana na UKIMWI. Mtunzi anasema, “*Sasa nitakufa. Nitakufa vibaya eti wanasema hata Mmh!...Robby anataka kuvuka barabara mara gari linakuja kwa kasi linamgonga Robby anaanguka chini, huku povu likimtoka kinywani. Watu wanahisi kuwa amekufa kwa shinikizo la damu.*” Hakutaka kufariki kutokana na ugonjwa wa aibu na ndiyo sababu akaamua kuchukua njia ya mkato. Robby alijirusha barabarani na kusababisha ajali ambapo aligongwa na gari. Hivyo basi jamii ikaamini kuwa Robby alifariki kutokana na ajali ya barabarani lakini ukweli wa mambo ni kuwa alijiua kwani aliamini kwamba hata angeishi, angekufa kama Davina alivyokufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI.

Katika jamii inayorejelewa, inabainika kuwa baadhi ya watu hawakutaka kuhusishwa na ugonjwa wa aibu, laana na fedheha. Hii ndiyo sababu baadhi yao wakaona bora wafe kwa kuhusika katika ajali au hata kujitoa uhai kwa kujinyonga. Hili ni jambo la

kusikitisha kwa maana jamii hii ilikosa elimu na ufahamu kuwa mgonjwa wa UKIMWI anaweza kuishi kwa muda mrefu sawa na mwingine aliyeugua ugonjwa mwingine. Mgonjwa wa UKIMWI akipewa matibabu ya dawa za kupunguza makali na lishe bora, anaweza kuishi maisha marefu kama mtu mwingine aliye mzima. Jamii inayozungumziwa inaangamizwa kutokana na athari ya ugonjwa wa UKIMWI.

Mtunzi wa tamthilia ya **Giza** anayasawiri maisha ya Suzi na jamii yake. Mtunzi anatuonyesha namna mama yake alivyoathirika na ugonjwa wa UKIMWI na kisha akafariki na kuzikwa. Jamii hii inasawiriwa kuwa ya kimaskini kwa maana twaambiwa Suzi pamoja na dadake walikuwa wakimsadia mama fulani kufanya kazi. Suzi na jamii yake walikosa hata matibabu yafaayo kupunguza athari ya ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anatumia:

**144.** *Nakumbuka siku moja mama aliniita chumbani akafunua nguo na kunionyesha sehemu zake za siri, alikuwa na vidonda. Ni nyama tu alioza. Tulimzika mama. Baba wa kambo alikuwa akitutukana kila siku akidai mama ni shetani aliamua kumuua kwa kumnyonga. Sikuelewa hilo... Alifanya mapenzi kwa nguvu. Kila siku alikuwa akinibaka. Alimbaka hata mdogo wangu. (alitulia kisha akaita) dada upo? Naona giza, gizaaa! (Giza, uk.13)*

Mamake Suzi alikuwa ameathirika sana na ugonjwa wa UKIMWI. Alikuwa na vidonda katika sehemu zake za siri na nyama katika sehemu hizo ilikuwa imeoza. Ugonjwa wa UKIMWI ulimla sana na kuyaathiri maisha yake vibaya. Mwandishi anatumia, “*Nakumbuka siku moja mama aliniita chumbani akafunua nguo na kunionyesha sehemu zake za siri, alikuwa na vidonda. Ni nyama tu alioza. Tulimzika mama. Baba wa kambo alikuwa akitutukana kila siku akidai mama ni shetani aliamua kumuua kwa kumnyonga.*” Baba wa kambo alimuita mama Suzi kama shetani na hivyo aliamua kumuua kwa kumnyonga. Baba wa kambo alimnyonga mamake Suzi kwa vile hakutaka aonekane amefariki kutokana na ugonjwa wa aibu. Yalikuwa ni masikitiko makubwa sana kwa Suzi kupoteza mamake. Suzi anaona giza

maishani baada ya kupoteza mama yake kwa sababu ya UKIMWI, na isitoshe baba wa kambo akaanza kumfanyia kitendo cha kikatili. Alibakwa mara kadha wa kadha na baba wa kambo ambaye alimbaka dadake mdogo pia. Baba wa kambo aliazimia kukimaliza kizazi hiki na hivyo jamii ya kina Suzi iliona tu giza katika maisha yao. Matendo haya yote yanafanyika kwa sababu ya athari ya ugonjwa wa UKIMWI katika jamii.

Mwandishi wa tamthilia ya **Giza** anazidi kutupa mifano ya wahusika walioona giza maishani mwao baada ya kuathirika na ugonjwa wa UKIMWI. Maisha ya mdogo wa Suzi pia yalikatizwa na ugonjwa wa UKIMWI. Ugonjwa wa UKIMWI ulimfanya akadhoofika sana na hatimaye akafa mikononi mwa Suzi. Kifo cha mdogo wa Suzi kilikuwa pigo kwa Suzi ambaye aliona ulimwengu ukibaki tu giza na kumkosesha matumaini maishani mwake.

Suzi alikumbana na changamoto nyingi sana maishani mwake. Aliuguza mamake na dadake mdogo. Wote waliaga dunia na kumuacha akiwa ametamauka sana. Baada ya kudhoofika kwa muda mrefu, hatimaye anafariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Jamii nyingi zilikuwa zinaathirika vibaya kutokana na makali ya ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi anatueleza katika dondoo lifuatalo kuwa:

**145.** SUZI: *Ndipo nilipoishi, kule kibarazani nilifukuzwa eti maiti ilileta nuksi. (Mara Suzi anashindwa kuzungumza, anakohoa sana, anatapika mfululizo. Nuru anaenda kumwita Nesi, lakini anakuta Nesi anakunywa chai hajibu kitu, Nuru anaporudi anamkuta Suzi macho yameangalia juu. NURU: Analia sana. (Kicheko kikubwa kinatokea kila upande Nuru anaangaza huku na huko anasikia sauti HAKUNA MAISHA NDANI YA GIZA (Giza, uk.16).*

Maisha ya Suzi pia yalizimika kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Kabla ya kifo chake Suzi alifukuzwa Kibarazani akiitwa maiti iliyoleta nuksi. Katika dakika za mwisho za maisha yake, alishindwa kupumua, akakohoa sana na kutapika mfululizo.

Juhudi zilizofanywa kumwita Nesi ashughulikie matibabu ya Suzi hazikufaulu. Nesi alikuwa anakunywa chai na hakuwa na haja ya kuyanusu maisha ya mgonjwa. Mtunzi anasema, *“Ndipo nilipoishi, kule kibarazani nilifukuzwa eti maiti ilileta nuksi. Mara Suzi anashindwa kuzungumza, anakohoa sana, anatapika mfululizo. Nuru anaenda kumwita Nesi, lakini anakuta nesi anakunywa chai hajibu kitu, Nuru anaporudi anamkuta Suzi macho yameangalia juu.”* Hali hii ilichangia pakubwa katika kupunguza siku za Suzi katika ulimwengu huu. Kutokana na tabia ya Nesi, mwandishi anatuonyesha kuwa madaktari na wauguzi hawakutaka kuwatibu wagonjwa waliougua ugonjwa wa UKIMWI. Baadhi yao walihitaji kuhongwa ndipo wawahudumie wagonjwa walioathirika na UKIMWI. Wahudumu hawa waliendeleza unyanyapaa ambao ulichangia pakubwa katika kusababisha vifo vya waathiriwa wa UKIMWI. Ugonjwa wa UKIMWI uliangamiza watu wengi katika jamii kwa maana walikosa huduma stahiki kutoka kwa wale waliopaswa kuwapa huduma hiyo.

Mwandishi anaiendeleza dhamira kuhusu athari ya UKIMWI wakati anapotuonyesha vifo vya watu waliofariki mapema. Ugonjwa wa UKIMWI umewaangamiza watu wengi katika jamii na mtunzi alitaka kutoa taswira hiyo. Matendo na mienendo isiyofaa ya kujihusisha katika mapenzi kiholela ndiyo inayochangia pakubwa katika maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anasema:

**146.** *Mkifufuka mtalia na kamwe hamtanyamaza. Nitawaambia nini tukikutana kaburini? Dunia mlioniachia imejaa giza! Watoto na wajukuu wanapapasa. Hakuna anayemwona mwenzie, akipapasa akiona mwanamke halali yake, mbuzi halali yake, mtoto halali yake... Nitasimulia nini uovu umezidi giza limeongezeka (Giza, uk. 23-24).*

Katika dondoo lililo hapo juu, mwandishi anatuonyesha vifo vya watu wengi waliotangulia kufariki. Mtunzi anafichua kuwa, *“Mkifufuka mtalia na kamwe hamtanyamaza. Nitawaambia nini tukikutana kaburini? Dunia mlioniachia imejaa*



*giza! Watoto na wajukuu wanapapasa. Hakuna anayemwona mwenzie, akipapasa akiona mwanamke halali yake, mbuzi halali yake, mtoto halali yake...*” Msanii anasema kuwa waliotangulia kufa wakifufuka watalia na hawatanyamaza kwa sababu ya vifo vilivyotokana na maovu yaliyokuwa yakifanyika. Aidha, anatumia kuhusu uozo unaofanyika katika jamii kama vile kufanya mapenzi kiholela. Watoto na wajukuu walipapasana wakifanya mapenzi na wanawake na hata mbuzi. Mtunzi anasawiri picha ambapo hakika uovu ulikuwa umezidi sana katika ulimwengu uliokosa matumaini. Msanii pia anazidi kutuonyesha namna wananchi wa tabaka mbalimbali walivyokuwa wakiangamia kutokana na makali ya ugonjwa wa UKIMWI.

Ugonjwa wa UKIMWI haukubagua tajiri, maskini au mtu wa cheo fulani katika jamii. Twaelezwa kuwa hata yule Profesa Matongo naye alifariki kutokana na UKIMWI. Juhudi za baadhi ya matajiri kubadili damu kwa kuondoa ile ya virusi vya UKIMWI hazikufua dafu kwa maana watu waliendelea kufariki. Katika jamii iliyorejelewa, Dkt. Jumbe pia alifariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa umeivamia sana jamii inayorejelewa na wala haukubagua kwa misingi ya cheo, hali ya kiuchumi na kadhalika. Msanii anasema, *“Watu wanaisha maskini kwa matajiri, wataalamu na wasio wataalamu, wasomi na wanasisia sijui tuendako.”* (Giza, uk.30)

Kwa ujumla, giza lilikuwa limeighubika jamii kwa maana watu wa tabaka mbalimbali wakiwemo; maprofesa, madaktari, matajiri na maskini waliangamia. Ugonjwa wa UKIMWI haukuheshimu yeyote yule. Giza lilitokea kwa kila mmoja katika jamii bila ubaguzi wowote ule. Jamii ilikuwa inaangamia kwa kukosa elimu na ufahamu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Aidha, jamii haikuhamasishwa vya kutosha kuhusu makali ya ugonjwa wa UKIMWI.

Mtunzi wa tamthilia ya **Giza** pia ameendeleza dhamira yake ya athari ya UKIMWI pale anapoyaangazia maisha ya Nuru na mamake. Nuru anafariki baada ya kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI na Steve. Kwa sababu ya maenezi ya ugonjwa wa UKIMWI, baadhi ya watu katika jamii waliibuka na mbinu ambazo zingewawezesha kuukwepa ukweli kuhusu ugonjwa huu kwa muda tu. Mwandishi anasema:

**147.** ... *Steve aliniambia nimsamehe au aliniacha gizani! Mama hiyo ni zawadi tuliyokuletea watoto hao. (anafikiri) Lakini kama UKIMWI ni adhabu mbona hata watiifu wanakumbwa? (anasikia sauti) anapoteza fahamu. GIZA... Haya hata Nuru imezimwa na Giza (Giza, uk.41).*

Katika dondoo lililo hapo juu, mwandishi anatuonyesha namna maisha ya Nuru yalivyozimwa na UKIMWI. Nuru alidanganywa na Steve kupitia kwa njia za kifisadi akafaulu kumuoa ilhali alikuwa na ugonjwa wa UKIMWI. Steve alikuwa na virusi vya UKIMWI lakini alimhonga daktari akatoa majibu yaliyoonyesha kuwa hakuwa na virusi vya UKIMWI. Mhusika huyu alikosa maadili ya jamii. Watu kama vile Steve ni wahalifu ambao wanapaswa kupewa hukumu kali sana ili iwe funzo kwa wengine.

Hilo lilikuwa kosa kubwa sana na ilistahili daktari aliyehusika kuchukuliwa hatua kali za kisheria na hata kunyang'anywa cheti cha kuhudumu kama daktari. Nuru ambaye hakuwa na hatia pia anaangamia katika jamii na ulimwengu huu uliojaa maovu. Kwa kweli wahusika wengi katika tamthilia ya *Giza* wamepoteza maisha yao kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Kuna wahusika ambao wamepata UKIMWI kwa kutowajibika na wengine nao wakaupata UKIMWI bila hiari yao. Athari ya UKIMWI kwa kiasi katika jamii inayorejelewa imesababishwa na ukosefu wa uwajibikaji. Dhamira ya ukosefu wa uwajibikaji katika jamii ndiyo imejadiliwa katika sehemu inayofuata.

### 5.7 Ukosefu wa Uwajibikaji

Dhamira hii imewasilishwa kwa ngazi mbili katika hadithi ya “tahadhari bandia”. Katika ngazi ya kwanza, mwandishi anaumulika usimamizi wa chuo ambapo Wakesho alikuwa akisoma. Katika chuo hicho, kulikuwa na mikasa ya mara kwa mara ya kuzimika kwa nguvu za umeme. Matukio ya kuzimika kwa nguvu za umeme yaliwapa wanafunzi wahuni fursa ya kuwaporu, kuwaibia na hata kuwabaka wengine. Mwandishi anatueleza kwamba juhudi za wanafunzi kuutanabahisha utawala wa chuo kuhusu tatizo hili ziliambulia patupu kwani kila mara walipewa ahadi za mdomo. Maelezo haya yanatuonyesha kwamba utawala wa chuo ulikosa kuwajibika na ikawa kwamba wanafunzi waliendelea kubakwa Wakesho akiwa miongoni mwao.

Ngazi ya pili inahusu taaluma ya utabibu. Mwandishi wa hadithi hii anatueleza kwamba sheria za kitaaluma hazikuruhusu kuyatangaza matokeo ya uchunguzi mara ya kwanza kabla ya kuyathibitisha. Lakini ni kinaya katika hadithi hii kwamba daktari wa chuo aliyatangaza matokeo ya Wakesho pasipo kuzingatia sheria hii. Mtunzi anatueleza:

**148.** *Aliandikaandika na mara akamgeukia mwuguzi na daktari mwenzake akasema, ‘I think she is positive’ (Likizo ya Mauti, uk. 4).*

Huu ni ukiukaji wa sheria za taaluma ya utabibu zilizohitaji uchunguzi zaidi ufanyike kabla ya kuyatangaza matokeo. “I think she is positive” ni usemi ulio na maana kuwa Wakesho alikuwa na virusi vya UKIMWI. Daktari aliyetoa usemi huu alikiuka sheria na taratibu za utabibu. Ilihitajika kuwa matokeo lazima yathibitishwe zaidi ya mara moja kabla ya kutangazwa lakini daktari aliyetajwa anakiuka sheria hii na kutoa matokeo mapema zaidi. Matokeo haya yaliathiri vibaya sana maisha ya Wakesho mpaka akakosa matumaini maishani mwake. Aliamini kwamba alikuwa na virusi vya UKIMWI na hivyo akatatizika sana kisaikolojia.

Katika tamthilia ya **Giza**, mtunzi anasawiri hali ambayo inaonyesha ukosefu wa uwajibikaji uliodhihirishwa na manesi na madaktari. Wakati ambapo Suzi alikuwa mgonjwa mahututi hospitalini, Nuru alienda kumwita Nesi ili aishughulikie hali ya mgonjwa. Kilichoshangaza na kuhuzunisha ni kwamba nesi aliendelea tu na shughuli yake ya kunywa chai kama ambaye hakusikia chochote kutoka kwa Nuru. Kile kinachojitokeza katika jamii iliyorejelewa na mwandishi ni kuwa hawa manesi na madaktari walihitaji kuhongwa ndipo wawahudumie wagonjwa. Inasikitisha kwa vile manesi na madaktari hao walikuwa wameajiriwa na serikali na walikuwa wanapokea mshahara kila mwisho wa mwezi.

Licha ya ukosefu wa uwajibikaji, twaweza kusema kuwa nesi aliyekataa kuhudumia Suzi alikuwa na roho ya unyama akakosa ubinadamu. Aidha, madaktari hawakumjali mgonjwa wakati ambapo manesi walikuwa mbali naye. Kwa ujumla, wahudumu ambao wanatarajiwa kuwatibu wagonjwa katika tamthilia ya Giza wameendeleza dhamira ya mtunzi ya ukosefu wa uwajibikaji.

Katika riwaya ya **Pendo katika Shari**, msanii anazidi kuiangazia dhamira ya ukosefu wa uwajibikaji. Katika riwaya, Sulubu alikuwa ameambukiza mkewe Pendo virusi vya UKIMWI na hivyo kukawa na mzoano ambao uliwatenganisha na kwa muda Pendo akaenda kwao. Sulubu alikuwa anataka kumuoa Rehema lakini alikuwa amekosa pesa za tafrija ya ndoa na za kulipia mahari. Alitumia ujanja na kumlaghai mkewe kutia sahihi barua ambayo ilimpa idhini ya kuuza shamba. Alimdanganya mkewe kuwa angetumia pesa hizo kulipia karo ya watoto na ndiyo sababu Pendo akatia sahihi barua hiyo. Kinyume cha matarajio ya wengi, Sulubu alitumia pesa hizo katika tafrija ya ndoa yake na Rehema. Sulubu alikosa kuwajibika akakosa kulipa karo ya watoto

shuleni mpaka wakafukuzwa. Ilibidi chifu aandikie mwajiri wa Sulubu barua ya kuagiza mshahara wake ukatwe ili ufidie karo ya shule na kuwakimu wanawe.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, mhusika Ngoma alikosa kuiwajibikia jamaa yake. Mwanzoni alishiriki katika starehe za ulevi na kufanya mapenzi na wanawake nje ya ndoa. Ngoma alifanya mapenzi na mwanamke Queen aliyekuwa ameambukizwa virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Ngoma alikosa kuwajibika kwa maana aliendelea kufanya mapenzi na mkewe bila kinga na hivyo akamuambukiza virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Ukosefu wa uwajibikaji wa Ngoma ulimlazimu Tabu kuanzisha biashara ndogo ili aweze kukidhi mahitaji ya jamii yake. Ukosefu wa uwajibikaji wa Ngoma uliiletea jamii maangamizi kwa maana Tabu alifariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Aidha, Ngoma mwenyewe alifariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI.

Mtunzi wa riwaya ya **Kala Tufaha** aidha anatupatia mfano wa mhusika ambaye hakuwajibika. Mwalimu Selemani alikosa kuwajibika wakati ambapo alikataa kumruhusu Kibibi kuendelea na masomo ya sekondari baada ya kufanya vyema sana katika mtihani wa darasa la nane. Badala ya kupeleka Kibibi shuleni, anampeleka Imu ambaye hakufanya vyema kwenye mtihani. Kisa na maana kilikuwa kwamba Selemani hakutaka kumwelimisha mtoto wa kike. Aidha, anaruhusu Kibibi kwenda kufanya kazi ya uyaya ambapo alibakwa na Fumbwe na hata kupachikwa mimba. Kibibi alipotoroka kutoka kwa Fumbwe kutokana na unyama aliotendewa, mzee Selemani na mkewe wanaonyesha ukosefu wa uwajibikaji wakati wanapomfukuza binti yao bila kumpa nafasi ya kumsikiliza.

## **5.8 Hitimisho**

Katika sura hii, tumejadili kwa kina dhamira mbalimbali zilizowasilishwa na wasanii wa kazi teule zilizotumika katika utafiti huu. Katika sura hii, imebainika kwamba

lichu ya waandishi kutofautiana na kutoka katika mazingira tofauti, dhamira zao nyingi zinafanana. Baadhi ya dhamira hizo ni utamaushi, unyanyapaa, dhuluma dhidi ya mwanamke na kadhalika. Katika sura inayofuata, tumejadili dhima ya mtindo na namna fasihi inavyotumika katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI.

## SURA YA SITA

### DHIMA ZA MTINDO NA NAFASI YA FASIHI KATIKA KUKABILIANA NA UKIMWI

#### 6.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, tumejadili kwa kina dhamira mbalimbali zilizowasilishwa na waandishi wa kazi teule zinazozungumzia suala la UKIMWI. Tulibaini kuwa licha ya tofauti za misingi na mazingira, dhamira nyingi za waaandishi kuhusu UKIMWI zinalingana. Katika sura hii, tumeonyesha dhima za kimaudhui na kifani katika uandishi wa kazi ya fasihi na kujadili namna fasihi imetumika katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Katika sehemu hii, tutazifafanua dhima hizo mbili zilizotajwa na kisha tuonyeshe namna fasihi andishi inavyotumika katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI.

#### 6.1 Dhima za Kimaudhui

Lugha ya kitamathali katika maandishi teule ya fasihi andishi ina jukumu kubwa la kuuwasilisha dhamira na maudhui kwa jumla kwa wasomaji wake. Katika sura ya nne tulionyesha namna ambavyo lugha ya kitamathali imetumika katika kuliibua suala la UKIMWI. Sehemu hii inazijadili dhima za kimaudhui.

##### 6.1.1 Kumfikirisha msomaji

Wasanii walio na tajriba ya uandishi wa kazi za fasihi huwasilisha dhamira zao kwa ufundi mkuu. Wasanii hao hutumia tamathali za usemi kwa njia inayomfikirisha sana msomaji ndipo apate kuelewa dhamira au ujumbe unaolengwa katika kazi husika. Mwandishi wa riwaya ya *Ua la Faraja* ametumia taswira mbalimbali kama vile ‘soksi’ ambayo hutumika kurejelea kondomu. Hii inamhitaji msomaji kutafakari kwa makini ili aweze kuelewa dhamira mbalimbali zilizowasilishwa. Mwandishi anasema:

**149. Mambo kwa soksi! Mambo kwa soksi! Maji uyavulie nguo ndipo uyakoge! Ulapo ndizi usiimenye ila ivishe ganda! Jando la Raha Leo ni kuvishana magozi! (Ua la Faraja, uk.12)**

Katika dondoo lililonukuliwa, msanii ametumia usemi, “mambo kwa soksi.” Anasema, “*Mambo kwa soksi! Mambo kwa soksi! Maji uyavulie nguo ndipo uyakoge! Ulapo ndizi usiimenye ila ivishe ganda! Jando la Raha Leo ni kuvishana magozi!*” Katika muktadha huu, “soksi” limetumika kumaanisha mipira au kondumu ambayo huvalishwa katika sehemu za siri za mwanamume kabla ya kujamiiana. Mtunzi ametumia ulinganishi wa soksi kwa maana soksi huvaliwa kwanza kabla ya kuweka mguu kwenye kiatu. Aidha, mwandishi anasema, “ulapo ndizi usiimenye ila ivishe ganda.” Msemu huu pia una maana kuwa mtu lazima ajikinge kabla ya kufanya mapenzi. Katika muktadha mwingine, mwandishi wa *Ua la Faraja* aidha ametumia sitiari hii, “*Nani akutake wewe na hali umeshakokoteza mbegu za umeme mji mzima?*” (uk.76) Inabidi msomaji azitafakari taswira na sitiari hizi kwa uzingativu huku akizihusisha na tajriba yake ya mambo katika mazingira na kisha aziibue dhamira nyingi zilizofichika.

Uwezo wa kuihakiki kazi ya fasihi kwa kina huweza kumfanya msomaji kuwa mzalishaji wa maana tofauti zinazowasilishwa na maandishi teule ya fasihi andishi badala ya kuwa mtu wa kupokea tu chakula kilichopikwa kikawa tayari. Kezilahabi (1983) anaeleza kwamba, kazi ya fasihi kama ilivyo riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi, inahitaji kutungwa kwa namna ambayo itamfikirisha msomaji kidogo ili aweze kupata maana au dhamira katika kazi anayoisoma na huo ndio uhai wa kazi ya fasihi. Kazi ya fasihi ambayo imeandikwa moja kwa moja isiyomfikirisha kamwe msomaji, bila shaka itakuwa na upungufu mkubwa wa kisanaa. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, maneno kama vile “soksi”, “mkanda wa jeshi” yamezoeleka katika jamii iliyoorejewa kaika maandishi na yanafahamika katika makundi ya wazee, akina



mama na wasichana. Kutokana na kufahamika kwa maneno haya na wanajamii, wasomaji wanapokumbana nayo, inakuwa rahisi mno kupata dhamira ya mtunzi kama alivyokusudia kuiwasilisha.

Katika riwaya ya *Kala Tufaa*, msanii inaendeleza dhima ya kumfikirisha msomaji kupitia matumizi ya jazanda. Mwandishi anatoa mfano wa dudu lililokuwa na sura ya kutisha ambalo liliwadhulumu wanadamu. Katika mfano ufuatao mwandishi anasema:

**150. *Kala akikabiliana na dudu moja lililokuwa na sura ya kutisha lililodhulumu wanadamu. Dudu lenyewe kubwa na lenye macho makubwa na miguu mingi. Lilikuwa likiwaua wanadamu wala halikushughulika na wanyama wengine. Ajabu ni kwamba liliwalenga watu waliolikaribia au waliokuwa kwenye njia liipitayo (Kala Tufaha uk.63).***

Katika mfano ambao umedondolewa hapo juu, mwandishi hajaeleza moja kwa moja ujumbe ambao anapitisha kwa wasomaji. Anatumia mfano wa dudu ambalo lilikuwa na sura ya kutisha ambalo liliwadhulumu wanadamu. Anaendelea kusema kwamba, lilikuwa na macho makubwa na miguu mingi. Isitoshe halikushughulika na viumbe wengine isipokuwa wanadamu. Ujumbe wa mwandishi haujasilishwa kwa njia ya wazi na inabidi msomaji afikirie ndipo afasiri kile alichokilenga mwandishi.

Ni bayana kutokana na mfano huu kwamba mwandishi alikuwa anazungumzia ugonjwa wa UKIMWI kupitia kwa jazanda ya dudu. Ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa unatisha na ulienezwa kwa haraka katika jamii. Ugonjwa huu uliwaathiri wanadamu ambao waliukaribia peke yao. Mtindo huu wa uandishi unaupatia usanii uhai kwani msomaji haelezwi moja kwa moja kile kinacholengwa. Licha ya kumfikirisha msomaji, dhima nyingine ya lugha ya kitamathali ni kuhamasisha jamii. Dhima ya uhamasishaji ndiyo imejadiliwa katika sehemu ifuatayo.

### 6.1.2 Uhamasishaji wa Jamii

Kuhamasisha ni kuwapa watu mwanga au ufahamu kuhusu jambo fulani. Omary (2011) anaeleza kwamba uhamasishaji ni kitendo cha kuitaka jamii kufanya jambo fulani na kuacha kufanya jambo jingine kwa nia ya kuepuka madhara yanayoweza kupatikana kama hawatasikiliza maelezo ya mhamasishaji. Anaongezea kwamba jamii inaweza kukosa faida ambazo inaweza kuzipata kama haitasikiliza maelekezo ya mhamasishaji iwapo jambo analolihamasisha lina manufaa ya kiuchumi, kijamii na kitamaduni. Katika riwaya ya **Pendo katika Shari**, mwandishi kupitia kwa mhusika Almasi anaonyesha namna uhamasishaji unavyotekelezwa. Anasema:

**151. *Unajua kwamba pale karibu na madukani kuna kituo cha VCT? Hapo mwalimu amesema kwamba wale watu wanaougua UKIMWI huenda kupimwa na kupewa dawa za kutumia. Tena akasema dawa hizo huwa hazilipiwi. Hutolewa bure na serikali (Pendo Katika Shari, uk. 40).***

Katika dondoo lililo hapo juu, Almasi anamhamasisha mamake atembelee kituo cha VCT ili apewe dawa za kumsaidia kukabiliana na virusi vya UKIMWI. Anasema, *“Unajua kwamba pale karibu na madukani kuna kituo cha VCT? Hapo mwalimu amesema kwamba wale watu wanaougua UKIMWI huenda kupimwa na kupewa dawa za kutumia. Tena akasema dawa hizo huwa hazilipiwi. Hutolewa bure na serikali.”* Almasi anamueleza mamake kwamba mwalimu wao alikuwa amewaeleza kuhusu kituo hicho cha VCT. Hiki ni kituo ambapo wagonjwa wanaougua ugonjwa wa UKIMWI hupimwa kwa hiari. Hii ina maana kuwa mgonjwa mwenyewe ndiye hufanya uamuzi wa kuijua hali yake ya afya. Anamuelekeza pale ambapo kituo cha VCT kilikuwa na anamfahamisha kuwa wagonjwa wa UKIMWI huwa wanapimwa na kupewa dawa za bure ambazo hutolewa na serikali. Almasi analichukua jukumu la kumhamasisha mamake ili aweze kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI.

Katika riwaya ya **Kala Tufaha**, mwandishi ametumia jazanda kuhamasisha jamii. Kwa sababu ya madhara ambayo ugonjwa wa UKIMWI ulikuwa unaitetea jamii, waandishi tofauti walibuka na mbinu ya kuutundika ujumbe wa kuwahamasisha wanajamii mahali popote ambapo wangeupata kwa urahisi. Mpango huu ulikusudiwa kupunguza visa vya maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI. Katika dondoo linalofuata, msanii anasema:

**152.** *Ukutani mlitundikwa karatasi na mabango yenye ujumbe tofautitofauti kuhusu afya. Moja lilisema, “Kinga yashinda tiba”, jingine likanadi “uvutaji sigara wadhuru afya yako”Kubwa ya yote ni hilo bango kubwa lililonadi kwa wino mwekundu: “Jihadhari!” Lilikuwa na picha ya tufaha kubwa lililoiva kwelikweli. Linaonekna kama mtu kaliuma upande mmoja. Tufaha lenyewe lilikuwa na mdudu aliyefanana na kiwavi alijitokeza katika sehemu iliyong’atwa. Dudu lenye macho makubwa, sura ya kutisha lakini limetabasamu. Kando ya picha ya tufaha, pamechorwa picha ya watu wawili, mwanamume na mwanamke wa umri wa makamo. Wote wamelikodolea macho tufaha, wakionekana kulimezea mate. Kando yao pamechorwa jichwa linalotisha likiwa limetoa macho na ulimi. Jichwa lenyewe si la binadamu, si la mnyama! Chini yake hayo maandishi. “JIHADHARI” (Kala Tufaha, uk.181).*

Dondoo lililonukuliwa hapo juu limewasilishwa kijazanda ili limfikirishe sana msomaji. Msanii anasema, *“Ukutani mlitundikwa karatasi na mabango yenye ujumbe tofautitofauti kuhusu afya. Moja lilisema, “Kinga yashinda tiba,” jingine likanadi “uvutaji sigara wadhuru afya yako”Kubwa ya yote ni hilo bango kubwa lililonadi kwa wino mwekundu: “Jihadhari!” Lilikuwa na picha ya tufaha kubwa lililoiva kwelikweli. Linaonekna kama mtu kaliuma upande mmoja. Tufaha lenyewe lilikuwa na mdudu aliyefanana na kiwavi alijitokeza katika sehemu iliyong’atwa.”*

Mwandishi ametumia jazanda kwenye maelezo ambayo ametoa hapo juu. Jazanda ni mbinu ambapo mwandishi anaelezea matukio fulani kupitia kwa mafumbo. Katika muktadha huu, tufaha limelinganishwa na msichana. Msichana mwenyewe ana mdudu ambaye ni ugonjwa wa UKIMWI. Dudu lenye macho makubwa na sura ya kutisha linalotabasamu ni ugonjwa wa UKIMWI. Jicho linalotisha ni vifo vinavyotokea iwapo

mtu anaambukizwa na UKIMWI. Kuna picha ya mwanamume na mwanamke wa makamo ambao wamelikodolea macho tufaha na kulimezea mate. Picha hii inawakilisha vijana wa kike na wa kiume ambao wanatamani kufanya mapenzi. Isitoshe, chini yake kuna maandishi kwa herufi kubwa yanayosema ‘jihadhari.’ Neno ‘jihadhari’ limeandikwa kwenye bango kwa wino mwekundu kuonyesha hatari ya kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI iwapo watu hawatachukua hatua zinazofaa kujiepusha na maambukizi. Hivyo basi lugha hii ya kitamathali imetumika kuihamasisha jamii ijiepushe na ugonjwa hatari wa UKIMWI.

Tamathali za usemi kama kipengele cha mtindo kina dhima kubwa ya kufanya uhamasishaji kwa jamii ili ihakikishe kwamba inafanya kila linalowezekana kwa nia ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI. Tamathali za usemi zilizotumika katika maandishi teule yaliyotumika katika utafiti huu zinamhitaji kila mwanajamii kuchukua hatua stahiki katika kupambana na UKIMWI kwa nafasi yake bila kumuachia mmoja au taasisi fulani kufanya hivyo. Aidha, tamathali za usemi zina dhima kubwa ya kuihamasisha jamii kuogopa UKIMWI na kuuchukulia kama kizingiti kikubwa cha maendeleo ya mwanadamu, kwa vile hukatisha maisha ya mtu akashindwa kuafikia ndoto zake. Katika msingi huu, ni bayana kuwa kila mwanajamii akusikiliza na kuutekeleza uhamasishaji unaofanywa na tamathali za usemi katika maandishi teule ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi, maambukizi ya UKIMWI yatapungua kwa kiwango kikubwa. Pamoja na kuihamasisha jamii kujua ukweli kuhusu UKIMWI, lugha ya kitamathali ina dhima ya kufafanua mawazo ambayo yamejadiliwa katika sehemu ifuatayo.

### 6.1.3 Kufafanua Mawazo

Lugha za kitamathali katika maandishi teule ya fasihi andishi zina dhima ya kufafanua dhana tofauti zenye umuhimu na uhusiano kwa wanajamii husika. Kufafanua jambo ni kulitolea maelezo ya kina ili liweze kufahamika vyema mbele ya wote wanaopaswa kulifahamu jambo hilo kwa nia na maksudi ya msanii husika. Katika utafiti huu, tunaona kwamba tamathali za usemi zina dhima ya kufafanua namna mwathirika wa ugonjwa wa UKIMWI anavyoonekana.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, mwandishi anatuonyesha namna ambavyo Queen alikuwa ameathirika. Afya yake ilikuwa imeathirika kwa vile alikuwa ameambukizwa virusi vya UKIMWI. Tunapata maelezo ya ugonjwa wa UKIMWI kutokana na vile msanii anavyofafanua mawazo katika maelezo yake kupitia kwa taswira anayojenga. Mwandishi anafafanua mawazo kupitia kwa maelezo anayotoa kuhusiana na afya ya mhusika Queen. Anasema:

153. *Queen alikuwa amedhoofu sana. Mashavu yalikuwa yamebonyea, kifua kimesinyaa na ngozi yake ilikuwa imepauka na kuwa kavu kama mtu aliyekuwa kwenye mavumbi. Alikuwa amejitanda kanga safi, nyeupe zenye maua meusi. Kichwani alijifunga kitambaa, lakini nywele ambazo zilijitokeza pembeni mwa kitambaa zilikuwa zimelainika kama za mgonjwa wa utapia mlo (Ua la Faraja, uk.140).*

Katika dondoo lililo hapo juu, msanii anatumia taswira kueleza maumbile ya Queen baada ya kuanza kuathirika na UKIMWI. Msanii anatuonyesha namna Queen alivyokuwa amedhoofika, mashavu yakiwa yamebonyea na ngozi yake ikiwa imepauka na kuwa kavu. Anasema, “*Queen alikuwa amedhoofu sana. Mashavu yalikuwa yamebonyea, kifua kimesinyaa na ngozi yake ilikuwa imepauka na kuwa kavu kama mtu aliyekuwa kwenye mavumbi.*” Msanii anafafanua namna Queen alivyokuwa akionekana akisema kuwa, kichwani alikuwa amejifunga kitambaa lakini nywele ambazo zilijitokeza pembeni mwa kitambaa zilikuwa zimelainika kama za

mgonjwa wa utapia mlo. Maelezo haya yanafafanua maumbile na mavazi ambayo Queen alikuwa nayo wakati huo. Hivyo basi taswira iliyotumika imetekeleza dhima yake ya kufafanua hali halisi ya mhusika Queen. Mtu akiyasoma maelezo yaliyotolewa na mwandishi, anapata picha halisi ya afya ya Queen.

Katika riwaya ya **Kala Tufaha**, msanii aidha anatupa taswira ya mhusika Fumbwe ambaye pia ameathirika na ugonjwa wa UKIMWI. Mbinu mbalimbali za kitamathali zimetumika katika dondoo linalofuata kufafanua hali ya kiafya ya mhusika Fumbwe. Fumbwe alijihusisha katika maisha ya uzinzi na wanawake wengi hali iliyosababisha kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Msanii anatueleza:

**154.** *Mtu aliyekuwa akikanyaga ardhi ikitetemeka sasa hatazimiki amekonda mithili ya mfupa wa panya! Uso wake umejenga peto na makunyanzi ya daima. Amepata sura ya kikongwe wa umri wa miaka tisini na.....! Nywele zake zimepoteza weusi wa asili zikaanza kuiva kuwa rangi ya hudhurungi. Wala si nywele tena; zimelainika kama zitokazo kuwa singa, ama manyoya ya paka mzee! Zimetimka mfano wa manyoya ya kuku wa kidimu aliyenyeshewa. Midomo yake imekuwa miekundu mithili ya ile ya mlevi wa chang'aa. Macho yamechopoka na kuyafanya kuonekana makubwa kila saa na dakika. Amekuwa si wa kulala si wa kukaa! (Kala Tufaha, uk.169)*

Katika dondoo lililo hapo juu, mtunzi ametumia mbinu mbalimbali kutuchorea taswira ya mhusika Fumbwe. Mtunzi anatueleza kuwa, “*Mtu aliyekuwa akikanyaga ardhi ikitetemeka sasa hatazimiki amekonda mithili ya mfupa wa panya! Uso wake umejenga peto na makunyanzi ya daima. Amepata sura ya kikongwe wa umri wa miaka tisini na.....! Nywele zake zimepoteza weusi wa asili zikaanza kuiva kuwa rangi ya hudhurungi. Wala si nywele tena; zimelainika kama zitokazo kuwa singa, ama manyoya ya paka mzee!*” Fumbwe alikuwa na afya nzuri lakini punde tu alipoathirika na ugonjwa wa UKIMWI, tunamuona kama mtu aliyebadilika sana. Msanii anasema kuwa uso wake ulikuwa umejenga peto na makunyanzi na sura yake ikabadilika akawa kama kikongwe wa miaka tisini. Mtunzi anazidi kusema kuwa,

“nywele zake zilikuwa zimepoteza weusi wa asili na zikaanza kuiva kwa rangi ya hudhurungi. Midomo yake ilikuwa imegeuka miekundu mithili ya ile ya mlevi wa chang’aa.” Mtunzi akishirikisha matumizi ya taswira, tashbihi na tabaini anatufanya tuwe na picha halisi ya namna ambavyo mhusika Fumbwe alikuwa akionekana baada ya kuathirika na ugonjwa wa UKIMWI. Ufafanuzi wa mwandishi kupitia tamathali za usemi ndio unaotupatia ufahamu huu.

Mwandishi wa riwaya ya **Sitaki Iwe Siri** pia anatuchorea taswira ya mwathirika wa ugonjwa wa UKIMWI. Ugonjwa wa UKIMWI ulisitiriwa kama siri katika jamii inayorejelewa. Hii ndiyo sababu hata nyanya Mwalonga akakataa kuelezea wajukuu wake ugonjwa ambao uliwaua wazazi wao. Katika insha ambayo Musa aliandika ikashinda mashindano ya kuadhimisha siku ya UKIMWI duniani, mwandishi anatupatia hali iliyompata mhusika aliyejulikana kama Yuri. Mtunzi anasema:

**155. *Watu walikuwa wamenong’ona kuwa maumbile ya Yuri yamebadilika si haba. Kioo kilimwambia ukweli. Mwili wake ulikuwa umekondeana. Macho yalikuwa yamemwingia ndani. Mitulinga ilikuwa inaonekana huku mwili wake mzima ukinyong’onyea kama mkufu kwa sababu ya kuishiwa na nguvu. Laiti ungalimwona Yuri akiwa na siha yake (Sitaki Iwe Siri, uk.48).***

Kwa hakika ufafanuzi wa mwandishi unatupa picha kamili ya mhusika Yuri aliyeathirika na ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi anatumia, “*Watu walikuwa wamenong’ona kuwa maumbile ya Yuri yamebadilika si haba. Kioo kilimwambia ukweli. Mwili wake ulikuwa umekondeana. Macho yalikuwa yamemwingia ndani. Mitulinga ilikuwa inaonekana huku mwili wake mzima ukinyong’onyea kama mkufu kwa sababu ya kuishiwa na nguvu.*” Msanii anasema kuwa mwili wake ulikuwa umekondeana na macho yalikuwa yamemwingia ndani. Msanii anaongeza kuwa mitulinga ilikuwa inaonekana huku mwili wake mzima ukinyong’onyea kama mkufu kwa sababu ya kuishiwa na nguvu. Katika dondoo lililonukuliwa, ni wazi

kwamba msanii ameshirikisha mbinu kadha wa kadha kama vile tashbihi na taswira katika kutuelezea hali ya mwathirika wa ugonjwa wa UKIMWI. Maelezo haya yanatoa ufafanuzi wa mawazo katika riwaya kuhusu dhamira zinazohusiana na ugonjwa wa UKIMWI.

Kwa jumla, twaweza kusema kwamba mbinu za lugha na tamathali za usemi zimetumika katika maandishi teule ya fasihi andishi kufafanua mambo mbalimbali yanayowafika wanajamii. Dhamira kuhusu dhuluma kwa wanawake, unyanyapaa, uasherati, ukosefu wa uwajibikaji miongoni mwa nyingine zimefafanuliwa vyema na tamathali tofautitofauti za usemi. Licha ya dhima za kimaudhui, kuna dhima za kifani za tamathali za usemi. Dhima hizo za kifani ndizo ambazo zimeshughulikiwa katika sehemu inayofuata.

## **6.2 Dhima ya Tamathali za Usemi Kifani**

Fani ni jumla ya mbinu, mtindo na nyenzo anazotumia mwandishi kuiwasilisha dhamira na maudhui yake. Wamitila (2003) anasema kuwa mwandishi hawezi kusema analotaka kulisema bila ya kuitumia lugha. Lugha huwa na vikolezo au vitia ladha fulani na imesheheni mbinu za kila aina. Haiwezekani mwandishi kuiwasilisha dhamira yake au kuyapitisha maudhui yake bila ya kutegemea fani. Ikiwa mwandishi anataka kuwasiliana na msomaji wake vyema pamoja na kumshawishi na kumwathiri ipasavyo, lazima aiteue lugha yake vyema au ahakikishe kwamba lugha yake ina uwezo wa kuuwasilisha ujumbe huo. Uhusiano wa fani na maudhui ni muhimu sana na ni wa kutegemeana. Kwa msingi huo, tamathali za usemi zina dhima za kifani kama inavyofafanuliwa katika sehemu ifuatayo.



### 6.2.1 Kupamba lugha

Tamathali za usemi ni mojawapo ya vipengele vya matumizi ya lugha ambapo matumizi ya lugha kwa jumla ni kipengele cha kifani. Kipengele hiki kina mchango mkubwa katika kuipamba na kuirembua lugha kwa wasomaji wake. Lugha ya kitamathali inapotumika na msanii ina mchango mkubwa wa kuifanya iwe yenye kuwavutia wasomi wa kazi husika ya fasihi. Baadhi ya tamathali za usemi ni kama vile: tashbihi, sitiari, kinaya, tashhisi na chuku.

Matumizi ya tamathali za usemi yanatofautiana kutoka msanii mmoja hadi mwingine kwa sababu ya upekee. Wasanii walio na tajriba ya uandishi na waliobobea sana hutumia tamathali nyingi za usemi ikilinganishwa na wale ambao bado ni chipukizi. Aidha, upekee wa masimulizi ya mwandishi hujitokeza kupitia kwa tamathali za usemi. Msomaji huvutiwa kusoma kazi fulani ya fasihi kutegemea namna ambavyo mwandishi ameandika na kuiwasilisha.

Matumizi bora ya tamathali za usemi yataifanya kazi husika iwe ya kuvutia sana. Aidha, yataamwezesha msomaji wa kazi hiyo kuielewa kwa wepesi kwa maana atachochewa kuzidi kuisoma. Aidha, matumizi ya tamathali za usemi ndiyo yanayoleta upekee wa waandishi wanapotunga kazi zao. Tazama matumizi haya ya lugha ya mwandishi Omar (2008):

**156. *Picha yenyewe iliashiria enzi ambayo Ma' Asha alikuwa mwanamgeni kweli! Nywele nyeusi tititi! Mabegani kalaza matando. Ametoa tabasamu inayodhihirisha vibonyo kwenye mashavu. Meno yake meupe kisha yenye mwanya katikati. Macho yenyewe ya kikombe. Kwenye nyusi athari ya wanja inaonekana. Kaka kwenye gogo kisha kaegemeza kidevu chake kwenye kitanga cha kulia. Tufaha ashapewa habari nyingi, kisa cha mwenye picha. Si na Biti Mejumaa tu, hata na Ma' Asha mwenyewe (Kala Tufaha, uk.108).***

Katika dondoo lililo hapo juu, mwandishi ameipamba lugha kwa kushirikisha matumizi ya taswira na tanakali za sauti. Mtunzi anasema, “*Picha yenyewe iliashiria*

*enzi ambayo Ma' Asha alikuwa mwanamgeni kweli! Nywele nyeusi tititi! Mabegani kalaza matando. Ametoa tabasamu inayodhihirisha vibonyo kwenye mashavu. Meno yake meupe kisha yenye mwanya katikati. Macho yenyewe ya kikombe. Kwenye nyusi athari ya wanja inaonekana. Kaka kwenye gogo kisha kaegemeza kidevu chake kwenye kitanga cha kulia.”* Katika dondoo lililonukuliwa, kuna matumizi ya taswira na tanakali za sauti pamoja na uteuzi faafu wa msamiati unaoifanya lugha ivutie sana msomaji. Matumizi haya ya lugha yanaongeza vionjo na hivyo kuipamba. Maumbile ya Ma'Asha akiwa bado kijana yanawasilishwa vyema kwa msomaji kwa uteuzi wa lugha faafu kwa ufundi mkuu. Msanii anatupa taswira ya mhusika huyu anaposema nyeusi tititi, meno meupe yenye mwanya katikati na mwenye macho ya kikombe. Tamathali za usemi zina dhima ya kuipamba lugha na wakati wasomaji wanafurahia uzuri wa lugha hiyo wanapata dhamira zilizokusudiwa na msanii husika.

Waandishi mbalimbali hushirikisha matumizi ya tamathali kadha wa kadha wanapowasilisha ujumbe wao kwa lengo la kuifanya lugha ivutie msomaji. Katika riwaya ya Kala Tufaha, mwandishi anasema:

**157.** “ *Ninafanya nini kitandani? Sasa mazoea na chumba hiki; iweje leo nimechupa mipaka hadi ya kulala kitandani? Taratibu fikra zilimpa kung'amua lililotendeka...alijihisi kuwa na mavune mithili ya mtu aliyechekesha na kushinda kwenye kazi ya shokoa. Mara akapata maumivu makali katika eneo alilohofia. Papo hapo msichana wa wenyewe akapiga unyende na kukurupuka kutoka kitandani...Fumbwe alimvuta na kumkumbatia Kibibi ambaye sasa alikuwa kama mwehu...”* (Kala Tufaha uk.66)

Katika dondoo lililonukuliwa, mwandishi anatuelezea kisa kilichompata mhusika Kibibi wakati ambapo alibakwa na Fumbwe. Katika maelezo yaliyotolewa, mwandishi anashirikisha tamathali mbalimbali katika harakati zake za kupitisha ujumbe. Mbinu ya uzungumzi nafsia imetumika pale ambapo Kibibi anajiuliza pale alipojipata baada

ya kutoka usingizini. Aidha mtunzi ametumia taswira ili kutupa picha halisi ya kile kilichotendeka katika muktadha huu. Mwandishi vilvile ametumia tashbihi na tamathali zingine anaposema, *‘alijihisi kuwa na mavune mithili ya mtu aliyechekesha na kushinda kwenye kazi ya shokoa. Mara akapata maumivu makali katika eneo alilohofia. Papo hapo msichana wa wenyewe akapiga unyende na kukurupuka kutoka kitandani...Fumbwe alimvuta na kumkumbatia Kibibi ambaye sasa alikuwa kama mwehu...’*

Kutokana na dondoo hili, mwandishi ameshirikisha tamathali kadha wa kadha za usemi anapopitisha ujumbe wake kwa wasomaji. Matumizi ya mbinu ya uzungumzi nafsia, taswira na tashbihi inaweka vionjo kwa ujumbe na kuufanya uvutie msomaji. Matumizi kama hayo ya lugha humwezesha mwandishi kuipamba lugha anayotumia kupitisha ujumbe.

### **6.2.2 Uwezo wa msanii kuchagua muundo na mtindo wa kazi yake**

Msanii yeyote ana uhuru wa kuchagua muundo na mtindo ambao anaona unaweza kufanikisha dhamira yake kwa wasomaji wake. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kwamba fani katika kazi yoyote ya fasihi ya Kiswahili imeundwa kutokana na vipengele mbalimbali kama vile muundo, wahusika, mtindo, mandhari na matumizi ya lugha. Matumizi ya tamathali za usemi katika kazi yoyote ya fasihi yana dhima ya kumwezesha msanii kuchagua muundo na mtindo wa kazi yake. Tamathali za usemi zinamwezesha msanii kuchagua kuandika kazi yake ikiwa ni riwaya, tamthilia, hadithi fupi au hata ushairi. Tamathali za usemi zinamwezesha msanii kuichezea lugha jinsi apendavyo ili kuafikia lengo lake. Ujenzi wa wahusika, mandhari na vipengele vingine vya kifani vinategemea pakubwa matumizi ya tamathali za usemi. Baada ya

kuangalia dhima za kifani za tamathali za usemi, tumeshughulikia mchango wa kazi teule za fasihi katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI katika sehemu ifuatayo.

### **6.3 Mchango wa kazi teule za fasihi katika kukabiliana na UKIMWI**

Katika sehemu hii tumechunguza namna maandishi teule yaliyotumiwa katika utafiti huu yametumika katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI pamoja na kuwaonya wahusika kuhusu mienendo inayoweza kusababisha waambukizwe. Baadhi ya maandishi pia yanawapa moyo waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI kwa kuwapa matumaini ya kuweza kuendelea kuishi maisha ya kawaida.

Wakati wote msimulizi huwa na dhamira au mwelekeo fulani anaokusudia msikilizaji au msomaji wake kuupata. Katika uhakiki wa matini, Genette (1980) anaeleza kwamba ni vyema kuweza kutambua yafuatayo katika kazi yoyote; ni nani anaona, nani anawakilisha mtazamo wa msimulizi na nani anayezungumza. Tukizingatia kauli hii, mtazamo wa msimulizi umetuwezesha kuchunguza kusudi la masimulizi haya kama yenye lengo la kuonya wale ambao hawajapata maradhi ya UKIMWI kuepukana na mienendo inayoweza kuwaingiza katika janga hili. Aidha, maandishi haya yanapendekeza njia ya kufanya mapenzi salama ya kumwezesha mhusika kuepuka kuambukizwa. Aidha, mtazamo huo umetuwezesha kuona njia za kuwafariji wahusika walioathiriwa kwa kuwapa matumaini ya kuishi maisha ya kawaida. Sehemu ifuatayo inafafanua mambo haya kwa kina.

#### **6.3.1 Kuepukana na uasherati**

Waandishi mbalimbali katika maandishi teule wanaionya jamii dhidi ya uasherati ambayo ndiyo njia kuu ya kueneza maradhi ya UKIMWI. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005), msanii anaionya jamii dhidi ya uasherati kama njia inayoeneza maradhi ya UKIMWI. Katika riwaya, mhusika Queen alikuwa mwanamke mashuhuri

mtaani kwa urembo wake, msomi na mwenye cheo kikubwa kazini kwake. Ingawa hivyo, mwanamke huyo hakujiheshimu kwa kuwa alifanya mapenzi na wanaume wengi kama vile Ngoma na Omolo. Mwandishi anasema:

**158.** *Queen! Jina hili lilivuma akilini mwake kwa nguvu kama upepo wa kimbunga. Ni kweli kwamba mwanamke yule malaya amewajeruhi watu aliowapenda kiasi kile? Kama amedhuru Ngoma, basi hata dada yake amedhurika. Na kama hao wamedhurika, Omolo je, atakuwa amepona? Asubuhi ya usiku ile, Queen ndiye aliyepiga simu na kumwambia ana jambo la muhimu kumwambia Omolo. Pengine jambo lenyewe ni hizo habari za UKIMWI! upepo wa kimbunga. Wazo la Omolo kuweza kufanya mapenzi na malaya huyo lilimchafua moyo. Hakupenda kulifikiria. Akalirushia pembeni. Akamtazama dada yake. Alishindwa kummaliza (Ua la Faraja, uk.59-60).*

Ingawa mhusika Queen alikuwa mtu mashuhuri katika jamii, aliharibu umaarufu wake kwa kushiriki uzinzi. Alifanya mapenzi na wanaume wengi kama vile Ngoma na Omolo na kuchangia katika kueneza maradhi ya UKIMWI. Msanii anasema, “*Ni kweli kwamba mwanamke yule malaya amewajeruhi watu aliowapenda kiasi kile? Kama amedhuru Ngoma, basi hata dada yake amedhurika. Na kama hao wamedhurika, Omolo je, atakuwa amepona? Asubuhi ya usiku ile, Queen ndiye aliyepiga simu na kumwambia ana jambo la muhimu kumwambia Omolo. Pengine jambo lenyewe ni hizo habari za UKIMWI!*” Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, twaelezwa na msanii namna ambavyo Queen alitaka kufanya mapenzi kwa lazima na Omolo. Ilibidi atumie ujanja wa kuweka dawa ya kuamsha hisia kwa kinywaji cha Omolo ndipo akafaulu kufanya naye mapenzi.

Msanii anatufahamisha kwamba ni muhimu kuwa na mpenzi mmoja aidha kuwa waaminifu katika maisha ya ndoa. Iwapo mhusika Queen angekuwa na mpenzi mmoja, mke wa Ngoma aitwaye Tabu hangeambukizwa maradhi ya UKIMWI. Tabia na mwenendo wa uzinifu wa mhusika Queen ndio uliosababisha akaambukizwa ugonjwa wa UKIMWI uliomletea aibu mpaka akafikia kiwango cha kujinyonga.

Kama angeepuka uasherati, Queen hangemaliza maisha yake kwa njia ya aibu kwa kujitoa uhai.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, mhusika mwingine aliyekuwa malaya pale Tandika alikuwa Asha. Asha Mmayema alikuwa na rafiki Mzungu aliyeitwa Hastings. Kabla ya kifo chake, Hastings alimjengea Asha nyumba nzuri ya ghorofa na kumwachia pesa nyingi. Baada ya kifo cha Hastings, Asha hakutaka kuolewa na kwa sababu alikuwa na mali, hakutaka kujifunga katika ndoa. Alitaka uhuru na kutokana na uhuru huo akawa na uhusiano na wanaume wengi. Asha alikuwa na pesa zilizomfanya kuwa na uhuru wa kuwanunua wanaume. Yeye hakuwa mhitaji na hivyo aliweza kuchagua kufanya mapenzi na mwanaume aliyependa. Mwandishi anatuambia :

**159.** *Asha akacheka sana akasema ‘Sinunuliwi’. Nitakununua wewe kwa senti hamsini na busu moja shavuni. Msafiri akanyanyuka kwa nguvu na kutaka kumwendea pale alipo. Macho yake yalikuwa mekundu kwa shauku. Asha akacheka, akanyanyuka na kujifanya anataka kukimbia. Mwili wake ulikuwa mzito. Msafiri akamwendea (Ua la Faraja, uk.81).*

Uhuru wa Asha unampa kibali cha kushiriki mapenzi na Ngoma. Kutokana na uhusiano huu, Asha anapata UKIMWI kwa vile Ngoma alikuwa rafikiye Queen ambaye alikuwa ameambukizwa UKIMWI. Mwandishi anasema, “*Msafiri akanyanyuka kwa nguvu na kutaka kumwendea pale alipo. Macho yake yalikuwa mekundu kwa shauku.*” Kutokana na tabia na mienendo ya Asha tunaona maradhi haya yakiingia moja kwa moja katika ndoa ya Msafiri. Kwa mintarafu ya matukio haya, msimulizi anatahadharisha dhidi ya kushirikiana na wanawake malaya kama vile Queen na Asha. Iwapo wanaume watajihusisha na wanawake kama hawa, ni vyema, kutumia mipira ya kondomu kama alivyofanya Omolo. Omolo alilala na Queen lakini akatumia mipira na hivyo akaepuka kuambukizwa maradhi ya UKIMWI. Ujumbe wa mtunzi ni kwamba, jamii inapaswa kukomesha mienendo na tabia ya uzinzi wa

wahusika kama ville Asha ndipo iepukane na maenezi na usambazaji wa ugonjwa wa UKIMWI.

Katika riwaya ya **Kala Tufaha**, mtunzi pia anatuonyesha wahusika ambao walijihusisha na uasherati. Msanii anatueleza kuwa mhusika Fumbwe alishiriki uasherati sana baada ya kutengana na mke wake Hatima. Mtunzi anatueleza kuwa Fumbwe alifika mahali akawa mtu asiyepisha rinda kumaanisha kuwa alikuwa anafanya mapenzi kiholela. Mhusika Fumbwe anapofumana mke wake Hatima, aliamua kujiingiza katika ulevi pamoja na kufanya mapenzi na wanawake wengi na mwishowe kupata ndwele isiyotibika. Kauli hii inathibitika kutokana na tabia za Fumbwe ambaye anafanya mapenzi na wasichana wadogo hata ofisini. Mwandishi anatueleza kuwa:

**160.** *Baada ya muda mfupi, alitoka ndani msichana: alivaa nguo zilizoonya zaidi ya kusitiri. Harufu ya manukato ilimfuata alipopita. Alielekea walikokuwa wamekaa watu akasonga karibu na Tufaha. Yule bwana aliingia ndani. ‘Mpaka kesho’, alisema. ‘Haya kwa heri’, aliitikia mhazili. Simu ililia na yule msichana akarudi tena ofisini. Yaonekana mkutano wake na mwenye ofisi ulikuwa muhimu sana. Kikao chenyewe kilidumu kwa muda wa saa tatu. Msichana wa watu alipotoka mle ofisini alionekana kuchoka. Kibeti chake kwapani alifululiza mlangoni huku nyuma akiacha harufu kali ya marashi. Hakutaka kuwatizama waliokuwa ukumbini (Kala Tufaha, uk.119).*

Tabia na mienendo ya Fumbwe kujiingiza katika uasherati inadhihirika wazi katika dondoo lililo hapo juu. Msanii anatueleza kuwa, “*Baada ya muda mfupi, alitoka ndani msichana: alivaa nguo zilizoonya zaidi ya kusitiri. Harufu ya manukato ilimfuata alipopita. Alielekea walikokuwa wamekaa watu akasonga karibu na Tufaha. Yule bwana aliingia ndani. ‘Mpaka kesho’, alisema. ‘Haya kwa heri’, aliitikia mhazili.*” Hakutambua kwamba tabia hii hatimaye ingemletea madhara. Matokeo yalikuwa kwamba mwishowe alipata maradhi ya UKIMWI yaliyomtatiza mpaka yakamuua.

Mwandishi anapoiangazia tabia ya Fumbwe, anawatahadharisha wanawake kutojihusisha na wanaume wenye wapenzi wengi kwa vile tendo hili laweza kusababisha wapate maradhi ya UKIMWI. Kutokana na mifano hii, wasanii wanaonya dhidi ya uasherati kama njia mojawapo ya kujiepusha na maradhi ya UKIMWI. Ni wazi kuwa wahusika wengi wanaoambukizwa maradhi ya UKIMWI katika riwaya zilizotajwa wanashiriki katika uasherati unaowaletea maangamizi hatimaye. Wengi wao hatimaye hufariki.

Katika riwaya ya **Pendo katika Shari**, mwandishi anasawiri maisha ya mhusika Sulubu ambaye alimdhulumu mkewe kwa kujiingiza katika kufanya mapenzi kiholela. Hata marafiki wa Sulubu wanashuhudia kwamba Sulubu hakuwa mwaminifu katika maisha yake ya ndoa. Licha ya ushauri ambao Sulubu alipewa na marafiki zake, aliwapuza na kuendelea na tabia yake ya uzinifu. Mwandishi anataeleza:

**161. *Sulubu, mimi nakujua vizuri sana. Wewe una wapenzi chungu nzima na wengine hata huwajui majina yao. Kwa hivyo, huwezi kujua ni yupi atakayekuambukiza maradhi baadaye. Leo una Amina, kesho kwa Cheupe, kesho kutwa kwa Rosa. Huoni unajitia kitanzi? Unajua UKIMWI unaua maelfu ulimwenguni lakini unafikiri wewe huwezi kuwa mmoja wa hao maelfu? (Pendo katika Shari, uk. 30)***

Kutokana na dondoo lililo hapo juu, mwandishi anaionya jamii dhidi ya kujihusisha na wapenzi wengi na kufanya nao mapenzi kiholela. Mtunzi anasema, “*Sulubu, mimi nakujua vizuri sana. Wewe una wapenzi chungu nzima na wengine hata huwajui majina yao. Kwa hivyo, huwezi kujua ni yupi atakayekuambukiza maradhi baadaye. Leo una Amina, kesho kwa Cheupe, kesho kutwa kwa Rosa. Huoni unajitia kitanzi? Unajua UKIMWI unaua maelfu ulimwenguni lakini unafikiri wewe huwezi kuwa mmoja wa hao maelfu?*” Twaelezwa na msanii kuwa Sulubu alikuwa na wapenzi ambao hakuwajua wengine kwa majina. Zaidi ya hayo alikuwa anawabadilisha kama nguo na hangejua ni yupi ambaye angemuambukiza UKIMWI. Hatimaye, Sulubu



alipata maradhi ya UKIMWI kisha akawaambukiza wake zake Rehema na mtoto Pendo. Wanawake wote pamoja na mtoto Pendo walifariki baada ya kupata UKIMWI. Sulubu mwenyewe hatimaye alifariki kutokana na maambukizi ya maradhi haya. Hivyo basi mwandishi analenga kutufahamisha kuwa njia mojawapo ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni kujiepusha na tabia ya uasherati na badala yake kuzingatia maadili mema katika jamii. Aidha, ni vizuri kuzingatia mawaidha tunayopewa hususan kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI.

Katika tamthilia ya **Orodha**, mwandishi amewasawiri wahusika kadha wa kadha wakiwa na tabia ya kujihusisha katika mapenzi kiholela. Furaha na Mary ni mfano wa wahusika wa kike wanaojiingiza katika maisha ya uzinzi. Wahusika kama vile Salim, Kitunda, Padri James, Ecko na Juma wamesawiriwa kuwa watu wanaopenda kufanya mapenzi kiholela.

Mtunzi anapendekeza matumizi ya kondomu, uaminifu wa mapenzi, ufahamu na uelewa, uadilifu na uwajibikaji kama njia bora za kupambana na ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi ana msimamo kwamba njia bora ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI ni kuepukana na tabia za uasherati ambazo zinakiuka maadili ya jamii. Licha ya kuepuka uasherati kwa kuzingatia maadili ya jamii, wasanii katika kazi zilizoteuliwa katika utafiti huu wamependekeza matumizi ya mipira ya kondomu kama njia ya kupambana na UKIMWI. Sehemu inayofuata inajadili matumizi ya mipira ya kondomu kama njia nyingine ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI.

### **6.3.2 Matumizi ya mipira ya kondomu**

Waandishi wa kazi teule zilizotumiwa katika utafiti huu wanaangazia matumizi ya mipira ya kondomu kama njia bora ya kuepuka kuambukizwa maradhi ya UKIMWI. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, mwandishi kupitia mhusika Jose anaonyesha namna

ambavyo matumizi ya kondomu ni muhimu katika kuepuka maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI. Jose alifanya kazi ya kuhamasisha watu kuhusu matumizi ya ‘soksi’ au kondomu na ndiyo sababu pia alikuwa akifanya biashara ya kuuza kondomu. Wazo hili lilibainika zaidi kutokana na juhudi za Jose kuuza mipira ya kondomu pale Malaika baa kila jioni. Kila jioni alisikika akipaza sauti akisema:

**162. *Mambo kwa soksi! Mambo kwa soksi! Maji uyavulie nguo ndipo ukayaoge! Ulapo ndizi usiimenye ila ivishe gando! Jando la raha leo ni kuvishana magozi! ( Ua la Faraja, uk. 12)***

Kupitia Jose, mwandishi anasisitiza matumizi ya mipira ya kondomu katika kufanya ngono. Mtunzi anasema, “*Mambo kwa soksi! Mambo kwa soksi! Maji uyavulie nguo ndipo ukayaoge! Ulapo ndizi usiimenye ila ivishe gando.*” Kupitia kwa Jose, msanii anasema kuwa ukitaka kula ndizi, usiimenye ila uivishe gando. Aidha anaongeza kuwa mtu akitaka kuifurahia ngono salama hana budi kuvaa mipira au kondomu. Kulingana na Jose, dhana ya kuvishana mipira inafaa kuwa jukumu la watu wote iwapo wanajamii wangetaka kufanikiwa katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI.

Katika jamii kuna watu wengi ambao hawapendi kuvaa mipira ya kondomu wanapofanya mapenzi kwa maana wanaamini kuwa raha ya kufanya ngono inapungua mtu anapotumia mipira hiyo. Wazo hili linashadidiwa na mtunzi wa tamthilia ya **Kilio Chetu** kupitia mhusika Joti. Joti anajidai vile alivyompeleka msichana katika gesti ya Msomali na kufanya mapenzi. Anasema, “ Shiti wewe. Nini kondomu bwana! Pekepeku tu... Unaweza kula pipi na ganda lake wewe?” (uk. 18). Ni bayana kutokana na dondoo hili kwamba vijana hawakufurahia kutumia mipira ya kondomu. Matokeo yake yalikuwa kwamba Joti hatimaye aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Hivyo basi, ili jamii ipunguze uwezekano wa kupata au kuambukizwa virusi vya UKIMWI, pana haja ya wanajamii kuwajibika na kutumia mipira ya kondomu.

Mhusika mwingine ambaye alishangazwa na Jose ni Omolo. Sababu ni kwamba Jose alichukua tatizo la maradhi ya UKIMWI kama lake binafsi. Ingawa hivyo, Omolo alijua kuwa ilikuwa muhimu kutumia mipira wakati wa kufanya ngono. Omolo alikuwa rafikiye Queen ambaye walikuwa wamejuana katika shughuli za kazi. Queen na Omolo hata hivyo, walikuwa wamefanya mapenzi kwa kutumia mipira ya kondomu. Mwandishi anatumia:

**163.** *Kama Mima siku ile, Queen alishitushwa na kutotahiriwa kwa Omolo. Lakini yeye akawa mstaarabu. Hakucheka wala kughairi. Ila alikwenda kabatini akatoa mipira wa kiume, akamrushia Omolo akachukua na kuvaa. Na siku ikawa ya kwanza kwa Omolo kulifurahia tendo lile akiwa katika utu uzima wake. Mipira miwili ilitumiwa na siku ile aliporudi nyumbani kwake ilikuwa usiku. Alichoka sana. Hakuwa na hamu ya kwenda Malaika bar (Ua la Faraja, uk.52).*

Omolo alifurahia tendo lile bila wasiwasi wowote wa maambukizi. Mtunzi anatumia kuwa usiku ule Omolo alitumia mipira miwili akifanya mapenzi na Queen. Mtunzi anasema, *“Queen alishitushwa na kutotahiriwa kwa Omolo. Lakini yeye akawa mstaarabu. Hakucheka wala kughairi. Ila alikwenda kabatini akatoa mipira wa kiume, akamrushia Omolo akachukua na kuvaa. Na siku ikawa ya kwanza kwa Omolo kulifurahia tendo lile akiwa katika utu uzima wake. Mipira miwili ilitumiwa na siku ile aliporudi nyumbani kwake ilikuwa usiku.”* Hii inaonyesha kuwa iwapo wanajamii watatumia mipira watafurahia tendo la kujaminiana bila woga wowote. Japo Queen alitumia mipira, hakuwa akifurahia tendo lenyewe. Alimwambia Omolo aende akakamilishe tohara. Hii ina maana kwamba bado baadhi ya wanajamii hawatilii maanani matumizi ya mipira ya kondomu katika kukabiliana na maambukizi ya maradhi haya. Kwa maoni yao, matumizi ya mipira inawafanya wakose kufurahia ngono. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, Omolo anaepuka maradhi ya UKIMWI kwa

kutumia mipira ya kondomu. Japo Omolo hakupendezwa na kazi ya Jose, alijua kuwa mipira ya kondomu ilikuwa muhimu katika kuepuka maambukizi.

Katika riwaya ya **Ua la Faraja**, Ngoma alikuwa rafiki yake Queen lakini hawakutumia mipira ya kondomu ndiyo maana akaambukizwa UKIMWI. Tofauti na mhusika Omolo, Ngoma anatumia mipira na mkewe wakati tayari alikuwa amepata maradhi ya UKIMWI. Ngoma alisahau kuchukua tahadhari mapema wakati ambapo alikuwa akifanya mapenzi na Queen pamoja na wanawake wengine. Baada ya kushuku kwamba alikuwa ameambukizwa maradhi ya UKIMWI ndipo alipojifanya kuwa anatumia kinga wakati alipokuwa akifanya mapenzi na mke wake. Tunaambiwa na mwandishi:

**164.** *Ngoma alifanya kazi kubwa kulaghai mke wake mpaka akamwamini. Hivyo, siku ile walifanya tendo la ndoa kwa kutumia mipira. Lakini tendo lile lilikuwa geni kwao. Hakuna aliyefurahia. Walijiona kama wanacheza kama watoto wadogo wanaoigiza mchezo wa ndoa vichakani, maana umuhimu na heshima ya tendo lile vikapaushwa na kuweko kwa ukuta wa mpira, uliotenganisha miili na damu zao; ukuta ambao haukuwa na sababu kama kila mmoja wao angekuwa mwaminifu; ukuta ambao, katika hisia za Tabu, ulikuwa mwanzo wa kutenganisha miili na nafasi zilizounda unyumba wao (Ua la Faraja, uk.31).*

Mhusika Tabu anaona kwamba matumizi ya mipira katika ndoa yanafanya tendo lile la ngono lisifurahishe, kwake mipira inaleta utengano. Msanii anasema, *“Hivyo, siku ile walifanya tendo la ndoa kwa kutumia mipira. Lakini tendo lile lilikuwa geni kwao. Hakuna aliyefurahia. Walijiona kama wanacheza kama watoto wadogo wanaoigiza mchezo wa ndoa vichakani, maana umuhimu na heshima ya tendo lile vikapaushwa na kuweko kwa ukuta wa mpira, uliotenganisha miili na damu zao; ukuta ambao haukuwa na sababu kama kila mmoja wao angekuwa mwaminifu.”*

Tabu anasema kuwa huo ulikuwa mwanzo wa kutenganisha miili na nafsi zilizounda unyumba wao.

Tangu waoane, Ngoma na mke wake hawakuwahi kutumia mipira wa kondomu. Kama vile Queen, Tabu ni mhusika ambaye kwake matumizi ya mipira hayakumpa raha lakini mwandishi anatuonyesha kuwa iwapo tutatumia mipira tutaepuka maambukizi ya UKIMWI. Ngoma alitumia mipira wakati tayari alikuwa amepata maradhi yale na kumwambukiza mke wake. Lakini iwapo angetumia mipira mara ya kwanza na rafikiye Queen, hangemwambukiza mke wake. Kwa mujibu wa mtazamo wa mwandishi, tunaona akisisitiza kuwa tunaweza kuepuka maradhi ya UKIMWI iwapo wanajamii watazingatia matumizi ya mipira ya kondomu. Laiti wabusika wale waliokuwa *Malaika Bar* wangemsikiliza Jose, hawangepata maradhi ya UKIMWI.

Ingawa matumizi ya mipira ya kondomu yanaonekana kuwa njia bora ya kuzuia kuenea kwa maradhi ya UKIMWI, wazo hili limepata pingamizi kutoka asasi za kidini. Kulingana na Thavis (2009), kanisa Katoliki lilipinga matumizi ya mipira ya kondomu katika ndoa na kusisitiza elimu ya kujamiana kwa kuzingatia uaminifu. Viongozi hawa wa kidini wanasema kuwa kutegemea mipira ya kondomu katika kuzuia maambukizi ya maradhi ya UKIMWI kutawadanganya wanajamii, kwa sababu wakati mwingine mipira hii hupasuka. Kuhimiza matumizi ya mipira kutafanya wanajamii kushiriki katika ngono za kiholela na uasherati.

Kulingana na Katherya (2002), serikali na wanajamii wanafaa kusisitiza uaminifu katika uhusiano na wala si matumizi ya mipira ya kondomu. Maoni ya viongozi wa Kikatoliki ni mazuri lakini hayawezi kuwa ya uhalisia katika jamii ya kisasa. Ingawa walio katika ndoa wanaweza kujaribu kuwa waaminifu, ni takriban asilimia moja tu ambao watakuwa waaminifu. Kwa hivyo, wale ambao wanakosa uaminifu wanaweza kuepuka UKIMWI ikiwa watatumia mipira wakati wa kufanya ngono. Isitoshe, kuna vijana wengi ambao hawajaoa na ni vigumu sana katika jamii ya sasa kusema kuwa

vijana wote watajitunza na kuepuka kufanya mapenzi kabla ya ndoa. Ukweli ni kuwa vijana wanaofanya mapenzi kabla ya ndoa ni wengi kuliko wale wanaojitunza. Hivyo basi pana haja ya kuihamasisha jamii kutumia mipira ya kondomu kama njia ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Matumizi ya mipira pekee hayawezi kufaulu kwenye vita dhidi ya UKIMWI. Uwazi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI unaweza kuchangia pakubwa katika kukabiliana na ugonjwa huu. Sehemu inayofuata inajadili uwazi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI kama inavyojitokeza katika maandishi teule yaliyotumika katika utafiti huu.

### **6.3.3 Uwazi kuhusu UKIMWI**

Vita dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI vitafaulu tu iwapo jamii itakuwa na uwazi kuuzungumzia ili kupata maelezo ya kutosha kuhusu. Katika riwaya ya **Sitaki Iwe Siri**, mwandishi anaisawiri jamii ikijaribu sana kuuficha ukweli kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Nyanya Mwalonga alijaribu sana kuwaficha wajukuu wake kuhusu maradhi yaliyowaua wazazi wao. Alikuwa na hofu kuu kuwafahamisha ugonjwa uliomuua mtoto wake Matano na mke wake. Ugonjwa wa UKIMWI uliogopwa na haungetajwa tu kwa uwazi hadharani. Kitendawili cha kifo cha wazazi wa Musa kilimchochea afanye utafiti wa ugonjwa wa UKIMWI.

Musa alishiriki katika shindano lililoandaliwa na Shirika la Afya Ulimwenguni pamoja na Wizara ya Afya kuadhimisha siku ya UKIMWI ulimwenguni. Katika shindano hili, Musa aliibuka mshindi kwa kuandika insha nzuri sana kuhusu mada ya “Sitaki Iwe Siri”. Hii ina maana kwamba ugonjwa wa UKIMWI haukustahili kuwekwa kama siri kinyume cha mawazo ya nyanya Mwalonga. Nyanya anakiri kwamba alitaka kuwaficha wajukuu wake kuhusu chanzo cha vifo vya wazazi wao

lakini mwandishi anasema kuwa nyakati za kuuficha ugonjwa wa UKIMWI zilikuwa zimepita. Mwandishi anasema:

**165.** *Asante kwa kunipa fursa hii. Mimi nitasema machache sana. Kwanza nashukuru wote mnaoelimisha kizazi hiki cha baadaye ambacho kitachukua mahala petu. Maanake sisi tumekwisha kuzeeka. Ni sadfa kwamba siri niliyoighubika kwa miaka mingi ili wajukuu zangu wasiijue imefichuliwa. Wajukuu wangu hawa ni mayatima. Wazazi wao walifariki kutokana na maradhi ya UKIMWI, nao wakabaki mikononi mwangu. Waliponiuliza kilichowaua wazazi wao, niliwajibu kuwa ni maradhi. Nilitaka iwe siri lakini sasa Musa huyu ameandika insha ya ushindi. Sitaki Iwe Siri. Hii ni hatua muhimu katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI... (Sitaki Iwe Siri, uk.66).*

Nyanya Mwalonga anakiri kuwa aliwaficha wajukuu wake siri ya ugonjwa ambao uliwaua wazazi wake. Anakiri kwamba alitaka ugonjwa uliowaua Matano na mke wake ubakie siri. Msanii anasema, *“Ni sadfa kwamba siri niliyoighubika kwa miaka mingi ili wajukuu zangu wasiijue imefichuliwa. Wajukuu wangu hawa ni mayatima. Wazazi wao walifariki kutokana na maradhi ya UKIMWI, nao wakabaki mikononi mwangu. Waliponiuliza kilichowaua wazazi wao, niliwajibu kuwa ni maradhi. Nilitaka iwe siri lakini sasa Musa huyu ameandika insha ya ushindi. Sitaki Iwe Siri. Hii ni hatua muhimu katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI...”*

Mwandishi anatueleza kutokana na dondoo lililonukuliwa kwamba njia nyingine ya kukabiliana na maradhi ya UKIMWI ni kuwa wazi kuyazungumzia.

Jamii inapokuwa na uwazi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, itaelewa zaidi na hivyo itachukua hatua za tahadhari kuuepuka. Lakini mtazamo wa wanajamii kama wa nyanya Mwalonga wa kuuficha na kutouzungumzia ugonjwa huu inauendeleza ugonjwa wa UKIMWI badala ya kuuzuia. Hii inatokana na sababu kwamba watu wasipouzungumzia na kuelewa zaidi ugonjwa huu, watazidi kuathiriwa nao. Hivyo basi mwandishi wa riwaya ya *Sitaki Iwe Siri* anasisitiza kuwa njia bora ya kupambana

na ugonjwa wa UKIMWI ni kwa kuufanyia utafiti sawa na alivyofanya Musa na kuuweka wazi na kuuzungumzia kwa uhuru badala ya kuufanya uwe siri.

Baadhi ya wanajamii waliamini kuwa ugonjwa wa UKIMWI ulitokana na uchawi na kwamba kuna waganga ambao wanautibu. Watu kama hawa wanakosa kuwa wazi na kusema ukweli kuhusu chanzo cha ugonjwa wa UKIMWI. Licha ya baadhi ya wanajamii kuamini kuwa ugonjwa wa UKIMWI ulitokana na uchawi, wengine hawakutaka utajwe wala kuelezwa hadharani hata kama ulisababisha kifo fulani.

Mwandishi anatueleza:

**166. *Jirani: mimi naonelea kungefanyika jitihada niwapelekeni kwa fundi mmoja aitwaye Chongo. Huyo bwana hashindwi kitu. Mtu anawarudisha msikule nyumbani atashindwa nini tena? (Kilio Chetu, uk.35-36)***

Baadhi ya wanajamii kama vile Jirani waliamini kuwa kulikuwa na watu katika jamii ambao hawangeshindwa na ugonjwa wa UKIMWI. Msanii anasema, “*niwapelekeni kwa fundi mmoja aitwaye Chongo. Huyo bwana hashindwi kitu. Mtu anawarudisha msikule nyumbani atashindwa nini tena?*” Imani ya watu kama hawa ilikuwa hatari sana kwenye vita dhidi ya UKIMWI. Kupitia kwa mhusika Mjomba, mwandishi anapinga wazo la kupeleka mtoto kwa mganga. Katika tamthilia, msanii anatuonyesha namna ambavyo waganga walivyokuwa wakiwatapeli watu kwa kisingizio cha kuwaponya. Lengo la waganga lilikuwa kuwatapeli na kuwafilisisha wateja wao kwa manufaa yao binafsi. Juhudi za waganga hazikufua dafu kwa vile wagonjwa waliendelea kufariki tu. Waganga ni kati ya wanajamii ambao hawakutaka ukweli usemwe kuhusu ugonjwa wa UKIMWI kwa manufaa ya kibinafsi. Msanii anatueleza kuwa njia salama ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI ni kuwa wazi na kuuzungumzia hadharani.



Kwa ujumla, mwandishi anapendekeza kwamba wanajamii wakubali kwamba ugonjwa wa UKIMWI upo na bado tiba yake haijapatikana. Katika tamthilia ya **Giza**, mwandishi anatueleza kwamba njia bora ya kupambana na maradhi ya UKIMWI ni kuwa wazi na kutoficha chochote kinachofungamana na maradhi haya. Mwandishi anasema:

**167.** Msimulizi: *Mmeyasikia hayo? Mmesikia! Haya UKIMWI ni kwa maskini. Wakubwa, viongozi hawaugui UKIMWI ila shinikizo la damu, Kansa na kufa ghafla. Jamii hii inakwenda wapi? Nani atasema Wazi ana UKIMWI ili jamii ione na ijifunze, tutazaa watoto Wenye UKIMWI mpaka lini? (Giza, uk.22)*

Kupitia dondoo lililonukuliwa, mwandishi anatuonyesha namna ambavyo jamii bado inauficha ukweli kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Mtunzi anasema, “*Mmesikia! Haya UKIMWI ni kwa maskini. Wakubwa, viongozi hawaugui UKIMWI ila shinikizo la damu, Kansa na kufa ghafla. Jamii hii inakwenda wapi? Nani atasema Wazi ana UKIMWI ili jamii ione na ijifunze, tutazaa watoto Wenye UKIMWI mpaka lini?*” Katika jamii inayorejelewa, ni watu maskini ambao husemekana wamekufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Watu mashuhuri na hasa viongozi wanapofariki kutokana na UKIMWI, jamii haiko tayari kukubali kuwa wamekufa kutokana na UKIMWI. Jamii zao hutangazia waombolezaji kwamba marehemu amefariki kutokana na magonjwa mengine kama vile shinikizo la damu, malaria au ugonjwa wa moyo lakini si UKIMWI. Matendo kama haya yanaficha ukweli kuhusu UKIMWI na hivyo kuufanya uendeleo kuangamiza maisha ya watu katika jamii. Mwandishi ana msimamo kuwa njia bora ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni kuwa jasiri na kutangaza hadharani kwamba fulani amefariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Uwazi huu unaweza kuchangia pakubwa katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI.

Mwandishi wa tamthilia ya **Orodha** anapendekeza wanajamii wawe wazi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Anasema kuwa iwapo mtu amefariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI, jamii iwe tayari kutangaza hivyo bila kuficha na kuyasingizia magonjwa mengine kuwa chanzo cha kifo. Katika tamthilia ya *Orodha*, mwandishi amemtumia mhusika Mama Furaha kuendeleza ujumbe huu. Anatumia:

**168.** *Mama Furaha: Na katika jina la Mungu, ukweli ni lazima usemwe! Yeye si wa kwanza wala hatakuwa wa mwisho iwapo hatutaukubali ukweli! Marafiki zangu, ndugu zangu wanakijiji... lazima tukumbuke kwamba Furaha aliteseka kutokana na virusi hivi vya kutisha, kama vile ambavyo ni lazima tukumbuke zile siku ambazo laana ilimpata, wakati alipokuwa anang'ara amejawa na ucheshi... na uhai (Orodha, uk.3).*

Katika tamthilia ya **Orodha**, mwandishi anatumia upinzani uliotoka kwa wanajamii wakati ambapo Mama Furaha alipotaka kusema ukweli kuhusiana na kifo cha mtoto wake. Msanii anasema, “*Na katika jina la Mungu, ukweli ni lazima usemwe! Yeye si wa kwanza wala hatakuwa wa mwisho iwapo hatutaukubali ukweli! Marafiki zangu, ndugu zangu wanakijiji... lazima tukumbuke kwamba Furaha aliteseka kutokana na virusi hivi vya kutisha...*” Mama Furaha hakutaka kuficha chochote kuhusiana na kifo cha bintiye. Alitangaza hadharani kuwa alikufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI jambo ambalo halikupokelewa vyema na baadhi ya wanajamii. Katika wasia wake, Furaha aliandika orodha ya mambo ambayo alitaka yasomwe kuhusiana na kifo chake wakati wa mazishi yake. Wanaume wote ambao walikuwa na uhusiano wa kimapenzi naye walikuwa na hofu kuu sana kuhusu jambo hilo. Wale waliohusika walikuwa pamoja na; Kitunda, Ecko, Salim na Padri James. Wahusika hawa walikosa amani na wakatumia kila mbinu kuhakikisha kuwa wanavuruga mpango huo.

Inasikitisha kuwa hata Padri James hakutaka ukweli usemwe kuhusu kifo cha Furaha kwa maana alijua kuwa pia aliohusika katika kufanya uzinzi naye. Katika siku ya

mazishi, Mama Furaha alijaribu akasoma ile orodha na kutangaza wazi kuwa mwanawe alikufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Ukweli ukisemwa, jamii itatambua namna ugonjwa wa UKIMWI unavyoangamiza watu na hivyo kuchukua tahadhari kuepukana nao. Ukweli ukisemwa, jamii itapata changamoto na kuchukua tahadhari kuepukana na mienendo inayoweza kuhatarisha afya na maisha ya watu. Pamoja na uwazi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, uaminifu katika maisha ya ndoa ni muhimu kwenye vita dhidi ya UKIMWI. Uaminifu katika maisha ya ndoa ndio umejadiliwa katika sehemu inayofuata kama njia mbadala ya kupambana na UKIMWI.

#### **6.3.4 Uaminifu katika maisha ya ndoa**

Wasanii mbalimbali wanatueleza kwamba njia nyingine ambayo inaweza kutumika kuyafanya maradhi ya UKIMWI kudhibitika ni wanajamii kuwa waaminifu katika maisha ya ndoa. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, wahasika Ngoma na Msafiri wanawaambukiza wake zao UKIMWI kwa kuwa hawakuwa waaminifu katika maisha yao ya ndoa. Ngoma alikuwa mume wa Tabu lakini alikuwa akifanya mapenzi na Queen aliyekuwa mwanamke mzinifu. Ngoma alipata maradhi ya UKIMWI na kumwambukiza mkewe Tabu. Ngoma aidha alifanya mapenzi na Asha na kumfanya Msafiri aliyekuwa mpenzi wa Asha kuambukizwa. Omolo alijua haya na alipokuwa kule *Malaika Bar*, aliwaona Ngoma na Asha wakizozana. Msimulizi anauliza:

**169.** *Ngoma na Asha walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Pia, Omolo alikwishawahi kumfumania Ngoma nyumbani kwa Queen. Alikuwa anaijua tabia ya uzinzi ya jirani yake. Ikiwa Queen alikuwa mgonjwa, bila shaka amemwambukiza Ngoma kama hawakutumia mipira. Je, mzozo ule unahusiana na yale aliyoyakuta Queen siku ile? (Ua la Faraja, uk.71)*

Katika dondoo lililo hapo juu, inabainika kuwa Ngoma na Asha walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Vilevile Ngoma na Asha walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Hii ina

maana kuwa mhusika Ngoma alikuwa katika uhusiano wa kimapenzi na wanawake wengi sana. Msanii anatumia, “*Ngoma na Asha walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Pia, Omolo alikwishawahi kumfumana Ngoma nyumbani kwa Queen. Alikuwa anaijua tabia ya uzinzi ya jirani yake. Ikiwa Queen alikuwa mgonjwa, bila shaka amemwambukiza Ngoma kama hawakutumia mipira. Je, mzozo ule unahusiana na yale aliyoyakuta Queen siku ile?*” Katika muktadha huu, msanii anatumia kwamba Queen alikuwa anaugua ugonjwa wa UKIMWI. Ikiwa Queen alikuwa anaugua ugonjwa wa UKIMWI, bila shaka alimwambukiza Ngoma na wakati huo huo iwapo Ngoma alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Asha, bila shaka alimwambukiza. Kwa upande mwingine, Asha naye alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Msafiri na hivyo basi kumuambukiza. Ni wazi kwamba ingawa Ngoma alikuwa ameo hakuwa mwaminifu na ndiyo sababu ilimfanya kumwambukiza mke wake UKIMWI. Alifanya mapenzi na Queen na Asha bila kutumia mipira.

Mwandishi wa riwaya hii anasawiri mhusika mwingine aliyekosa uaminifu katika maisha yake ya ndoa. Msafiri alikuwa ameo lakini pia alikosa uaminifu katika maisha yake ya ndoa. Msafiri alikuwa akiendesha magari ya masafa marefu na wakati mwingi hakuwa anaishi na mkewe. Sababu hii ilimfanya ajiingize katika uhusiano wa kimapenzi na wanawake nje ya ndoa. Msafiri alikuwa rafikiye Asha na kwa kuwa alikuwa akija baada ya muda, hangejua Asha alikuwa asherati. Asha alikuwa ameyapata maradhi ya UKIMWI kutoka kwa Ngoma. Msafiri anayapata maradhi haya kutoka kwa Asha na kwa vile alikuwa na mke, akamwambukiza kutokana na ukosefu wake wa uaminifu. Msafiri angeyapuka maradhi ya UKIMWI iwapo angekuwa mwaminifu katika maisha yake ya ndoa.

Katika riwaya ya **Pendo Katika Shari**, mwandishi anamchora mhusika Sulubu kama mfano wa watu katika jamii ambao walikosa kabisa uaminifu katika maisha yao ya ndoa. Sulubu alikosa uaminifu ambao ulisababisha akapata maradhi ya UKIMWI. Licha ya kutahadharishwa na marafikize, Sulubu aliwapuuza na kuendelea tu na tabia yake ya uzinzi ambayo hatimaye ilimletea madhara. Mwandishi anatueleza:

**170.** *Sulubu mimi nakujua vizuri sana. Wewe una wapenzi chungu nzima, na Wengine huwajui hata majina yao. Kwa hivyo, huwezi kujua ni yupi atakayekuambukiza maradhi baadaye. Leo una Amina, kesho una Cheupe, kesho kutwa kwa Rosa. Huoni unajitia kitanzi? Unajua UKIMWI umewaua maelfu ulimwenguni lakini unafikiri wewe huwezi kuwa mmoja wa hao maelfu (Pendo Katika Shari, uk.30).*

Sulubu alikuwa na wapenzi wengi hata wengine ambao hakuwajua kwa majina. Sulubu alikuwa anawabadilisha wanawake kama nguo. Mwandishi antueleza, “*Sulubu mimi nakujua vizuri sana. Wewe una wapenzi chungu nzima, na Wengine huwajui hata majina yao. Kwa hivyo, huwezi kujua ni yupi atakayekuambukiza maradhi baadaye. Leo una Amina, kesho una Cheupe, kesho kutwa kwa Rosa. Huoni unajitia kitanzi? Unajua UKIMWI umewaua maelfu ulimwenguni lakini unafikiri wewe huwezi kuwa mmoja wa hao maelfu.*” Sulubu alitahadharishwa na rafikiye kuhusu hatari ya tabia yake ya uzinzi lakini hakusikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Matendo haya ya Sulubu yalisababisha akaambukizwa maradhi ya UKIMWI. Sulubu hatimaye alimwambukiza mkewe Pendo na Rehema ambao waliaga dunia kutokana na athari ya ugonjwa wa UKIMWI.

Hivyo basi mwandishi wa riwaya ya **Pendo katika Shari** anatufahamisha kwamba iwapo Sulubu angalikuwa mwaminifu katika ndoa yake, hangaliwaambukiza wake zake na mtoto ambao walifariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Hivyo basi njia nyingine ambayo jamii inaweza kuizingatia kwenye vita dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI ni kudumisha uaminifu katika maisha ya ndoa.

Mhusika Fumbwe katika riwaya ya **Kala Tufaha** anapata ugonjwa wa UKIMWI kutokana na ukosefu wake wa uaminifu katika ndoa. Ndoa ya Fumbwe haikuwa na uaminifu kwa vile mkewe Hatima pia alikosa uaminifu katika maisha yake ya ndoa. Jamii ya Fumbwe ilikuwa na shida kubwa kwa maana mke na mume walikosa kuishi maisha ya uaminifu. Msanii anatueleza:

**171.** *Siku zote huzuni imemtawala Fumbwe asione raha ya kuishi. Mke aliyemtwaakiwa hana chochote akamshughulikia kimasomo hadi yake kupata stashahada ya elimu-jamii. **Malipo yake kumla kivuli tena nyumbani kwake. Ndiyo na yeye alikuwamo na jicho la nje. Lakini mengi aliyafanyia nje. Pengine mara moja tu aliwahi kujisahau akayafanya nyumbani (Kala Tufaha, uk.126).***

Inaonekana wazi kwamba ndoa kati ya Hatima na Fumbwe inavunjika kwa sababu wote hawakuwa waaminifu. Mwandishi anasema, “**Malipo yake kumla kivuli tena nyumbani kwake. Ndiyo na yeye alikuwamo na jicho la nje.**” Fumbwe alimbaka Kibibi na kumpachika mimba Hatima anapokwenda kuzuru wazazi wake kule kijijini. Kibibi alikuwa ameenda kwa Fumbwe kusaidia kufanya kazi ya uyaya. Fumbwe kwa upande wake alimfumania Hatima akiwa na Chongea alipomhadaa Hatima kuwa ameenda kuwazuru wazee wake kijijini. Tukio hili lilimfanya Fumbwe kuachana na Hatima na kuanza kujiingiza katika ulevi na uasherati uliochangia hatimaye kuambukizwa maradhi ya UKIMWI. Ukosefu wa uaminifu katika ndoa ni hali hatari kwa maana linaweza kuivunja ndoa kwa haraka. Aidha, tendo hilo linaweza kusababisha maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa.

Katika hadithi ya **Likizo ya Mauti**, msanii anayasawiri maisha ya Mzee Gogo ambaye pia alikuwa ameo akiwa familia. Mzee Gogo alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na msichana mdogo aliyejulikana kama Ulimbo. Mzee huyu alimchukua msichana Ulimbo na akampeleka likizo nje ya nchi. Mzee Gogo aligharamika sana ili kuhakikisha kuwa kipenzi chake kinafurahia likizo ya mbali. Mzee Gogo alijihusisha

katika uhusiano wa kimapenzi na msichana ambaye umri wake haukuwa halali. Mzee Gogo alighafilika asikumbuke kuwa ziraili jipya lililozuka kivyake likawashinda hata vigogo wa sayansi na maarifa lilikuwa tayari mawindoni kila mahali na kila wakati. Ziraili hilo lilimnasa Mzee Gogo kwa sababu baada ya starehe zake zote na kipenzi chake, alianza kujuta kwa kupuuzwa ushauri aliokuwa amepata. Aliupata ugonjwa wa UKIMWI ulioanza kumla na hivyo kuiletea jamaa yake madhara makubwa na aibu kuu.

Waandishi wa kazi hizi teule wanaangazia ndoa hizi kwa lengo la kuwaonya wanajamii dhidi ya tabia ya uasherati. Katika kufanya hivyo, wanahimiza uaminifu katika ndoa kama njia ya kuepuka kuambukizwa maradhi ya UKIMWI kwenye ndoa. Katika kuyashadidia maoni haya, wanaharakati wote wanaoshughulika katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI wanasisitiza kuhusu uaminifu katika ndoa. Wazo hili limeungwa mkono na asasi za kidini ambazo zinasisitiza uaminifu katika ndoa kama njia bora ya kudhibiti kuenea kwa maradhi ya UKIMWI.

Kwa mintarafu ya hayo, Baba Mtakatifu wa kanisa Katoliki aliorodhesha njia za kudhibiti kuenea kwa maradhi haya. Kulingana na Baba Mtakatifu, njia hizo ni kama vile: kutozini, kuwa waaminifu katika ndoa na kukabiliana na umaskini (BBC, 2005). Licha ya kuwa waaminifu katika maisha ya ndoa, vita dhidi ya UKIMWI vinaweza kufaulu iwapo jamii itapinga ubabadume au taasubi za kiume. Njia hii imejadiliwa katika sehemu ifuatayo.

### **6.3.5 Kupinga taasubi za kiume**

Taasubi za kiume ni hali ambapo wanaume wanajiona bora kuliko wanawake na kuwachukua kama viumbe duni wasio na usemi wowote kuhusiana na maamuzi

muhimu ya familia. Aidha ni tabia ya wanaume kuwadhalilisha wanawake na kuwaona kama wasio na umuhimu mkubwa katika ustawi na maendeleo katika jamii.

Waandishi katika maandishi teule wanakashifu taasubi za kiume kama njia inayayofanya maradhi ya UKIMWI kuenea. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, Ngoma anamdunisha mke wake kiasi cha kumwambukiza maradhi haya. Ngoma alikuwa tajiri kutokana na biashara yake lakini hakuutumia utajiri huo kwa manufaa ya jamaa yake. Zamani alipopata pesa alidhani furaha ya maisha iko kwenye anasa hata kama anamkirihi mke wake. Ngoma alipata pesa nyingi kutokana na biashara yake lakini alizitumia tu kwenye anasa. Alikunywa pombe na wanawake kama vile Queen na Asha na aghalabu alifika kwake usiku wa manane bila kumwogopa mkewe Tabu. Utajiri huu ulimpa Ngoma kiburi akamdharau mkewe kwa kuwa hakuwa na mapato yakilinganishwa na aliyoyapata Ngoma katika biashara yake. Ngoma alijistarehesha na wanawake na marafiki zake Mpemba na Zito na hivyo kuipuuza familia yake.

Taasubi za kiume zilimfanya Ngoma kumdharau mke wake kiasi cha kufanya mapenzi na wanawake na kurudi nyumbani akiwa amelewa na kunukia marashi ya wanawake wengine. Tabia ya Ngoma ya kufanya mapenzi na wanawake wengi nje ya ndoa ilimfanya Ngoma akapata ugonjwa wa UKIMWI aliosambazia mke wake. Katika kufanya maamuzi kuhusu jamii yao, tunaona Ngoma ndiye aliyehusika. Kwa mfano, Ngoma ndiye aliyefanya Tabu kuacha dini yake ya Kikristo na kujiunga na Uislamu. Aidha, katika kufanya mapenzi, yeye ndiye anayeamua kutumia mipira. Hii inajidhihirisha pale Ngoma anapomlaghai Tabu kuwa watu, hata wanandoa hutumia mipira. Ngoma anayafanya haya yote wakati alipokuwa amesikia fununu kuwa Queen alikuwa anagua ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi anaeleza:



**172.** *Kesho yake pia Ngoma alirudi nyumbani mapema, ila alikuwa amelewa sana. Tabu alikataa kunywa pombe ile. Baada ya chakula cha jioni walipokwenda kulala Ngoma alimpa mke wake pakiti mbili za mipira ya kiume akamwambia, 'Ma` Juma, siku hizi magonjwa ni mengi. Hujui sisi wanaume tunakopita. Mimi naona tunapotaka kukutana tutumie hii mipira (Ua la Faraja, uk.138).*

Bila mashauriano yoyote msanii anatueleza kuwa Ngoma alimpa mke wake pakiti mbili za mipira ya kiume akamwambia atumie. Msanii antueleza, “*Baada ya chakula cha jioni walipokwenda kulala Ngoma alimpa mke wake pakiti mbili za mipira ya kiume akamwambia, 'Ma` Juma, siku hizi magonjwa ni mengi. Hujui sisi wanaume tunakopita. Mimi naona tunapotaka kukutana tutumie hii mipira.*” Ngoma alidai kuwa magonjwa yalikuwa mengi na hivyo palikuwa na haja wao kuitumia mipira ya kiume. Kauli kama hizi ambazo zilikuwa nzito zilitoka tu kama amri bila mjadala wala maelewano yoyote. Ngoma alifanya uamuzi huu akiwa amechelewa kwa vile tayari alikuwa ameshaambukiza mkewe ugonjwa wa UKIMWI. Ingawa Tabu alijua mume wake hakuwa mwaminifu, hangemwambia atumie mipira kwa sababu mume wake hangekubali. Aidha, katika riwaya, Ngoma alikataa kukidhi mahitaji ya jamii na kujihusisha kwa mapenzi na wanawake nje ya ndoa bila kujali. Alikuwa akifika nyumbani akinuka marashi ya wanawake. Tabia hii ilimpa kiburi akafanya mambo jinsi apendavyo. Mtunzi anashauri kuwa vita dhidi ya UKIMWI vitafaulu iwapo tutapinga tabia hii mbaya ya taasubi za kiume.

Katika riwaya ya **Pendo katika Shari**, mwandishi anamchora mhusika Sulubu akiendeleza taasubi ya kiume. Sulubu aliamini kuwa UKIMWI ni ugonjwa wa wanawake na yeye kamwe hangeweza kuwa na ugonjwa huo. Hali hii ilimfanya hata kukataa kupimwa ili kuijua hali yake. Mwandishi anasema:

**173.** *Kwa nini ulikataa kupimwa na daktari? Matano alimuuliza Sulubu baada ya kimya kirefu. Nani, mimi? Unadhani mimi naweza kuwa na magonjwa ya wanawake? Sulubu alimuuliza kwa ufidhuli ule ule.*

*Sikiliza mwenzangu. UKIMWI si ugonjwa wa wanawake peke yao... Si unambazwa na wanawake tu, alitamka Sulubu. Wajua baadhi ya wanaume hunishangaza. Watazurura huko na baada ya kupatwa na magonjwa ya zinaa, wanawalaumu wanawake, hata wake zao. Kwani magonjwa hayo huishi na wanawake pekee? (Pendo katika Shari, uk.29)*

Sulubu aliamini kuwa UKIMWI ni ugonjwa wa wanawake na hivyo hakuona sababu ya kupimwa ili kuthibitisha iwapo alikuwa na virusi vya UKIMWI au la. Sulubu alisisitiza kuwa haingewezekana kupatwa na ugonjwa wa UKIMWI kwani aliamini kuwa wanawake tu ndio wanaoambukizwa magonjwa kama hayo. Mwandishi anatueleza, *“Kwa nini ulikataa kupimwa na daktari? Matano alimuuliza Sulubu baada ya kimya kirefu. Nani, mimi? Unadhani mimi naweza kuwa na magonjwa ya wanawake?”* Mtazamo kama wa Sulubu ni wa kusikitisha kwa maana hakuna magonjwa ambayo yaweza kuwa ya jinsia moja tu. Wanaume wengi waliofungwa na minyororo ya utamaduni waliamini kuwa chochote kibaya katika jamii kilitokana na wanawake. Wanaume wengine huwa wanatembea kwa njia mbaya na wanapopata magonjwa, huwa wanawalaumu wanawake kuwa chanzo cha magonjwa hayo. Tabia hii ya ubabadume ndiyo inayochangia kuendeleza ugonjwa wa UKIMWI katika jamii ambapo wanaume hujiona kuwa na uhuru wa kufanya lolote, kwa mfano kufanya uzinifu nje ya ndoa.

Kwenye riwaya ya **Kala Tufaha**, ubabadume wa mhusika Fumbwe unamfanya kujihusisha na tabia ya uasherati inayosababisha apate maradhi ya UKIMWI. Alihusika katika kumbaka Kibibi aliyekuwa yaya wao na aidha alikuwa akijihusisha na vitendo vya uzinifu na wasichana wadogo kwenye afisi yake kazini. Fumbwe anafurahia baada ya kumfumanika mke wake kwa vile waliachana hatimaye. Aliona kuwa sasa alikuwa amepata uhuru wa kufanya anasa lakini tabia yake ya uzinifu ilimletea maradhi ya UKIMWI.

Onyango (2007) anaunga mkono wazo kuwa taasubi ya kiume ni kikwazo kikubwa katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI. Anashikilia kwa nguvu na itikadi za jamii zinaelekea kuwapendelea wanaume na katika hali hii wanawake ndio wanaoathirika kuhusiana na maambukizi ya UKIMWI. Hii inatokana na misingi ambayo inawapendelea wanaume na kuwadhalilisha wanawake. Waandishi wa kazi teule za riwaya waelekea kuukashifu ubabadume kama njia inayochangia kuenea kwa maradhi ya UKIMWI. Tabia hii ikikomeshwa, itachangia pakubwa katika kupunguza maambukizi ya UKIMWI miongoni mwa wanawake katika jamii. Licha ya vita dhidi ya taasubi za kiume, unyanyapaa hauna budi kupigwa vita iwapo tunatarajia kushinda vita dhidi ya UKIMWI. Sehemu ifuatayo inajadili namna vita dhidi ya unyanyapaa vyaweza kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI.

### **6.3.6 Kupinga unyanyapaa**

Mwandishi wa riwaya ya **Ua la Faraja** anaangazia vita dhidi ya unyanyapaa kama njia nyingine ya kukabiliana na maradhi ya UKIMWI. Uvumbuzi wa maradhi ya UKIMWI uliititiza jamii kabla ya kudhibitiwa na kueleweka kama maradhi yanayofanya mwili kupunguza kinga ya maradhi. Katika nyakati za mwanzo kulikuwa na semi tofauti zilizotumika zikayafanya maradhi haya yatishe. Baadhi ya watu waliuita uchawi, kifo, laana, ugonjwa mpya usio na tiba na kadhalika. Utambuzi wa ugonjwa wa UKIMWI kwa matumizi ya msamiati uliotajwa ulifanya walioathirika kuhisi kunyanyapaishwa. Baada ya utafiti wa kina kufanywa, wanajamii walipata ufahamu wa kutosha kuhusu ugonjwa wa UKIMWI.

Baada ya kipindi fulani, jamii ikaanza kuwa na mwitiko chanya kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Usemi uliokuwa ukitumiwa awali ukaanza kubadilika polepole. Wanajamii hawa wakaanza kuyatania majina kwa kuita ugonjwa huu majina kama vile; Mdudu,

mwiba, kudura na kwa kufanya hivyo wanajamii wakaanza kuwa na mwitiko chanya kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Wanajamii walipoanza kuutania ugonjwa wa UKIMWI ina maana kuwa walikuwa wameukubali na hivyo kuchukua hatua za tahadhari kukabiliana nao bila woga mwingi.

Njia nyingine ambayo inaweza kutumika kupambana na ugonjwa wa UKIMWI ni kwa kuonyesha upendo kwa walioathirika. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, mhusika Tabu alipogundua kuwa ameambukizwa maradhi ya UKIMWI alilia sana. Mhusika huyu alisononeka ikifahamika kuwa yeye alikuwa mwaminifu katika ndoa lakini ni mumewe Ngoma ambaye alikuwa amemuambukiza ugonjwa huo. Mwandishi anatueleza:

**174.** *Naye Tabu alifarjika sana. Wakati mwingine matani ya Abu kwa Asha yalimfanya asahau matatizo yake, akatabasamu au kuchangia utani. Hivyo, polepole bila kujua, watoto walifanikiwa kumrudisha mama yao katika hali ya kawaida. Grace pia alichangia kwa kumpa moyo dadake asiwe na shaka, abaki na imani na asubiri kwa kupima iwapo alikuwa ameambukizwa (Ua la Faraja, uk.113).*

Kutokana na dondoo lililonukuliwa hapo juu, ni bayana kwamba upendo wa familia ya Tabu unafaulu kumrudisha Tabu katika hali yake ya kawaida na kumfanya asahau kuwa ameambukizwa. Msanii anatueleza kwamba, “*Wakati mwingine matani ya Abu kwa Asha yalimfanya asahau matatizo yake, akatabasamu au kuchangia utani. Hivyo, polepole bila kujua, watoto walifanikiwa kumrudisha mama yao katika hali ya kawaida. Grace pia alichangia kwa kumpa moyo dadake asiwe na shaka, abaki na imani na asubiri kwa kupima iwapo alikuwa ameambukizwa.*” Mwandishi anasisitiza kuwa ni bora kuwaonyesha upendo walioathirika. Mtazamo hasi wa chuki na utengano unaodhihirishwa na wahusika Ngoma katika riwaya ya *Ua la Faraja*, Fumbwe katika *Kala Tufaha* na Sulubu katika *Pendo Katika Shari* unawafanya wahusika walioathirika kufa haraka sana kutokana na upweke. Wasanii wa kazi teule

za riwaya wanakashifu chuki dhidi ya waliougua na kuhimiza upendo pamoja na kuwafurahia waathiriwa kama njia ya kupiga vita unyanyapaa.

Kupitia kwa riwaya teule, waandishi wanapendekeza kuwa kupiga vita unyanyapaa ni kutoa huduma kwa wanaougua. Daktari Hans katika riwaya ya *Ua la Faraja* anaonyesha Tabu upendo na kumpa tumaini la kukabiliana na maradhi ya UKIMWI. Mwandishi anasema, Dkt. Hans amempa Tabu matumaini kuwa hata akipima na kupata kuwa ana virusi vya UKIMWI, anaweza kuyarefusha maisha yake. Daktari anamueleza Tabu kuwa akiutunza mwili wake vizuri, anaweza kuishi zaidi hata ingawa ana virusi vya UKIMWI. Anasema kuwa mwathiriwa akifuata masharti ya daktari kama vile maelekezo kuhusu lishe bora, matibabu ya maradhi ya kawaida na kutumia dawa za kupunguza kasi ya kuongezeka kwa virusi, anaweza kuishi maisha marefu tu kama mtu yeyote yule.

Licha ya kumpa Tabu matumaini, Tabu alipopimwa na kupatikana ana virusi, Dkt. Hans anamwonyesha upendo. Licha ya Dkt. Hans, jamii ya Tabu ilimwonyesha upendo kwa kumpatia matumaini ya kuishi. Msanii anasisitiza kuwa mwathiriwa wa UKIMWI akionyeshwa upendo na kupewa matumaini, anaweza pia kuishi maisha marefu. Mwandishi anasema:

**175. *Umenionyesha upendo, asante. Hata nikiugua nitakumbuka yote uliyosema na wewe nitakukumbuka. Hutangulia mbali, tutakula pamoja. Nitakuorodhesha katika wagonjwa wangu. Nitakuuguza, tutaugua sote, mimi na wewe...Tabu akamtazama tena. Akatabasamu na machozi yakaanza tena kutoka Hans akayafuta. Sasa usilie tena. Jiandae kuishi na virusi, ukiwalea watoto wako mpaka hapo tutakapo fika mwisho (Ua la Faraja, uk.194).***

Daktari Hans ameonyesha upendo kwa Tabu. Mtunzi anasema, “*Umenionyesha upendo, asante. Hata nikiugua nitakumbuka yote uliyosema na wewe nitakukumbuka.*” Dkt. Hans anamueleza Tabu kuwa atamuorodhesha kama mgonjwa

wake na kwamba wataugua wote. Tabu alipotoa machozi, Dkt. Hans alikuwa tayari kumpanguza. Anamueleza mgonjwa wake ajiandae kuishi na virusi akiwalea watoto wake mpaka pale Mungu atamfikisha. Tabu alihisi kufarijika kwa maana aliona mtu ambaye alihisi yale aliyopitia. Dkt. Hans alimpa matumaini Tabu kwa kumwonyesha upendo mkuu. Kitendo hiki kilimfanya Tabu kuhisi kupendwa na hivyo kupata matumaini ya kuishi maisha marefu.

Katika jamii zetu, kuna watu ambao wana mtazamo hasi kwa waathiriwa wa ugonjwa wa UKIMWI. Wao huwatenga na kuwabagua wagonjwa wa UKIMWI na matendo kama haya huwaathiri wagonjwa kwa njia hasi. Wagonjwa kama hawa huhisi kuchukiwa na huathirika kisaikolojia kiasi cha kuwafanya wasiishi maisha marefu. Tabia kama hii huendeleza unyanyapaa lakini mtunzi anapendekeza tuupinge unyanyapaa ndipo tuwape wagonjwa muda wa kuishi zaidi. Msanii anapendekeza upendo kama wa Dkt. Hans kama njia ambayo pia inaweza kutumika katika kupambana na virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Licha ya upendo katika vituo vya afya na matibabu, jamii kule nyumbani zinapaswa kuwa katika mstari wa mbele katika kuonyesha upendo kwa maana hapo ndipo mwathirika hukaa kwa muda mrefu.

Katika riwaya ya **Kala Tufaha**, mhusika Fumbwe alipolazwa hospitalini, daktari Kala alimhudumia vyema kwa kumwonyesha upendo na kumjali sana. Fumbwe alihisi kupendwa na kufarijika mpaka akaufungua moyo wake kwa Dkt. Kala. Ni sadfa kuwa Kala alikuwa amekutana na babake na kumhudumia pasipo kujua kuwa yeye ndiye babake. Mtunzi anatueleza:

**176.** *Maskini Fumbwe! Ndwele zimemtoa nyumbani akaja piga kambi hospitalini. Mafao yake ya kustaafu yote huenda kwa matibabu. Bahati yake kukumbana na daktari kijana mchangamfu, daktari Kala Tufaha. Kijana mzuri sana huyu, Mungu amweke, husema Fumbwe. Hatuna nasaba naye na muone jinsi anavyonishughulikia, wala si mtu wa kitu kidogo. Daktari Kala Tufaha hakosi kila siku kumpitia*

*mgonjwa wake kumjulia hali. Awe kazini asiwe kazini atapata wasaa wa kumpitia Fumbwe. Ikitokea asafiri, huwapigia wenziwe simu hapo hospitalini kujulia hali ya mgonjwa wake (Kala Tufaha, uk.170).*

Fumbwe alipolazwa hospitalini baada ya kulemewa na ugonjwa, alipata huduma ya kipekee kutoka kwa daktari Kala. Kala hakukosa hata siku moja kumpitia mgonjwa wake na kumjulia hali. Alijaribu sana kila siku, awe kazini au akose kuwa kazini kupata wasaa wa kumpitia mgonjwa wake na kumjulia hali. Hata akiwa safarini huwapigia wenzake simu ili kumjulia hali mgonjwa wake. Mtunzi anaeleza, “*Bahati yake kukumbana na daktari kijana mchangamfu, daktari Kala Tufaha. Kijana mzuri sana huyu, Mungu amweke, husema Fumbwe. Hatuna nasaba naye na muone jinsi anavyonishughulikia, wala si mtu wa kitu kidogo. Daktari Kala Tufaha hakosi kila siku kumpitia mgonjwa wake kumjulia hali. Awe kazini asiwe kazini atapata wasaa wa kumpitia Fumbwe. Ikitokea asafiri, huwapigia wenziwe simu hapo hospitalini kujulia hali ya mgonjwa wake.*” Mwandishi anatoa wito kwa huduma bora ya kuwajali wagonjwa kutoka kwa madaktari na wauguzi kama njia bora ya kupiga vita unyanyapaa. Tunaonyeshwa namna Fumbwe anavyoshughulikiwa na Dkt. Kala na hivyo mwandishi anawataka madaktari wote waige mfano wa daktari huyu kwa kuwashughulikia wagonjwa huku wakiwaonyesha upendo. Kupitia mbinu hii, unyanyapaa utapigwa vita na tutafaulu katika vita vyetu dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI. Kama njia ya kuonyesha upendo kwa wagonjwa wao, tunaona Dkt. Hans na Dkt. Kala wakijiweka katika tajriba ya wahusika, wanawazia maisha yao, wanaweka fikra na hisia zao pamoja nao na kuanza kuandika sura mpya ya maisha ambayo msuko wake umetibuliwa na maradhi haya.

Tunaona madaktari hawa wakiwapa matumaini na kuwasaidia kukadiria thamani ya maisha, mipango ya maisha, mirathi na vilevile kuwa nao katika upeo huu wa

mgogoro wa nafsi, mwili na akili. Waandishi wa kazi teule zilizotumika katika utafiti huu wanaonyesha kuwa kuna haja ya madaktari kuwauguza waathiriwa bali sio tu kuwapa dawa. Madaktari wanafaa kujiweka katika hali ya waathiriwa na kuwauguza katika upendo na tumaini kama wanavyofanya Dkt. Hans na Dkt. Kala. Hii ni hatua chanya na inaleta matumaini makuu kwenye vita vya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Kwa mwelekeo kama huu, tunaweza kuupiga vita unyanyapaa na kuwawezesha waathiriwa kuwa na maisha marefu.

Katika riwaya ya **Pendo katika Shari**, mwandishi anaonyesha namna jamaa ya Sulubu inavyomwonyesha upendo wakati ambapo alikuwa amelazwa hospitalini. Licha ya madhila ambayo Sulubu alikuwa ameifanyia aila yake, wakati wanapotambua kwamba anaugua ugonjwa wa UKIMWI, wanamshughulikia kwa upendo na kumpa matumaini. Jamii haikutaka kulipiza kisasi lakini badala yake ikaonyesha upendo mkuu kwa Sulubu alipopatikana akiugua maradhi ya UKIMWI.

Msanii anatueleza:

**177. *Baba, tumekuja kukuambia kwamba tunakupenda na tunakujali. Aliponena maneno haya, Sulubu machozi yalianza kuchungulia machoni. Alifyatuka kwa kiganja cha mkono wake, akawatazama wanawe kwa huzuni. Tunajua unaugua UKIMWI, aliongeza Almasi, lakini sisi tunaamini kuwa ukiishi maisha mazuri na ukila vizuri, hutateseka. Maneno ya watoto hao yaliwastajaabisha wale waliokuwa pale. Pendo hakuweza kutamka neno bali alisimama kando ya kitanda huku akitikisa kichwa, ishara ya kukubaliana na yale yaliyotamkwa na wanawe (Pendo katika Shari, uk.59).***

Kwa mshangao wa Sulubu, watoto na mke wake walimpa moyo na kumfariji. Mtunzi anasema, *“Baba, tumekuja kukuambia kwamba tunakupenda na tunakujali. Aliponena maneno haya, Sulubu machozi yalianza kuchungulia machoni. Alifyatuka kwa kiganja cha mkono wake, akawatazama wanawe kwa huzuni. Tunajua unaugua UKIMWI, aliongeza Almasi, lakini sisi tunaamini kuwa ukiishi maisha mazuri na ukila vizuri, hutateseka.”* Watoto walimtembelea Sulubu



hospitalini na wakamueleza kuwa wanampenda. Walimueleza kuwa walifahamu alikuwa anaugua ugonjwa wa UKIMWI lakini walimhakikishia kuwa akiishi maisha mazuri na kula vizuri hatateseka. Sulubu hakutarajia haya akikumbuka mateso ambayo alikuwa ameipatia jamii yake. Mwandishi anatusihi tusahau tofauti zetu na kuwashughulikia wagonjwa vyema na kwa njia hii tutawapa matumaini ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI kwa ujasiri mkuu. Sulubu alihisi upendo wa familia yake licha ya maovu yote aliyokuwa amewafanyia.

Njia nyingine ambayo inaweza kutumika kupambana na ugonjwa wa UKIMWI ni kwa jamii kuukubali ugonjwa huu na kukabiliana nao pasipo kuwatenga waathirika. Ni vyema kuukubali ugonjwa wa UKIMWI bila kuukana. Katika tamthilia ya *Kilio Chetu*, mwandishi anakusudia kuifahamisha jamii isiwatenge watu wanaougua ugonjwa wa UKIMWI. Katika kutolea kauli hii ithibati, mwandishi anasema:

**178. *Mgonjwa asitengwe kwa maana UKIMWI huambukizwi kwa hewa au kuwa pamoja. Mgonjwa apewe chakula bora na yanapojitokeza magonjwa mengine kama Malaria apelekwe hospitali kwa tiba (Kilio Chetu, uk.37).***

Baadhi ya watu katika jamii iliyosawiriwa na mwandishi waliamini kuwa ugonjwa wa UKIMWI unaweza kumpata mtu akitangamana na mwathiriwa wa ugonjwa huo. Sababu hii inawafanya watu wawaepuke na kuwaambaa wagonjwa wa UKIMWI. Kuwaogopa wagonjwa wa UKIMWI ni sawa na kunyanyapaisha na hali kama hii huwavunja moyo waathiriwa na hata kupunguza siku zao za kuishi. Mwandishi anapendekeza kuwa wagonjwa wa UKIMWI wanapotokea, wanapaswa wapewe chakula bora na wapelekwe kwa matibabu na wala si kutorokwa. Mtunzi anapendekeza, “*Mgonjwa asitengwe kwa maana UKIMWI huambukizwi kwa hewa au kuwa pamoja. Mgonjwa apewe chakula bora na yanapojitokeza magonjwa mengine kama Malaria apelekwe hospitali kwa tiba.*” Mwandishi anashauri kuwa

tusiwabague wagonjwa wa UKIMWI kwa kuwa na imani potovu kuhusiana na ugonjwa huu. Aidha, jamii inapaswa kuwashughulikia vyema wagonjwa wa UKIMWI kwa kuwapatia lishe bora, upendo na matibabu. Hali kama hii inaweza kuwafanya wagonjwa kama hawa kuishi maisha marefu.

Mwandishi wa hadithi ya “Tahadhari Bandia” anapendekeza kwamba njia ambayo inaweza kutumika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni kupinga unyanyapaa. Kwa mujibu wa hadithi hii, unyanyapaa unasababisha jamii kuwatenga na kuwadhulumu waathirika wa UKIMWI. Hali hii huwaathiri wagonjwa wengi kisaikolojia na hata kusababisha wengi wao kupoteza maisha yao mapema sana. Asasi mbalimbali za jamii kama vyo vya mafunzo, mashirika ya serikali na yasiyo ya serikali yanapaswa kuwakubali wagonjwa wa UKIMWI kama wagonjwa wengine na kuepuka kuwatenga. Iwapo wagonjwa wa UKIMWI watachukuliwa kama watu wa kawaida pasipo kuwabagua, wataendelea kuishi kwa muda mrefu na kutekeleza majukumu mbalimbali kama raia wengine. Hili litawapa matumaini ya kuendelea kuishi. Licha ya kupinga unyanyapaa, elimu na mafunzo kuhusu UKIMWI ni muhimu katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Sehemu inayofuata inashughulikia elimu na mafunzo kama njia ya kupambana na UKIMWI.

### **6.3.7 Kutoa elimu, mafunzo na kupunguza bei ya dawa za UKIMWI**

Njia nyingine ambayo inaweza kutumika katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni kwa jamii kuhakikisha kwamba vijana wanapata elimu na mafunzo ya kijinsia kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Baadhi ya wazazi hawachukui jukumu la kuwapa watoto wao mafunzo. Baadhi yao husingizia dini na mila kuwa kizuizi kwao. Katika tamthilia ya *Kilio Chetu*, mwandishi anaonyesha athari ya kukosa elimu hii pale anaposema:

**179. *Basi watoto wakaendelea kudhoofika kwa kukosa elimu ya jinsia, Dubwana lile likaendelea kuwadhuru, wakateketea. Vifo vikawazoa... Vikawazoa...vikawazoa (Kilio Chetu, uk.3).***

Katika dondoo lililo hapo juu, mwandishi anaonyesha namna ambavyo vijana wanaangamia kwa kukosa maelezo na ufahamu kuhusu masuala yanayowaelekeza kujiingiza kwa uasherati unaowaletea mauti. Mtunzi anaeleza, “*Basi watoto wakaendelea kudhoofika kwa kukosa elimu ya jinsia, Dubwana lile likaendelea kuwadhuru, wakateketea. Vifo vikawazoa... Vikawazoa...vikawazoa.*” Anasema dubwana ambalo ni ugonjwa wa UKIMWI limeendelea kudhuru na kuangamiza maisha yao. Inabainishwa kuwa vifo vingi sana vimetokea miongoni mwa vijana kwa sababu ya ukosefu wa elimu kuhusu UKIMWI. Mwandishi anapendekeza kwamba njia bora ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni kwa vijana kupewa elimu ya familia, ikiwemo ya jinsia. Watoto wanapaswa kuambiwa wazi kuhusu masuala ya mapenzi, ngono na hatima yake. Elimu inayopendekezwa inalenga kuwaonyesha vijana na watoto madhara ya kufanya ngono kabla ya ndoa.

Mwandishi wa tamthilia ya **Giza** anatueleza kuwa wanaohusika na hasa viongozi serikalini hawajatoa elimu na mafunzo ya kutosha kuhusu UKIMWI. Ni jukumu la viongozi walio mamlakani kuhakikisha kuwa wanayashughulikia maslahi ya raia wao. Katika jamii inayorejelewa inaonekana kwamba viongozi wamezembea kazini badala ya kuwajibika. Mwandishi anasema:

**180. *Nuru: ...madawa na huduma zote zinaishia mijini, vijijini watu hawajapewa elimu juu ya UKIMWI. Wanachojua ni kula pesa na kuimba maredioni na majukwaani juu ya kondomu. Kondomu tu ndio wanaona dawa ya UKIMWI (Giza, uk.18).***

Mtunzi anawakashifu viongozi serikalini kwa kutowajibika kuhusu uhamasishaji wa jamii dhidi ya UKIMWI. Katika tamthilia ya **Giza**, mtunzi analalama kuwa, “**madawa na huduma kuhusu UKIMWI zinaishia katika sehemu za mijini.**”

**Wanachojua ni kula pesa na kuimba maredioni na majukwaani juu ya kondomu”** Serikali imewasahau watu wa sehemu za vijijini kwa kukosa kuwapa madawa na elimu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Vingozi wanaohusika wanasahau kuwa katika sehemu za mashambani kuna watu wengi sana ambao wanakosa elimu na ufahamu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI.

Msanii anawalaumu viongozi kwa kushiriki ufidadi na kutumia vibaya pesa zilizotengwa kupambana na UKIMWI. Wanachofahamu viongozi ni kuimba na kutangaza kila mahali kuhusu kondomu wanayoona kuwa njia bora ya kupambana na UKIMWI. Viongozi wanasahau kuwa hata hiyo kondomu wanayoiimba na kuitangaza, inahitaji elimu ndipo itumiwe kwa njia bora. Mwandishi anatueleza kwamba njia bora ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI ni kutoa elimu na mafunzo ya kutosha kuhusu UKIMWI kwa wakazi wa sehemu za mashambani. Mtunzi anasema kwamba ni muhimu elimu kuhusu UKIMWI iwafikie watu wa matabaka mbalimbali katika jamii. Aidha mafunzo na elimu kuhusu UKIMWI itawafanya watu kutofikiria kwamba UKIMWI ni ugonjwa unaoletwa na urogenitali au ushirikina. Msanii anatueleza kuwa mawazo kama ya mhusika Nuru katika tamthilia ya *Giza* ndiyo yanayoendelea kusambaza ugonjwa wa UKIMWI. Mhusika Nuru na wengine katika jamii wanaamini kuwa ugonjwa wa UKIMWI unasababishwa na urogenitali.

Mawazo kama haya yatawafanya watu kuendelea kujihusisha na visa vya uasherati wakijua kuwa UKIMWI hautokani na urogenitali huo. Waganga ni matapeli katika jamii ambao huchezea tu saikolojia ya mtu kwa lengo la kujiendeleza kiuchumi. Jamii inastahili ipewe mafunzo ya kutosha ili isiuchukulie UKIMWI kama ugonjwa utokanao na urogenitali. Vijana ni kundi ambalo liko katika hatari ya maambukizi na hivyo serikali kupitia kwa vyombo vyake mbalimbali inapaswa kuchukua hatua madhubuti

kuhakikisha kuwa elimu kuhusu ngono inawafikia vijana katika sehemu zote za taifa au jamii. Ufahamu huu utawafanya watu wamakinike na wazingatie njia za kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI.

Njia nyingine ambayo inaweza kutumika katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni kupunguza gharama ya dawa zinazotumika kupunguza makali ya ugonjwa huo. Ugonjwa wa UKIMWI aghalabu huwavamia sana watu ambao hawana uwezo wa kiuchumi wa kununua dawa za kupunguza makali. Bila matibabu na lishe bora, mwathiriwa huwa katika hatari ya kuangamizwa na ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi wa tamthilia ya *Giza* anatueleza:

**181.** *Nuru: Kila siku wanaimba kuhusu UKIMWI na dawa za kuongeza siku, Je, ni walala hoi wangapi wanazipata? Kila wanalolisema ni sauti ya Mwendawazimu (Giza, uk.18).*

Baadhi ya wakazi wa jamii iliyotumiwa na mwandishi katika utunzi wake ni maskini walala hoi. Mtunzi anasema, “*Kila siku wanaimba kuhusu UKIMWI na dawa za kuongeza siku, Je, ni walala hoi wangapi wanazipata?*” Wanalamika kuwa viongozi serikalini huwa wanaimba kila siku kuhusu dawa za kuongeza siku kwa waathiriwa wa UKIMWI lakini baadhi ya watu huwa hawazipati. Mhusika Suzi na jamaa yake ni mfano wa watu katika jamii walioishi kwa umaskini. Wakati mwingine unapata kuwa watu maskini ndio wanaopenda sana kujihusisha na masuala ya mapenzi na ngono. Kuna wale ambao wamedai kuwa watu maskini wanajihusisha na ngono kwa maana wao hawana njia nyingine bora ya burudani.

Kutokana na sababu hiyo, utakuta kuwa kuna visa vingi sana vya maambukizi ya UKIMWI miongoni mwao. Watu kama hawa wanakosa uwezo wa kiuchumi wa kupata matibabu ya kutosha. Hivyo basi mwandishi anapendekeza kwamba njia bora ambayo inaweza kutumika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni kupunguza bei ya

dawa za kupunguza makali na ikiwezekana zitolewe bure. Huduma zote kuhusu ugonjwa wa UKIMWI zikiwa za bure, jamii itakuwa imepiga hatua kubwa sana kwenye vita vya kupambana na UKIMWI. Aidha, uzingativu wa maadili bora ni njia nyingine ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Sehemu inayofuata inajadili njia hii kama mojawapo inayoweza kutumiwa kupambana na ugonjwa wa UKIMWI.

### **6.3.8 Kuzingatia maadili ya jamii**

Maadili ni tabia au mwenendo bora unaokubalika kuzingatiwa na jamii husika. Mwandishi wa tamthilia ya **Giza** anatueleza kwamba njia bora ya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni kuzingatia maadili katika jamii. Vijana wa vyuo vikuu wanapaswa kujiepusha na tabia ya kujihusisha na mapenzi kiholela ili waepuke kuupata ugonjwa wa UKIMWI. Vijana wengi katika tamthilia ya *Giza* wamesawiriwa kuwa na wapenzi wengi na njia hii inahatarisha maisha yao. Uwezekano wa kuupata ugonjwa wa UKIMWI uko juu sana iwapo mhusika atafanya ngono na watu wengi. Aidha, mwandishi anatueleza kwamba, kama mtu amepatwa na ugonjwa wa UKIMWI, si vyema kuusambaza kimakusudi kwa wengine. Mwandishi anatueleza:

**182. Mona: *Mbona nishanasa wengi wanajigonga tu. Siachi vitu, mbona mimi pia hawakunihurumia?* Sauti: *Hakuna atakayebaki, labda milima (Giza, uk.29-30).***

Msanii anatuonyesha namna ambavyo mhusika Mona amejiingiza katika kusambaza ugonjwa wa UKIMWI kwa kufanya mapenzi na yeyote aliyekuwa tayari. Mona hayazingatii maadili mema. Mtunzi anasema, “***Mbona nishanasa wengi wanajigonga tu. Siachi vitu, mbona mimi pia hawakunihurumia?***” Mona anadai kufanya hivyo kwa maana anasema kuwa yeye pia hakuhurumiwa ndipo akaupata ugonjwa wa UKIMWI. Ni wazi kutokana na dondoo lililo hapo juu kwamba tabia ya Mona ni ya kulipiza kisasi. Mona ameamua kuwa hawezi kuangamia peke yake.

Katika baadhi ya vyuo vikuu hapa nchini Kenya, kulikuwa na kisa kinachokaribiana na hiki ambapo msichana mmoja alipogundua kuwa alikuwa na virusi vya UKIMWI, alijiachilia na kufanya mapenzi na watu wengi sana. Wakati ulifika ambapo msichana aliyehusika alitoa orodha ndefu ya wanaume ambao alikuwa amefanya nao ngono na hivyo kuwaambukiza virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Tabia kama hii ni hatari sana kwani inaweza kuiangamiza jamii yote. Hivyo basi mwandishi anashauri kuwa, wale ambao wameupata ugonjwa wa UKIMWI wasiusambaze kwa kisasi bali wayazingatie maadili ya kijamii kwa kujitunza.

Uchunguzi wa wataalamu wa matibabu umeonyesha kuwa ukijihusisha katika kufanya ngono na watu wengi ukiwa na virusi vya UKIMWI utakuwa unahatarisha maisha yako zaidi kwani virusi vitaongezeka maradufu mwilini mwako.

Mwandishi wa hadithi fupi ya “tahadhari bandia” anatoa pendekezo lingine la kupambana na ugonjwa wa UKIMWI. Katika hadithi hii, msanii anataeleza kuwa sheria za kitaaluma hazikuruhusu kuyatangaza matokeo ya uchunguzi wa mara ya kwanza kabla ya kuyadhihirisha na kuyathibitisha. Baadhi ya madaktari katika hadithi hii wanayangaza matokeo kwa mgonjwa kabla ya kuthibitishwa. Matokeo kama haya yanaweza kudhuru maisha ya mtu kisaikolojia. Mhusika Wakesho aliathirika vibaya sana mpaka akaanza kutengwa na jamii kwa kutuhumiwa kuwa na virusi vya UKIMWI.

Uchunguzi zaidi ulipofanywa, ilitokea kwamba Wakesho hakuwa na virusi vya UKIMWI. Mtunzi anapendekeza kwamba wauguzi na madaktari wanapaswa kumakinika katika utekelezaji wa majukumu yao. Wafanyakazi hawa ni wa umuhimu mkubwa katika maisha ya wagonjwa. Kauli zao na matendo yao yanaweza kuyaponya ama kuyaangamiza maisha ya wagonjwa. Mwandishi anapendekeza hawa

wafanyakazi kufuata sheria na maadili ya kazi na hasa kwa kutoa matokeo ya uhakika kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Aidha, namna ambavyo matokeo yanatangazwa inaweza kumpatia mwathirika matumaini ya kuishi ama kukatiza maisha yake.

#### **6.4 Hitimisho**

Sura hii imejadili vipengele viwili muhimu sana katika utafiti huu. Kwanza, imejadili dhima ya mtindo katika uwasilishaji wa dhamira kuhusu UKIMWI. Aidha, sura hii imejadili kwa kina namna ambavyo maandishi teule ya fasihi andishi yametumika kwenye vita vya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Baadhi ya njia zilizopendekezwa kupambana na UKIMWI ni pamoja na kuepuka uasherati, kupinga unyanyapaa, kuzingatia maadili katika jamii, kuwa waaminifu katika maisha ya ndoa miongoni mwa zingine. Sura inayofuata imetoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.



## **SURA YA SABA**

### **MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI**

#### **7.0 Utangulizi**

Sura iliyotangulia imejadili dhima ya mtindo na kujadili kwa kina namna maandishi teule ya fasihi yametumika kwenye vita vya kupambana na UKIMWI. Katika sura hii ya mwisho tumetoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu uliochunguza mitindo ya uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika maandishi teule ya fasihi andishi. Sehemu ya kwanza ya sura hii ni utangulizi, nayo sehemu ya pili inashughulikia muhtasari wa utafiti. Matokeo ya utafiti huu yamejadiliwa katika sehemu ya tatu. Sehemu ya nne imetoa hitimisho la utafiti huu huku sehemu ya tano ikibainisha mchango wa kazi hii ya utafiti. Sehemu ya sita imetoa mapendekezo ya utafiti.

#### **7.1 Muhtasari wa Utafiti**

Utafiti huu ulihakiki mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika kazi teule za fasihi andishi. Sura ya kwanza iliweka msingi wa tasnifu ambapo masuala ya kinadharia yaliwasilishwa. Miongoni mwa masuala ya kimsingi yaliyoshughulikiwa katika sura hiyo ni kama vile: usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo, nadharia tete, upeo na mipaka ya utafiti. Aidha, umuhimu wa utafiti na sababu za kuchagua mada zilifafanuliwa. Sura ya pili iliwasilisha mapitio ya maandishi kisha ikatoa kiunzi cha nadharia. Katika sura ya tatu, vipengele vilivyojadiliwa ni mbinu za utafiti zilizotumika kuifanikisha kazi hii. Katika sura ya nne, nilichanganua data inayohusu mitindo mbalimbali ya uwasilishi wa dhamira za UKIMWI. Nilihakiki mbinu za lugha na tamathali za usemi katika riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Kwenye sura ya tano, nilijadili dhamira mbalimbali kwenye maandishi teule kuhusu UKIMWI. Dhamira

zinazohusu suala la UKIMWI kutoka kwa riwaya, tamthilia na hadithi fupi ziliibuliwa. Dhima ya mtindo na namna ambavyo fasihi inatumika kukabiliana na janga la UKIMWI ilishughulikiwa katika sura ya sita. Sura ya saba imetoa hitimisho la tasnifu. Hitimisho hilo limetoa muhtasari wa kila sura. Maelezo yametolewa kulingana na malengo ya utafiti. Hatimaye, sura hii imetoa matokeo na mapendekezo ya tafiti ambayo yaweza kufanywa na watafiti wengine baadaye.

## **7.2 Mahitimisho ya Utafiti**

Mbali na suala kuu la utafiti lililokuwa kuchunguza mitindo ya uwasilishi iliyotumiwa na wasanii katika kufanikisha dhamira kwenye riwaya, tamthilia na hadithi fupi, utafiti huu ulikuwa na malengo matatu mahsusi. Malengo hayo yalikuwa: kuchanganua namna mitindo tofauti ya uwasilishi imetumika kuibua suala la UKIMWI katika kazi teule za fasihi andishi; kujadili dhamira mbalimbali zinazowasilishwa kwenye kazi teule za fasihi andishi kuhusu UKIMWI; kufafanua dhima ya mtindo katika uwasilishaji wa dhamira na kutathmini mchango wa kazi teule za fasihi andishi katika kukabiliana na janga la UKIMWI. Sehemu inayofuata inayajadili matokeo ya utafiti kwa misingi ya kila lengo.

### **7.2.1 Matumizi ya mitindo tofauti ya uwasilishi katika kuliibua suala la UKIMWI kwenye kazi teule za fasihi andishi**

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa kuchanganua namna mitindo tofauti ya uwasilishi imetumika kuibua suala la UKIMWI katika kazi teule za fasihi andishi. Kwa kuzingatia lengo la kwanza, utafiti huu uligundua kwamba tamathali za usemi na mbinu zifuatazo zilitumika kwa wingi na takriban wasanii wote kuwasilisha suala la UKIMWI. Tamathali hizo za usemi na mbinu za lugha ni pamoja na: tashbihi, kuchanganya ndimi, methali, taswira, misemo na mdokezo. Utafiti huu pia uligundua

kwamba tamathali zingine za usemi na mbinu zingine za lugha zilitumika ingawa kwa kiwango cha chini ikilinganishwa na zile zilizotajwa. Mifano ya tamathali za usemi na mbinu hizo ni pamoja na: sitiari, jazanda, tashhisi, balagha, utohozi, tasfida, ushairi, nyimbo, mbinu rejeshi, tanakali za sauti, takriri, tabaini, kejeli, barua na matumizi ya lafudhi tofautitofauti.

Utafiti huu pia uligundua kwamba waandishi wa riwaya ndio waliotumia tamathali za usemi nyingi zaidi kuliko wengine kwenye maandishi teule yaliyotumika katika utafiti huu. Mtafiti alibaini kwamba hali hii ilichangiwa na urefu wa maandishi ya riwaya ambapo msanii ana uhuru wa kujieleza akitumia maneno mengi ikilinganishwa na utanzu wa tamthilia na hadithi fupi.

Utafiti huu aidha uligundua kwamba waandishi wa hadithi fupi zilizoteuliwa kwenye utafiti huu walitumia tamathali chache za usemi zaidi ikilinganishwa na waandishi wa riwaya na tamthilia. Maandishi yao mengi yaliwasilishwa kwa lugha kavu ya kawaida. Aidha, hadithi fupi huhitaji mtunzi abane mambo mengi katika juhudi zake za kupitisha ujumbe. Licha ya tamathali za usemi na mbinu zilizotajwa kutumiwa na wasanii wengi, utafiti huu uligundua kwamba waandishi walitofautiana katika matumizi yao ya lugha na tamathali za usemi.

Kila msanii aliteua tamathali za usemi alizooni kuwa bora kutumia na hivyo kutofautiana na mwingine. Hivyo basi katika utafiti huu tuligundua kwamba baadhi ya tamathali za usemi na mbinu za lugha hazikutumiwa na waandishi wengine. Uzito wa matumizi ya tamathali za usemi husika ulitegemea msanii na mtindo aliuona kuwa bora kuwasilisha ujumbe wake. Hivyo basi kila msanii alikuwa na upekee wake.

Maoni ya mtafiti kulingana na lengo la kwanza ni kwamba, waandishi mbalimbali wanapaswa kujaribu sana washirikishe mbinu kadha wa kadha katika kazi zao. Wazo hili limejikita kwenye msingi wa Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo iliyoweka msisitizo wake katika nafasi ya ujumi wa lugha katika kazi za fasihi. Kwa mujibu wa nadharia hii, lugha ya fasihi iliangukiwa kuwa ilitumia ujumi katika kueneza fikra au ujumbe. Hivyo basi, si vyema kupata mwandishi ametumia tashbihi kupita kiasi huku mbinu zingine zikitumika kwa uchache na zingine kututumiwa kabisa. Juhudi ambazo nimependekeza zitachangia pakubwa katika kuboresha uandishi wa kazi za kisani.

### **7.2.2 Dhamira mbalimbali zinazowasilishwa kwenye kazi teule za fasihi andishi kuhusu UKIMWI**

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kubainisha dhamira mbalimbali zinazowasilishwa kwenye kazi teule za fasihi andishi kuhusu UKIMWI. Utafiti huu uligundua kwamba licha ya tanzu kuwa tofauti na waandishi kuwa tofauti, kazi zao zilikuwa na dhamira zilizofanana. Katika utafiti huu, dhamira zilizoibuka sana kuhusiana na suala la UKIMWI ni pamoja na: kuporomoka kwa maadili ya jamii, unyanyapaa, utamaushi, kuvunja usiri kuhusu ugonjwa wa UKIMWI na athari ya ugonjwa wa UKIMWI.

Ingawa waandishi walitoka katika jamii zilizo na historia, itikadi, uchumi, siasa na utamaduni tofauti, janga la UKIMWI linaziathiri kwa njia sawa. Hivyo basi mtazamo wa jamii tofauti kuhusu ugonjwa wa UKIMWI unalingana licha ya tofauti ya masuala hayo mengine yaliyotajwa. Ingawa wasanii wa tanzu za riwaya, tamthilia na hadithi fupi wanafanana katika dhamira zao kuhusu UKIMWI, wanatofautiana katika vipengele vingine vya maudhui.

Katika utafiti huu nadharia, ya uhakiki wa kimtindo inatuwezesha kuonyesha kuwa lugha ndicho chombo cha kipekee anachoweza kutumia mwandishi katika kuelezea

ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Kupitia kwa uchanganuzi wa tamathali za usemi na mbinu za lugha katika maandishi teule ya fasihi andishi, tumebaini kuwa mbinu mbalimbali za lugha itumiwayo katika uandishi huwezesha uwasilishaji wa maudhui na dhamira kwa njia mwafaka inayoleta mvuto wa kipekee. Aidha, imejitokeza wazi kutokana na uchanganuzi huu kuwa mitindo mbalimbali ya lugha iliyotumika katika matini za kifasihi huathiri namna ujumbe wake unavyopokelewa na kueleweka. Hii pia huathiri namna msomaji wa matini yake anavyoelewa na kupokea ujumbe wenyewe. Utafiti wetu umedhihirisha kwa uwazi kuwa mtindo ni uti wa mgongo katika kufafanua ujumbe wa mwandishi. Mtindo huonyesha ni kwa jinsi gani sifa za lugha iliyotumika katika kujenga ujumbe pamoja na kuuwasilisha huleta mvuto katika usomaji ili kuupokea ujumbe huo kama ulivyokusudiwa na mwandishi.

Kupitia kwa utafiti huu, tumefaulu kuonyesha kuwa njia inayomsaidia mwandishi kupitisha ujumbe ndiyo maarufu zaidi. Muhimu zaidi katika utafiti huu ni kwamba lugha kama kipengele cha kufafanua mtindo ina mawanda mapana ya kutumika na hivyo huweza kuzua maana mbalimbali. Ni jukumu la mwandishi kuifinyanga lugha kwa ubunifu fulani ili iweze kuwasilisha ujumbe kama alivyokusudia.

Katika utafiti huu, mtafiti aligundua kwamba tanzu za riwaya, tamthilia na hadithi fupi zilikuwa na dhamira zilizolingana kuhusu suala la UKIMWI. Waandishi wakizingatia upekee wao katika uandishi waliwasilisha dhamira zilizofanana kuhusiana na suala la UKIMWI. Hivyo basi mtindo waweza kulinganishwa na vazi katika mwili wa mwanadamu ambapo mitindo ya mavazi haiwezi kubadilisha sura na maumbile ya mtu.

### **7.2.3 Dhima ya mtindo na mchango wa fasihi andishi katika kukabiliana na janga la UKIMWI**

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kufafanua dhima ya mtindo katika uwasilishaji wa dhamira na kutathmini mchango wa kazi teule za fasihi andishi katika kukabiliana na janga la UKIMWI. Utafiti huu ulibaini dhima katika viwango viwili: kiwango cha kwanza kilihusisha dhima za kimaudhui zilizoshirikisha kumfikirisha msomaji, uhamasishaji wa jamii na ufafanuzi wa mawazo. Kiwango cha pili kilihusisha dhima za tamathali za usemi kifani. Kiwango hiki kilihusisha kupamba lugha na kumwezesha msanii kuchagua muundo na mtindo wa kazi yake.

Utafiti huu aidha ulibaini mchango wa kazi teule za fasihi andishi katika kukabiliana na UKIMWI. Njia ambazo waandishi wa tanzu mbalimbali za fasihi andishi wamependekeza katika kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI ni pamoja na; kuepukana na tabia ya uasherati, matumizi ya mipira ya kondomu iwapo mhusika lazima afanye mapenzi, kuwa na uwazi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, kuwa na uaminifu katika maisha ya ndoa, kupinga taasubi za kiume, kupinga unyanyapaa, kutoa elimu na mafunzo kwa vijana na jamii kwa jumla, kupunguza bei ya dawa za kupunguza makali, kuzingatia maadili bora katika jamii na mwisho kuukubali UKIMWI na kupambana nao bila kuwanyanyasa na kuwatenga waathirika. Njia zilizotajwa zikizingatiwa kikamilifu, kuna uwezekano na matumaini ya kupunguza kabisa visa vya maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI.

Utafiti huu umehakiki mtindo katika uwasilishaji wa dhamira za UKIMWI kwenye tanzu tatu za fasihi andishi ambazo ni: riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Utafiti huu ulizingatia maandishi teule katika tanzu hizo tatu za fasihi andishi. Utafiti huu umebaini kuwa mtindo unaotumika katika fasihi una athari kubwa sana katika uamuzi

wa namna ujumbe utakavyopokelewa. Hii ina maana kwamba, ujumbe hauwezi kueleweka bila kuwepo kwa njia maalum ya kuuelezea kwa hadhira husika. Hivyo basi, mtindo ni nguzo kuu katika kazi yoyote ya kisanaa kwani hufanya kazi ya kuifafanua kazi hiyo ieleweke ipasavyo. Muhimu zaidi ni kwamba, utafiti huu umebainisha kuwa ujumbe mmoja waweza kuwasilishwa kwa njia na mitindo tofauti. Matokeo ya utafiti huu yanachangia pakubwa maendeleo ya taaluma ya Kiswahili kama inavyodhihirika katika sehemu inayofuata.

### **7.3 Mchango wa Utafiti**

Utafiti huu umebainisha kwamba fasihi na hususan fasihi andishi inaweza ikatumika kuwasilisha ujumbe wa masuala ibuka yanayoikumba jamii. Utafiti huu umefichua kwamba, mbali na sayansi, fasihi inaweza kutumiwa kukabiliana na maradhi ya UKIMWI. Mbali na kuwaburudisha wanajamii, ujumbe muhimu unaowahusu wanajamii unaweza kupitishwa kupitia kwa fasihi.

Ujumbe unaowasilishwa unaweza kuwasaidia wanajamii kuepuka maambukizi ya maradhi ya UKIMWI pamoja na kuwafariji na kuwapa matumaini waathiriwa wa UKIMWI. Utafiti huu ni muhimu kwani umehakiki mtindo katika tanzu za fasihi andishi: riwaya, tamthilia na hadithi fupi na hivyo kutoa mwanga katika kuzielewa mbinu kwenye kazi husika. Kazi yoyote ya fasihi huandikwa ili isomwe na kupokeza ujumbe kama ulivyokusudiwa na mwandishi. Aidha, utafiti huu umechangia katika kuiendeleza fasihi ya Kiswahili kwani utarejelewa na watafiti wa baadaye. Isitoshe, la umuhimu zaidi katika utafiti huu ni kwamba, lugha kama kipengele cha kufafanua mtindo ina mawanda mapana ya kutumika na hivyo huweza kuzua maana mbalimbali.

Tasnifu hii ni muhimu katika kuongeza idadi ya maandishi ya kitaaluma kuhusu mawasiliano ya UKIMWI. Mbali na kuongezea maandishi yanayohusu mawasiliano

ya UKIMWI, tasnifu hii ina uwezo wa kuchochea wasanii na wanaisimu wengine kufanya tafiti zaidi katika uwanja wa maandishi na mawasiliano kuhusu UKIMWI.

Uwanja wa utafiti ni mpana zaidi. Kwa sababu hiyo, utafiti wetu umeshughulikia sehemu moja tu kwa misingi ya malengo ya utafiti pamoja na upeo na mipaka ya utafiti wetu. Hata hivyo, bado kuna maeneo na sehemu nyingi ambazo bado hazijafanyiwa utafiti. Katika sehemu inayofuata, tumetoa mapendekezo ya baadhi ya sehemu ambazo tunaona zaweza kufanyiwa utafiti ili kuziba baadhi ya mapengo ya kitaaluma ambayo bado hayajazibwa.

#### **7.4 Mapendekezo ya Utafiti**

Utafiti huu ulishughulikia mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Mbali na tanzu hizo, utafiti zaidi unaweza kufanywa kwenye sehemu zingine zinazokaribiana na utafiti huu. Utafiti unaweza kufanywa kuhusu mtindo wa uwasilishi wa dhamira za UKIMWI katika ushairi, tendi na novela. Aidha, utafiti huo unaweza kuwa wa kulinganisha na kulinganua mitindo ya uandishi tofauti inayotumiwa na wasanii kuibua suala la UKIMWI katika kazi teule za fasihi andishi. Utafiti wetu ulizingatia riwaya nne, tamthilia tatu, na hadithi fupi tatu pekee. Yapo maandishi mengi ambayo yameandikwa katika tanzu zilizotajwa na utafiti zaidi unaweza kufanywa ukizingatia maandishi ambayo hayakushughulikiwa katika utafiti huu.

Utafiti unaweza kufanywa ukizingatia nadharia tofauti kando ya Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo tuliyoizingatia katika utafiti. Vilevile katika utafiti wetu, tulikuwa na malengo matatu mahsusi yaliyotuongoza kufanya utafiti. Utafiti mwingine unaweza kufanywa kwa kuibuka na malengo tofauti na yale tuliyoibua katika utafiti wetu. Utafiti unaweza kufanywa kubaini kwa nini baadhi ya mbinu za lugha na tamathali za



usemi hazitumiwi sana na wasanii kuwasilisha ujumbe wao. Aidha, utafiti linganishi waweza kufanywa kulinganisha na kulinganua matumizi ya tamathali za usemi katika tanzu za fasihi andishi.

Utafiti waweza kufanywa kutathmini ufaafu wa njia zilizopendekezwa kupambana na ugonjwa wa UKIMWI kama vile; kuepukana na uasherati, matumizi ya kondomu, kupinga unyanyapaa, elimu na mafunzo kwa vijana miongoni mwa zingine.

Utafiti pia waweza kufanywa kuhakiki mitindo ya uwasilishi wa dhamira za UKIMWI za waandishi wa ukanda wa Afrika Mashariki ikilinganishwa na waandishi wa Afrika Magharibi au Kusini ili kuona ulinganifu na tofauti zao. Utafiti huo unaweza kulinganisha riwaya au tamthilia kutoka Afrika Mashariki na riwaya au tamthilia kutoka Afrika Magharibi ama Afrika Kusini.

Kuna haja ya kufanya utafiti zaidi pia ili kubainisha namna suala la UKIMWI limeshughulikiwa katika tanzu za fasihi simulizi. Utafiti huo unaweza kuzingatia mitindo ya uwasilishi wa UKIMWI kwenye nyimbo, mashairi simulizi, ngano na tanzu zingine za fasihi simulizi. Utafiti wa fasihi simulizi aidha uonyeshe namna ambavyo tanzu husika zaweza kutumika kukabiliana na suala la UKIMWI. Pamoja na hayo, utafiti waweza kufanywa kulinganisha na kulinganua ili kuona namna ambavyo uandishi wa tanzu za fasihi andishi na fasihi simulizi umetumika katika kuliibua suala la UKIMWI katika jamii.

## MAREJELEO

- Airhinenbuwa, C.O., & Obegonm, R. (2000). A Critical assesment of Theories/Models used in Health Communication for HIV/AIDS. *Journal on Health Communication*, Vol. 5-1 International.
- Agu, I. E. (2008). ‘*A Linguistic Stylistic Analysis of Soyinka’s The Interpreters.*’ Unpublished PhD Thesis Federal University of Technology Yola.
- Annensia, A. (2015). *Lugha ya Picha kama Mbinu ya kukabiliana na UKIMWI: Mifano katika Nyimbo za Kinyankole.* Unpublished PhD Thesis, Moi University.
- Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*; Belmont: Wadsworth Publishing Company.
- Boerma, T., & Walker, N. (2003). *Estimates of HIV/AIDS Prevalence from National Population based Surveys as a new gold Standard.* *Lancet* 362: 1929-1931.
- Buffon, G. (1930). *Buffon’s Discourse on Style.* Paris Librairie: Hatier Publishers.
- Bogdan, R., & Bilken, S.K. (eds.) (1992). *Qualitative Research of Education: An Introduction to Theory and Methods*; Boston: Allyn and Bacon.
- Balisidya, M.L. (1977). “*Mabadiliko Katika Fasihi Simulizi ya Wagogo.*” Tasnifu ya Uzamili, DSM: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.
- Craswell, J.W. (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative and Mixed Methods Approaches*; Los Angeles: SAGE Publications.
- Cain, D., & Wenzake. (2011). Language Choice and Sexual Communication among Xhosa Speakers in Cape Town, South Africa: Implications for HIV Prevention Message Development. *Health Education Research Journal* XXVI (3), 476-488.
- Chapman, N. (1982). *The Language of English Literature* : London: Edward Arnold.
- Cohen, L., & Manion, C. (1980). *Research Methods in Education*; London: Croom Helm Ltd. IIEP.
- Coombes, H. (1953). *Literature and Criticism.* London: Penguin.
- Crystal, D., & Davy, D. (1969). *Investigating English Style.* London: Longman Group.
- Crystal, D. (1997). *The Cambridge Encyclopaedia of Language* (2nd Ed): Cambridge: Cambridge University Press.

- Futterer, R. (2007). *Culture Specificity of HIV/AIDS Media Materials: A Media Analysis and Comparison of the Film Projects “Eschageada UKIMWI Datoga” (“Datoga’ Let’s be Aware of Aids”) and “WATU WA WATU” (“People for People”)*. Tasnifu ya Uzamifu.
- Gachara, M. (2005). *A Pragmatic Analysis of The Language Used to Campaign Against HIV/AIDS: A Case Study of Kikuyu Speakers in Nairobi and Nyeri*: Unpublished M.A Thesis, Kenyatta University.
- Gamble, T.K., & Gamble, M. (2002). *Communication Works*: New York: Mac Graw Hill.
- Good, G.V. (1966). *Essentials of Educational Research*: New York: Maridith Publications Company.
- Goode, W., & Halt, J. (1981). *Methods in Social Research*: Auckland: MCGraw-Hill International.
- Gunduza, C. (1998). *Mchango wa Kazi za Fasihi katika Kuhamasisha Jamii kuhusu Athari za UKIMWI*. Tasnifu ya Uzamili. (Isiyochapishwa)
- Iribemwangi, P. I. (2007). *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Jilala, H. (2004). *Giza*. Bukoba: Angaza Initiative Company Ltd.
- Jilala, H. (2008). *The Artistic Uses of Metaphors in Constructing Meanings and Messages in New Generation Songs in Tanzania*. MA Dessertation (Unpublished) University of Dar es Salaam.
- Holman, C. H. (1960). *A Handbook to Literature*. New York: Odyssey.
- Hussein, E. (1970). *Mashetani*, Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Indangasi, H. (1988). *Stylistics*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Jansen, C. (2000). A fire station in your body: Metaphors in Educational Texts on HIV/AIDS. *Southern African Linguistics and Applied Languages Journal* XXVIII (2), 133-139.
- Jansen, C. na Wengine (2010). A fire in your body: Metaphors in Educational Texts on HIV/AIDS. *Southern African Linguistics and Applied Languages Journal* XXVIII (2), 133- 139.
- Jones, R. (1996). *Talking Aid in Hong Kong: Cultural Models in Public Health Discourse* : Asia: Asia Pacific Media Educator.

- Jackobson, R. (1960). "Closing Statement: Linguistics and Poetics." Katika: Thomas A. Sebeok, ed. *Style In Language*, Cambridge MA: MIT Press, UK 350-377. Iliyochapishwa katika J-J., Weber, ed. *The Stylistics Reader*, London: Arnold, 1966, UK 10-15.
- Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani yetu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam Publishing House.
- Kahigi, K. K. (1994). Lugha katika vitabu vya watoto. Katika Kahigi K.K (Mh), *Kioo cha Lugha: Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*. Juzuu, Na. 1. (Uk. 21-36)
- Kahigi, K. K (1995). Lugha Katika Vitabu Vya Watoto: Katika Kahigi K.K (Mh), *Kioo Cha Lugha: Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Saalam*. Juzuu na 1 uk. 21-36
- Karanja, M. W. (2014). "Matumizi ya Sitiari, Tashbiha na Taashira Katika Diwani ya Sauti ya Dhiki" Tasnifu ya Uzamili Isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kathanya, M. (2002). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Islands. Augustine College.
- Kawegere, F. F. (2009). *Mateso Mwathirika wa UKIMWI*: Nairobi: Phoenix Publishers.
- Kerlinger, F.W. (1978). *Foundations of Behavioural Research*,: New Delhi: Surjeet Publications.
- Kezilahabi, E. (1983). *Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kezilahabi, E. (1988). *Nagona* : Dar es Salaam : Dar es Salaam University Press.
- Kezilahabi, E. (1990). *Mzingile* : Dar es Salaam : Dar es Salaam University Press.
- Kimani, H. W. (2006). *Uwiano wa Picha na Matini Katika Mabango ya Matangazo ya UKIMWI. Mtazamo wa Kisemiotiki*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Isiyochapishwa).
- King'ei, K., & Kobia, J. (Wahariri) (2007). *Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Kinara, G. (2012). "Maudhui ya UKIMWI Katika Riwaya ya Kiswahili." Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).
- Kitsao, J. (1982). "An Investigation of Themes in Swahili Literature and an Application of Stylostatistics to Chosen Texts." Tasnifu ya Uzamifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

- Khamis, S. A. (2012). “*Riwaya mpya ya Kiswahili. Utandawazi au Utandawizi? Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili Inavyodai.*” Bayreuth University.
- Kothari, C. R. (1980). *Research Methods and Techniques*: New Delhi: Wiley Eastern Ltd.
- Kothari, C. R. (1990). *Research Methods: Methods and Techniques*: New Delhi: Wiley Eastern Ltd.
- Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*: New Delhi: New Age International Publishing Ltd.
- Kobia, M. (2008). *Taswira za Kiuana Katika Nyimbo za Tohara za Wanaume Miongoni mwa Waigembe*. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Isiyochapishwa).
- Kuhenga, C. (1977). *Tamathali za Usemi za Kiswahili*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Kumar, R. (1999). *Research Methodology: A Step by Step Guide for Beginners*: New Delhi: SAGE Publication.
- Kumar, R. (2007). *Research Methodology: A Step by Step Guide for Beginners 2<sup>nd</sup> ed.*, New Delhi: SAGE Publication.
- Lakoff, G., & Johnson, M. (1980). *Metaphors We Live By*. Chicago: University of Chicago Press.
- Leininger, M. M. (1985). “Ethnography and Ethnonursing; Model and Models of Qualitative Data Analysis.” Katika M.M Leininger (Ed.), *Qualitative Research Methods in Nursing*. Uk. 37-73. Oro lando FL: Grune & Stratton.
- Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*, New York: Longman Group Inc. Limited.
- Leech, G., & Short, M. (1981). *Style in Fiction: An Introduction to English Fictional Prose*. London: Longman.
- Leech, G., & Short, M. (2002). *Style in Fiction: A linguistic Introduction to Fictional Prose*. New York: Longman Limited.
- Leech, G. (2007). *Style and Fiction: A Linguistic Introduction to Fictional Prose*. New York: Longman Ltd.
- Lugwiri, P. L.(2011). “*Sitiari, Taashira na Tashbihi katika Utenzi wa Tambuka.*” Tasnifu ya Uzamili. (Isiyochapishwa) Chuo Kikuu Cha Nairobi.

- Macharia, J. W., & Kadenyi, M. M. (2006). "African Universities and Their Responses to HIV/AIDS Pandemic." Katika Mugenda na wenzake. *The role of African in the attainment of millennium development goals*, Nairobi: Kenyatta University.
- Magwaza, J. (2003). HIV/AIDS Discourses in Kwazulu Natal. Katika Emevwo, B.J Mathangwane na D. Odallo. *The Discourse of HIV/AIDS in Africa*, University of Botswana.
- Masebo, J., & Nyangwine, N. (2008). *Nadharia ya Fasihi*. Dar es Salaam. Nyambari Nyangwine Publishers.
- Matundura, B. (2008). *Sitaki Iwe Siri*, Nairobi: Sasa Sema Publishers.
- Maundeni, T. (2003). Cultural Factors In The Spread of HIV/AIDS. *Southern African Linguistics and Applied Languages Journal XXVIII* (2), 133-139.
- Mbatiah, A.M. (2002). *Kamusi ya Fasihi*: Nairobi: Standard Textbooks, Graphics and Publishing.
- Medical Aid Foundation, (2010). *Kilio Chetu*: Dar es Salaam. Tanzania Publishing House Ltd.
- Miles, J. (1971). *Language in Social Groups*: California: Stanford University Press, Stanford.
- Mkufya, W. E. (2005). *Ua la Faraja*: Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Ltd.
- Mlacha, S. A. (1989). "The Use of Metaphor in Kezilahabi's Novel: Rosa Mistika," *Katika Kiswahili, Juzuu namba 56*:Dar es Salaam: TUKI uk. 25-35.
- Mlacha, S. A. K., & Madumulla, J. S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*: Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mohochi, E. (1995). *Fani katika Hadithi Fupi ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili. (Isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Egerton.
- Mohamed, S. A. (1977). *Asali Chungu*. Nairobi: Shungwaya Publishers.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili; Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi* :Nairobi: EAEP
- Mohamed, S. A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mosha, D. (2002). *Matumizi ya Lugha katika Sherehe za Kumfunda Mwali Miongoni mwa Wazaramo*. Tasnifu ya Uzamifu. (Isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Musumba, S. (2012). *Riwaya za Watu wa Gehama*: Tasnifu ya Uzamili. (Isiyochapishwa).

- Mutembei, A. K. (2001). Poetry and HIV AIDS in Tanzania: *Changing Metaphors and Metonymies in Haya Oral Traditions*: Leiden University: CNWS Publications. Vol 101.
- Mutembei, A. K., & Wengine. (2002). Communicating about HIV/AIDS- Changes in Understanding and Coping with help of Language in Urban Kagera, Tanzania: *Journal of Asian and Africana Studies* 37 (1), 1-6
- Mutembei, A. K. (2009). *UKIMWI Katika Fasihi ya Kiswahili, 1992-2006* : Dar es Salaam: TATAKI.
- Mutembei, A. K. (2011). A comparative Study of Plays on AIDS From Tanzania and The USA: Katika J. K. Makokha, na wenzake. *East African Literature. Essays on written and Oral traditions*: Berlin: Lagos Verlag pp 415 pg 415- 435
- Mkangi, K. (1995). *Walenisi*: Dar es Salaam: EAEP.
- Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*: Dar es Salaam: Education Publishers and Distributors Ltd.
- Msokile, M. (1993). *Msingi wa Uhakiki wa Kifasihi*: Dar es Salaam: East African Educational Publishers.
- Moto, F. (2004). Towards a Study of Lexicon of Sex and HIV/AIDS. *Nordic Journal of African Studies* XIII (3), 343-362.
- Momanyi, C. (2008). *Pendo Katika Shari*. Nairobi. Longhorn Kenya Publishers.
- Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mulokozi, M. M., & Kahigi, K.K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH
- Mulokozi, M. M. (1984). “ Utunzi wa Riwaya ya Historia, ” *Katika Mulika namba 22*, Dar es Salaam: TUKI uk. 1-10
- Ngara, E. (1982). *Stylistic Criticism and the African Novel*: London: Heinmann.
- Njogu, K., & Chimera, R.M. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K., & Wafula, R. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nyandiba, C. (2013). *Uchanganuzi wa Mikakati ya Kiisimu ya Mawasiliano katika Diskosi za VVU/UKIMWI Miongoni mwa Abagusii*. Tasnifu ya Uzamifu ya Chuo Kikuu cha Moi.

- Ogechi, N. O. (2002). *Trilingual Code Switching in Kenya: Evidence from Ekegusii, Kiswahili, English and Sheng*. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Hamburg.
- Ogechi, N. O. (2006). The Language of Sex among University Students in Kenya. *Stichproben – Vienna Journal of African Studies* (9), pg. 123-145.
- Olali, T. (2010). Structure and Anti-Structure of Swahili Novel: A Stylistic Analysis “Babu Alipofufuka.” *The Nairobi Journal of Literature* no: 6.
- Omar, B. (2005). *Kala Tufaha*: Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Omari, S. (2007). Fasihi of Simulizi na Jinsia. Mifano kutoka nyimbo za watoto Tanzania. Katika Massamba (mhr). *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*(uk. 98-106)
- Omary, M. (2011). “Siasa Katika Ushairi wa Kiswahili wa Kezilahabi: Uchunguzi wa Karibu Ndani (1988) na Dhifa (2008),” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam”
- Ongarora, D. O. (2002). “African Languages in Development Prospects and Encumbrances, Katika: Owino, R.F (mh) (*SPEAKING AFRICAN*), *African Language for Education and Development*.
- Ongarora, S. (2007). “Mtindo katika Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.” Tasnifu ya Uzamili (Isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Page, C. (2000). *Report on the Global HIV/AIDS Epidemic*. UNAIDS; World Bank.
- Reynolds, S. (2006). *Orodha*. Dar es Salaam. Macmillan Adan.
- Robert, C. B., & wengine, (2010). HIV/AIDS related knowledge, attitudes and behavior Katika *Demographic and Health Survey 2008-2009*. Nairobi: USAID.
- Robson, C. (2007). *How to do a Research Project. A guide for Undergraduate Students*: Carton Victoria: Blackwell Publishing.
- Rotich, K. (2018). *Simulizi za virusi vya UKIMWI zinavyodhihirika katika nyimbo za jamii za Kenya kibaadausasa*. Tasnifu ya Uzamifu ya Chuo Kikuu cha Moi. Isiyochapishwa.
- Senkoro, F. E. M. (1976). “Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili,” Katika *Kiswahili Juzuu, namba 46/2, Dar es Salaam: TUKI uk. 74-82*.
- Senkoro, F. E. M. (1982). *Fasihi*: Dar es Saalam: Press and Publicity Centre.
- Senkoro, F. E. M. (1993). *Fasihi*: Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.



- Senkoro, F. E. M. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi*: Dar es Salaam KAUTTU Limited.
- Senkoro, F.E. M. (2012). *Fasihi*: Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Serwadda, D. (1985). Slim Disease. A new Disease in Uganda and its Association with HTLV- III Infection. *The Lancet*, (19) 2, 849- 852.
- Simpson, P. (2004). *Stylistics: A Resource Book for Students*: London: Routledge.
- Syambo, B. K., & Mazrui, A.M. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*: Nairobi: East African Publishers.
- Socrar, P. (2009). *Teaching Taboo Topics without talking about them. An Epistemic study of a New Approach to HIV/AIDS Prevention Education in India*, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Stanford.
- Taylor, S. J., & Bogdan, R. (1984). *Introduction to Qualitative Research Methods: The Search for Meanings*. New York: John Wiley & Sons.
- Thavis, J. (2009). "Pope's Condom Comments latest Chapter in Sensitive Church Discussion"  
<http://www.catholicnews.com/data/stories/cns/0901232.htm.7/10/2011>
- Tunmer, G. (1973). *Stylistics*: New York: Hazell Watson & Viney Limited.
- TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*: (Toleo la 2). Nairobi: Oxford University Press.
- Too, M. (2010). *Fani Katika Tamthilia ya Nguzo Mama*: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).
- Too, M. (2011). "Matumizi ya Lugha katika Tamthilia ya Nguzo Mama." Tasnifu ya Uzamili (Isiyochapishwa) Chuo Kikuu Cha Nairobi.
- UNAIDS, (2012). *World Aids Day*. The Standard, Tuesday, December 4, 2012. Nairobi: Standardmedia.
- Veliswa, M. (2009). *Intercultural Communication in Three Eastern Cape HIV/AIDS Clinics*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu Cha Rhodes.
- Wales, J. (2001). *A Dictionary of Stylistics*: ( 2nd Edition) Harlow: Pearson Education Ltd.
- Walibora, K., & Mohamed, S. (2010). *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine* : Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.
- Wamitila, K. W. (2002(a)). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake* : Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

- Wamitila, K. W. (2002(b). *Bina- Adamu*: Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K. W. (2003(a). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*, Nairobi: Focus Publishers.
- Wamitila, K. W. (2003(b). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*: Nairobi: Focus Publishers Limited.
- Wamitila, K. W. (2004). *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*: Nairobi: Focus Publications Limited.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*: Nairobi: Vide Muwa Publishers Ltd, Kenya.
- Wamitila, K. W. (2013). “Mikakati ya Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili” Katika *Mulika namba 32, TATAKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*.
- Wambua, S. M. (2001). *Mtindo wa Nyimbo za Kakai Kilonzo* : Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Isiyochapishwa)
- Wanyonyi, C. (2009). “Sintaksia, Italiki, Lugha ya Kitamathali, Tasfida, Ishara za Uashiraji na Masuala ya Balagha katika Riwaya ya Nguzo za Mama.” Tasnifu ya Uzamili. (Isiyochapishwa) Chuo Kikuu Cha Nairobi.
- Warford, G. (2001). *Doing Quality Educational Research. Continuum. The Tower Building*: London : New York.
- Wilkson, T., & Bhandakar, S. (19770. *Methodology and Technology of Social Research*: Bombay: Himalaya Publishing House.
- Yin, G. (1984). *Case Study Research: Design and Methods*, (2nd eds) Thousand Oaks Gliff: SAGE Publishers.
- Young, P.V. (1984). *Scientific Social Surves and Resesarch*: Englewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.

## VIAMBATISHO

**Kiambatisho cha 1: Ua la Faraja**

1. *Asha akapita. Kila aliyekumbwa na wimbi hilo la manukato hakuweza kujizuia kupandisha pumzi ili yamuingie sawasawa. Wanaume wote walimtaazama kwa shauku kama simba anavyokodolea pofu nyikani (Ua la Faraja, uk.10)*
2. *Akamkabidhi lile shati. Omolo akalichukua na kwenda mpaka dirishani. Akalivaa. Alifungua mkanda wa suruali ili achomekee shati. Sasa alijisikia tamaa ya ajabu ya kufanya tendo, tendo alilolichukua na kulikataa. Alipojitahidi kuvaa nguo, ile tamaa ya mwili ilimjia na kumzoa kama wimbi kali la bahari na kuzidi kumsukuma kinyume cha matarajio yake. Queen alipomuona anahangaika, akacheka kicheko ambacho kilizidi kumsisimua Omolo. (Ua la Faraja, uk. 52)*
3. *Siyo kweli mjomba Omolo. Wewe hujui kiini cha yote. Mimi mwislamu, najua huo wajibu, na ni haki kwa Mzazi kusesitiza kwa watoto jambo la suala. Lakini siyo mzee Ngoma wa kuniambia hekima hiyo! Mimi namuona kama shetani tu... (Ua la Faraja, uk.119 -120)*
23. *Polepole, Queen alinyata mpaka pale alipokuwa. Akachutuma huku ameshikilia glasi ya pombe iliyonywewa nusu, “ Which are your favourites ” Alimuuliza kwa sauti ya kilevi, huku akiweka mkono wenye glasi ya pombe begani kwa Omolo. Hakuwa ametulia. Alikuwa anayumba kiasi ... Queen alisema huku akichukua glasi ya Omolo. Akatia Duncan robo ya ile glasi, kisha akaenda kwenye friji na kuchukua juice aliyoiandaa rasmi kwa ajili ya Omolo toka asubuhi siku ile. (Ua la Faraja, uk.50-51)*
24. *You teach me Swahili, I teach you English Asha akaitikia kwa kichwa. Mtalii akatoa saa kama ya mwanariadha na kumwonyesha Asha akisema, Two hours Swahili, two hours English (Ua la Faraja, uk. 85)*
30. *Mambo kwa soksi! Mambo kwa soksi! Maji uyavulie nguo ndipo uyakoge! Ulapo ndizi usiimenye ila ivishe ganda! Jambo la raha leo ni kuvishana magozi! (Ua la Faraja, uk.12)*
31. *Kero ya ulevi ikawa imepungua nyumbani. Lakini kupungua kwake hakukumletea furaha Tabu, kwani hisia zake zilimpa ilani kwamba kulikuwa na kiini kichungu zaidi katika hayo mabadiliko ya tabia ya mumewe. Ijapokuwa hakuna aliyemfunulia mwenziwe moyo wake na kutoa dukuduku yake waziwazi, kwa kila mmoja kulikuwa na hofu. Hofu ilikuwa kwamba: majuto ni mjukuu, mwisho huja kinyume. (Ua la Faraja, uk.115-116)*
32. *Kama unaweza, hebu mfanye yeye na mimi tuzoeane ili nimchunguze vizuri. Lakini kwa sasa, la muhimu ni kwamba Grace aepuke kufanya mapenzi naye. Hatujui pengine ni chui aliyevaa ngozi ya kondoo. Simba mwendapole ndiye mla nyama. (Ua la Faraja, uk. 256- 257)*
44. *Akaka kwenye kochi akisoma kitabu na kumsubiri Queen alete shati lake avae, amalize kinywaji; aondoke. Alishangaa kuona hisia ngeni zinamjia. Damu yake*

*ilisismka. Kichwa kilikuwa kama kinavimba Miguuni joto lilianza kupanda, alijisikia hamu ya kimwili ya ajabu imemwingia. Kwa kuwa hakuwa na mazoea ya kunywa pombe kali akadhani hivyo ndivyo ulevi wa Duncan ulivyokuwa. (Ua la Faraja, uk.51)*

45. *Queen alikuwa amedhoofu sana. Mashavu yalikuwa yamebonyea, kifua kimesinyaa na ngozi yake ilikuwa imepauka na kuwa kavu kama mtu aliyekuwa kwenye mavumbi. Alikuwa amejitanda kanga safi, nyeupe zenye maua meusi. Kichwani alijifunga kitambaa, lakini nywele ambazo zilijitokeza pembeni mwa kitambaa zilikuwa zimelainika kama za mgonjwa wa utapia mlo. (Ua la Faraja, uk.140)*
51. *Kupanda mchongoma, kushuka ndio ngoma. Hoja hii ilimwandama Ngoma. Zamani alipopata pesa alidhani furaha ya maisha iko kwenye anasa hata kama akimkirihhi mke wake. Sasa anasa zimemwegesha katikati ya miiba. Kila alipogusa akakuta panachoma. Alilala akiwaza, na usingizi ulimjia muda mrefu baada ya mke wake kulala. (Ua la Faraja, uk.138)*
52. *Alipofika chumbani akavua nguo zote na kujifunga kanga. Kabla ya kujifunga akaukagua mwili wake uliodhoofu. Hivi ndiye mimi Queen, nimefika hali hii? Alijiuliza. Unene wote uliomba umbile zuri ulikwishasinyaa, amekuwa mweusi, weusi usiovutia. Ilikuwa kama nuru ya mwili wake imeingia giza. Sehemu zake za siri zilitoa harufu kali kutokana na vidonda vilivyomshambulia nje na ndani. (Ua la Faraja, uk. 147- 148)*
69. *Msafiri alikuwa amelewa, lakini alijitahidi kuongea kwa kupima kauli zake. Akauliza, wewe una mume? Hapana. Sipendi wanaume. Asha akajibu. Kwa nini? Sipendi kuchungwa...sipendi utumwa. (Ua la Faraja, uk.79)*
70. *Twajua Juma amekukosea...Grace alisema. Kosa kubwa...Ila wewe ni mzazi, sharti umsamehe... Omolo alishauri. Sisamehe! Juma siyo mwanangu. Sasa niambie bwana Omolo, utanisaidia kuuza hayo magari au hutanisaidia? (Ua la Faraja, uk.222)*
71. *Huna sababu ya kutaka kufungua kesi.Maelewano mazuri baina yako na baba yako yanatosha. Amekuita, nenda ukasikilize alichokuitia. Yule mtu ni mgonjwa, hivi karibuni atakufa...(Ua la Faraja, uk.238)*
83. *Nani akutake wewe na hali umeshakokoteza mbegu za umeme mji mzima? (Ua la Faraja, uk. 76)*
84. *Asha aliingia, alikuwa pekee yake.Watu walimkodolea macho. Katika miaka ile ulikuwa msimu wa wanaume kupenda wanawake wanene, wenye matako makubwa na kifua kilichoja maziwa. Asha alikuwa na kila sifa ya umbile hilo. Mwili wake mnene wenye matako yaliyojaa ulijiweka vizuri kwenye nguo ile ya aina yake. Alipotembea, matakao yakiangukiana kwa utepetepe huku yakitingisika kwa mdundo na mwendo wake. Alijijua alivyo na alifanya kila jitihada kuwaonyesha wanaume waliotazama umbile lake. (Ua la Faraja, uk.9-10)*
85. *Pendo na Chiku wakamshambukia, na wewe Yakobo unampa kichwa azidi kutupigia kelele! Mtu kama aogopa magonjwa achana na ngono! Ya nini kuvalishana mipira?! (Ua la Faraja, uk.12 )*

86. *Mimi naona ni busara zaidi kupiga vita tabia ya watu kushabikia ngono. Kwenye sinema, kwenye miziki yote ya Kiafrika, kila Mahali ni hamasa ya ngono. Muziki umekosa maana zaidi ya kunengua na kuonyesha uhodari wa viuno vya ngono. Pigeni vita ushabiki na sanaa ya kushabikia ngono. (Ua la Faraja, uk.13)*
87. *Kila siku nimekuonya; Acha! Hukunisikia. Ulijiona rijali sana kuvamia kila mzoga wa kike uliokuta. Sasa umeniletea gonjwa. Eti tujadiliane! Nijadiliane na mtu ambaye hata sasa ananuka harufu za uasherati...? (Ua la Faraja, uk.27)*
88. *Sauti zao zilijaa mzaha na ukorofi wa kike kwa mwanamume. Macho yalimtazama huku kope zikipesha kwa ishara ya kushawishi. Sauti zao za pamoja zilikuwa na mkwaruzo kidogo na wororo wenye kuamsha hisia za kiume. (Ua la Faraja, uk.4)*
89. *Mtu wiki mbili mpaka tatu, unamuacha mke anaganda kwa baridi na wanaume tupo, tubaki kumkodolea macho tu? ... unadhani mimi mjinga? Sisi hatucheleweshi ngoma miguuni kaka! Ukipata uwanja funga mabao uondoke. Usiku kucha umelala kwa mwanamke unangoja nini? (Ua la Faraja, uk. 9)*
90. *Mima alivua nguo. Omolo akazidi kushangaa, Mima alimvua suruali. Alipovua nguo ya ndani ndipo aliposhikwa na mshangao mkubwa... nilikuwa nakutaka. Nilivutiwa nawe tufanye mapenzi. (Ua la Faraja, uk.21)*
91. *Yawezekana Queen ameniambukiza? Nitaliepukaje janga hili? Kwa nini nilifanya uzinzi? Hivi ni kweli huu ndio mwanzo wangu wa kuelekea kaburini? (Ua la Faraja, uk.30)*
92. *Na siku ile ikawa ya kwanza kwa Omolo kulifurahia tendo lile akiwa katika utu uzima wake... (Ua la Faraja, uk. 52)*
103. *Hapana, namsikitikia mke wake Ngoma. Yule mama ni mstaarabu sana. Ingawaje mumewe ni mlevi wa kutupwa, yeye anawalea wanawe kwa adabu kwelikweli. Sasa ukiambiwa pengine Ngoma kamhukumu kifo. (Ua la Faraja, uk.15)*
104. *Tabu alianza kulia kwa uchungu mwingi. Kwa kawaida ya mila za kwao, ilikuwa aibu kubwa kwa mama na mwanawe wa kiume kujadili mambo ya namna ile wote machozi yalizidi kuwatoka, kila mmoja akitafakari na kulia kwa nafsi yake. Lakini kiini cha kilio chao kilikuwa ugonjwa wenye sifa mbaya, kashfa, aibu, laana na udaku wa kila aina na mateso makubwa ya nafsi za wadhurika. (Ua la Faraja, uk.38)*
105. *Kama yapo waliyosimulia wakristo, basi ataishia kwenye moto milele. Lakini kama hadithi ya mbinguni na pepo ni uongo, mtu atakwenda wapi akifa? Ni kweli watu wakifa wanaisha na kupotea hivi hivi? Kuna umuhimu gani basi wa kuwepo kwa watu duniani? (Ua la Faraja, uk.68)*
126. *Siku aliyompatia kazi Grace, Omolo alishtushwa na kauli za bwana Ngoma wakati alipokuwa anazozana na mkewe. Ngoma alikuwa anatoka akiuliza sababu na mbinu iliyotumika kumwomba Omolo msaada wa ajira hiyo. Amekusaidia wewe kama nani? (Ua la Faraja, uk.18)*

127. *Juma alimchukia baba yake kwa kutomjali mamake na kumsababisha ajishughulishe na biashara ya kupika vitumbua na chapati,kuuza genge la mboga ili apate pesa za kujinunulia mahitaji yake. Ngoma alikuwa tajiri... Sasa Juma alijiuliza; kama baba yake ana pesa nyingi za kulewa pombe, kwa nini mama yake anaishi maisha ya kimaskini? (Ua la Faraja, uk.34)*
128. *Omolo alipenda kujiuliza swali hili akimaanisha; faida ya maisha ni nini? Kwa nini mtu ahangaikie kufanya kazi ili apate pesa, akishazipata azitumie ziishe? Kuna manufaa gani au raha gani ya ajabu iliyowafanya watu wayahangaikie maisha? Alishangaa kwa nini hata yule mwenye maisha ya shida anapougua na kukaribia kifo hafurahi kwisha kwa shida zake akifa bali huhangaika kujitibu ili apone aendelee na shida zake. (Ua la Faraja, uk.23)*
129. *Adhabu gani hii? Alisema mwenyewe huku akila. Kweli aliyaona maishani adhabu: kuzaliwa, kuyaonja na kisha kunyang'anywa na kifo! Raha zote hazikuwa na maana tena. Zimepotea kwenye kumbukumbu yake. Kilichokuwemo kichwani mwake ni yale mawazo ya kuukaribia mwisho wake. (Ua la Faraja, uk.68)*
152. *Mambo kwa soksi! Mambo kwa soksi! Maji uyavulie nguo ndipo uyakoge! Ulapo ndizi usiimenye ila ivishe ganda!Jando la Raha Leo ni kuvishana magozi!(Ua la Faraja, uk.12)*
153. *Queen alikuwa amedhoofu sana. Mashavu yalikuwa yamebonyea, kifua kimesinyaa na ngozi yake ilikuwa imepauka na kuwa kavu kama mtu aliyekuwa kwenye mavumbi. Alik. uwa amejitanda kanga safi, nyeupe zenye maua meusi.Kichwani alijifunga kitambaa, lakini nywele ambazo zilijitokeza pembeni mwa kitambaa zilikuwa zimelainika kama za mgonjwa wa utapia mlo. (Ua la Faraja, uk.140)*
159. *Asha akacheka sana akasema 'Sinunuliwi'. Nitakununua wewe kwa senti hamsini na busu moja shavuni. Msafiri akanyanyuka kwa nguvu na kutaka kumwendea pale alipo. Macho yake yalikuwa mekundu kwa shauku. Asha akacheka, akanyanyuka na kujifanya anataka kukimbia. Mwili wake ulikuwa mzito. Msafiri akamwendea (Ua la Faraja, uk.81).*
158. *Queen! Jina hili lilivuma akilini mwake kwa nguvu kama upepo wa kimbunga. Ni kweli kwamba mwanamke yule malaya amewajeruhi watu aliwapenda kiasi kile? Kama amedhuru Ngoma, basi hata dada yake amedhurika. Na kama hao wamedhurika, Omolo je, atakuwa amepona? Asubuhi ya usiku ile, Queen ndiye aliyepiga simu na kumwambia ana jambo la muhimu kumwambia Omolo. Pengine jambo lenyewe ni hizo habari za UKIMWI! Wazo la Omolo kuweza kufanya mapenzi na malaya huyo lilimchafua moyo. Hakupenda kulifikiria. Akalirushia pembeni. Akamtazama dada yake. Alishindwa kummaliza. (Ua la Faraja, uk.59-60)*
162. *Mambo kwa soksi! Mambo kwa soksi! Maji uyavulie nguo ndipo ukayaoge! Ulapo usiimenye ila ivishe gando! Jando la raha leo ni kuvishana magozi! ( Ua la Faraja, uk. 12)*
163. *Kama Mima siku ile, Queen alishitushwa na kutotahiriwa kwa Omolo. Lakini yeye akawa mstaarabu. Hakucheka wala kughairi. Ila alikwenda kabatini akatoa mpira wa kiume, akamrushia Omolo akachukua na kuvaa. Na siku ikawa ya kwanza kwa Omolo kulifurahia tendo lile akiwa katika utu uzima wake. Mipira miwili ilitumiwa na siku ile*

*aliporudi nyumbani kwake ilikuwa usiku. Alichoka sana. Hakuwa na hamu ya kwenda Malaika bar. (Ua la Faraja, uk.52)*

- 164.** *Ngoma alifanya kazi kubwa kulaghai mke wake mpaka akamwamini. Hivyo, siku ile walifanya tendo la ndoa kwa kutumia mipira. Lakini tendo lile lilikuwa geni kwao. Hakuna aliyefurahia. Walijiona kama wanacheza kama watoto wadogo wanaoigiza mchezo wa ndoa vichakani, maana umuhimu na heshima ya tendo lile vikapaushwa na kuwoko kwa ukuta wa mpira, uliotenganisha miili na damu zao; ukuta ambao haukuwa na sababu kama kila mmoja wao angekuwa mwaminifu; ukuta ambao, katika hisia za Tabu, ulikuwa mwanzo wa kutenganisha miili na nafasi zilizounda unyumba wao. (Ua la Faraja, uk.31)*
- 169.** *Ngoma na Asha walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Pia, Omolo alikwishawahi kumfumania Ngoma nyumbani kwa Queen. Alikuwa anaijua tabia ya uzinzi ya jirani yake. Ikiwa Queen alikuwa mgonjwa, bila shaka amemwambukiza Ngoma kama hawakutumia mipira. Je, mzozo ule unahusiana na yale aliyoyakuta Queen siku ile? (Ua la Faraja, uk.71)*
- 172.** *Kesho yake pia Ngoma alirudi nyumbani mapema, ila alikuwa amelewa sana. Tabu alikataa kunywa pombe ile. Baada ya chakula cha jioni walipokwenda kulala Ngoma alimpa mke wake pakiti mbili za mipira ya kiume akamwambia, 'Ma` Juma, siku hizi magonjwa ni mengi. Hujui sisi wanaume tunakopita. Mimi naona tunapotaka kukutana tutumie hii mipira. (Ua la Faraja, uk.138)*
- 174.** *Naye Tabu alifarijika sana. Wakati mwingine matani ya Abu kwa Asha yalimfanya asahau matatizo yake, akatabasamu au kuchangia utani. Hivyo, polepole bila kujua, watoto walifanikiwa kumrudisha mama yao katika hali ya kawaida. Grace pia alichangia kwa kumpa moyo dadake asiwe na shaka, abaki na imani na asubiri kwa kupima iwapo alikuwa ameambukizwa. (Ua la Faraja, uk.113)*
- 175.** *Umenionyesha upendo, asante. Hata nikiugua nitakumbuka yote uliyosema na wewe nitakukumbuka. Hutangulia mbali, tutakula pamoja. Nitakuorodhesha katika wagonjwa wangu. Nitakuuguza, tutaugua sote, mimi na wewe...Tabu akamtazama tena. Akatabasamu na machozi yakaanza tena kutoka Hans akayafuta. Sasa usilie tena. Jiandae kuishi na virusi, ukiwalea watoto wako mpaka hapo tutakapo fika mwisho. (Ua la Faraja, uk.194)*

## Kiambatisho cha 2: Kala Tufaha

4. *Mtoto wa watu alikaa kando ya barabara kwenye nyasi ili ashushe pumzi. Alitamani sana kuutua mzigo aliokuwa ameubeba lakini haikuyumkini mara moja. **Alikuwa mfano wa punda kihongwe mbeba mizigo aliyechoka kwenda; siku zote hudinda akahiari kufilia mbali kama kuendelea na safari.**(Kala Tufaha : uk. 5-6)*
5. *Si kupenda kwangu. Nimeghilibiwa na Shetani. Alisema Fumbwe katika hali ya kubembebeza. Kibibi hakutaka kusikia hili au lile. **Alikuwa amepania kwenda zake nje; mbali na nyumba hiyo aliyoiona mithili ya jahanamu. Aliinuka na kuja alikokuwa Fumbwe. Akajibidiisha kumsukuma wala asiweze chochote.** (Kala Tufaha, uk. 68)*
6. *Usiwe na shaka. Alisema Bi Kidawa. Nitamwandikia huyo bwana barua kwanza. Atatubu kwa kukuchezea kama kikaragosi. Wajua wanaume wengi wanataka kuwachezea wasichana na hilo silikubali. Nipo hapa kutetea wanawake wenzangu. (Kala Tufaha, uk. 99)*
46. *Wenye gari hili walikuwa katika dunia yao tofautitofauti. Hewa ndani ya gari ilikuwa na mchanganyiko wa harufu, kuanzia za wavuta sigara, wenye kunuka vikwapa, wenye majasho. Almuradi kukawa na uvundo moja kwa moja! Gari lilivyojaa kuandamana na harufu hiyo ilikuwa taabu kupumua. **Zaidi ya hiyo dhiki ya harufu, kuna hao wasafiri kadhaa wa kiume waliojisukumiza kwa maksudi kwa wenzao wa kike.**(Kala Tufaha, uk.14)*
47. *Jumba hilo lilikuwa na uwanja mkubwa. Limezingirwa kwa ua wa zege. Kuuzunguka huo ua kwa upande wa ndani kulikuwa na miti iliyokuwa imehasiwa na kupogolewa ikasalia nadhifu. Uani hapakuwa na athari ya majani wala karatasi, ishara kwamba mazingira ya jumba hilo yalikuwa safi... majumba hayo yalikuwa na malango makubwa, nayo pia yalizungushiwa nyua za zege. Kila jumba likawa na walinzi wa langoni. Kulikuwa na ulinzi wa kipekee katika mtaa huu, hivi kwamba hata panya hangeweza kuingia bila kugunduliwa! (Kala Tufaha, uk.53)*
53. *Aliupitisha mkono wa kulia katika sehemu ya juu ya paja lake. Hapo akathibitikiwa na ukweli! Hapakuwa na kizuizi chochote. Vidole vyake vilipata unyevunyevu... alijihisi kuwa na mavune mithili ya mtu aliyekesha na kushinda kwenye kazi ya shokoa. Mara akapata maumivu makali katika eneo alilohofia! **Papo hapo msichana wa wenyewe akapiga unyende na kukurupuka kutoka kitandani.** (Kala Tufaha, uk.66)*
54. *Siku zote huzuni ilimtatwala asione raha ya kuishi. Mke aliyemtwa akiwa hana chochote. Akimshughulikia kimasomo hadi yake kupata stashahada ya elimujamii. **Malipo yake kumla kivuli, tena nyumbani kwake. Ndiyo na yeye alikuwa na jicho la nje.** Lakini mengi akiyafanyia nje. Pengine mara moja tu aliwahi kujisahau akafanyia nyumbani. (Kala Tufaha, uk.176)*
114. *Mbona Imu hakupita vizuri na baba alimtafutia shule ya upili. Kwa nini anayathamini sana masomo ya kakangu na kunitekeleza mimi? Kama kuzaliwa msichana, nilitaka mimi?" aliwaza huku akilengwalengwa na machozi. (Kala Tufaha, uk.15)*
115. *Hana sutua yoyote mbele ya mumewe, mwalimu Selemani Chai. **Yeye mwanamke, akisema atakayemsikiliza ni nani?**Baba mtu ashakata kauli masomo ya Kibibi ndio*



*basi. Bi Habiba tangu hapo hajawahi kumwinulia mumewe ulimi. (Kala Tufaha, uk.17)*

116. *Mwalimu Selemani ameshapanga na rafiki yake huyo wa hapo mferejini kuhusu ndoa ya watoto wao wawili. Kitinda mimba wa mzee Majembe yuafanya kazi Uarabuni. Atakuja likizo nyumbani baada ya miaka miwili. Pengine hapo kutakuwa na mpango wa posa au hata ndoa yenyewe. Kibibi hayajui haya lakini mama mtu keshambiwa na kuonywa kutomwarifu. Aila ya majembe, wote hawana habari ila huyo mzee mwenye nyumba. (Kala Tufaha, uk.20)*
117. *..... Alishuku kulikuwa na jambo lililotendeka ambalo si la kawaida. Alivuta fikra kujaribu kukumbuka mambo. Hakupata lolote la maana kwa wakati ule. Aliupitisha mkono wake wa kulia katika sehemu ya juu ya paja lake. Hapo akathibitika na ukweli! Hapakuwa na kizuizi chochote. Vidole vyake vilipata unyenyekevu. Kibibi aliingiwa na kiwewe. (Kala Tufaha, uk. 65-66)*
118. *Sitaki kabisa kukuona kwangu. Izara uliyotushushia inatutosha. Nasema nyumba yangu hii uione paa na moshi. (Kala Tufaha, uk.19)*
119. *Sijui kahongwa au nini! Mpaka lini wanawake tutabaki kwenye dhiki hii? Wangapi waliotendwa kama mimi? Wakienda kwenye vyombo vya sheria wanakumbana na waume? (Kala Tufaha, uk.100)*
120. *Dhiki zaidi ni hao askari wa manispaa; wasipotaka rushwa wanamtaka yeye. (Kala Tufaha, uk.132)*
150. *Kala akikabilia na dudu moja lililokuwa na sura ya kutisha lililodhulumu wanadamu. Dudu lenyewe kubwa na lenye macho makubwa na miguu mingi. Lilikuwa likiwaua wanadamu wala halikushughulika na wanyama wengine. Ajabu ni kwamba liliwalenga watu waliolikaribia au waliokuwa kwenye njia liipitayo (Kala Tufaha uk.63).*
152. *Ukutani mlitundikwa karatasi na mabango yenye ujumbe tofautitofauti kuhusu afya. Moja lilisema, “Kinga yashinda tiba”, jingine likanadi “uvutaji sigara wadhuru afya yako”Kubwa ya yote ni hilo bango kubwa lililonadi kwa wino mwekundu: “Jihadhari!” Lilikuwa na picha ya tufaha kubwa lililoiva kwelikweli. Linaonekana kama mtu kaliuma upande mmoja. Tufaha lenyewe lilikuwa na mdudu aliyefanana na kiwavi alijitokeza katika sehemu iliyong’atwa. Dudu lenye macho makubwa, sura ya kutisha lakini limetabasamu. Kando ya picha ya tufaha, pamechorwa picha ya watu wawili, mwanamume na mwanamke wa umri wa makamo. Wote wamelikodolea macho tufaha, wakionekana kulimezea mate. Kando yao pamechorwa jichwa linalotisha likiwa limetoa macho na ulimi. Jichwa lenyewe si la binadamu, si la mnyama! Chini yake hayo maandishi. “JIHADHARI” (Kala Tufaha, uk.181)*
154. *Mtu aliyekuwa akikanyaga ardhi ikitetemeka sasa hatazimiki amekonda mithili ya mfupa wa panya! Uso wake umejenga peto na makunyanzi ya daima. Amepata sura ya kikongwe wa umri wa miaka tisini na.....! Nywele zake zimepoteza weusi wa asili zikaanza kuwa rangi ya hudhurungi. Wala si nywele tena; zimelainika kama zitokazo kuwa singa, ama manyoya ya paka mzee! Zimetimka mfano wa manyoya ya kuku wa kidimu aliyenyeshewa. Midomo yake imekuwa miekundu mithili ya ile ya*

*mlevi wa chang'aa. Macho yamechopoka na kuyafanya kuonekana makubwa kila saa na dakika. Amekuwa si wa kulala si wa kukaa! (Kala Tufaha, uk.169)*

- 156.** *Picha yenyewe iliashiria enzi ambayo Ma' Asha alikuwa mwanamgeni kweli! Nywele nyeusi tititi! Mabegani kalaza matando. Ametoa tabasamu inayodhihirisha vibonyo kwenye mashavu. Meno yake meupe kisha yenye mwanya katikati. Macho yenyewe ya kikombe. Kwenye nyusi athari ya wanja inaonekana. Kaka kwenye gogo kisha kaegemeza kidevu chake kwenye kitanga cha **kulia**. Tufaha ashapewa habari nyingi, kisa cha mwenye picha. Si na Biti Mejumaa tu, hata na Ma' Asha mwenyewe. (Kala Tufaha, uk.108)*
- 157.** *“ Ninafanya nini kitandani? Sasa mazoea na chumba hiki; iweje leo nimechupa mipaka hadi ya kulala kitandani? Taratibu fikra zilimpa kung'amua lililotendeka...alijihisi kuwa na mavune mithili ya mtu aliyechekesha na kushinda kwenye kazi ya shokoa. Mara akapata maumivu makali katika eneo alilohofia. Papo hapo msichana wa wenyewe akapiga unyende na kukurupuka kutoka kitandani...Fumbwe alimvuta na kumkumbatia Kibibi ambaye sasa alikuwa kama mwehu...” (Kala Tufaha uk.66)*
- 160.** *Baada ya muda mfupi, alitoka ndani msichana: alivaa nguo zilizoonya zaidi ya kusitiri. Harufu ya manukato ilimfuata alipopita. Alielekea walikokuwa wamekaa watu akasonga karibu na Tufaha. Yule bwana aliingia ndani. 'Mpaka kesho', alisema. 'Haya kwaheri', alitikia mhazili. Simu ililia na yule msichana akarudi tena ofisini. Yaonekana mkutano wake na mwenye ofisi ulikuwa muhimu sana. Kikao chenyewe kilidumu kwa muda wa saa tatu. Msichana wa watu alipotoka mle ofisini alionekana kuchoka. Kibeti chake kwapani alifululiza mlangoni huku nyuma akiacha harufu kali ya marashi. Hakutaka kuwatizama waliokuwa ukumbini. (Kala Tufaha, uk.119)*
- 171.** *Siku zote huzuni imemtawala Fumbwe asione raha ya kuishi. Mke aliyemtwa akiwa hana chochote akamshughulikia kimasomo hadi yake kupata stahhada ya elimu-jamii. **Malipo yake kumla kivuli tena nyumbani kwake. Ndiyo na yeye alikuwamo na jicho la nje.** Lakini mengi aliyafanyia nje. Pengine mara moja tu aliwahi kujisahau akayafanya nyumbani. (Kala Tufaha, uk.126)*
- 176.** *Maskini Fumbwe! Ndwele zimemtoa nyumbani akaja piga kambi hospitalini. Mafao yake ya kustaafu yote huenda kwa matibabu. Bahati yake kukumbana na Dkt kijana mchangamfu, Dkt. Kala Tufaha. Kijana mzuri sana huyu, Mungu amweke husema Fumbwe. Hatuna nasaba naye na muone jinsi anavyonishughulikia, wala si mtu wa kitu kidogo. Dkt. Kala Tufaha hakosi kila siku kumpitia mgonjwa wake kumjulia hali. Awe kazini asiwe kazini atapata wasaa wa kumpitia Fumbwe. Ikitokea asafiri, huwapigia wenziwe simu hapo hospitalini kujulia hali ya mgonjwa wake. (Kala Tufaha, uk.170)*

### Kiambatisho cha 3: *Pendo Katika Shari*

7. *Matano aliwashauri rafikize Sulubu na Makelele na kuwatahadharisha dhidi ya ugonjwa wa ukimwi uliokuwa ukiua watu kila uchao. **Lakini hawa walimpuuza na kumuona kama jongoo asiyeweza kupanda mtungi.** Walimsuta na kumwambia hajui maisha ni nini. Wewe wajitia ushamba bwana. Unajifanya mshago. Hujui maisha ni mafupi na ni lazima ule raha kwani karaha yaja. (Pendo katika Shari, uk.13)*
8. *Wakati huu Sulubu alikuwa akilia mithili ya mtoto mdogo, hasa alipofahamu sasa kuwa huenda ikawa yeye ndiye aliyesababisha vifo vya Rehema na wanawe. Isitoshe, huenda ndiye anayemuua Pendo taratibu. Haya yalimtia uchungu mno. (Pendo katika Shari, uk. 51)*
9. *Sulubu, alimtaazama usoni na macho yao yakakutana. **Sulubu huruma ilimvaa alipomwona mkewe akisota na kukohoa mfululizo kama anayeugua pumu.** Aliangalia ile kamba aliyoshikilia kana kwamba alitaka impe jibu la matatizo yake. (Pendo katika Shari, uk.54)*
33. *Hakutaka kumkabili Pendo na matokeo hayo. Kwa hivyo, akaamua kumpigia mumewe simu ili afike afisini mwake haraka iwezekanavyo. Dkt. mbona sikuelewi? Mtoto amezidiwa au amefariki? Sulubu alitaka kujua analoitiwa. Sikiliza Sulubu, **mtu hakatai wito, hukataa analoitiwa.** (Pendo Katika Shari, uk. 21)*
34. *Rehema ni mhazili wako, ni mfanyikazi wako afisini. Kwa nini unafanya ushuba na mtumishi wako? Bwana, hii ni aibu sana! Mkeo alipokuwa hospitali Rehema alihamia kwako. Je, umemfukuza Pendo ili umfanye Rehema mkeo? **Ha! uzuri wa mkakasi, ndani kipande cha mti.** (Pendo katika Shari, uk.31)*
55. *Jambwe! Mke gani wewe unayenizalia majanajike tu hapa nyumbani! Alibweka. Mimi nitatiwa kundini vipi na wenzangu ikiwa sina mtoto wa kiume atakayenirithi? Alipumua kwa nguvu kisha akaendelea kufoka. Basi ikiwa unataka uamuzi ni huu. Toka na majike yako urudi kwenu. **Wewe unadhani nilitoa mahari uje unizalie virukanjia hapa?** (Pendo katika Shari, uk. 6)*
56. *Walirudi na Sulubu lakini walipofika nyumbani, Rehema alikuwa katika dakika za mwisho duniani. Mama yake alijaribu kumsemesha lakini hakufumba jicho wala kufungua kinywa. Sulubu alipoulizwa na wakwe zake iwapo alijaribu kumpeleka mkewe hospitali, **aliwajibu kuwa dawa za hospitali hazikufua dafu.** (Pendo katika Shari, uk.45)*
57. *Baadhi yao pia waliweza kukumbana uso kwa uso na janga hilo la ukimwi. Walimtaazama Pendo kwa masikitiko, wakijua fika kwamba alikuwa anasubiri mauti. Waliwatazama wale wanawe na kutokwa na machozi, kwani **uyatima uliwakodolea macho** (Pendo katika Shari, uk.60)*
72. *Ah! Pendo, singetaka mtengane na mumeo. **Lakini yale ya kumleta hadi mwako nyumbani... nilisema potelea mbali nitakwambia.** Leo hii huna budi kujua mbivu na mbichi dada. Bi Sauda alieleza. Usoni alionyesha huruma na machoni kajawa na tuhuma. Angalikuwa na njia angalimwauni Pendo. (Pendo Katika Shari, uk.15)*

73. ...wale madaktari wenziwe walimkabidhi vijitabu kadha ili akavisome na kuelewa vyema jinsi anavyopaswa kuishi. Sulubu alivitazama na kutikisa kichwa huku akitutuma, *No this cant be... Why me? Hii haiwezekani...? Kisha machozi yakaanza kumtoka mfululizo. (Pendo Katika Shari, uk.51)*
121. *Kila wakati macho yalikuwa utosini akimtamani mwanamke yeyote aliyepita mbele yake. Tabia hiyo ilimfanya mkewe kumtoroka kwani alikuwa anampiga kila mara na kumfukuza ili aweze kustarehe na warembo aliowabadilisha kama nguo.(Pendo Katika Shari, uk.12)*
122. *Ijapokuwa Sulubu ana umati wa wasichana wanaohiari awabadilishe kama nguo, yupo mmoja kati yao ambaye amemganda kama funza... unajua anakoishi msichana huyo? Pendo alimuuliza huku akiukubali ukweli huo wa mambo. Sijui mwenzangu kama ningalijua, ningalikuwa nishamtia adabu mimi mwenyewe bila usaidizi wako. Lakini mbona hujaniambia haya yote Sauda! Ah! Pendo, singetaka mtengane na mumeo...lakini ya kumleta hadi mwako nyumbani... nilisema potelea mbali nitakwambia. Leo hii huna budi kujua mbivu na mbichi dada. (Pendo Katika Shari, uk.14-15)*
123. Sulubu naye alizidi kukaza kamba ya uhasama baina yake na mkewe. Pesa zake zikawa adimu kupatikana kama alivyokuwa yeye. Kamwe hakutaka mkewe aanzishe biashara ya aina yoyote ili kuyakimu baadhi ya mahitaji yake. Kila alipomwomba mumewe pesa za chakula, nguo au hata za matibabu ya mtoto wao mchanga, Sulubu alimtilia huku akimtolea kule. Aidha, alizidisha ujeuri akawa haambiliki hasemezeki. (Pendo Katika Shari, uk.15-16)
124. *Walimpa Pendo ushauri kuhusu hali yake hiyo kisha Pendo akawaza na kuelekea nyumbani. Alipokaribia nyumba yake, alipata mshtuko mwingine. Vitu vyake vyote vilikuwa vimetupwa nje, wakiwemo wanawe ambao walijiketia pale nje kwa huzuni. Walipomwona mama yao, walimkimbia, kila mmoja akiwa na kisa kumweleza. Alikuwa na watu wengine wawili wakatoa vitu vyote. Almasi alianza, alikuwa amekasirika sana. Alitutukana na kutufukuza sote nje. Tatu alipomuuliza mbona anatoa vitu vyetu nje, alimpiga kofi na kumrusha nje... Tatu alilia sana. (Pendo Katika Shari, uk.25)*
125. *Walirudi na Sulubu lakini walipofika nyumbani, Rehema alikuwa katika dakika zake za mwisho duniani. Mama yake alijaribu kumsemesha lakini hakumfumbua jicho wala kufungua kinywa. Sulubu alipoulizwa na wake zake iwapo alijaribu kumpeleka mkewe hospitali, aliwajibu kuwa dawa za hospitali hazikufua dafu. Usiku huo, Rehema aliaga dunia. Bi Kibibi hakuweza kustahimili. Alipiga ukwenzi mkali uliofanya majirani kumiminika nyumbani kwa Sulubu. Walimpata Sulubu akilia kama mtoto mdogo.(Pendo Katika Shari, uk.45)*
150. *Unajua kwamba pale karibu na madukani kuna kituo cha VCT? Hapo mwalimu wale watu wanaougua UKIMWI huenda kupimwa na kupewa dawa za kutumia. Tena akasema dawa hizo huwa hazilipiwi. Hutolewa bure na serikali. (Pendo Katika Shari, uk. 40)*
161. *Sulubu, mimi nakujua vizuri sana. Wewe una wapenzi chungu nzima na wengine hata huwajui majina yao. Kwa hivyo, huwezi kujua ni yupi atakayekuambukiza maradhi baadaye. Leo una Amina, kesho kwa Cheupe, kesho kutwa kwa Rosa. Huoni unajitia*

*kitanzi? Unajua UKIMWI unaua maelfu ulimwenguni lakini unafikiri wewe huwezi kuwa mmoja wa hao maelfu? (Pendo Katika Shari, uk. 30)*

- 170.** *Sulubu mimi nakujua vizuri sana. Wewe una wapenzi chungu nzima, na wengine huwajui hata majina yao. Kwa hivyo, huwezi kujua ni yupi atakayekuambukiza maradhi baadaye. Leo una Amina, kesho una Cheupe, kesho kutwa kwa Rosa. Huoni unajitia kitanzi? Unajua UKIMWI umewaua maelfu ulimwenguni lakini unafikiri wewe huwezi kuwa mmoja wa hao maelfu.(Pendo Katika Shari, uk.30)*
- 173.** *Kwa nini ulikataa kupimwa na Dkt.? Matano alimuuliza Sulubu baada ya kimya kirefu. Nani, mimi? Unadhani mimi naweza kuwa na magonjwa ya wanawake? Sulubu alimuuliza kwa ufidhuli ule ule. Sikiliza mwenzangu.UKIMWI si ugonjwa wa wanawake peke yao... Si unasambazwa na wanawale tu, alitamka Sulubu. Wajua baadhi ya wanaume hunishangaza. Watazurura huko na baada ya kupatwa na magonjwa ya zinaa, wanawalaumu wanawake, hata wake zao. Kwani magonjwa hayo huishi na wanawake pekee? (Pendo Katika Shari, uk.29)*
- 179.** *Baba, tumekuja kukuambia kwamba tunakupenda na tunakujali.” Aliponena maneno haya, Sulubu machozi yalianza kuchungulia machoni. Alifyatuka kwa kiganja cha mkono wake, akawatazama wanawe kwa huzuni. “Tunajua unaugua UKIMWI,” aliongeza Almasi, “lakini sisi tunaamini kuwa ukiishi maisha mazuri na ukila vizuri, hutateseka.” Maneno ya watoto hao yaliwastajaabisha wale waliokuwa pale. Pendo hakuweza kutamka neno bali alisimama kando ya kitanda huku akitikisa kichwa, ishara ya kukubaliana na yale yaliyotamkwa na wanawe. (Pendo Katika Shari, uk.59)*

#### Kiambatisho cha 4: *Sitaki Iwe Siri*

10. *Kwa kuwa mtu hakatai wito, hukataa aitiwalo, Musa naye alijipata akirudisha kitabu chake haraka mkobani na kukimbia kwenda eneo la paredi. Wanafunzi walifyatuka kama mishale ungedhani ni wanajeshi kwenye vita vya kwanza vya dunia. (Sitaki Iwe Siri, uk.16)*
11. *Musa alionekana mwenye furaha baada ya kusikia tangazo hilo maalum. Moyo wake ulidunda kama kengele ya kanisa. Alihisi msukumo wa aina fulani ukimchochea kushiriki katika shindano hilo. (Sitaki Iwe Siri, uk. 20)*
12. *Dhihaka za watu hasa marafiki zake kuwa Yuri alikuwa amekwisha kazi na hata kutemewa mate zilimtesa sana. Kila uchao, dhihaka hizo ziliukereza moyo wake kama msumeno ukatao mbele na nyuma. Alipiga moyo konde kuyakomesha mateso hayo ima fa ima. (Sitaki Iwe Siri, uk.49)*
35. *Ilikuwa saa mbili kasorobo hivi. Chambilecho Wahenga, mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo. Kila mwanafunzi akiacha alichokuwa akifanya na kutimua mbio kwenda kwenye eneo la paredi. Kwa kuwa mtu hakatai wito, hukataa aitiwalo. Musa naye alijipata akirudisha kitabu chake haraka mkobani na kukimbia kwenda eneo la paredi. Wanafunzi walifyatuka kama mishale ungedhani ni wanajeshi kwenye vita vya kwanza vya dunia. (Sitaki Iwe Siri, uk.16)*
36. *Kwa muda huo wote, Musa, Haki na Ukwa walikuwa wamekaa macho kujionea tukio hilo na kulifuatilia hatua kwa hatua. Walishangazwa na jinsi mambo yalivyokuwa yanafanywa kule hospitalini. Kwa hakika hawakukosea wahenga waliposema kwamba, kuishi kwingi ndio kuona mengi. Walikuwa tayari kujifunza mengi katika ziara yao ya hospitalini. (Sitaki Iwe Siri, uk.33)*
48. *Nyanya alitumia raslimali nyingi kugharamia matibabu yao, lakini ndwele hiyo haikusikia dawa kutwa kucha, afya zao zilizidi kudhoofika. Wakakonda kama ng'onda na macho yao kuwaingia ndani. Mbavu zao zikaweza kuhesabika. Kafara nazo zikawa kazi bure. Hatimaye, nyanya alienda kwa waganga wa miti shamba, tanguri na hirizi. (Sitaki Iwe Siri, uk.10)*
49. *Watu walikuwa wamenong'ona kwamba maumbile ya Yuri yalikuwa yamebadilika si haba. Kioo kilimwambia ukweli. Mwili wake ulikuwa umekondeana. Macho yalikuwa yamemwingia ndani. Mitulinga ilikuwa inaonekana huku mwili wake mzima ukinyongo'nyea kama mkufu kwa sababu ya kuishiwa nguvu. Laiti ungalimwona Yuri akiwa na siha yake. (Sitaki Iwe Siri, uk.48)*
50. *Musa alisimama kutoka mahala pake, akawa nusu anatembea nusu anakimbia. Wanafunzi na wazazi walimpungia Musa misitu ya mikono. Alipofika mbele ya jukwaa, wanahabari walikuwa wameshika nafasi zao. Miangaza kutoka kwenye kamera za wanahabari waliopiga picha ilionekana ikiwaka kama umeme. Kila mpiga picha alitaka kunasa picha nzuri ya Musa Matano. (Sitaki Iwe Siri, uk.63)*

58. *Kutwa kucha, afya zao zilizidi kudhoofika. Wakakonda kama ng'onda na macho yao kuwaingia ndani. Mbavu zao zikaweza kuhesabika. Kafara nazo zikawa kazi bure. Hatimaye, nyanya alienda kwa waganga wa miti shamba, tunguri na hirizi. (Sitaki Iwe Siri, uk.10)*
134. *Vifo hivyo vilikuwa vimeutia kovu moyo wake. Yusufu na mke wake waliougua kwa muda mrefu sana na hatimaye kusalimu amri. Nyanya alitumia rasilimali nyingi kugha ramia matibabu yao, lakini ndwele hiyo haikusikia dawa. Kutwa kucha, afya zao zilizidi kudhoofika. Wakakonda kama ng'onda na macho yao kuwaingia ndani. Mbavu zao zikaweza kuhesabika. Kafara nazo zikawa kazi bure. Hatimaye, nyanya alienda kwa waganga wa mitishamba, tunguri na hiziri. (Sitaki Iwe Siri, uk.10)*
135. *Ah... ni mada nzuri sana. UKIMWI ni miongoni mwa masuala ibuka katika jamii zetu za ulimwengu wa sasa. Suala la UKIMW halijazungumziwa na kuwekwa wazi katika jamii. Kwa sababu ya ugonjwa huu kuchukuliwa kuwa ni mwiko. (Sitaki Iwe Siri, uk.24)*
136. *Nyanya alihangaishwa sana na habari hiyo. Siri ambayo nimekuwa nikiweka jinsi kaburi linavyohifadhi siri hatimaye itajulikana! Nyanya aliwaza huku akikubali ombi la Musa. (Sitaki Iwe Siri, uk.28)*
137. *Ni sadfa kwamba siri mliyoghubika kwa miaka mingi ili wajukuu zangu wasiijue imefichuliwa. Wajukuu wangu hawa ni mayatima. Wazazi wao walifariki kutokana na maradhi ya UKIMWI, nao wakabaki mikononi mwangu. Waliponiuliza kilichowaua wazazi wao niliwajibu kuwa ni maradhi. Walipotaka kujua ni maradhi yepi, nilidinda kuwaambia. Nilitaka iwe siri lakini sasa Musa huyu ameandika insha ya ushindi – Sitaki Iwe Siri. Hii ni hatua muhimu katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI... (Sitaki Iwe Siri, uk. 66)*
155. *Watu walikuwa wamenong'ona kuwa maumbile ya Yuri yamebadilika si haba. Kioo kilimwambia ukweli. Mwili wake ulikuwa umekondeana. Macho yalikuwa yamemwingia ndani. Mitulinga ilikuwa inaonekana huku mwili wake mzima ukinyong'onyea kama mkufu kwa sababu ya kuishiwa na nguvu. Laiti ungalimwona Yuri akiwa na siha yake. (Sitaki Iwe Siri, uk.48)*
165. *Asante kwa kunipa fursa hii. Mimi nitasema machache sana. Kwanza nashukuru wote mnaoelimisha kizazi hiki cha baadaye ambacho kitachukua mahala petu. Maanake sisi tumekwisha kuzeeka. Ni sadfa kwamba siri niliyoighubika kwa miaka mingi ili wajukuu zangu wasiijue imefichuliwa. Wajukuu wangu hawa ni mayatima. Wazazi wao walifariki kutokana na maradhi ya UKIMWI, nao wakabaki mikononi mwangu. Waliponiuliza kilichowaua wazazi wao, niliwajibu kuwa ni maradhi. Nilitaka iwe siri lakini sasa Musa huyu ameandika insha ya ushindi. Sitaki Iwe Siri. Hii ni hatua muhimu katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI... (Sitaki Iwe Siri, uk.66)*

### Kiambatisho cha 5: Orodha

13. *Mwanakijiji wa 1: Ndiyo, yeye ni kama punda wa kijiji... Mpe karoti na kila mtu anaweza kumpanda! (Orodha, uk.18)*
14. *Taswira ya kumaliza sehemu ya chumba cha kulala inabaki imeganda. Wanakijiji ni kama mizuka inayopita taratibu kwenye sehemu hiyo – au wameganda katika mikao hadi inapokuwa zamu yao kuongea. (Orodha, uk.25)*
74. *Mama Furaha: Yalikuwa maombi yake ya mwisho kabla ya kufa, kwamba niseme maneno machache... hakika, hutanikatalia hilo, Padri!... Asante (Akijiweka sawa)... Familia yangu... wanakijiji, asanteni kwa kuhudhuria hii leo. Siku ya huzuni ya mazishi ya binti yangu mpendwa. Furaha... (Orodha, uk.2).*
75. *Baba: Kweli! Haiwezekani! Kutwa ninafanya kazi kwa bidii kwenye ardhi yetu ili tuyalishe matumbo yetu... (akigutia). Mama Furaha, chakula changu kiko tayari! Karibu nitakufa njaa hali nyie mbu wadogo mwaionyonya damu yangu yote! (Orodha, uk.4)*
76. *Mama Furaha: Nisingependa ufanye hivyo, iwapo hutujali, Padri: Furaha alitaka isomwe na kusikiwa kwa mara ya kwanza kwenye mazishi. Hata sisi hatujaisoma... (Orodha, uk.36)*
81. *Baba... Mama Furaha, chakula changu kiko tayari! Karibu nitakufa njaa hali nyie mbu wadogo mwinyonya damu yangu yote! (Orodha, uk.4)*
82. *Bw Ecko: Tafadhali mpenzi niite... (Anambusu mkono wake) Chaka! Nani ambaye hajapata kuliona ua hili zuri likizungukazunguka kijijini! Umenenepa mno, mpenzi... na katika sehemu zote zinazostahili! (Furaha anasifiwa na amefurahi) (Orodha, uk.6)*
93. *Mary: (Akimvuta Furaha kando). Nimekwambia hawa vijana ni burudani... hata yule mshamba Juma. Sikia, pata burudani na kuwa mwema. Kwa Ecko. Anaweza kukununulia vitu vingi sana! Unadhani wasichana wadogo kijijini hapa wanapataje viatu vipya, magauni na mabegi mapya mapya ili wapendeze... wapendeze kiasi cha kuwavutia vijana wazuri wa kiume! (Orodha, uk. 8)*
94. *Padri James:... Kwa watu hawa, mimi ndiye Padri wao... lakini mimi pia ni mwanadamu! Nafanya kila niwezalo kufanya ... na bado, kwangu yaelekea kwamba alikwishabikiriwa, kwa hiyo ingeleta tofautitofauti gani? Nilidhani hata ningeliweza kumliwaza? Lakini mtu, lazima awe mwangalifu... katika jumuiya ndogo namna hii... taarifa husafiri... wakati wote... kitu fulani huropokwa. (Orodha, uk. 10)*
110. *Salim:... Oh, wakati huu wadogo wako wanalala wapi? Furaha: Niliposhikwa na ugonjwa, wakahamia chumba kingine. Usiku nilikuwa nikiwasumbua! (Orodha, uk.28)*



- 138.** *Mama Furaha: Kama waweza kuendelea... (Anasubiri hadi watu wote wanapokuwa makini)... Baadhi ya watu kijijini wanasema Furaha alikufa kwa Malaria; kuna wengine wanasema alikufa kwa kifua kikuu, baadhi wanasema kwamba amerogwa. Lakini minong'ono mliyosikia hapa kijijini ni ukweli... binti yangu amekufa... kwa UKIMWI. (Orodha, uk.3)*
- 168.** *Mama Furaha: Na katika jina la Mungu, ukweli ni lazima usemwe! Yeye si wa kwanza wala hatakuwa wa mwisho iwapo hatutaukubali ukweli! Marafiki zangu, ndugu zangu wanakijiji... lazima tukumbuke kwamba Furaha aliteseka kutokana na virusi hivi vya kutisha, kama vile ambavyo ni lazima tukumbuke zile siku ambazo laana ilimpata, wakati alipokuwa anang'ara amejawa na ucheshi... na uhai. (Orodha, uk.3)*

## Kiambatisho cha 6: *Kilio Chetu*

15. *Wanapukutika kama majani ya kiangazi. (Kilio Chetu, uk.1)*
16. *Kakanyaga nyaya? Mbona wengine wanasema kafa kwa UKIMWI. Wewe nawe, unakuwa nyumanyuma kama koti? Mtu aliyekufa kwa kukanyaga nyaya maana yake kafa kwa UKIMWI. (Kilio Chetu, uk.5)*
77. *Watu walitoka upele, wengine waliharisha, mara nywele kunyonyeka na vifo kufuatia. Watu walipukutika, wapakutika, kama majani ya kiangazi. Wapakutika... (Kilio Chetu, uk.1)*
78. *Na toka lini jamii yetu ikaruhusu kukalishana kitako na vitoto ukivieleza habari ya ngono? Mie nikae hapa nafungua kinywa changu (Anaigiza): Sasa wanangu mfanye hivi... na vile na vile mimba itatokea... uchuro huo! (Kilio chetu, uk.12)*
79. *Kulikuweco matajiri na kulikuwepo na maskini. Watu waliishi kwa furaha. Punde dubwana kubwa likakiingilia kisiwa kile na kukawa kutafutana. (Aigiza) Dubwana likaleta balaa kisiwani. Kila aliyeguswa na dubwana alidhurika. Watu walitoka upele, wengine waliharishwa, mara nywele kunyonyoka na vifo vikafuatia. (Kilio Chetu, uk.1)*
80. *Ulitumia kondomu? Shiti wewe. Nini kondomu bwana. Pekupeku tu. (Kwa dharau) Unaweza kula pipi na ganda lake wewe? Sasa tuone basi. Leo mtoto kanitolea nje kabisa tena mkali pilipili si kitu. (Kilio Chetu, uk.19)*
95. *Mimi nawashangaa hata wale akina mama. Wengi wao wamesoma mpaka wamemaliza vidato. Unawakuta wamekaa na watoto wao wanaangalia picha za matusi... (Anacheka)... Shoga, watu tumechanganyikiwa. Tumeibomoa ghala imara ya kuhifadhi maadili yetu. Ghala tuliyojenga kwa miti yetu ya asili. Na sasa tunatukuza ghala iliyojengwa kwa miti dhaifu ya kijenzi. Miti inayougua kama mabua. Miti ambayo haipatikani kwa urahisi hapa kwetu. (Kilio Chetu, uk.8)*
96. *Haya angalia mwaka wa 1991 watoto 38 darasa la tatu walipata mimba; mwaka huo huo watoto 230 darasa la nne walipata mimba. Najua nikikutajia darasa la pili huwezi kuamini. (Kilio Chetu, uk.15)*
97. *Leo si ndio siku ya picha ya 'X'? Umesahau?... Aa toa ushamba wewe. Hujui mkanda wa video wa ngono? Mambo ya mapenzi."Vijana wanajidai kwamba nchi yao ni ya demokrasia na hiyo wanajiamulia kila walipendalo. Vijana wanasema, Siyo zamani akina mama utasikia: Vibaya kuangalia magazeti ya mapicha ya uchi mtaota... Sinema za 'X' ni kwa wakubwa tu siku hizi tunaangalia vyote, nani anaota. (Kilio Chetu, uk.20)*
98. *ANNA: Utakufa Suzi, umeishafanya kosa kwa nini ufanye kosa lingine? SUZI: Mbona Salma alitoa mimba na wala hajafa? ANNA: Sawa hajafa, hiyo ni kudra ya Mwenyezi Mungu, lakini unajuaje kama yeye ni mzima? Je, kama ameharibu kizazi kwa kutoa mimba? Wewe unasema Salma huyo mmoja, mimi ninawafahamu watu wanne waliokufa kwa kutoa mimba. Suzi, ni hatari usitoe rafiki yangu. (Kilio Chetu, uk. 32-33)*

139. *Wakabandika mabango kupeana tahadhari, lakini watoto wakateketea kwa kukosa habari zozote za kuwaokoa. Wakubwa kukwepa lawama wakajitetea. Mwiko kuzungumzia mambo haya kwa watoto. Dini inakataza, Oh! Mila haziruhusu. (Kilio Chetu, uk.2)*
166. *Jirani: mimi naonelea kungefanyika jitihada niwapelekeni kwa fundi mmoja aitwaye Chongo. Huyo bwana hashindwi kitu. Mtu anawarudisha msikule nyumbani atashindwa nini tena? (Kilio Chetu, uk.35-36)*
178. *Mgonjwa asitengwe kwa maana UKIMWI huambukizwi kwa hewa au kuwa pamoja. Mgonjwa apewe chakula bora na yanapojitokeza magonjwa mengine kama Malaria apelekwé hospitali kwa tiba. (Kilio Chetu, uk.37)*
179. *Basi watoto wakaendelea kudhoofika kwa kukosa elimu ya jinsia, Dubwana lile likaendelea kuwadhuru, wakateketea. Vifo vikawazoa ...Vikawazoa... vikawazoa. (Kilio Chetu, uk.3)*

### Kiambatisho cha 7: Giza

25. Hii *sweet* nitakutumia *message bye!* (Giza, uk. 5)
26. *Wewe Nuru, eti Mai kaniambia kuwa Davina aliyekuwa girlfriend wa Robby amefariki.* (Giza, uk.8)
27. *.Nuru unatakiwa kuwa mwangalifu kwa maana utapata kichaa cha UKIMWI. Unawaza vile ambavyo havipo! Utashindwa kufanya mambo yako na UKIMWI usiupate na maisha yawe marefu na magumu. Be careful.* (Giza, uk.19)
59. *Nuru, we mzuri kama jina lako nadhani hata thamani yako ni kubwa kama jina lako lilivyo na thamani. (Kimya, Nuru hajibu, Mona aligundua kuwa alikuwa akiongea peke yake na Nuru alikuwa akilia.) Nuru: Vipi shoga mbona unanikata utumbo mwenzio? Umefikwa na nini?* (Giza, uk.6)
60. *Sipendi kukumbuka siku hiyo, kwani nilimzoea mdogo wangu na aliniacha peke yangu kwenye dunia yenye giza... Mah! Pole Suzi! Duniani ni kufunga mkanda...(Giza, uk.15)*
61. *Hai! (anapita kijana amevaa fulana imeandikwa kwa herufi kubwa) UNARINGA UMEPIMA GIZA.* (Giza, uk.18)
106. *SUZI: Mdogo wangu alianza kuugua. Yule mama alivyoona hivyo alitufukuza... Hakutusaidia. Nilitumia peesa zangu kumhudumia. Alipopimwa alikutwa na virusi vya UKIMWI. Mama alitufukuza na akaturushia mizigo yetu nje na mshahara akininyima.* (Giza, uk.14-15)
107. *SUZI: Ndipo nilipoishi, kule kihazarani nilifukuzwa eti maiti ilileta nuksi. (Mara Suzi anashindwa kuzungumza, anakohoa sana, anatajika mfululizo. Nuru anaenda kumwita Nesi, lakini anakuta Nesi anakunywa chai hajibu kitu, Nuru anaporudi anamkuta Suzi macho yameangalia juu) Giza aa gizaaaa (...)* (Giza, uk.16)
108. *Dkt.: Wagonjwa hawa wanasumbua sana inapaswa wakae nyumbani tu. (anamgeukia Nuru) Una hela za kununulia maji ya dripu?* (Giza, uk. 36)
109. *MONA: Huku, majungu tupu. Watu wote wananifahamu na jinsi ninavyougua. Siendi tena. Nuru bye (Nuru anaenda kwake anamkuta Steve anagaragara, anatajika ovyo.)* (Giza, uk.34)
130. *Nuru: Nasoma ili iweje? Sioni sababu ya kusoma kwani sitapata nafasi ya kufaidi matunda ya mateso shuleni. Hata wazazi wangu walionizaa na kunigharamia maisha yangu hawatapata nafasi ya kufurahia matunda ya kazi yao bali wataambulia huzuni na mateso pamoja na majuto yasiyoisha (anainua macho na kutazama juu) Nini maana ya maisha? Eti ninasoma nipate digrii ya nini? Mbona naona giza tu! Giza! Giza! Aaah! Sioni mbele niendako wala nyuma nitokako.* (Giza, uk.7)
131. *Robby: Davina! Davina! Kweli amekufa! Lakini... sina hakika. Nakumbuka rafiki yangu Kapu alionionya juu ya mapenzi yangu na Davina, sikumsikiliza. Sasa nitakufa. Nitakufa vibaya eti wanasema hata Mmh! Kitu inakatika. Basi zangu*

*zimekwisha. Niache chuo. Nikasubiri kifo. Kufa kibudu, kifo cha majuto. Robby mie hata sijaishi bado. Eeh niliishi lini? Sitakuwa na familia wala kazi, sitayaona maisha. Maisha ambayo kila mtu huyapitia. Nasoma ili iweje? Nasogeza siku? Maskini baba na mama yangu! Wangejua. (Giza, uk.10)*

132. *SUZI: Wasamaria walinisaidia kumzika. Na maisha yangu tangu siku hiyo yakabadilika nikawa sitafuti tena chakula, cha nini? Namtafutia nani? Basi nikaanza kuugua sana na kila siku nilikunywa asprini. (Giza, uk.16)*
133. *MONA: Najua naenda kufa (anawaza) hivi kweli huu ni UKIMWI? Mbona Robby alikufa kwa ajali ya gari? (Giza, uk.26)*
142. *Davina alikuwa mpenzi wa afisa wa usalama Mori. Mori alifariki yapita miaka minne. Alikufa kwa UKIMWI na kwa vile Davina kaishi miaka minne zaidi basi watu wanaamini Mori hakufa kwa UKIMWI. Jambo usilolijua ni sawa na usiku wa kiza. Vipi hawa watu waliaminiana! (Anamgeukia Mona, anamtazama kwa jicho la huruma, machozi yanamtoka anasema) Mona niambie Steve yuko wapi? (Giza, uk. 9)*
143. *Sasa nitakufa. Nitakufa vibaya eti wanasema hata Mmh!...Robby anataka kuvuka barabara mara gari linakuja kwa kasi linamgonga Robby anaanguka chini, huku povu likimtoka kinywani. Watu wanahisi kuwa amekufa kwa shinikizo la damu) ...Robby huyooo! Zake ziliishia hapo. Hakuweza kujua ukweli wa kifo cha Davina. Waliobaki nyuma pia wako gizani. Hivyo ndivyo giza lilivyotanda kila kona ya maisha.(Giza, uk.10-11)*
144. *Nakumbuka siku moja mama aliniita chumbani akafunua nguo na kunionyesha sehemu zake za siri, alikuwa na vidonda. Ni nyama tu alioza. Tulimzika mama. Baba wa kambo alikuwa akitutukana kila siku akidai mama ni shetani aliamua kumuua kwa kumnyonga. Sikuelewa hilo... Alifanya mapenzi kwa nguvu. Kila siku alikuwa akinibaka. Alimbaka hata mdogo wangu. (alitulia kisha akaita) dada upo? Naona giza, gizaaa! (Giza, uk.13)*
145. *SUZI: Ndipo nilipoishi, kule kibarazani nilifukuzwa eti maiti ilileta nuksi. (Mara Suzi anashindwa kuzungumza, anakohoa sana, anatajika mfululizo. Nuru anaenda kumwita Nesi, lakini anakuta nesi anakunywa chai hajibu kitu, Nuru anaporudi anamkuta Suzi macho yameangalia juu.NURU: Analia sana. (Kicheko kikubwa kinatokea kila upande Nuru anaangaza huku na huko anasikia sauti HAKUNA MAISHA NDANI YA GIZA. (Giza, uk.16)*
146. *Mkifufuka mtalia na kamwe hamtanyamaza. Nitawaambia nini tukikutana kaburini? Dunia mlioniachia imejaa giza! Watoto na wajukuu wanapapasa. Hakuna anayemwona mwenzie, akipapasa akiona mwanamke halali yake, mbuzi halali yake, mtoto halali yake... Nitasimulia nini uovu umezidi giza limeongezeka. (Giza, uk. 23-24)*
147. *... Steve aliniambia nimsamehe au aliniacha gizani! Mama hiyo ni zawadi tuliyokuletea watoto hao. (anafikiri) Lakini kama UKIMWI ni adhabu mbona hata watiifu wanakumbwa? (anasikia sauti) anapoteza fahamu. GIZA... Haya hata Nuru imezimwa na Giza. (Giza, uk.41)*

- 167.** *Msimulizi: Mmeyesikia hayo? Mmesikia! Haya UKIMWI ni kwa maskini. Wakubwa, viongozi hawaugui UKIMWI ila shinikizo la damu, Kansa na kufa ghafla. Jamii hii inakwenda wapi? Nani atasema Wazi ana UKIMWI ili jamii ione na ijifunze, tutazaa watoto Wenye UKIMWI mpaka lini? (Giza, uk.22)*
- 180.** *Nuru: ...madawa na huduma zote zinaishia mijini, vijijini watu hawajapewa elimu juu ya 58ya UKIMWI. Wanachojua ni kula pesa na kuimba maredioni na majukwaani juu ya kondomu. Kondomu tu ndio wanaona dawa ya UKIMWI. (Giza, uk.18)*
- 181.** *Nuru: Kila siku wanaimba kuhusu UKIMWI na dawa za kuongeza siku, Je, ni walala hoi wangapi wanazipata? Kila wanalolisema ni sauti ya Mwendawazimu. (Giza, uk.18)*
- 182.** *Mona: Mbona nishanasa wengi wanajigonga tu. Siachi vitu, mbona mimi Pia hawakunihurumii. Sauti: Hakuna atakayebaki, labda milima. (Giza, uk.29-30)*

**Kiambatanisho cha 8: Likizo Ya Mauti Na Hadithi Nyingine**

17. *Wakesho najua u msiri kama kaburi au tuseme kama giza. (Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine, uk.1)*
18. *Alikuwa amekonda taabani na alionekana mwembamba kama ng'onda. Wakesho aliinama na kuanza kutetemeka kwa nguvu na kuguna kama mtu aliyeshikwa na kifafa ghafla. (Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine uk.2)*
28. *Kwa nini unanipenda ilhali huko tayari kujitolea nafsi yako kwangu? Ama kweli, wamesema wazee kuwa, **You can-not eat your cake and have it! You see you want me but not to the extent of wanting to marry me... I think you have missed the point.** (Likizo ya Mauti, uk.81)*
29. *Si neno, Darling, mimi niko very familiar with these cities. Lakini nafikiri wamebadilisha route kidogo. Pengine nitakuelezea baadaye wapi tunapita. Seriously, I hope you are having a good time, Honey! (Likizo ya Mauti, uk.70)*
37. *Maradhi na usumbufu aliokuwa nao Wakesho ulisababishwa na matukio kadha yaliyomkumba ndani ya mwaka mmoja uliotangulia. Kama walivyonena wavyele, **Hapana msiba usiokuwa na mwenziwe.** Hiyo ni busara iliyokuwa na ukweli usiopingika kwani anayetarajia suluhu, sharti ajiandae kwa vita. (Likizo ya Mauti, uk. 2)*
38. *.Akipenda chongo huita kengeza na pia kuwa, **Kipendacho roho ni dawa.** Alikuwa yu radhi kungoja hadi mwisho wa dahari kusudi ampate Wakesho. Aliamini fika kuwa, ndoa hufungwa mbinguni na pia Hauchi hauchi, unakuja. (Likizo ya Mauti, uk.3)*
39. *Alijilaumu kwa kuweka imani yake kwa wapelelezi hawa badala ya kumkabidhi Mungu Mweza wa shida zote za moyo wake. **Ama kweli alisahau kuwa bidii ya mja haiondoi kudura.** (Likizo ya Mauti, uk.6)*
62. *Juhudi zao za kuutanabisha utawala wa chuo kuhusu tatizo hili ziliambulia patupu. (Likizo ya Mauti, uk. 4)*
63. *Yaliyogomelea msumari wa mwisho juu ya jenze lake. (Likizo ya Mauti, uk.4)*
64. *Wakesho hakujibu kwa muda mrefu na alionekana bado kapotea katika lindi lake la fikira akiwaza na kuwazua. (Likizo ya Mauti, uk.6)*
99. *Hili si jambo la kufanyia mzaha kwani unajua kwamba tayari **ninayo familia yangu wala sio dhamira yangu kuvunja nadhiri niliyoiweka katika ndoa yangu.** Kwani kuwa wapenzi ni sharti kwanza tuoane? (Likizo ya Mauti, uk.81)*
100. *Mzee Gogo alichelea kutiwa mbaroni kwa kufanya mapenzi na msichana ambaye umri wake haukuwa halali. Hata hivyo alisahau kwamba ingawa aliweza kuupea mkono wa sheria na macho ya wanajamii wengine, kunalo moja liliomponyoka... Alighafilika asikumbuke kuwa ziraili jipya liliozuka kivyake likawashinda hata*

*vogogo wa sayansi na maarifa lilikuwa tayari mawindoni kila mahali na kila wakati!*  
**(Likizo ya Mauti, uk.82)**

- 111.** *Ingawa alikuwa na nguvu na uwezo wa kuifanya mitihani hiyo, Wakesho hakuruhusiwa na alihisi ubaguzi na unyama katika uamuzi huo. (Likizo ya Mauti, uk.4)*
- 112.** *Kinachoniuma zaidi sio maradhi haya ya UKIMWI ikiwa ndiyo hatima yangu ya maisha lakini ni kule kukimbiwa na marafiki na wenzangu wote kwa umoja wao. Nitawezaje kuukabili ulimwengu wakati ambapo hata Jimi, mchumba wangu ameniasi kwa hatia ya jambo ambalo sikulisababisha? Huu ni unyama kamili. Hiki ndicho kilele cha unafiki wa binadamu. (Likizo ya Mauti, uk.5)*
- 115.** *Alivutiwa na barua mbili tu katika furushi zima. Moja ilitoka katika shirika moja la kijamii lililoitwa, Bright Future Limited ambamo Wakesho alikuwa amepeleka maombi ya kazi. Barua yenyewe ilikuwa na mistari miwili tu na ilisema; 'Haya ni kuhusu maombi yako ya kazi katika shirika hili. Kutokana na hali yako ya sasa, shirika hili haliwezi kukuajiri ingawa umetimiza masharti yanayotakiwa. (Likizo ya Mauti, uk.5)*
- 148.** *Aliandikaandika na mara akamgeukia mwuguzi na Dkt. mwenzake akasema, 'I think she is positive'. (Likizo ya Mauti, uk. 4)*



### Kiambatisho cha 9: Alidhani Kapata Na Hadithi Nyingine

19. *Laniambia sasa, jembe linalitumikia kweli, hela zinaingia kama mafuriko ya El nino! Wajua linavyoanza barua” kipenzi cha moyo wangu ...na kutamatisha kwa metahli kwamba, “Akupendaye kwa dhati ya moyoni! (Alidhani Kapata na Hadithi nyingine, uk.85)*
20. *Sio kwamba nimejiachia sawa na bendera ya kupeperushwa na upepo, hashu. Miye mara nyingi hujiona kama simba mawindoni; nikimwona paa miye naye kiwa pundamilia, vilevile; sungura naye, hana bahati lau nitampiku kwa kasi. (Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine, uk.89)*
40. *Natamani lau ningelipata fursa ya kurudi huko chuoni-bila shaka ningelilakabiwa bookworm au pengine Vicky Mabuku! Kweli majuto ni mjukuu! Lau ningelijitahidi kweli, nikajua nilifuatia nini huko chuoni, ningelikuwa mwingine na pengine leo! (Alidhani Kapata, uk.87)*
41. *Usijeshangaa ukanunua blue moja, ukajikuta wajumbua mbele ya Voltaire au hao Coakroach wako chuoni. Pole dada; japo msiba wa kujitakia hauna kilio. Hivi alikupa hela za kutosheleza matibabu? (Alidhani Kapata, uk.94)*
65. *Miye falsafa yangu maishani, ni usimwamshe aliyelala, usije ukalala Mwenyewe naaamini kwamba, ulimwengu wa leo ni kutoka, ukaona, ukalenga, ukafuma. Basi!. (Alidhani Kapata, uk.85)*
66. *Pole dada Francesca; ubaya sina, ila naomba ufahamu sio kila n’gombe ana kupe umdandie mgongoni, kumdonoa! (Alidhani Kapata, uk.91)*
101. *Lakini shoga, pana tatizo sugu; darling wangu , mume wa watu! Hilo jike linaloninyima hewa kupumua, aibu kamishna wa polisi-kitengo cha ujasusi! Lakini kwa sasa, sioni haja ya kumsukuma Voltaire hadi ukingoni; anifaa kweli. (Alidhani Kapata, uk.86)*
102. *France, waniliza nduguyo hapa! yaani, zaidi ya kuwa huna fadhila kuwa Ngufumali unatembea na Voltaire mume wa watu, bado na hao cockroach unao Tena wawili? Ndio tuseme washindana na nani au nini vile bibi?(Alidhani Kapata, uk.88 )*

**Kiambatisho cha 10: Kiti Cha Moyoni Na Hadithi Nyingine**

21. *Alihudhuria kwa roho safi ili kusuluhia kaida na kawaida ya jumuiya ya Kambi Miwa. Ilibidi avumilie kama anayetwisha makaa ya moto kichwani. (Kiti cha Moyoni, uk. 80)*
22. *Unatafuta nini hapa?” “Nilikuwaa...aaa!” “Eeh! Nimekuona unapitapita hapa sijui mara ngapi... unatafuta nini? Kimya . Unarandarandaje hapa kama mtu anayewashwa na upupu? (Kiti cha Moyoni, uk. 84)*
42. *Anakumbuka kujishaua kwa Salome na mabezo na mapuuza yake. Mwasame alitaka kumchukia, kumbeza, kumpuuza pia. **Dawa ya moto ni moto. Akupendaye Mpende na mche asiyekupenda. (Kiti cha Moyoni, uk.82)***
43. *Ni nini hiki nasikia kuhusu mume wako? Umesikia upepo na ujinga na udaku mtupu. Kunradhi bibiye! Unaniita bibiye, nimekuzalia nani? Samahani **Mwasame wewe pilipili usiyoila inakuwashia nini?**(Kiti cha Moyoni, uk. 84)*
67. *Ingawa arusi ya Salome ilikuwa chanzo cha kero na hasira kwa Mwasame, alipiga moyo konde kuhudhuria kwa roho safi. Alihudhuria kwa roho safi ili kusuluhisha kaida na kawaida za jumuiya ya Kambi Miwa. **(Kiti cha Moyoni, uk.80)***
68. *Aha! Unajifanya mjuaji, eeh! Ila utaendelea kula mwande,” alitamka Salome kwa dharau. Salome alisonya na kukurupuka ghafla na kumwacha Mwasame kwenye mataa. **(Kiti cha Moyoni, uk. 82)***
140. *Majoni amerudi. Alikuwa akitembea mwendo wa kinyonga. Amenyongea. Ni mkondefu na mwenye macho yaliyojizika kwenye uso uliosawijika... Gurudumu la afya ya Majoni lilikuwa limetobokea Mbale. Kohoakohoa zake zilikuwa mwanzo zinaeleweka kwa maana watu wakikohoa tangu hapo. Watu hukohoa kisha kikohozi kikaisha. Lakini kikohozi chake kikawa hakiishi naye akawa hana siha, hana udole...watu wakaanza kusema labda mwenzetu amekanyaga waya. **(Kiti cha Moyoni, uk.86)***
141. *Yote Mwasame anayakumbuka. Anakumbuka kwamba hata nyasi ilikuwa haijaota kwenye kaburi la lofa kabla majasho hayajaanza kummwagika kumtafuta mtoto wa kwanza-wake yeye Mwasame na malkia wa moyo wake. Pamoja na dhoofuhali ya malkia, wakampata mtoto mvulana... lakini baada ya vikohozi visivyokwisha na kuendesha tena, malkia na Petro makao yao ni viungulima viwili vilivyosimama uani, kila mmoja na msalaba alioutengeneza Mwasame kwa nguvu zake haba kwa roho safi. **(Kiti cha Moyoni, uk.88)***